# JUMA TAKATIFU NA MKUBWA

**CENTRE MISSION ORTODOXE**
**KOLWEZI ZAIRE**
**1997**

# M A T A N G U L I Z I

Kwa baraka ya Mitropoliti wetu wa Afrika ya Kati na Mkubwa wa Ekwateri yote Bwana Arkiaskofu TIMOTHEOS, tunatayarisha hii Kitabu ya Juma Takatifu na Mkubwa na Siku Kuu ya Paska katika lugha ya Swahili sababu ya kusaidia Mapadri, Washemasi, Waimbaji na Waaminifu Waorthodoksi wetu kwa kutimiza vema Ibada yote ya Paska ya Ufufuo wa Bwana, Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu, kwa ajili sisi wanadamu.

Tunatumainia ya kama kila mumoja wetu hatafazaika tena moyoni mwake kwa kutafuta huku na kule wapi atapata Ibada ao wimbo fulani wakati wa Juma Mkubwa na Paska. Hii Kitabu ni tayari na tunamushukuru Bwana wetu Yesu Kristu na tunamuitoa kwa Utukufu Wake ya milele.

**CENTRE MISSION ORTODOXE KOLWEZI ZAIRE**
**1997**

# JUMA TAKATIFU NA MKUBWA

## SIKU YA KWANZA MKUBWA
## SALA YA ASUBUI (ORTHROS)

*Hii Sala ya Asubui tutaisoma mu Juma ya Matawi Mangaribi katika Desturi ya Kanisa yetu, kwa sababu kesho Mu Kazi Moja asubui, watu wote karibu wataenda ma kazi yao.*

**PADRI**: Abarikiwe Mungu wetu daima. . .
**MWIMBAJI**: Amina
**PADRI**: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako. Mufalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. . .
**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .
**PADRI**: Kwa kuwa ufalme, uwezo na utukufu ni wako. . .
**MSOMAJI**: Amina. Bwana hurumia *(Mara kumi na pili).*

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme wetu.

**ZABURI** 19(20)
Bwana akujibu siku ya taabu; jina la Mungu wa Yakobo likunyanyue; akutumiekusaidia toka pahali patakatifu na kukupatisha nguvu toka Sayuni; akumbuke zabihu zako zote, na kupokea sadaka yako ya kuteketezwa. Akupe hamu ya moyo wako, na kutimiza mashauri yako yote. Tutashangilia wokovu wako, kwa jina la Mungu wetu tutasimamisha bendera zetu;sasa ninajua ya kuwa Bwana anaokoa mupakaliwa wake; atamujibu toka mbingu zake takatifu na nguvu ya kuokoa ya mukono wake wa kuume. Wengine wanaamini magari na wengine farasi; Lakini sisi tutataja jina la Bwana Mungu wetu. Wameinama na kuanguka; Lakini sisi tumenyanyuliwa na tunasimama. Okoa, Bwana; Mufalme atujibu wakati tunapoita.

ZABURUI 20(21)
Mufalme atafurahi kwa nguvu yako, ee Bwana; na kwa wokovu wako ataona shangwe nyingi sana! Umemupa hamu ya moyo wake, wala hukuzuiza maombi ya midomo yake. Kwa sababu ulimutangulia na baraka ya vitu vizuri; Unaweka taji ya zahabu safi juu ya kichwa chake. Alikuomba uhai, ukamupa; Hata siku nyingi kwa milele na milele. Utukufu wake ni mukubwa katika wokovu wako; Heshima na enzi unaweka juu yake. Maana umemufanya mubarikiwa zaidi kwa milele; Umemufurahisha kwa furaha mbele yako. Kwa kuwa mufalme anaamini Bwana, na kwa sababu ya wema wake aliye juu sana hatatikisika. Mukono wako utapata adui zako zote; Mukono wako wa kuume utawapata wanaokuchukia. Utawafanya kuwa kama tanuru ya moto, kwa wakati wa hasira yako. Bwana atawameza katika gazabu yake, na moto utawakula. Utaharibu matunda yao na kuyaondosha katika inchi, na wazao wao katika wana wa watu. Kwa sababu walikusudi mabaya juu yako; Waliwaza hila, wasiyoweza kutimiza. Kwa maana utawafanya kugeuza mugongo wao, utatayarisha na kamba za upinde wako juu ya uso wao. Utukuzwe, ee Bwana, kwa nguvu zako; nasi tutaimba na
kusifu uwezo wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .
**PADRI**: Kwa kuwa ufalme, uwezo. . .

**MSOMAJI**: Amina.
Ee Bwana okoa taifa lako na bariki urizi wako. Ukiwapa wafalme kushinda juu ya wakafiri, na kuilinda jamii yako kwa Msalaba wako.

Utukufu kwa Baba. . .
Ewe Kristu Mungu, uliyeinuliwa kusudi Msalabani, uipe jamii ile jipya iliyo na jina lako, rehema yako. Uwafurahishe wafalme wetu waaminifu na nguvu yako, ukiwatunza na kushinda juu ya washindani, wakifurahiwa kwa agano jipya, silaha, ya amani, alama isioshindika.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION
Ewe Mzazi-Mungu, Msifiwa pia, Uhifazi kuogopa na kusioshindika, usitupe maombi yetu, Mwema we. Tegemeza jamii ya waorthodoksi, uwaokoe hawa ambao umewamrisha kuwa wafalme, uwape ushindi toka mbinguni, kwa kuwa umemzaa, Mungu, U peke yako Mbarikiwa.

**PADRI**: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tuakuomba, utusikilize na utuhurumie.
**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya Wakristu watawa na Waorthodoksi wote.
**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu *(jina lake)* na kwa ajili ya ndugu zetu wote.
**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*
**PADRI**: Kwa kuwa u Mungu mwenye huruma, tena Mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote. . .
**MWIMBAJI**: Amina. Kwa jina la Bwana bariki, ee Padri.

**PADRI**: Kwa Utatu Mutakatifu, Wenye asili moja, Muumba wa uhai, usiotengeka, utukufu uwe daima. Sasa na siku zote, hata milele na milele.

***MSOMAJI** ataanza kusoma EKSAPSALMOS.*

Utukufu kwa Mungu juu pia, na nchini amani, urazi kwa wanadamu *(mara tatu).*
Ee Bwana, uifungue midomo yangu, na kinywa changu kitazinena sifa zako *(mara mbili).*

**ZABURI** 3: Mwenye kutulinda ni Mungu
Bwana, watesi wangu wamezidi kwangu! Wao ni wengi wanaosimama juu yangu. Wao ni wengi wanaoniambia nafsi yangu, hana wokovu kwa Bwana. Lakini wewe, ee Bwana, ni ngabo yangu pande zote; Utukufu wangu, na mwenye kunyanyua kichwa changu, nimelia kwa Bwana na sauti yangu, naye amenijibu toka mulima wake mutakatifu. Nililala na kupata usingizi; nikaamka; kwa kuwa Bwana amenitegemeza. Sitaogopa elfu kumi za watu waliojipanga juu yangu, pande zote. Simama, ee Bwana; uniokoe, ee Mungu wangu; Maana umepiga kituguta cha adui zangu zote; umevunja meno ya waovu. Wokovu ni wa Bwana; Baraka yako iwe juu ya watu wako.

*Na tena:* Nililala na kupata usingizi; nikaamka; kwa kuwa Bwana amenitegemeza.

**ZABURI** 37 (38): Kukiri zambi.
Ee Bwana, usinihamakie katika gazabu yako; wala usiniazibu kwa ukali wa hasira yako. Kwa sababu mishale yako imenichoma, na mkono wako umenipata. Hakuna uzima katika mwili wangu kwa sababu ya gazabu yako; wala hakuna afya mifupani mwangu kwa sababu ya zambi yangu. Kwa sababu zambi zangu zimenifunikiza kichwa changu; kama muzigo kunishinda.

Vidonda vyangu vinanuka, vimeoza, kwa sababu ya upumbafu wangu. Nimepindika na kuinama sana; muchana kutwa ninakwenda nikiomboleza. Kwa sababu viuno vyangu vinajaa homa; wala hakuna uzima katika mwili wangu. Mimi ni zaifu na nimepondwa sana; nimeugua kwa sababu ya masumbuko ya moyo wangu. Bwana, hamu yangu yote ni mbele yako; na kuugua kwangu hakufichwi mbele yako. Moyo wangu unapigapiga, nguvu zangu zimeniacha; Nayo nuru ya macho yangu imeniondokea. Wanaonipenda na rafiki zangu wanasimama mbali na pigo langu; na jamaa zangu wanasimama mbali. Wao vilevile wanaotafuta uzima wangu wananiwekea mitego; nao wanaotafuta kuniumiza wanasema maneno mabaya, na wanawaza hila muchana kutwa. Lakini mimi ni kama kiziwi, sisikii; nami ni kama bubu asiyefungua kinywa chake.

Ndiyo, mimi ni kama mutu asiyesikia, asiye na mabishano kinywani mwake. Kwa sababu ndani yako, ee Bwana, ninaweka tumaini langu; wewe utajibu, ee Bwana Mungu wangu. Kwa sababu nilisema: Wasije wanafurahi juu yangu; wakati muguu wangu unapoteleza wanajikuza juu yangu. Kwa maana mimi ni karibu na kusita, na huzuni yangu ni mbele yangu daima. Kwa maana nitapasha uovu wangu; na kuhuzunika kwa zambi yangu. Lakini adui zangu ni wazima, wenye nguvu; nao wanaonichukia bule wamekuwa wengi. Wao vilevile wanaolipa mabaya kwa mema ni watesi kwangu kwa sababu ninafuata kitu kilicho chema. Usiniache, ee Bwana. Ee Mungu wangu, usiwe mbali nami. Ufanye haraka kunisaidia, ee Bwana wokovu wangu.

*Na tena:* Usiniache, ee Bwana; ee Mungu wangu, usiwe mbali nami. Ufanye haraka kunisaidia, ewe Bwana wokovu wangu.

**ZABURI** 62 (63): Kiu kwa kutumikia Mungu.

Ee Mungu, wewe ni Mungu wangu; asubui mapema nitakutafuta; nafsi yangu inaona kiu kwako, mwili wangu unakutaka sana, katika inchi ya kukauka na ya kuchoka, isiyo na maji. Hivi nilikutazama katika pahali patakatifu, nione uwezo wako na utukufu wako. Maana wema wako ni muzuri kuliko uzima; midomo yangu itakusifu. Hivi nitakubariki ningali hai; nitanyanyua mikono yangu kwa jina lako. Nafsi yangu itashibishwa kwa mafuta na vinono; na kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya furaha; wakati ninapokumbuka juu ya kitanda changu, na ninawaza juu yako katika makesha ya usiku. Maana wewe umekuwa musaidia wangu, na katika kivuli cha mabawa yako nitafurahi. Nafsi yangu inakufuata sana; mukono wako wa kuume unanitegemeza. Lakini wale wanaotafuta nafsi yangu, ili kuiharibu, watashuka kwa pande za chini za inchi. Watatolewa kwa uwezo wa upanga; watakuwa sehemu za imbwa za mwitu. Lakini mufalme atafurahia Mungu; kila mutu anayeapa kwa yeye atashangalia; kwa maana vinywa vyao vinavyosema uwongo vitafungwa.

*Na tena:* Wakati ninapokukumbuka juu ya kitanda changu, na ninawaza juu yako katika makesha ya usiku. Maneno wewe umekuwa musaidia wangu katika kivuli cha mabawa yako nitafurahi. Nafsi yangu inakufuata sana, mukono wako wa kuume unanitegemeza.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Alliluya, Alliluya, Alliluya, utukufu kwako, ee Mungu, *(Mara tatu).*

Bwana hurumia *(mara tatu)*. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

*Elezo: Padri Ile wakati anatokea mlangoni wa kaskazini na atasimama mbele ya Ikone ya Bwana Yesu; ambako atakapoendelea kusoma sala I2 kwa siri, zile zilizobaki wakati alipokuwa katika pahali patakatifu. Anapoisha sala zote I2, atabusu Ikone ya Bwana Yesu miguuni na nyuma yake ataingilia mlangoni wa kusini.*

***MSOMAJI*** *anaendelea na Eksapsalmos ku Zaburi Sita.*

**ZABURI** 87(88): Kilio cha mugonjwa

Ee Bwana, Mungu wa wokovu wangu, nimelia muchana na usiku mbele yako: Maombi yangu yaingie mbele yako; utege sikio lako kwa kilio changu, maana nafsi yangu inajaa taabu, na uzima wangu unakaribia Hadeze. Nimehesabiwa pamoja nao wanaoshuka shimoni; mimi ni kama mutu asiye na musaidia. Nimetupwa katikati ya wafu, kama waliouawa wanaolala kaburini, usiowakumbuka tena; nao wametengwa mbali na mukono wako. Umenilalisha katika shimo la chini sana, katika pahali pa giza, vilindini. Gazabu yako imenilemea sana, na umenitesa kwa mawimbi yako yote. Wao wanaonijua umewatenga mbali nami; umenifanya kuwa chukizo kwao; nimefungwa, wala siwezi kutoka. Jicho langu linaharibika kwa ajili ya mateso yangu; kila siku nilikuita, ee Bwana, nimenyosha mikono yangu kwako. Utaonyesha maajabu yako kwa wafu? Wao waliokufa watasimama na kukusifu? Wema wako utasimuliwa kaburini? Ao uaminifu wako katika uharibifu? Maajabu yako yatajulikana gizani, na haki yako katika inchi ya usahaulifu?

Lakini nimelia kwako, ee Bwana, na asubui maombi yangu yatakuwa mbele yako. Kwa nini unatupa nafsi yangu, Bwana? Kwa nini unanifichia uso wako? Nimeteswa na hali ya kufa tangu ujana wangu; ningali ninavumilia hofu yako ninafazaishwa. Hasira yako kali imepita juu yangu; maogopesho yako yamenikatilia mbali. Yamenizunguka kama maji muchana kutwa; yamenizunguka pamoja. Mupenzi na rafiki umetenga mbali nami, nao wanaonijua ni giza.

Na tena: Ee Bwana, Mungu wa wokovu wangu, nimelia muchana na usiku mbele yako: Maombi yangu yaingie mbele yako, utege sikio lako kwa kilio changu.

**ZABURI** IO2 (IO3): Bariki Bwana. Bariki Bwana, ee nafsi yangu; na vyote vilivyo ndani yangu, vibariki jina lake takatifu. Bariki Bwana, ee nafsi yangu, wala usisahau baraka zake zote; anayesamehe maovu yako yote; anayeponyesha magonjwa yako yote; anayekomboa uzima wako toka shimoni; anayekutia taji ya wema na rehema; anayeshibisha kinywa chako na vitu vizuri; hata ujana wako unafanywa mupya kama tai. Bwana anafanya mambo ya haki, na hukumu kwa wote wanaoteswa. Amejulisha Musa njia zake, wana wa Israeli matendo yake. Bwana anajaa huruma, ni mwenye neema, hakasiriki upesi, na anajaa rehema. Hatakemea siku zote; wala hatachunga hasira yake milele. Hakututendea sawasawa na zambi zetu, wala hakutulipa sawasawa na maovu yetu. Maana sawasawa mbingu zilivyo juu sana kupita inchi, kwa kadiri ile rehema yake ni kwao wanaomwogopa. Kama mashariki ilivyo mbali na mangaribi, ndivyo alivyoweka makosa yetu mbali nasi. Kama Baba anavyohurumia wana wake, ndivyo Bwana anawahurumia wanaomwogopa. Kwa maana anajua mwili wetu; anakumbuka ya kuwa sisi nimavumbi. Lakini mutu, siku zake ni kama majani; kama ua la shamba, divyo anavyokua. Maana upepo unapita juu yake, nalo haliko; na pahali pake hapatalijua tena. Lakini wema wa Bwana ni tangu milele hata milele juu yao wanaomwogopa, na haki yake kwa wana wa wana; kwao wanaoshika agano lake, na kwao wanaokumbuka maagizo yake ili kuyafanya. Bwana amesimamisha kiti chake cha ufalme mbinguni; na ufalme wake unatawala vitu vyote. Bariki Bwana, ninyi malaika zake. Ninyi wenye uwezo kwa nguvu, munaotenda neno lake, mukisikiliza sauti ya neno lake. Barikini Bwana, ninyi majeshi yake yote; ninyi watumishi wake, munaofanya mapenzi yake. Barikini Bwana, ninyi matendo yake yote, pahali popote pa utawala wake. Bariki Bwana, ee nafsi yangu.

Na tena: Pahali po pote pa utawala wake: bariki Bwana, ee nafsi yangu.

**ZABURI** I42(I43): Maombi kwa kusaidia na kuongozwa.

Sikia maombi yangu, ee Bwana, usikilize kusihi kwangu; katika uaminifu wako unijibu, katika haki yako. Usihukumu mutumishi wako; maana machoni mwako hakuna mutu aliye hai atahesabiwa haki. Maana adui amefuata nafsi yangu; amepiga uzima wangu chini hata udongo.

Amenikalisha katika pahali pa giza, kama wale waliokufa zamani. Kwa hivi roho yangu imezimia ndani yangu; Moyo wangu ndani yangu ni ukiwa. Ninakumbuka siku za kale; ninafikili

matendo yako yote; ninawaza kazi ya mikono yako. Ninakunyoshea mikono yangu; nafsi yangu inaona kiu kwa wewe, kama inchi inayochoka. Fanya mbio kwa kunijibu, ee Bwana; roho yangu inazimia; usinifichie uso wako; nisiwe kama wao wanaoshuka shimoni. Unifanye kusikia wema wako asubui; kwa maana ninakutumainia wewe; unijulishe njia nitakayoikwenda; kwa maana ninakunyanyulia nafsi yangu. Uniponyeshe, ee Bwana, na adui zangu, ninakukimbilia unifiche. Unifundishe kufanya mapenzi yako; kwa maana wewe ndiwe Mungu wangu; Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki. Unipatize uzima, ee Bwana, kwa ajili ya jina lako; kwa haki yako utoe nafsi yangu katika taabu. Na kwa wema wako ukatilie mbali adui zangu, na kuwaharibu wote wanaotesa nafsi yangu; kwa maana mimi ni mutumishi wako.

Na tena: Ee Bwana, katika uaminifu wako, unijibu, katika haki yako, usihukumu mutumishi wako. *(mara ya Pili)*. Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Alliluya, alliluya, alliluya utukufu kwako, ee Mungu *(mara tatu)* Matumaini yetu, utukufu kwako.

*Kisha Eksapsalmos* ***PADRI*** *atasema Irinika na Mwimbaji ataimba Alliluia.*
*(mara Ine)*

Sauti ya Mnane

**MSOMAJI**: Vituo: 1)Ee Bwana, tangu usiku roho yangu kwa sala inaongojea alfajiri Yako, maana amri zako ni nuru duniani.

**MWIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

**MSOMAJI**: Vituo: 2)Jifunzeni haki, ninyi wote wakaaji wa dunia.

**MWIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

**MSOMAJI**: Vituo: 3)Wivu utangukia watu wapotevu, sasa moto itawateketeza maadui zako.

**MWIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

**MSOMAJI**: Vituo: 4)Mwaajibu, ee Bwana, uwazibu vikali kwa mateso Wenye sifa wote wa dunia.

**MWIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

Wimbo. Sauti ya Mnane.

Tazama Bwana Arusi anakuja katikati ya usiku, heri mtumishi atakuta mwenye kuamka; msiyestahili ni yule atamkuta mwenye kulala. Ee roho, usilale kusudi usitolewe ku mauti na kuondolewa ku ufalme; lakini amkaulalamike: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe Mungu Wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie. *(mara tatu)*

*Kama tunaimba hii tropari (Wimbo )mara ya pili ku mwisho yake tunaimba hivi:*

Kwa maombezi ya Watakatifu wako wote. *Na ile mara ya tatu tunaimba hivi*: Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu utuhurumie.

**PADRI** ao **SHEMASI**: Tena na tena ku amani tumuombe Bwana.

**MWIMBAJI**. Bwana hurumia.

**PADRI**: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, ee Mungu kwa neema yako.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia.

**PADRI**:  Tumukumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi  kila mumoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.

**MWIMBAJI**:  Kwako, ee Bwana

**PADRI**:  Kwa kuwa nguvu ni yako, na ufalme, na uwezo, na utukufu ni wako, waBaba, na wa Mwana na Roho Mutakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele.

**MWIMBAJI**:  Amina.

*Somo la Zaburi **KATHISMA** ya Ine*

Wimbo ya **KATHISMA**   Sauti ya kwanza.

Tazama siku ya mateso tukufu inapambazuka duniani kama jua; tazama siku ya wokovu: Kristu anateswa kwa kutaka kwake. Yeye Mwenyi kushika ulimwengu mkononi mwake anakubali kupanua Mikono yake msalabani sababu ya kuokoa mwanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(Mara ingine hii)*

*Somo la Zaburi  **KATHISMA** ya tano*

Wimbo wa **KATHISMA**    Sauti ya kwanza.

Ee Mwamzi msiyeonekana, namna gani ulionekana mwilini? Namna gani unaweza kuuawa kwa mikono ya watu wasiyo na sheria, ukihukumu hukumu yetu kwa mateso yako. Na tena kwa sauti moja, ee Neno, tusifu, tuheshimu na tutukuze uwezo wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . (*Mara ingine hii).*

*Somo la Zaburi **KATHISMA** ya Sita.*

*Wimbo wa **KATHISMA**. Sauti ya mnane.*

Leo inapambazuka alfajiri ya mateso ya Bwana. Kujeni na mavazi ya arusi tuendeni kukutana naye. Muumba anajongea kwa kuitikia Msalaba, mateso na lufu. Pilato anamuhukumu, mtumwa anampiga kichwani, Bwana anaivumilia kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Tumulalamikie: Ee Kristu Mungu mpenda wanadamu, utuondolee zambi sisi wenyi kukutukuza na imani yako takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote  *(Mara ingine hii).*

**PADRI**:   Na tumsihi Bwana wetu atustahilishe, kusikiliza Evangelio Takatifu.

**MWIMBAJI**:  Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**PADRI**:  Hekima; inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.

**MWIMBAJI**:  Na kwa roho yako.

Somo la Evangelio Takatifu ilivyoandikwa na Mwevangelizaji Matayo. (21, 18-43), tusikilize.

**WAIMBAJI**:  Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

**PADRI**:

Basi asubui wakati alipokuwa akirudi mujini, alikuwa na njaa. Na akiona mutini kando ya njia, akaukwendea, hakuona kitu juu yake, ila majani tu, akauambia: Yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele. Mutini ukakauka mara moja. Na wakati wanafunzi walipoona, wakashangaa wakisema:  Namna gani mutini umekauka mara moja? Yesu akajibu, akawaambia: Kweli ninawaambia ninyi, kama mukiwa na imani pasipo kuona shaka, mutafanya, si neno hili la

mutini tu, lakini mutauambia mulima huu:  Uondoshwe na kutupwa katika bahari, na litafanyika. Na vitu vyote mutakavyoomba katika maombi kama mukiamini, mutapokea. Na wakati alipokuja katika hekalu, wakubwa wa makuhani na wazee wa watu walikuja kwake wakati alipokuwa akifundisha, wakasema:  Ni kwa amri gani unafanya maneno haya? Na ni nani aliyekupa amri hii? Yesu akajibu, akawaambia:  Nitawauliza ninyi ulizo moja vilevile, nanyi kama mukinijibu, nitawaambia ninyi vilevile kwa amri gani ninafanya maneno haya. Ubatizo wa Yoane ulitoka wapi? Toka mbingu ao toka watu? Wakabishana katikati yao wakisema:  Tukisema:  Toka mbingu; atatuambia sisi:  Kwa nini basi hamukumwamini? Lakini kama tukisema:  Toka watu; tunaogopamakutano; kwa maana wote wanaona Yoone kuwa nabii. Wakajibu Yesu wakisema:

Hatujui. Naye akawaambia:  Wala mimi siwaambii ninyi kwa amri gani ninafanya maneno haya. Lakini munafikili nini? Mutu mumoja alikuwa na wana wawili, akakwendea yule wa kwanza, akamwambia:  Mwana, kwenda utumike leo katika shamba la mizabibu. Akajibu na kusema:  Sitaki; lakini nyuma akatubu, akakwenda. Akakwendea wa pili, akamwambia hivi vilevile. Akajibu na kusema:  Ninakwenda, bwana; lakini hakwenda. Nani katikati yao wawili aliyefanya mapenzi ya baba yake? Wakasema:  Wa kwanza. Yesu akawaambia:  Kweli ninawaambia ninyi, Watoza kodi na makahaba wanaingia katika ufalme wa Mungu mbele yenu. Kwa sababu Yoane alikuja kwenu kwa njia ya haki, nanyi hamukumwamini; lakini watoza kodi na makahaba walimwamini; nanyi, wakati mulipoona, hamukutubu nyuma na kumwamini. Sikieni mufano mwingine:  Kulikuwa mutu mumoja mwenye myumba aliyepanda shamba la mizabibu, akazunguka na boma la miti, akachimba shimo la kukamua matunda ndani yake, akajenga munara na kupangisha walimaji, akakwenda safari katika inchi nyingine. Na wakati wa matunda ulipokuwa karibu, akatuma watumwa wake kwa wale walimaji apokee matunda yake. Walimaji wakatwaa watumwa wake, wakapiga mumoja, na kuua mwingine, na walitupia mwingine mawe. Akatuma tena watumwa wengine kupita wale wa kwanza, wakawatendea hivi vilevile. Lakini mwisho akawatumia mwana wake akisema:  Wataheshimu mwana wangu. Lakini wale walimaji, wakati walipoona yule mwana, wakasemezana katikati yao:  Huyu ni muriti; kujeni tumwue na tutwae uriti wake. Wakamukamata, wakamutupa inje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Basi, wakati bwana ya shamba la mizabibu atakapokuja, atafanyia wale walimaji nini? Wakamwambia:  Ataangamiza vibaya wale watu wabaya, na atapangisha walimaji wengine katika shamba lile la mizabibu, watakaomupa matunda yake kwa wakati wao. Yesu akawaambia:

Hamukusoma katika maandiko:  Jiwe walilokataa wajengaji, hili limekuwa kichwa cha pembe; neno hili limetoka kwa Bwana, ni ajabu kwa macho yetu?  Kwa sababu ya neno hili ninawaambia ninyi:  Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu na taifa lingine watapewa, wenye kuzaa matunda yake.

**WAIMBAJI**:  Utukufu kwako, ee Bwna, utukufu kwako.

*Kisha Zaburi 50(51) tunasoma.*

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako; sawasawa na wingi  wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe; ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu; na uzima maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako; na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu; ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao

ningeitoa, hufurahi kwa sadaka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa; halafu watatoa ngombe ndume juu ya mazababu yako.

## KANUNI

WIMBO 1 HIRMOS Sauti ya mbili
Bahari ilitikisika tena haikuwezekana. Lakini Mungu akaiamuru ikauke. Waana wa Israeli wakaivuka pakavu. Tumuimbie Bwana, kwani amejitukuza. Utukufu kwako, ee Mungu Wetu, utukufu kwako. *(mara ya pili)*

TROPARIA
Kwa mapendo yake isiyokadirika, Neno la Mungu Kristu anawaonyesha wafuasi wake hivi aliye: Mungu tena mutu, yeye alipochukua hali ya mtumwa, hakujivuna hivi alikuwa Mungu, yeye aliyevaa utukufu.

Utukufu kwa Baba. . .
Nimekuja kusaidia mimi mwenyewe huyu nilivaa hali yake, mimi Muumba wake. Nimekuja na umungu wangu wote kwa adamu mwenye kuanguka. Mimi Mungu mvumilivu, nimekuja kutoa uzima wangu kama ukombozi.

**KATAVASIA**: Bahari ilitikisika. . .

**SHEMASI** ao **PADRI**: Ektenia Kidogo: Tena na tena ku amani. . .

**KONDAKION.** Sauti ya Mnane
Yakobo alilia kupotea kwa mwana wake, na yeye mheshimiwa Yosefu alipopanda katika gari yake, akatukuzwa kama mfalme Mshindi wa furaha ya mwanamuke Mmisri akatukuzwa kwa huyu mwenyi kujua moyo wa mwanadamu tena mwenyi kuleta utukufu usiyoharibika.

**IKOS**
Tuchange machozi yetu na yale ya Yakobo, tugawanye maombolezo yake juu ya Mtakatifu Yosefu mwenye kukumbukiwa milele ambaye mwili wake ulikuwa katika utumwa, lakini roho yake ilikuwa huru tena aliyetawala usiyoharibika. Hapa tunasoma Sinaksario Ya Watakatifu ya Leo. Ku mwisho yake tunasome hivi:

*Hapa tumasoma Sinaksario ya watakatifu ya leo. Ku mwisho yake tunasoma hivi:*

Hii siku ya Mkazi moja Mkubwa tunakumbuka makumbusho ya mwenye heri Yosefu, mtoto wa Yakobo aliyeuzishwa na ndugu zake katika Misri. Tena tunakumbuka ile mutini kando ya njia Yesu Kristu alipita na kuifiga, nayo ikakauka maramoja (Matayo 21, 19).

WIMBO YA MNANE
HIRMOS
Moto kali iliyowaka ikatetemeka kwa vijana Watakatifu wenyi roho safi, wenyi mwili usiyo na doa. Moto isiyokufa ukazimika, hii wimbo ikasikilika kwa milele: Tukuzeni Bwana, enyi viumbe vyake vyote, na msifuni milele. *(mara ya pili)*

Tunamsifu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu Bwana.

Wote watawatambua ninyi kwamba ni Wafuasi wangu kama munashika amri zangu, ndivyo alivyowaambia Mwokozi marafiki zake wakati wa mateso yake. Nawapa ninyi amani pamoja na wote, muwe wanyenyekevu katika roho na mutainuliwa. Ninyi wenye kujua ya kwamba mimi ni Bwana, imbeni na kunitukuza milele.

Sasa na siku zote. . .

Kati yenu uwezo usiwe kama ule wa wapagani: amri yao si yangu, uzulumu wao umenyanganywa. Kama mmoja wenu anataka kuwa wa kwanza, sherti awe mtumishi wenu. Ninyi wenye kujua ya kwamba mimi ni Bwana imbeni na kunitukuza milele.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana.

**KATAVASIA**: Moto kali iliyowaka. . .

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo na kumutukuza.

***PADRI** ao **SHEMASI** ataweka ubani katika chetezo na ataifukiza Kanisa.*

WIMBO YA TISA

HIRMOS

Ee Kristu, ulitukuza Mama yako aliyekuzaa, ni katika yeye, ee Muumba wetu, ulivaa mwili wenyi kufanana na wetu ambao ulizima nayo zambi zetu. Vizazi vyote vinamuita mwenyi heri na vinakutukuza. *(mara ya pili)*

Utukufu kwa Baba. . .

Mukatae takataka zote za tamaa, pokeeni maarifa ya kweli ya ufalme waMungu; ndivyo ulivyowaambia wafuasi wako, Wewe uliye hekima kamili: Kwa hiimaarifa mutatukuzwa, mutangaa kuliko jua.

Sasa na siku. . .

Ee Bwana, uliwaambia Wafuasi wako: Muwe mfano wangu, msitamainie ukubwa, jinyenyekezeni; kunyweni kikombe ninachokunywa ili mtukuzwe pamoja nami
katika ufalme wa Baba.

**KATAVASIA**: Ee Kristu ulitukuza. . .

**SHEMASI** ao **PADRI** atasema Ektenia kidogo.

**EKSAPOSTILARION**. Sauti ya tatu.

Ninaona Chumba chako cha arusi chenye kupambwa vizuri, ee Mwokozi wangu, na sina na mavazi ya kuingia nayo. Uangazie nguo ya nafsi yangu, ee Muletaji-nuru, na uniokoe. *(mara tatu)*

## MASIFU

Kila mwenye pumzi amsifu Bwana. Musifu Bwana katika mbinguni, musifu Bwana katika pahali palipo juu. Sifa inafaa kwako, ee Mungu.

Mumusifu ninyi Malaika zake zote. Mumusifu nguvu yake yote. Sifa inafaa kwako, ee Mungu.

*Kama tunataka tunasoma ma Shairi ya Zaburi 148 na 149. Kama hatutake tunaanza hivi:*

Musifuni kwa matendo yake makuu, msifuni kwa kadiri ya wingi wa usiku wake.

*Tunaimba sasa hii wimbo ya chini.*
Sauti ya Kwanza
Bwana alipoenda katika mateso yake ya kutaka, akawaambia Mitume wake njiani: Tazameni tunapanda ku Yerusalema, na huko Mwana wa mutu atatolewa kama ilivyoandikwa juu yake. Tuendeni sisi pia, tumfwate na roho yenyi kutakaswa. Tusulubiwe pamoja naye kwa kutoka kwake tena tufe ku furaha za hii uzima kusudi ya kuishi mara ingine pamoja naye na kumusikiliza akisema: Siende katika Yerusalema ya dunia sababu ya kuteswa, naenda kwa Baba yangu aliye Baba yenu, kwa Mungu wangu aliye Mungu wenu, tena nitawapeleka ninyi mpaka ku Yerusalema ya mbinguni, mpaka ku ufalme wa mbingu.

Kituo: Musifuni kwa mvumo wa baragumu, musifuni kwa kinanda na kinubi. *(Mara ingine hii)*

Kituo: Musifuni kwa ngoma na kucheza, musifuni kwa nzenze na filimbi.
Sauti ya tano
Enyi waaminifu, tazameni imekuja mateso ya wokovu ya Kristu Mungu wetu, tutukuzeni uvumilivu wake wa kweli ili kwa huruma yake atufufue pamoja naye, sisi tuliyouawa na zambi, kwani Yeye ni Mwema tena Mpenda wanadamu.

Musifuni kwa matoazi yavumayo tamu; musifuni kwa matoazi yavumayo sana. Kwa mwenye pumuzi na amsifu Bwana. *(mara ingine hii wimbo ya yulu).*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Sauti ya Tano
Ee Bwana, wakati ulipokuwa njiani ukienda ku mateso yako sababu ya kuwasabitisha Wafuasi wako, ukawatwaa pembeni na ukawambia: Namna gani munaweza kusahau maneno yangu? Nimekuisha kuwaambia ninyi ya kwamba kama yanavyosema Maandiko, Nabii wote atakufa paka ku Yerusalema. Tazameni imekuja wakati niliyowaambia: Najitoa mikononi mwao, watanizarau, watanipigilia Msalabani, wataniweka kaburini, nitakuwa kwao mufu mchafu; lakini muwe imara kwani nitafufuka siku ya tatu kwa ajili ya furaha ya waaminifu, sababu ya uzima wa milele.

***PADRI*** *ao mukubwa ya Kanisa anasoma:*

## DOKSOLOGIA KIDOGO

Kwa kuwa utukufu ni Wako, ee Bwana Mungu wetu, na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina Utukufu kwa Mungu juu pia, nchini amani urazi kwa wanadamu. Tukusifu, tukuhimidi, tukusujudu, tukutukuza, tukushukuru, maana utukufu wako ni mkuu. Ee Bwana mfalme, Mungu wa juu mbinguni, Baba mwenyezi, ee Bwana Mwana wa pekee Yesu Kristu na wewe Roho Mtakatifu. Ee Bwana, Mungu we, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, unazibeba zambi za dunia utuhurumie, unazibeba zambi za dunia. Upokee ombi letu, uliyeketi kuume kwa Baba na utuhurumie. Kwa kuwa Mtakatifu wa pekee, Bwana wa pekee, Yesu Kristu katika utukufu wa Mungu Baba. Amina. Kila Mangaribi nitakuhimidi, nitalisifu jina lako la milele, hata milele na milele. Ee Bwana wewe ni kimbilio letu, kizazi baada ya kizazi. Mimi nilisema: Ee Bwana, unihurumie, uiponye roho yangu, maana nimekutendea zambi. Ee Bwana, nimekimbilia kwako, unifundishe kutenda mapenzi yako, maana ndiwe Mungu wangu. Maana kwako wewe iko chemchem ya uzima; katika mwangaza

wako tutaona mwangaza. Onyesha huruma yako kwao wakujue. Ee Bwana, utujalie usiku huu, kutulinda na zambi. Umehimidiwa, ee Bwana Mungu wa Baba zetu jina lako limesifiwa, na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, tumevyokutumaini wewe. Ee Bwana, umehimidiwa, unifundishe zilizo haki zako. Ee Rabi, umehimidiwa, unifahamishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana huruma yako ni ya milele; usiache kutuangalia sisi viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki, kukuimbia ni kwako, utukufu ni wako, wa Baba na wa Mwana na wa Roho Mtaklatifu, sasa na siku zote,
hata milele na milele. Amina.

EKTENIA MUKUBWA

**SHEMASI** ao **PADRI**: Tumalize ombi letu la asubui kwa Bwana.
**WAIMBAJI**: Bwana hurumia
Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.
**WAIMBAJI**: Bwana hurumia.
Siku hii kubwa kamili, takatifu, tulivu, bila zambi tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji watasema kwa kila maombi ya Padri:* Utupe, ee Bwana.

Malaika wa amani, mwongozi mutumainifu, mulinzi wa roho na mwili yetu, tuombe. . .

Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe kwa Bwana.

Vilivyo vyema na vifaayo kwa roho zetu kwa amani na toba, tuombe. kuimarisha maisha yetu inabaki katika amani na toba, tuombe kwa bwana.

Tuombe ili mwisho wetu uwe kikristu, kwa amani, bila maumivu, bila aibu, tena kutuona teto njema ya kiti cha hukumu cha Kristu.

Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote; ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristo Mungu.

**PADRI**: Kwa kuwa U Mungu wa huruma, wa rehema na kuwapenda wanadamu, kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
**PADRI**: Amani kwa wote.
**WAIMBAJI**: Na kwa roho yako.
**PADRI**: Tuinamie vichwa vyetu mbele kwa Bwana.
**WAIMBAJI**: Kwako, ee Bwana.

***PADRI** kwa siri anasoma hii sala:*
Ee Bwana, uliye ukikaa, juuni, unavisimamisha vilivyo chini, tena kwa jicho lako lilio kuviona vyote unauangalia ulimwengu wote, tumekuinamia shingo la roho na la mwili, tunakuomba ewe Mtakatifu wa Watakatifu. Uunyoshe mkono wako juu ya sisi kuuona kutoka katika makao yako matakatifu, ukatubariki sisi wote, ukatusamehe kila kosa tul**IKOS**a kwa kutaka wala si kwa kutaka, utupe sisi vyema vyako vilivyo hapa duniani na huku ulimwenguni wa kuja.

***PADRI*** *anapaza sauti na anasema:*

Kwa kuwa kutuhurumia na kutuokoa ni kwako, ee Mungu wetu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## APOSTIKHA

Sauti ya Tano.

Ee Bwana, mama ya watoto wa Zebedeo hakusikia fumbo ya kweli ya umwilisho wako, na akakuomba uwape watoto wake viti vya heshima vya ufalme wa hii dunia. Lakini wewe, pahali pa viti vya heshima, ni kikombe cha mauti unawaahidi marafiki zako; hii kikombe unasema kuikunywa wa kwanza; ni utakaso wa zambi zetu, na tena tunalalamika: Ee Wokovu wa roho zetu, utukufu kwako.

Kituo 1: Ee Bwana, asubui tulijazwa na rehema yako tena tulifurahi. Tumefurahiwa siku zote za maisha yetu. Tunaweza kufurahiwa kwa ajili ya siku tulizozarauliwa, kwa ajili ya miaka tuliyoteswa. Tazama watumishi na viumbe vyako, ongoza wana wao.

Sauti ya Tano

Ee Bwana, wakati ulipowafundisha Wafuasi wako hekima kamili, ukawaambia: Musiwe kama wapagani wenye kuwatawala wadogo; isiwe hivi kwenu ninyi Wafuasi wangu, kwani mimi nilipenda kuwa maskini. Wa kwanza kati yenu atakuwa mtumishi wa wote; huyu mwenyi kuamuru kama yule mwenyi kutii; muheshimiwa kabisa kama wa mwisho kabisa. Kwa sababu nimekuja mimi mwenyewe kusaidia Adamu kwa umaskini wake, na kutoa uzima wangu, kama ukombozi wa wale wenyi kunilalamikia: utukufu kwako.

Kituo 2: Nuru ya Bwana Mungu wetu iwe nasi, uwe mwema ku kazi ya mikono yetu, uwe mwema ku kazi ya mikono yetu.

Sauti ya Mnane.

Enyi ndugu, tuogopeni, tutetemeke ili tusiazibiwe kama mti usiyozaa matunda; tutoe matumda ya toba yetu kwa Kristu mwenye kutupatia rehema yake kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. .

Sauti ya Mnane.

Nyoka alipata Eva katika mwanamke Mmisri, akajaribu kwa hila kumudanganya Yosefu; huyu akaiacha nguo yake, akakimbia zambi kama Adamu mbele ya kuanguka kwake, alipokua uchi, hakujua zambi. Kwa maombezi yake, ee Kristu, utuhurumie.

**PADRI**: Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako, ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Utatu Mutakatifu. . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . Baba yetu. . .

**PADRI**: Kwa kuwa ufalme, na uwezo. . .

**KONTAKION**

Yakobo alilia kupotea kwa mwana wake, na yeye mheshimiwa Yosefu alipopanda katika gari yake, akatukuzwa kama mfalme-Mshindi wa furaha ya mwanamuke Mmisri. Akatukuzwa kwa Huyu mwenyi kujua moyo wa mwanadamu, tena mwenyi kuleta utukufu usiyoharibika.

Bwana hurumia *(Kumi na mbili).*
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wa thamani kuwashinda wakeruvi. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Padri:
**PADRI**: Aliye ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ee Mfalme wa mbinguni, sabitisha imani, tuliza mataifa, leta amani duniani, linda hii Kanisa Takatifu na hii mji, weka katika makao ya wenye haki baba zetu na ndugu zetu waliyolala tena pokea toba yetu na kukiri kwetu, kwani ndiwe mwema tena mpenda wanadamu.

*Kisha tunafanya Metania(kupika magoti) tatu na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria.*

Ee Bwana na Rabi wa uzima wangu, ondoa mbali nami roho ya uvivu, ya utawanyiko, ya kutawala wengine na maneno ya bure.

Unipe roho ya usafi, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo, mimi mtumishi wako.

Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi zangu tena nisimuhukumu ndugu yangu, kwani umehimidiwa milele na milele. Amina.

*Kisha tunafanya Metania kidogo Kumi na mbili na kisha moya Metania mukubwa na kusema:* Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi. . .

***PADRI*** *anafanya Kuaga ( Apolisis).*
Bwana alipoteswa kwa kutaka kwake kwa ajili ya wokovu wetu, Bwana Kristo Mungu wetu kweli, kwa maombi ya Mama yako Mtakatifu asiye na doa wala na lawama kamili, kwa uwezo wa Musalaba mheshimiwa na mhuishaji, kwa ulinzi ya Majeshi maheshimiwa ya mbinguni juu yasisi na mwili, kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtangulizi, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, Watukufu, wasifiwa kamili, ya Mashahidi Watakatifu, Watukufu, washindaji wazuri, ya wa Padri Watawa na wabebaji-Mungu, ya Mutakatifu Msimamizi wa Kanisa, ya Yoakimu na Anna Wababu Mungu, Watakatifu na wenye haki, ya Mutakatifu *(ya hii siku)*makumbusho yake leo, hata ya Watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe, yu Mungu mwema, mrahimu, na mpenda wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

**MSOMAJI**: Amina.

*Kesho Mukazi Moja asubui tutasoma ma Saa ya Kwanza, Saa ya Tatu, ya Sita naya Tisa. Utapata ma Saa yote mu Kitabu cha Saa Mkubwa (OROLOGION MEGA).*
*Kisha ma Zaburi yao tunasoma:*
Utukufu kwa Baba. . . na Apolitikion:
Tazama Bwana Arusi anakuja katikati ya usiku, heri mtumishi atakuta mwenye kuamka;msiyestahili ni yule atamkuta mwenye kulala. Ee roho yangu, usilale kusudi usitolewe ku mauti na kuondolewa ku ufalme; lakini amka ulalamike: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe Mungu wetu, kwa maombezi ya Bikira Mama yako, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION

*Theotokion iko ndani ya Saa ya Kwanza, inaanza hivi:* Namuna gani tutakuita ewe Mujaliwa neema?. . .

*Kisha TRISAGION ya Saa ya kwanza tunasoma hii **KONTAKION**:*

Yakobo alilia kupotea kwa mwana wake, na yeye mheshimiwa Yosefu alipopanda katika gari

yake, akatukuzwa kama mfalme-Mshindi wa furaha ya mwanamuke Mmisri. Akatukuzwa kwa Huyu mwenyi kujua moyo wa mwanadamu, tena mwenyi kuleta utukufu usiyoharibika.

*Siku ya kwanza Mkubwa, siku ya mbili Mkubwa na siku ya Tatu Mkubwa ku Saa ya Tatu, ya Sita na ya Tisa tunasoma Evangelia yote tatu ya Mtakatifu Matayo, ya Mtakatifu Marko na ya Mtakatifu Luka na ile ya Mtakatifu Yoanne mpaka ku sehemu ya 13 mstari wa 30, kwa namna ifwatayo: Mtakatifu Matayo siku ya kwanza ku Saa ya Tatu na ya Sita;Mtakatifu Marko siku ya kwanza ku Saa ya Tisa na siku ya pili ku Saa ya Tatu; Mtakatifu Luka siku ya mbili ku Saa ya Sita na ya Tisa, na siku ya Tatu ku Saa ya Tatu; Mtakatifu Yoane siku ya Tatu ku Saa ya Sita na ya Tisa.*

*Saa ya Tatu na ya Sita:*

*Ku Saa ya Tatu Zaburi za Saa **KATHISMA** ya Saba. Ku Saa ya Sita **KATHISMA** ya Mnane na ku Saa ya Tisa hakuna **KATHISMA**.*

*Ku Saa ya Sita kisha Theotokion ya Saa (Kama vile hatuna nguvu juu ya zambi zetu nyingi. )Tunasoma Tropari ya Unabii Sauti ya Sita:*

Na sikitiko tunanguka ku miguu yako tena tunakutolea maombi yetu, ee Bwana wa ulimwengu, kwani ndiwe Mungu wa wenye kutubu.

**PROKIMENON** Sauti ya Ine:

Wakati Bwana aliwarudisha wafungwa katika Sayuni, tulikuwa kama ndoto.

Kituo: Hapa kinywa chetu kilijazwa na furaha tena ulimi wetu ukajazwa na shangwe.

Somo la Unabii wa Ezekieli 1, 1-21

Na ilikuwa katika mwaka wa makumi tatu, kwa mwezi wa ine, kwa siku ya tano ya mwezi, wakati nilipokuwa katikati ya wafungwa kwa muto Kebari, mbingu zikafunguliwa, nikaona maono ya Mungu. Kwa siku ya tano ya mwezi uliokuwa mwaka wa tano wa kuhamishwa kwa mufalme Yoyakinu, neno la Bwana likakuja kwa kusudi kwa Ezekieli, kuhani, mwana wa Buzi, katika inchi ya Wakaldea, kwa muto Kebari; na mukono wa Bwana ulikuwa juu yake pale. Nikaangalia, natazama, upepo wa tufani ukatoka kwa kaskazini, wingu kubwa, na moto ukipigapiga, na kungaa pande zake zote, na toka katikati yake kama rangi ya kaharabu, toka kati ya moto. Na toka kati yake ulikuja mufano wa viumbe hai vine. Na kuonekana kwao kulikuwa hivi; walikuwa na sura ya mutu. Na kila mumoja alikuwa na nyuso ine, na kila mumoja wao alikuwa na mabawa mane. Na miguu yao ilikuwa miguu sawa; na wayo wa miguu yao ulikuwa kama wayo wa mungu wa ndama; wakangaa kama rangi ya shaba iliyisukuliwa sana. Na walikuwa na mikono ya mutu chini ya mabaya yao kwa pande zao ine; nao wane walikuwa na nyuso zao na mabawa yao hivi; mabawa yao yameungana; hawakugeuka wakikwenda; wakaendelea kila mumoja kuelekea mbele. Kwa maneno ya mufano wa nyuso zao, walikuwa na uso wa mutu; nao wane walikuwa na uso wa simba kwa mukono wa kuume; nao wane walikuwa na uso wa ngombe ndume kwa mukono wa kushoto; wao wane walikuwa na uso wa tai vilevile. Na nyuso zao na mabawa yao yalikuwa mbalimbali kwa upande wa juu; mabawa mawili ya kila

mumoja yaliungana, na mawili yalifunika miili yao. Wakaendelea kila mumoja kuelekea mbele; walikwenda pahali roho ilipotaka kwenda, hawakugeuka wakati walipokwenda. Kwa maneno ya kuonekana kwa viumbe hai, kuonekana kwao kulikuwa kama makaa ya moto yanayowaka, kama kuonekana kwa mienge, ukakwenda huku na huku katikati ya viumbe hai; moto ukangaa, umeme ukatoka katika moto. Viumbe hai wakapiga mbio, wakarudi kama kuonekana, kwa kumulika kwa umeme. Basi wakati nilipotazama vile viumbe hai, tazama, gurudumu moja juu ya inchi kando ya viumbe hai kwa nyuso zao ine moja moja. Kuonekana kwa magurudumu na kazi yao kulikuwa kama rangi ya zabarajadi; nayo mane yalikuwa na mufano mumoja, na kuonekana kwao na kiazi yao ilikuwa kama gurudumu ndani ya gurudumu. Wakati yalipokwenda, yalikwenda kwa pande zao ine, hayakugeuka wakati yalipokwenda. Nazo pete zao zilikuwa ndefu juu na za kuogopesha; nayo mane yalikuwa na pete zao zikijaa na macho pande zote. Na wakati viumbe hai walipokwenda, magurudumu yakakwenda kando yao, na wakati viumbe hai waliponyanyuliwa toka inchi, magurudumu yalinyanyuliwa. Kila pahali roho ilipotaka kwenda, wakakwenda; pahali roho ilipotaka kwenda, na magurudumu yalinyanyuliwa kando yao; kwa maana roho ya kiumbe hai ilikuwa ndani ya magurudumu. Wakati wale walipokwenda, haya yakakwenda; na wakati wale waliposimama, haya yakasimama, na wakati wale waliponyanyuliwa toka inchi, magurudumu yakanyanyuliwa kando yao; kwa maana roho ya kiumbe hai ilikuwa ndani ya magurudumu.

**PROKIMENON** Sauti ya Sita.
Zaburi 126(127) Kama Bwana hajenge nyumba, wajengaji wanasumbuka bure.
Kituo: Kama Bwana halinde mji, zamu anakesha bure.

*Tunasoma hii wimbo:*
Huruma yako itufikie upesi, kwani tumetaabika sana. Utusaidie, ee Mungu Mwokozi wetu, kwa ajili ya utukufu wa Jina Lako. Utuokoe, utusamehe zambi zetu kwa ajili ya Jina Lako.
MSOMAJI: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .
**KONTAKION**: Yakobo alilia kupotea. . . *(Angalia kwa Saa ya kwanza)* Bwana hurumia *(mara kumi na Ine),*
Wakati wote na saa yote. . . *(Angalia mu Kitabu: MEGA OROLOGION*)
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Uliye watanani. . . Kwa jina la Bwana, bariki, eePadri:
**PADRI:** Mungu atufazili, na kutubariki, atuangazie uso wake, na kutuhurumia.

*Kisha tunafanya Metania wakubwa ya Mtakatifu Efremi wa Siria, sawa vile ku Saa ya Kwanza.*
Kisha TRISAGION.
**PADRI**: Kwa kuwa ufalme. . . Musomaji: Bwana hurumia *(mara tatu)* na Padri Sala ya Saa Sita: Ee Mungu na Bwana wa majeshi. . .
**PADRI**: Kuaga

*Kisha tunaendelea ya kusoma Saa ya Tisa*

# ESPERINOS NA LITURGIA YA WENYI KUTAKASWA

**SHEMASI**: Ee Rabi, himidi.
**PADRI**: Abarikiwa Ufalme wa Baba, na wa Mwana na wa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MWIMBAJI**: Amina. Njooni tumwinamie. . . **ZABURI** 103(104).

Ektenia Mkumbwa
Ku amani tumwombe Bwanna.

*(Sawa inavyoandikwa mu Kitabu ya Liturgia)*

**KATHISMA** Kumi na Mnane.
*Kisha Utukufu kwa Baba ya kwanza ya **KATHISMA** Padri atafanya Ektenia Kidogo:*

**PADRI:** Tena na tena ku amani tumwombe Bwana. .
*Padri kwa siri anasoma sala ya Antifono ya kwanza*

***MSOMAJI** ataendelesha kusoma Sehemu ya Pili ya **KATHISMA**. Kisha Utukufu kwa Baba. . . ya Pili Padri atasema Ektenia Kidogo na Msomaji ataendelesha kusoma Sehemu ya Tatu ya **KATHISMA**.*

*Kisha mwisho ya **KATHISMA** Padri atasema mara ingine Ektenia kidogo na Waimbaji wataimba: Bwana nimekuita, unisikilize. . .*

*Wataanza kuimba mashairi:*

Kama wewe Bwana, ukihesabu maovu, ee Bwana, nani atasimama? Lakini usamehe pamoja nawe, ili uogopwe.

Bwana alipoenda katika Mateso yake ya kutaka. . .

*(Angalia MASIFU ya Asubui).*

Enyi waaminifu. . .
Ee Bwana, wakati ulipokuwa njiani. . .

*Kisha ataendelesha kuimba Wimbo ya APOSTIKHA:*

Ee Bwana, mama wa Watoto wa Zebedeo. . .
Ee Bwana, wakati ulipowafundisha Wafuasi. . .
Enyi ndugu, tuogopeni. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Nyoka alipata Eva katika Mwanamuke Mmsri. . .

*(Angalia APOSTIKHA ya Asubui).*
*Padri anafanya kuingia kidogo pamoja na Evangelio.*

**PADRI**: Hekima. Simameni.
**MWIMBAJI**: Mwangaza Upole (Ilaron)
**SHEMASI**: Mangaribi **PROKIMENON**.

Somo ya Unabii.
**PROKIMENON**, Sauti ya Sita. **ZABURI** 133.
Bwana akubariki toka Sayuni yeye aliyeumba mbingu na dunia.
Kituo: Heri wenyi kumuogopa Bwana, wenyi kutembea katika njia zake.

Somo ya Kitabu cha Kutoka 1, 1-20

Na haya ni majina ya wana wa Israeli walioingia Misri; kila mutu na nyumba yake wakakuja pamoja na Yakobo. Rubeni, Simeoni, Lawi, na Yuda, Isakari, Zebuluni na Benyamina; Dani na Nafutali, Gadi na Aseri. Na nafsi zote zilizotoka viunoni mwa Yakobo zilikuwa nafsi makumi saba. Na Yosefu alikuwa katika Misri mbele. Yosefu akakufa, na ndugu zake zote, na kizazi

kile chote. Wana wa Israeli wakazaa, wakazidi sana, na kuongezeka, wakakuwa hodari sana sana; inchi ikajaa nao. Akakuwa mufalme mupya juu ya Misri asiyejua Yosefu. Akawaambia watu wake: Tazameni, watu wa wana wa Israeli wamekuwa wengi, nao ni hodari kuliko sisi; basi tuwatendee kwa akili; wasiongezeke na isiwe wakati vita itakapotokea waungane na adui

zetu wapigane nasi na kupanda toka inchi. Kwa hivi wakaweka wasimamizi wa utumwa juu yao kuwatesa kwa mizigo. Wakajengea Farao miji ya kuwekea akiba, Pitomu na Ramisesi. Lakini hata kadiri walivyowatesa ndivyo wakazidi kuwa weingi na kuenea. Wakachukizwa kwa sababu ya wana wa Israeli. Wamisri wakatumikisha wana wa Israeli kwa nguvu; wakawatia maisha

yao uchungu kwa utumwa mukali, na chokaa na matofali, kwa utumwa wote wa mashamba, kila utumwa waliowatumikisha kwa nguvu. Mufalme wa Misri akasema na wazalisha wa Waebrania, jina la mumoja lilikuwa Sifura, na jina la mwingine Pua; akasema: Wakati munapozalisha wanawake wa Waebrania, mukiwaona kwa pahali pa kuzaa; mutoto akiwa mwanamume, halafu mutamwua; lakini akiwa mwanamuke, halafu ataishi. Lakini wazalisha wakaogopa Mungu,

wala hawakufanya kama mufalme wa Misri alivyowaagiza, lakini wakaacha watoto wanaume wazima. Mufalme wa Misri akaita wazalisha, akawaambia: Kwa nini mulifanya neno hili na kuacha watoto wanaume hai? Wazalisha wakamwambia Farao: Kwa maana wanawake wa Waebrania si kama wanawake wa Wamisri; kwa sababu wao ni wenye uzima mwingi, nao wanazaa wakati muzalisha hajafika bado karibu nao. Mungu akatendea wazalisha mema; watu

wakaongezeka, wakakuwa hodari sana.

**PROKIMENON** Sauti ya Mnane.
**ZABURI** 128. Tunawabariki ninyi kwa jina la Bwana aliyeumba mbingu na dunia.
Kituo: Wamenizunguka tangu ujana wangu.

Musomaji anapaza sauti: Hamuru.
*(Baraka ya Padri).*

**PADRI:** Hekima. Simameni. Nuru ya Kristu inangaza mwanadamu wote.

Musomaji: Somo la Kitabu cha Yobu 1, 1-12.

Kulikuwa na mutu katika inchi ya Uzi, jina lake Yobu; mutu yule alikuwa mukamilifu na mwenye haki, aliyeogopa Mungu, na kuepukana na uovu. Walizaliwa kwake wane saba na binti watatu. Mali yake vilevile ilikuwa kondoo elfu saba, na ngami elfu tatu, na jozi za ngombe ndume mia tano, na punda wake mia tano, na watu wa nyumba, wengi sana: Hivi mutu huyu alikuwa mukubwa kuliko wana wote wa mashariki. Nao wana wake wakakwenda, wakafanya

karamu nyumbani mwa kila mumoja wao kwa siku yake; wakatuma na kuita ndugu zao wasichana watatu ili wapate kula na kunywa pamoja nao. Na ilikuwa wakati siku za karamu zilipokuwa karibu kwisha, Yobu akatuma na kuwatakasa, akaamka asubui mapema, akatoa sadaka za kuteketezwa kama hesabu yao yote ilivyokuwa: Maana Yobu akasema: Hakose wana wangu wamekosa na kutukana Mungu mioyoni mwao. Yobu akafanya hivi siku zote. Basi ilikuwa siku moja wakati wana wa Mungu walipokuja kujiweka mbele ya Bwana, naye Shetani alikuja katikati yao vilevile. Bwana akamwambia Shetani: Unatoka wapi? Shetani akajibu Bwana, akesema: Ninatoka katika kuzungukazunguka duniani na kutembea huku na huku ndani yake. Bwana akamwambia Shetani: Umeangalia mutumishi wangu Yobu? Maana hakuna mumoja kama yeye duniani, mutu mukamilifu na wa haki, mwenye kuogopa Mungu na kuepukana na uovu. Shetani akajibu Bwana, akasema: Yobu anaogopa Mungu bule? Wewe

hukumuzunguka yeye na nyumba yake, na vyote alivyo navyo, kwa boma pande zote? Umebariki kazi ya mikono yake, na mali yake imeongezeka inchini. Lakini nyosha sasa mukono wako, na gusa vyote alivyo navyo, naye atakufuru mbele ya uso wako. Bwana akamwambia Shetani: Tazama, vyote alivyo navyo ni mukononi mwako; lakini usinyoshe mukono wako juu yake mwenyewe. Basi Shetani akatoka mbele ya uso wa Bwana.

*Kisha somo ya Yobu, Padri anabariki msomaji hivi:*
Amani kwako.

**SHEMASI**: Hekima.
***PADRI*** *anasimama mbele ya Meza Takatifu na anafukiza na chetezo na anaimba hii wimbo:*

Maombi yangu ya elekezwe kama uvumba mbele yako. Kunyanyua kwa mikono yangu, kama zabihu ya Mangaribi.

***PADRI*** *atasoma Shairi:*
Bwana nimekuita, unisikilize. Unisikilize, ee Bwana. Bwana nimekuita unisikilize; usikie sauti ya kusihi kwangu. Wakati ninapokuita, unisikilize, ee Bwana.

**MWIMBAJI**: Maombi yangu ya elekezwe. . .

**PADRI**: Uniweke mulinzi, ee Bwana, mbele ya kinywa changu uchunge mulango wa midomo yangu.

**MWIMBAJI**: Maombi yangu ya elekezwe. . .

**PADRI**: Usisukume moyo wangu kwa kitu kibaya, nifanye matendo ya uovu.

**MWIMBAJI**: Maombi yangu ya elekezwe. . .

**PADRI**: Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
*(Sasa anasimama mbele ya Meza ya Proskomidi).*

**MWIMBAJI**. Maombi yangu ya elekezwe. . .

***PADRI*** *anaimba peke yake:* Maombi yangu ya elekezwe" *mupaka:* "kwa mikono yangu"

***MWIMBAJI*** *ataendelesha:* Kama zabihu ya Mangaribi.

***PADRI*** *anafukiza na chetezo waaminifu wote na Kanisa na kisha anasema:*

Hekima. Simameni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.
**MWIMBAJI**: Na kwa roho yako.

Somo la Evangelio Takatifu ilioandikwa na Mwevangelisti Matayo, (24, 3-35)tusikilize.
**MWIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Na wakati walipokuwa ameketi juu ya mulima wa Mizeituni, wanafunzi wakamukwendea peke yao wakisema: Utuambie, maneno haya yote yatakuwa wakati gani? na nini alama ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia Yesu akajibu, akawaambia: Angalieni musidanganyiwe na mutu. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema: Mimi ndiye Kristu, na watadanganya

watu wengi. Na mutasikia habari za vita na matetesi ya vita, angalieni musiogope kwani sharti maneno haya yatimie, lakini mwisho wenyewe haujakuja bado. Maana taifa litapigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme, yatakuwa njaa na matetemeko ya inchi kwa pahali mbalimbali. Lakini

maneno haya yote ni mwanzo wa uchungu. Halafu watawatoa ninyi kuteswa na kuwaua ninyi, na mutachukiwa na mataifa yote kwa agili ya jina langu. Halafu watu wengi watakwaa, na watatoana na kuchukiana. Na manabii wengi ya uwongo watasimama na kudanganya watu wengi. Na kwa sababu uovu utaongezeka, mapendo ya watu wengi yatapoa. Lakini mwenye kuvumilia hata mwisho ataokolewa. Na Habari Njema hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, na halafu mwisho utakuja. Basi wakati munapoona chukizo la uharibifu lililosemwa na Danieli nabii, likisimama kwa pahali patakatifu (yeye anayesoma afahamu), halafu wale walio katika Yudea wakimbie kwa milima, naye aliye shambani asirudi kuchukua nguo yake. Lakini, ole wao wenye mimba, na wale wanaonyonyesha siku zile! Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku yasabato, kwa sababu yatakuwa mateso makubwa, kama haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala hayatakuwa kamwe. Na kama siku zile zisingalifupizwa, kama asingeokolewa mutu ye yote, lakini siku zile zitafupizwa kwa ajili ya wachaguliwa. Na wakati mutu atakapowaambia ninyi: Tazama, Kristo ni hapa, ao kule, musiamini. Kwa sababu makristo ya owongo watsimama, na manabii ya owongo, nao wataonyesha alama kubwa na maajabu wapate kudanganya kama ikiwezekana, hata wachaguliwa. Tazama, nimekwisha kuwaonya ninyi mbele. Basi kama wakiwaambia ninyi: Tazama yeye ni jangwani, musitoke. Tazama, yeye ni katika nyumba vya ndani nyumbani, musisadiki. Kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaonekana hata mangaribi, hivi kuja kwa Mwana wa watu kutakavyokuwa vile. Kwa maana

pahali maiti inapolala, pahali tai watakapokusanyika. Lakini mara moja nyuma ya mateso ya siku zile, jua litatiwa giza, wala mwezi hautatoa nuru yake, na nyota zitaanguka toka mbinguni, na nguvu za mbingu zitatikisika, halafu alama ya Mwana wa watu itaonekana mbinguni, na mataifa yote ya dunia wataomboleza, nao wataona Mwana wa watu akikuja katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mukubwa. Naye atatuma malaika zake na sauti kubwa ya baragumu, nao watakusanya wachaguliwa wake toka pepo ine, toka mwisho huu wa mbingu mupaka mwisho ule. Basi mujifundishe mufano huu kwa mutini: Wakati tawi lake linapochipuka na kutoa majani yake, munajua wakati wa jua kali ni karibu, nanyi vilevile wakati munapoona maneno haya yote, mujue ya kuwa yeye ni karibu, hata kwa milango. Kweli ninawaambia ninyi, KIzazi hiki hakitapita hata maneno haya yote yatakapotimia. Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kabisa.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Kisha Evangelio Shemasi atasoma Sala ya Wakathekomeno na kisha tunaendelea Liturgia ya vyenyi kutakaswa.*

***WAIMBAJI*** *wataimba Keruviko hii:*

Sasa ezi za mbinguni bila kuwaona, wanaabudu pamoja nasi. Kwani tazama Mfalme wa Utukufu anaingia. Tazama matoleo ya sisi, ni kamili wanaisindikiza. Tukaribie na imani na juhudi, ili tusharikie ku uzima wa milele. Alliluia

*Ile wakati ya Ushirika (KINONIKON) waimbaji wataimba hii:*

Onjeni natazameni, kwani Bwana ni Mwema. Alliluia.

*Pa fasi ya*: Tumeona nuru ya kweli. . . *tunaimba hii wimbo:*

Nitamutukuza Bwana kila wakati, sifa yake kinywani mwangu siku zote; mkate wa mbinguni na kilauri cha uzima wa kuonja na muone kama Bwana ni mwema;Alliluia, Alliluia, Alliluia.

*Ile wakati Padri anakakabula Antidoro kwa Waaminifu musomaji anasoma hii Zabur**i** 33(34)*

Nitabariki Bwana wakati wote;sifa yake itakuwa kinywani mwangu daima. Nafsi yangu itajisifu katika Bwana; wapole watasikia na watafurahi. Musifu Bwana pamoja nami, na tutukuze jina lake pamoja. Nilitafuta Bwana, naye alinijibu, na kuniponyesha toka woga zangu zote. Wakamutazama, na walitiwa nuru; na nyuso zao hazitaona haya milele. Masikini huyu akalia, Bwana akamusikia, akamwokoa toka taabu zake zote. Malaika ya Bwana anapiga kambi kuzunguka wale wanaomwogopa, na anawaokoa. Onjeni mwone ya kuwa Bwana ni mwema; Heri mutu anayemuweka tumaini lake. Ogopeni Bwana, ninyi watakatifu wake;kwa sababu wale wanaomwogopa hawahitaji kitu. Wana-simba wanahitaji, wanaona njaa;Lakini wao wanaotafuta Bwana hawatakosa kitu cho chote kilicho chema. Njooni, ninyi watoto, munisikilize;nitawafundisha ninyi woga wa Bwana. Ni nani mutu yule anayetaka uzima, na anayependa siku nyingi ili apate kuona mema? Uzuize ulimi wako na ubaya, na midomo yako na kusema hila. Uache mabaya ukatende mema;tafuta salama, na kuifuata. Macho ya Bwana yanatazama wenye haki, na masikio yake ni wazi kwa kusikia kilio chao. Uso wa Bwana ni juu yao wanaotenda mabaya, aondoshe ukumbusho wao duniani. Wenye haki walilia, na Bwana alisikia, na kuwaponyesha toka taabu zao zote. Bwana ni karibu na wenye moyo wa kuvunjika, na anaokoa wenye roho ya toba. Mateso ya mwenye haki ni mengi;Lakini Bwana anamuponyesha nayo yote. Anachunga mifupa yake yote;haukuvunjika hata mumoja. Uovu utaua mwovu;nao wanaochukia wenye haki watahukumiwa. Bwana anakomboa nafsi ya watumishi wake;wala hawatahukumiwa wote wanaomuwekea yeye kimbilio lao.

Na **ZABURI** 144(145)

Nitakutukuza, Mungu wangu, ee Mufalme;na nitabariki jina lako milele na milele. Nitakubariki kila siku;na nitasifu jina lako milele na milele. Bwana na mukubwa, na mwenye kusifiwa sana;na ukubwa wake hauwezi kutafutikana. Kizazi kimoja kitasifu kazi zako kwa kingine, na kitatangaza matendo yako ya uwezo. Nitafikili enzi ya utukufu ya heshima yako, na kazi zako za ajabu nitazifikili. Na watu watataja uwezo wa matendo yako ya kuogopesha;nami nitasimulia ukubwa wako. Wao watasema ukumbusho wa wema wako mukubwa, na wataimba haki yako. Bwana ni mwenye neema na anajaarehema, polepole kwa kukasirika na mwenye rehema nyingi. Bwana ni mwema kwa watu wote;na rehema zake ni juu ya kazi zake zote. Kazi zako zote zitakushukuru, ee Bwana; na watakatifu wako watakubariki. Watasema juu ya utukufu wa ufalme wako;kujilisha wana wa watu matendo yake ya uwezo, na utukufu wa enzi ya ufalme wake. Ufalme wako ni ufalme wa milele, na mamlaka yako ni ya vizazi vyote. Bwana anategemeza wote wanaoanguka, na kuwanyanyua wanaoinama chini. Macho ya watu wote yanakungojea;nawe unawapa chakula chao kwa wakati wake. Unafungua mukono wako, na kushibisha hamu ya kila kilicho hai. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote, na mwenye

neema katika kazi zake zote. Bwana ni karibu nao wote wanaomwitia, nao wanaomwitia kwa kweli. Atatimiza hamu yao wanaomwogopa;atasikia kilio chao na kuwaokoa. Bwana anachunga wote wanaomupenda; lakini waovu wote atawaharibu. Kinywa changu kitapasha sifa ya Bwana;na miili yote wabariki jina takatifu milele na milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia (*maratatu*). Rabi, mtakatifu barikia.

**PADRI**: Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu. . .

*Leo Mangaribi tutasoma Sala ya Usiku (Apodipno Mkubwa). Angalia mu Kitabu: Orologio Mukubwa.*

# SIKU YA MBILI MKUBWA

## SALA YA ASUBUI (ORTHROS)

*Mwanzo wa Ibada: Tazama siku ya kwanza Mkubwa. Somo la Zaburi* ***KATHISMA*** *ya Tisa.*

**KATHISMA**. Sauti ya Ine. (O ipsothis en to Stavro)
Enyi ndugu, tuwe na mapendo ya Bwana Arusi, nuru zetu zitayarishwe; fazila zetu ziangae tena imani ya kweli iwe na nuru! Tuwe tayari kama mabikira wenyi akili wa Bwana kusudi tuingie pamoja naye ku karamu ya Arusi. Kwa sababu Bwana Arusi aliye Mungu anawatolea wote kama zawadi utukufu usiyoharibika.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine hii wimbo)*

*Somo ya Zaburi* ***KATHISMA*** *ya Kumi.*

**KATHISMA**. Sauti ya Ine.
Tazama shauri ya makafiri juu yako, ee Mwokozi. Ni wivu na uovu wa makuhani na waandishi waliyoifunga na kumusukuma Yuda ku utoaji. Akaenda bila haya kukutana na hawa watu waovu na akawaambia: Mutanipa nini kama ninamutoa mikononi mwemu? Ee Bwana, samehe roho zetu ku hukumu ya hii namna.
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . (*mara ingine hii wimbo*).

*Somo la Zaburi.* ***KATHISMA*** *ya Kumi na moja.*

**KATHISMA**. Sauti ya Mnane.
Yuda amevutwa kwa feza, kwa chuki yake amesimama juu ya Rabi wake, amefanya fitina na anatafuta kunitoa. Alipoondolewa nuru, anapata giza. anasikilizana juu ya bei tena anauzisha huyu asiye na bei. Ee Bwana, huyu maskini aliyekutoa amejitundika. Utusamehe hii uovu, ee Kristu Mungu wetu, utupe maondoleo ya zambi zetu sisi wenye kushangilia na mapendo mateso yako takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(Mara ingine hii wimbo).*

Somo la Evangelio kama ilivyoandikwa na Mtakatifu Matayo 22, 15-46. 23, 1-39.
Kisha Wafarisasyo wakakwenda na kufanya shauri namna wanavyoweza kumutega katika masemo yake. Wakatuma kwake wanafunzi wao pamoja na Waherode wakisema: Mwalimu, tunajua ya kama wewe ni mutu wa kweli, na unafundisha njia ya Mungu katika kweli, wala hufikili mutu, kwa maana hutazami sura za watu. Utuambie basi, Unafikili nini? Ni halali kumupa Kaisari kodi, ao sivyo? Lakini Yesu akafahamu uovu wao, akasema: Kwa nini munanijaribu, ninyi wadanganyifu? Munionyeshe feza ya kodi. Wakamuletea dinari. Akawaambia: Mufano huu ni wa nani, na anwani hii? Wakamwambia: Ni ya Kaisari. Halafu akawaambia: Lipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu. Na wakati waliposikia, wakashangaa, wakamwacha, wakakwenda zao. Siku ile Wasadukayo wanaosema ya kwamba hakuna ufufuko, walikuja kwake; wakamwuliza, wakisema: Mwalimu, Musa alisema, kama mutu akikufa, naye hana watoto, ndugu yake ataoa muke wake ili apatie ndugu yake muzao. Basi tulikuwa na ndugu saba; wa kwanza akaoa, akakufa, na kwa kuwa hana muzao, akaacha muke wake kwa ndugu yake; vivyo hivyo wa pili vilevile, na wa tatu, hata wote saba.

Mwisho wa wote, yule mwanamuke akakufa. Basi katika ufufuko, atakuwa muke wa nani katika wale saba? Maana wao wote walikuwa naye. Lakini Yesu akajibu, akawaambia: Munakosa kwa

sababu hamujui maandiko wala uwezo wa Mungu. Kwa maana katika ufufuko hawaoi wala hawaolewi, lakini watakuwa kama malaika mbinguni. Tena kwa maneno ya ufufuko wa wafu, hamukusoma muliloambiwa na Mungu akisema: Mimi ni Mungu wa Abrahamu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? Mungu si Mungu wa wafu, lakini wa walio hai. Na wakati makutano waliposikia, wakashangaa kwa mafundisho yake. Lakini Wafarisayo, wakati waliposikia ya kama alifunga kinywa cha Wasadukayo, wakakusanyika. Mumoja wao, mwana-sheria, akamwuliza akimujaribu: Mwalimu, katika torati, amri gani iliyo kubwa? Akamwambia: Upende Bwana Mungu wako na moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ni amri iliyo kubwa na ya kwanza. Na ya pili inafanana nayo ni hii: Penda jirani yako kama wewe mwenyewe. Katika amri hizi mbili inategemea torati yote na manabii. Basi wakati Wafarisayo walipokusanyika, Yesu akawauliza, akisema: Munafikili nini juu ya Kristo? Yeye ni mwana wa nani? Wakamwambia: Mwana wa Daudi. Akawaambia: Basi namna gani Daudi katika Roho anamwita Bwana, akisema: Bwana alimwambia Bwana yangu: Uketi kwa mukono wangu wa kuume, hati ninapoweka adui zako chini ya miguu yako? Basi Daudi akimwita Bwana, yeye ni mwana wake namna gani? Wala hakuna mutu aliyeweza kumujibu neno, wala tangu siku ile hakuna mutu aliyesubutu kumwuliza neno tena. (23, 1-39)Halafu Yesu akawaambia makutano na wanafunzi wake, akisema: Waandishi na Wafarisayo wanaketi katika kiti cha Musa; basi maneno yote wanayowaambia ninyi kutenda, muyashike na kuyatenda; lakini musitende kwa mufano wa matendo yao; kwa maana wanasema, lakini hawatendi. Ndiyo, wanafunga mizigo mizito iliyo michungu kwa kuvumilia juu ya mabega ya watu, lakini wao wenyewe hawataki kuigusa hata na kidole chao. Lakini matendo yao yote wanatenda ili watazamwe na watu; kwani wanafanya hirizi zao mupana, na wanaongeza pindo za mavazi yao, na wanapenda pahali pa mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masunagogi, na kusalimiwa katika masoko, na kuitwa na watu: Rabi. Lakini ninyi musiitwe Rabi, kwa maana mumoja ni mwalimu wenu; nanyi wote ni ndugu. Wala musiite mutu baba yenu duniani; kwa sababu mumoja ni Baba yenu, aliye mbinguni. Wala musiitwe mwalimu; kwani mumoja ni mwalimu wenu, ndiye Kristo. Lakini yeye aliye mukubwa katikati yenu atakuwa mutumishi wenu. Naye anayejitukuza mwenyewe, atanyenyekezwa, naye anayejinyenyekeza mwenyewe, atatukuzwa. Lakini ole wenu, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munafungia watu ufalme wa mbinguni. Kwa maana ninyi hamwingii ninyi wenyewe, wala wale wanaoingia, hamuwaachi kuingia. Ole wenu, ninyi waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munakula nyumba za wajane, na kwa hila munaomba maombi marefu, kwa hivi mutapata hukumu iliyo kubwa zaidi. Ole wenu, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa maana munazunguka bahari na inchi kufanya mutu mumoja kuwa mugeuzi; na akikwisha kufanyiwa, munamufanya kuwa mwana wa Gehena mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe. Ole wenu, ninyi viongozi wapofu wanaosema: Mutu anayeapa kwa hekalu, si kitu, lakini mutu anayeapa kwa zahabu ya hekalu, yeye amejifunga kwa kiapo. Ninyi wapumbafu na vipofu, maana ni nini iliyo kubwa kupita, zahabu, ao hekalu lililotakasa zahabu? Na: Mutu anayeapa kwa mazahabu, si kitu, lakini mutu anayeapa kwa sadaka iliyo juu yake, amejifunga kwa kiapo. Ninyi vipofu, maana nini iliyo kubwa kupita, sadaka, ao mazabahu inayotakasa sadaka? Basi mutu anayeapa kwa mazabahu, anaapa kwa mazabahu, na kwa vitu vyote vilivyo juu yake. Naye anayeapa kwa hekalu, anaapa kwa hekalu, na kwa yeye anayekaa ndani yake. Naye anayeapa kwa mbingu, anaapa kwa kiti cha ufalme cha Mungu, na kwa yeye anayeketi juu yake. Ole wenu, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munalipa zaka ya munanaa na bizari na jira, lakini mumeacha mambo makubwa kupita ya sheria, hukumu, na rehema, na imani; lakini imewapasa ninyi kufanya maneno haya pasipo kuacha yale mengine. Ninyi viongozi wapofu, munaochuja imbu na kumeza ngamia. Ole wenu, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Maana munasafisha inje ya kikombe na sahani, alkini ndani zimejaa unyanganyi na tamaa. Wewe Mufarisayo mupofu, safisha kwanza ndani ya kikombe na ya sahani, hata inje zao ziwe safi

vilevile. Ole wenu, Waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwani munafanana na makaburi yaliyopakaliwa pembe, yanayoonekana vizuri sana kwa inje, lakini ndani yanajaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. Hivi ninyi vilevile kwa inje munaonekana kuwa wenye haki mbele ya watu, lakini ndani munajaa udanganyifu na uovu. Ole wenu waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munajenga makaburi ya manabii, na kupamba makaburi ya wenye haki, mukisema: Kama sisi tungalikuwa kwa siku za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. Hivi munajishuhudia wenyewe ya kwamba ninyi ni wana wao walioua manabii. Jazeni basi kipimo cha baba zenu. Ninyi nyoka, ninyi wana wa majoka, mutakimbia hukumu ya Gehena namna gani? Kwa hivi tazama, ninawatumia ninyi manabii na watu wenye akili na waandishi, wengine katikati yao mutawaua na kuwasulibisha; na wengine katikati yao mutawapiga katika masunagogi yenu, na kuwasulibisha, na wengine katikati yao mutawapiga katika masunagogi yenu, na kuwafukuza muji kwa muji; hata juu yenu ije damu yote ya haki iliyomwangika duniani, toka damu ya Abeli mwenye haki, hata damu ya Zekaria, mwana wa Barakia muliyemwua kati ya pahali patakatifu na mazabahu. Kweili ninawaambia ninyi, Maneno haya yote yatakuja juu ya kizazi hiki. Ee Yerusalema, Yerusalema, unaona manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kukusanya watoto wako pamoja, kama vile kuku anavyo kusanya watoto wake chini ya mabawa yake, lakini ninyi hamukutaka. Tazameni, nyumba yenu imeachwa kwenu tupu. Kwani ninawaambia ninyi, Hamutaniona kamwe tangu sasa hata mutakaposema, Amebarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

**ZABURI** 50(51). *(Angalia ukurasa:*
**SHEMASI**: Ektenia Kidogo

**KONTAKION** Sauti ya mbili
Ee roho yangu, waza ku saa ya kufa, na tetemeka, ee maskini, ukiwaza mtiniuliyoondolewa! Ongeza na nguvu talanta uliyopokea; Kesha tena lalamika: Ee Kristu, usitufungie mlango wa Chumba chako cha karamu.

**IKOS**
Una tena na wakati, amka na lalamika: Nimekosa juu, ee Mwokozi, usiniondoe kama mtini usiyozaa matunda, lakini kwa rehema yako, ee Kristu, hurumia roho ambayo, inapojaa na woga, inalalamika kwako: Usitufungie mlango wa Chumba chako cha karamu, ee Kristu.

*Sasa tunasoma Sinaksario ya Watakatifu wa hii siku. Kisha tunasoma hivi:*

Hii siku ya Kazi mbili Mkubwa na Takatifu tunakumbuka Mufano wa ma Bikira Kumi tunasoma katika Evangelio ya Kristu.

***KANUNI*** *ya wimbo wa mbili*

## KANUNI

HIRMOS Sauti ya mbili.
Wimbo wa Mnane
Vijana watakatifu watatu hawakutii ku amri ya mzulumu. Walipotupwa katika tanuru ya moto wakamuungama Mungu wakiimba: Enyi wote, viumbe vya Bwana, mtukuzeni Bwana

Utukufu kwako, , ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Tuache uvivu wetu wote, na taa zetu zenyi kuwaka tuendeni kukutana na Kristu, Bwana Arusi msiyekufa, tukiimba: Tukuzeni Bwana, enyi viumbe vyote vya Bwana.

Tunatukuza Baba, Mwana na Roho Mutakatifu Bwana.
Ijapokuwa katika roho zetu mafuta ya zabihu haikose, hatutapitisha bure saa ya karamu sababu ya kwenda kununua ingine, lakini tutaimba: Tukuzeni Bwana, enyi viumbe vyote vya Bwana.

Sasa na siku zote. . .
Ninyi muliopokea neema ya Mungu kama talanta, kwa nguvu yenu muistahilishe na msaada wa Kristu aliyewapayo tena imbeni: Tukuzeni Bwana, enyi viumbe vyote vya Bwana.

Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana
**KATAVASIA**: Tuache uvivu wetu wote, na taa zetu. . . .

**SHEMASI**: Muzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo, na kumtukuza.

HIRMOS Wimbo ya Tisa
Ulichukua tumboni mwako Mungu asiye na mipaka, tena ulizaa furaha ya dunia; tunakuimbia, ee Bikira Mtakatifu kamili.

Utukufu kwa Baba. . . .
Ee Mwema kamili uliwaambia Wafuasi wako: Kesheni, kwani hamujui saa nitakapokuja mimi Bwana kulipa kila mmoja kadiri ya matendo yake.

Sasa na siku zote. . .
Wakati wa majilio yako ya ajabu, ee Rabi, uniweke katika kundi la kondoo kuume kwako, bila kuona makosa yangu mengi.

**KATAVASIA**: Ulichukua tumboni mwako Mungu asiye na mipaka. . . .

**SHEMASI**: Ektenia Kidogo.

**EKSAPOSTILARION**
Ninaona chumba chako cha arusi chenye kupambwa vizuri, ee Mwokozi wangu, na sina na mavazi ya kuingia nayo. Uangazie nguo ya nafrsi yangu, ee Muletaji-nuru, na uniokoe. *(mara tatu).*

## MASIFU

Kila mwenye pumzi amsifu Bwana. . .

**ZABURI** 148, **ZABURI** 149.
*Toka Zaburi 150 tunaanza kuimba hii shairi:*

Musifuni kwa matendo yake makuu, msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.

Sauti ya kwanza.
Nitaingia je mimi musiye stahili katika ukuu wa Watakatifu wako. Nikisubutu kuingia katika nyumba ya Arusi, nguo yangu litanitoa maana haiko ya arusi Malaika watanifukuza Bwana safisha basi mataka ya moyo wangu na uniokoe wewe mupenda wanadamu.

Musifuni kwa mvumo wa baragumu, musifuni kwa kinanda na kinubi. *(mara ingine hii wimbo).*

Musifuni kwa ngoma na kucheza, musifuni kwa nzenze na filimbi.

Sauti ya pili

Ee Kristu, roho yangu ya uvivu inalala, sikumpata Bwana Arusi wangu, yeye taa yenye kuangaa na moto wa fazila. Tazama nimekuwa kama mabikira wapumbafu wasioshurulika wakati wa kazi. Usinifungie mlango wa rehema yako, ee Rabi, na ukitikisa usingizi wangu wa giza, uniamshe, uniingize katika nyumba yako pamoja na mabikira wenyi akili, humo wanakutukuza daima masauti safi ya wenye haki wakiimba: Ee Bwana, utukufu kwako.

Musifuni kwa matoazi yavumayo tamu, musifuni kwa matoazi yavumayo sana. Kwa mwenye pumuzi na amsifu Bwana. *(mara ingine hii wimbo*)

Utukufu Kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Sauti ya Ine

Umesikia hukumu ya yule aliyeficha talanta yake, ee roho yangu, usifiche neno la Mungu. Tangaza maajabu yake, zidisha vipaji vyake sababu ya kuingia katika furaha ya Bwana wako.

*Padri mkubwa ao Msomaji:* Kwa kuwa utukufu ni wako, ee Bwana Mungu wetu, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

DOKSOLOGIA KIDOGO

**PADRI**: Tumalize ombi letu ku asubui kwa Bwana.

## APOSTIKHA

Sauti ya Sita.

Kujeni, enyi waaminifu tumtumikie wepesi Bwana, kwani amewapa watumishi wake Uzuri wake. Kila mmoja azidishe maarifa ya neema: mmoja alete hekima akitenda mema; mwingine ajazwe na kazi ya kuangaza ndugu zake, kama mtumishi mwaminifu afundishe neno kwa wasiokujua; huyu aliye mtajiri awagawanyie maskini mali yake. Hivi tutazidisha talanta yenye ku kopeshwa kwa wote, wasimamizi waaminifu wa neema, tutastahili furaha ya Rabi. Ee Kristu Mungu, utupeyo, kwani wewe ni mpenda wanadamu.

Kituo: Ee Bwana, asubui tulijazwa na rehema yako na tulifurahi. Tumefurahiwa siku zote za maisha yetu. Tunaweza kufurahiwa kwa ajili ya siku ulizotuzarau, kwa ajili ya miaka tuliteswa. Tazama watumishi na viumbe vyako, ongoza wana wao.

Ee Yesu, wakati utakapokuja na utukufu wako pamoja na majeshi ya Malaika kukaa pa kiti chako cha hukumu, usinitenge mbali nawe, ee Mchungaji mwema! Unajua njia zenyi kuongoza kuume kwako; za uovu ni njia za kushoto. Usinipoteze pamoja na mbuzi, uso wenyi kuchafuliwa na zambi kama nilivyo; uniweke kuume kwako pamoja na kondoo, ee mpenda wanadamu.

Kituo: Nuru ya Bwana Mungu wetu iwe nasi, uwe mwema ku kazi ya mikono yetu, uwe mwema ku kazi ya mikono yetu.

Ee Bwana Arusi wangu mwenyi kuangaa na uzuri kati ya wanadamu wote! Wewe uliyetualika ku karamu ya kiroho nyumbani mwako! Univue mimi manguo mbaya ya zambi, ukiniunganisha

ku mateso yako, tena univike utukufu wa uzuri wako, unifanye kuwa mwalikwa wa nuru wa ufalme wako, kwani umejaa na rehema.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Sauti ya Saba

Ee roho yangu, Rabi, anakupa talanta, pokea hii zawadi na woga. Kopesha kwa huyu aliyekupa, uwape maskini na umufanye Bwana kuwa Rafiki yako. Ili uweze kusimama kuume kwake wakati atakapokuja katika utukufu wake na kusikia hii maneno ya furaha: Ingia, ee mutumishi wangu, katika furaha ya Rabi wako. Kwa rehema yako kubwa, ee Mwokozi, unistahilisha mimi mpotevu ku hii furaha.

**PADRI**: Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako, ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .

**PADRI**: Kwa kuwa ufalme, na uwezo. . .

***MSOMAJI*** *anasoma* ***KONTAKION****:*

Ee roho yangu, waza ku saa ya kufa, na tetemeka, ee masikini, ukiwaza mtini uliyoondolewa! Ongeza na nguvu talanta uliyopokea;Kesha tena lalamika: Ee Kristu, usitufungie mlango wa Chumba chako cha karamu.

Bwana hurumia *(mara Kumi na mbili).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Padri.

**PADRI**: Aliye ahimidiwe Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

***PADRI*** *ao Mukubwa ya Kanisa:*

Ee Mfalme wa mbinguni, sabitisha imani, tuliza mataifa, leta amani duniani, linda hii Kanisa takatifu na hii mji weka katika makao ya wenye haki Baba zetu na ndugu zetu waliyolala tena pokea toba yetu na kukiri kwetu, kwani ndiwe Mwema tena mpenda-wanadamu.

*Kisha tunafanya Metania kubwa tatu na mara moja tunasema sala ya Mtakatifu Efremi ya Siria:*

*Kisha Kuaga (Apolisis) sawa jana.*

# SALA YA MANGARIBI (ESPERINOS) NA LITURGIA YA VYENYI KUTAKASWA MU KAZI MBILI MKUBWA

**PADRI**: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote. . .

**MSOMAJI**: Njooni tumwinamia. . . Kisha **ZABURI** 103 (104)

**MWIMBAJI anaimba**: Bwana nimekuita. . . Sauti ya kwanza.

*Troparia ile tuliimba asubui ku Orthros (Masifu na Apostikha). Nikusema:*

Nitaingia je, mimi msiye stahili. . . *(mara mbili).*
Ee Kristu, roho yangu ya uvivu inalala. . *(mara mbili).*

Umesikia hukumu ya yule aliyeficha talanta. . . *(mara mbili).*
Kujeni, enyi Waaminifu tumtumikie wepesi. . . *(mara mbili).*
Ee Yesu, wakati utakapokuja na utukufu wako. . .
Ee Bwana-Arusi wangu mwenyi kuangaa na uzuri. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Sauti ya Saba
Ee roho yangu, Rabi, anakupa talanta, pokea hii zawadi. . .

**PADRI**: Mangaribi (esperas) **PROKIMENON**.

MWANGAZA UPOLE (ILARON)

Somo ya Unabii.

**PROKIMENON** Sauti ya sita

**ZABURI** 131(132). Simama, ee Bwana, mpaka ku mapumziko yako, wewe na Safina ya nguvu yako.

Kituo: Umukumbuke, ee Bwana, Daudi na wema wake wote.

Somo la kitabu cha Kutoka 2, 5-10

Binti ya Farao akashuka aoge mutoni; vijakazi wake wakatembea kando ya muto. Akaona safina katika majani, akatuma kijakazi wake kuitwaa. Na wakati alipoifungua, akaona mutoto; na tazama, mutoto muchanga akalia. Akamuhurumia, akasema: Huyu ni mumoja wa wana wa Waebrania. Halafu ndugu yake musichana akamwambia binti ya Farao: Niende na kukuitia aya ya wanawake wa Waebrania akunyonyeshee mutoto? Binti ya Farao akamwambia: Kwenda. Musichana akakwenda, akaita mama ya mutoto. Binti ya Farao akamwambia: Chukua mutoto huyu uninyonyeshee, na nitakupa mishahara yako. Mwanamuke akatwaa mutoto, akamunyonyesha. Mutoto akakua, akamuleta kwa binti ya Farao, akakuwa mwana wake. Akaita jina lake Musa, akasema: Kwa sababu nilimutoa katika maji.

**PROKIMENON** Sauti ya Ine: Ni vema tena ni vizuri ndugu waishi wote pamoja.

Kituo: Ni manukato kichwani yenyi kushuka ku ndevu, ku ndevu ya Aroni.

(*Baraka ya Padri):* Nuru ya Kristu inangaza mwanadamu wote.

Somo la Kitabu cha Yobu 1, 13-22.

Na ilikuwa siku moja wakati wana wake na binti zake walipokuwa wakikula na kunywa mvinyo nyumbani mwa ndugu yao mukubwa, mujumbe alifika karibu na Yobu, akasema: Ngombe walikuwa wakilima, na punda walikuwa wakikula karibu nao: na Wasaba waliwaangukia na kawatwaa: ndiyo wamewa watumishi kwa ukali wa upanga; nami peke yangu nimepona kukuletea habari. Angali alipokuwa akisema, mwingine akafika vilevile, akasema: Moto wa Mungu umeanguka toka mbinguni, umeteketeza kondoo na watumishi na kuwaharibu; nami peke yangu nimepona kukuletea habari. Na angali alipokuwa akisema, mwingine akafika vilevile, akasema: Wakaldea walifanya vikosi vitatu, wakaangukia ngamia na kuwatwaa, ndiyo, na wamewa watumishi kwa ukali wa upanga; nami peke yangu nimepona, kukuletea habari. Na angali alipokuwa akisema, mwingine akakuja vilevile, akasema: Wana wako na binti zako walikuwa wakikula na kunywa mvinyo nyumbani mwa ndugu yao mukubwa: na tazama, upepo mukubwa ukatoka upande wa jangwa, ukapiga pembe ine za nyumba, ikaangukia vijana, nao

wamekufa: mimi peke yangu nimepona kukuletea habari. Halafu Yobu akasimama, akapasua jio lake, akanyoa kichwa chake, akaanguka kwa udonga, akaabudu; akasema: Mutupu nilitoka tumboni mwa mama yangu, na mutupu nitarudi tena kule; Bwana ametoa, na Bwana ametwaa; abarikiwe jina la Bwana. Katika maneno haya yote Yobu hakukosa wala kushitaki Mungu kwa upumbafu.

*Sasa Padri na Waimbaji sawa jana wataimba:* Maombi yangu ya elekezwe. . .

*Somo la Evangelio:* Matayo 24, 36-51, 25. 1-46 na 26, 2.

Lakini hakuna mutu anayejua habari za siku ile na saa ile, hata malaika walio mbinguni wala Mwana, ila Baba peke yake. Kwa maana kama zilivyokuwa siku za Noa, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwa Mwana wa watu. Kwa kuwa kama kwa siku zile mbele ya garika walivyokuwa wakikula na kunywa, wakioa na kuolewa, mupaka siku Noa alipoingia safina, na hawakujua hata garika ilipokuja na kuwaondosha wote; ndivyo kutakavyokuwa kuja kwa Mwana wa watu. Halafu watu wawili watakuwa shambani; mumoja atatwaliwa na mumoja ataachwa. Angalieni basi; kwa sababu hamujui siku Bwana yenu atakapokuja. Lakini tambueni neno hili, kama mwenye nyumba angalijua katika zamu gani mwizi atakapokuja, kama angaliangalia, wala asingaliacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa hivi muwe tayari; kwa sababu kwa saa musiyozani Mwana wa watu anakuja. Basi nani aliye mutumwa mwaminifu na mwenye akili, bwana yake aliyemuweka juu ya nyumba yake, kuwapa chakula chao kwa wakati wake? Heri mutumwa yule bwana yake anayemukuta akifanya hivi wakati anapokuja. Kweli ninawaambia ninyi, atamuweka juu ya vitu vyake vyote. Lakini mutumwa yule mubaya akisema moyoni mwake: Bwana yangu anakawia; na anaanza kupiga watumishi wenzake, na kula na kunywa pamoja na walevi; bwana ya mutumwa yule atakuja siku asiyozani na saa asiyojua, na atamukata vipande, na kumuwekea fungu lake pamoja na wadanganyifu, kule kutakuwa kulia na kusaga meno. 25, 1-46)Halafu ufalme wa mbinguni utafananishwa na mabikira kumi waliotwaa taa zao, wakatoka kwenda kukutana na bwana arusi. Watano wao walikuwawapumbafu na watano wenye akili. Kwa sababu wapumbafu wakati walipotwaa taa zao, hawakutwaa mafuta pamoja nao; lakini wenye akili walitwaa mafuta ndani ya vyombo vyao pamoja na taa zao. Basi wakati bwana arusi alipokawia, wao wote wakasinzia na kulala usingizi. Lakini saa sita ya usiku lilikuwa kelele: Tazama, bwana arusi! tokeni kukutana naye. Halafu mabikira wale wote wakaamka, wakatengeneza taa zao. Wale wapumbafu wakawaambia wenye akili: Mutupe sisi ya mafuta yenu; kwani taa zetu zinazimika. Lakini wale wenye akili wakajibu wakisema: Sivyo; hayatatosha sisi na ninyi; lakini kwendeni kwa wenye kuuza, mununue kwa ninyi wenyewe. Na wakati walipokwenda kununua, bwana arusi alikuja; nao waliokuwa tayari waliingia pamoja naye kwa arusi; mulango

ukafungwa. Halafu mabikira wale wengine wakakuja vilevile wakisema: Bwana, Bwana, utufungulie. Lakini akajibu, akisema: Kweli ninawaambia ninyi, Siwajui ninyi. Angalieni basi, kwa sababu hamujui siku wala saa. Maana ni kama mutu akisafiri katika inchi nyingine, akaita watumwa wake akaweka kwao mali zake. Akamupa mumoja talanta tano, na mwingine mbili, na mwingine moja; kila mutu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara moja yeye aliyepewa talanta tano akakwenda, akafanya biashara nazo, akapata talanta tano nyingine. Vilevile yeye aliyepewa talanta mbili, alipata mbili nyingine. Lakini yeye aliyepewa talanta moja, akakwenda zake, akachimba udongo, akaficha feza ya bwana yake. Basi nyuma ya siku nyingi bwana ya watumwa wale akakuja, akafanya hesabu pamoja nao. Naye aliyepata talanta tano alikuja, akaleta talanta tano nyingine, akisema: Bwana, umenipa talanta tano; tazama, nimepata talanta tano nyingine. Bwana yake akamwambia: Vema, mutumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa vitu vichache, nitakuweka juu ya vitu vingi; ingia katika furaha ya bwana yako. Naye aliyepewa talanta mbili alikuja, akasema: Bwana, umenipa talanta mbili; tazama, nimepata talanta mbili nyingine. Bwana yake akamwaambia: Vema, mutumwa mwema na mwaminifu; umekuwa mwaminifu kwa vitu vichache, nitakuweka juu ya vitu vingi; ingia katika furaha ya bwana yako. Naye aliyepewa talanta moja alikuja, akasema: Bwana, nilikutambua ya kama wewe ni mutu mugumu, ukivuna pahali usipopanda, na ukikusanya pahali usiposambaza; na niliogopa, nikakwenda na kuficha talanta yako katika udongo; tazama, unayo iliyo yako. Lakini bwana yake akajibu na kumwambia: Wewe mutumwa mubaya na mulegevu, ulijua ya kama ninavuna pahali nisipopanda, na kukusanya pahali nisiposambaza; basi ilikupasa kuweka feza yangu kwa wabadilisha feza, nami nikikuja ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi mwondoshe talanta kwake na kumupa yule mwenye talanta kumi. Kwa maana mutu mwenye kitu atapewa, naye atazidishwa tele; lakini yeye asiye na kitu ataondolewa hata kitu kile alicho nacho. Na mutupe mutumwa yule asiye na faida katika giza la inje; kutakuwa kulia na kusaga meno. Lakini wakati Mwana wa watu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika yote pamoja naye, halafu ataketi juu ya kiti cha utukufu wake; na mbele yake mataifa yote watakusanyika; naye atawatenga kama muchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi; na ataweka kondoo kwa mukono wake wa kuuma, lakini mbuzi kwa mukono wake wa kushoto. Halafu Mufalme atawaambia wale kwa mukono wake wa kuuma: Kujeni, ninyi muliobarikiwa na Baba yangu, muriti ufalme muliotengenezewa tangu kuumbwa kwa ulimwengu; kwani nilikuwa na njaa, nanyi mulinipa chakula; nilikuwa na kiu, nanyi mulinikunywesha; nilikuwa mugeni nanyi mulinikaribisha; mutupu, nanyi mulinivika; mugonjwa, nanyi mulikuja kunitazama; nilikuwa katika kifungo, nanyi mulikuja kwangu. Halafu wenye haki watamujibu wakisema: Bwana, wakati gani tulipokuona una njaa na tulikukulisha? ao una kiu, na tulikukunywesha? Na wakati gani tulipokuona mugeni, na tulikukaribisha? ao mutupu na tulikuvika? Na wakati gani tulipokuona mugonjwa, ao katika kifungo na tulikuja kwako? Na Mufalme atawajibu ka kuwaambia: Kweli ninawaambia ninyi, kwa kadiri mulivyotendea mumoja wa ndugu zangu, walio wadogo, mulinitendea mimi. Kisha atawaambia wale kwa mukono wake wa kushoto: Ondokeni kwangu, ninyi muliolaaniwa, mwende katika moto wa milele uliotengenezwa kwa Shetani na malaika zake; kwa sababu nilikuwa na njaa nanyi hamukunipa chakula; nilikuwa na kiu, nanyi hamukunikunywesha; mugonjwa, na katika kifungo, nanyi hamukuja kunitazama. Halafu wale vile watajibu wakisema: Bwana, wakati gani tulipokuona una njaa, ao una kiu, ao mugeni, ao mutupu, ao mugonjwa, ao katika kifungo, nasi hatukukutumikia? Kisha atawajibu akisema: Kweli ninawaambia ninyi, kwa kadiri musiyotendea mumoja wa hawa walio wadogo, hamukunitendea mimi. Na hawa wote watakwenda kuingia katika azabu ya milele; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele. 26, 1-2)Na ilikuwa wakati Yesu alipomaliza maneno haya yote, akawaambia wanafunzi wake: Munajua ya kama nyuma ya siku mbili Pasaka inakuja, na Mwana wa watu atatolewa asulibiwe.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Mfululizo wa Liturgia ya vyenyi Kutakaswa, sawa jana. .*

## SAA YA TATU NA SAA YA SITA

*Ku Saa ya tatu Zaburi za Saa zinafwatwa na **KATHISMA** ya Kumi na mbili.*
*Ku Saa ya Sita **KATHISMA** ya Kumi na Tatu. Ku Saa ya Tisa hakuna **KATHISMA**.*
*Ku Saa ya Sita kisha Theotokion ya Saa, Tropari ya Unabii.*

Sauti ya kwanza
Ee Mwokozi, wewe peke yako ni mtajiri wa rehema, samehe makosa yetu mengi; tena utustahilishe tuabudu Ufufuo Takatifu, kwa maombezi ya Mama Yako.

**PROKIMENON** Sauti ya Sita
Kwa maana kwa Bwana kuna rehema, kwake kuna kitulizo kubwa.
Kituo: Toka kuzimuni nakulalamikia: Ee Bwana, sikiliza sauti yangu.

Somo la Unabii wa Ezekieli 1, 21-28
Wakati wale walipokwenda, haya yakakwenda; na wakti wale waliposimama, haya yakasimama, na wakati wale waliponyanyuliwa toka inchi, marurudumu yakanyanyuliwa kando yao; kwa maana roho ya kiumbe hai ilikuwa ndani ya magurudumu. Na juu ya kichwa cha kiumbe hai ulikuwa mufano wa anga, kama rangi ya bilauri la kuogopesha imetandwa juu ya vichwa vyao kwa juu. Na chini ya anga mabawa yao yalikuwa sawa, kila moja kuelekea la pili; kila mumoja alikuwa na mawili yaliyofunika miili yao upande huu na kila mumoja alikuwa na mawili yaliyofunika miili yao upande ule. Na wakati walipokwenda, nikasikia sauti ya mabawa yao kama sauti ya maji mengi, kama sauti ya Mwenyezi, sauti ya makelele kama sauti ya jeshi; wakati waliposimama, wakashusha mabawa yao. Na kulikuwa sauti juu ya anga iliyo juu ya vichwa vyao; wakati waliposimama wakashusha mabawa yao. Na juu ya anga iliyokuwa juu ya vichwa vyao ulikuwa mufano wa kiti cha ufalme, kama kuonekana kwa yakuti samawi; na juu ya mufano wa kiti cha ufalme ulikuwa mufano kama kuonekana kwa mutu juu yake. Nikaona kama rangi ya kaharabu, kama kuonekana kwa moto ndani yake pande zote, toka kuonekana kwa viuno vyake na juu, na toka kuonekana kwa viuno vyake na chini, nikaona kama kuonekana kwa moto, na kungaa kulimuzunguka. Kama kuonekana kwa upinde ulio ndani ya wingu kwa siku ya mvua, vivyo hivyo kulikuwa kuonekana kwa kungaa pande zote. Kuonekana kwa mufano wa utukufu wa Bwana kulikuwa hivi. Wakati nilipouona, nilianguka kifudifudi, nikasikia sauti ya mumoja aliyesema.

**PROKIMENON** Sauti ya Ine.
Israeli amtumainie Bwana sasa hata milele.
Kituo: Ee Bwana. moyo wangu haukufurahiwa, macho yangu haikunyanyuliwa.

# SIKU YA TATU MKUBWA

## SALA YA ASUBUI (ORTHROS)

*Mwanzo wa Ibada: Ona siku ya kwanza Mkubwa*

*Somo la Zaburi **KATHISMA** ya Kumi na Ine.*

**KATHISMA** Sauti ya Tatu
Mwanamuke mwenye zambi alikuja kwako, ee Mpenda wanadamu; akamwangia miguu yako manukato yenyi kuchanganyika na machozi yake. Kwa neno moja tu ukamuokoa ku uvundo wa makosa yake. Lakini huyu aliyepumzika na neema yako, mfwasi wako mbaya aliikataa, tena anajipakaa matope wakati anapokuuzisha ku feza. Utukufu ku rehema yako, ee Kristu.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . . *(mara ingine hii wimbo)*

*Somo la Zaburi **KATHISMA** Kumi na Tano*

**KATHISMA**. Sauti ya Inne.
Ee Bwana hazina ya uzima, kwa kupenda feza Yuda mkosefu akawaza kukutoa, aliposirika, akaenda mbio kwa Wayuda na akawaambia makafiri hawa: Mutanipa nini kama nikiwatoleaye asulubiwe?

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(Mara ingine hii wimbo).*

*Somo la Zaburi **KATHISMA** Kumi na Sita*

**KATHISMA**. Sauti ya Kwanza
Mwanamuke mwenyi zambi analalamika, ee mwenyi rehema, anapaguza na mapendo miguu yako Takatifu na nywele zake, na moyoni mwake analia: Usinitupe, ee Mungu wangu! usinichukie, lakini pokea toba yangu tena uniokoe, kwani peke yako ndiwe mpenda wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Somo la Evangelio ilivyoandikwa na Mtakatifu Yoanne 12, 17-50
Basi makutano waliokuwa pamoja naye wakati alipoita Lazaro toka kaburi na kumufufua, walimushuhudia. Na kwa sababu hii makutano walikwenda kumukuta, kwa sababu wamesikia ya kuwa alifanya alama hii. Basi Wafarisayo walisemezana katikati yao: Munaona ya kama hamuwezi kufanya neno; tazama, dunia yote imekwenda kumufuata. Na palikuwa na Wayunani wengine katikati ya watu waliopanda kuabudu kwa karamu. Wao basi wakakuja kwa Filipo, aliye mutu wa Betesaida wa Galilaya, wakamwuliza, wakasema: Bwana, tunataka kuona Yesu. Na Filipo akakwenda, akamwambia Anderea, na tena Anderea na Filipo, pamoja wakamwambia Yesu. Yesu akawaambia, akisema: Saa imekuja, Mwana wa watu atukuzwe. Kweli, kweli ninawaambia ninyi, kama punza ya ngano isipoanguka kwa udongo na kufa, inakaa peke yake; lakini kama ilikufa, inazaa matunda mengi. Yeye anayependa uzima wake ataupoteza, naye anayechukia uzima wake katika ulimwengu huu atachunga hata uzima wa milele. Kama mutu akinitumikia, anifuate; na pahali nilipo, pale mutumishi wangu atakaa; kama mutu akinitumikia, Baba yangu atamuheshimu. Sasa roho yangu inafazaika; nami nitasema nini? Baba, uniokoe kwa saa hii. Lakini ni kwa sababu hii nimefika kwa saa hii. Baba, utukuze jina lako. Basi sauti ilitoka

katika mbingu: Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena. Basi makutano waliosimama karibu wakasikia, wakasema ya kwamba kulikuwa ngurumo; wengine walisema: Malaika amesema naye. Yesu akajibu, akasema: Sauti hii haikuwa kwa sababu yangu, lakini kwa sababu yenu. Sasa ni hukumu ya dunia hii; sasa mukubwa wa dunia hii atatupwa inje. Nami kama nikinyanyuliwa juu ya dunia, nitakokota watu wote kwangu. Alisema maneno haya, akionyesha ni mauti gani atakayukufa. Basi makutano wakamujubu: Sisi tumesikia katika torati ya kwamba Kristo anakaa hata milele; na namna gani unasema ya kama Mwana wa watu anapaswa kunyanyuliwa? Huyu Mwana wa watu ni nani? Basi Yesu akawaambia: Nuru ungali pamoja nanyi kwa saa kidogo. Mutembee mungali munayo ile nuru, giza lisiwashinde ninyi: sababu yeye anayetembea katika giza hajui pahali anapokwenda. Mungali muna nuru mwamini nuru, mupate kuwa wana wa nuru. Yesu alisema maneno haya, akaondoka akajificha kwao. Lakini hata alikuwa amefanya alama nyingi mbele yao, hawakumwamini: ili neno la nabii Isaya litimizwe alilolisema: Bwana, nani aliyeamini habari zetu? Na mukono wa Bwana amefunuliwa nani? Kwa sababu hii hawakuweza kuamini, kwa sababu Isaya alisema tena: Amepofusha macho yao, na amefanya migumu mioyo yao, Wasije wakakona kwa macho yao, wakafahamu kwa mioyo yao, Wakageuka, nikawaponyesha. Maneno haya aliyasema Isaya, kwa sababu aliona utukufu wake; na alisema habari zake. Lakini hata katika wakubwa wengi walimwamini, lakini kwa sababu ya Wafarisayo hawakukiri, wasije wakafukuzwa toka sunagtogi. Kwa maana walipenda sifa za watu kuliko sifa za Mungu. Yesu akapaza sauti, akasema: Yeye anayeniamini haniamini mimi tu, lakini yeye aliyenituma. Naye anayenitazama anamutazama yeye aliyenituma. Nimekuja niwe nuru katika dunia, ili mutu anayeniamini asikae katika giza. Na kama mutu akisikia maneno yangu, naye hayashiki simuhukumu: Kwa maana sikuja kuhukumu dunia, lakini kuokoa dunia. Yeye anayenikataa, na asiyepokea maneno yangu, ana mumoja anayemuhukumu; neno nililosema, lile litamuhukumu siku ya mwisho. Kwa sababu sikusema kwa mimi mwenyewe; lakini Baba aliyenituma alinipa amri ya maneno nitakayonena, na kuyasema. Na ninajua ya kama amri yake ni uzima wa milele; basi maneno haya ninayosema, ninayasema sawasawa Baba alivyoniambia.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

**ZABURI** 50(51)

## KANUNI

Sauti ya mbili WIMBO 3 HIRMOS
Umenisabitisha juu ya mwamba wa imani, ulinipa kushinda maadui zangu. Roho yangu inafurahiwa kukuimbia: Hakuna aliye mtakatifu kama wetu, hakuna aliya mwenyi haki kuliko wewe Bwana. *(mara mbili)*

Utukufu kwa Baba. . .
Mkusanyo wa wenyi majivuno, makafiri wanakusanyika kwa hii wazo mbaya ya kukuhukumu, ee Kristu Mkombozi wetu, wewe ambaye tanaimbia: Ni wewe Mungu wetu, hakuna aliye Mtakatifu ila wewe Bwana.

Sasa na siku zote. . .
Baraza mbaya ya makafiri kwa uasi juu ya Mungu inakusudia kumuua mwenyi haki kama muovu, Kristu ambaye tunaimbia: Ni wewe Mungu wetu, hakuna aliye Mtakatifu ila wewe Bwana.

**KATAVASIA**: Umenisabitisha juu ya mwamba. . . *(angalia yulu).*

**SHEMASI**: Ektenia ndogo.

**KONTAKION**. Sauti ya Ine.

Ewe Mwema kamili, nilikosa zaidi kupita mwanamuke mwenye zambi. Silete machozi, nasujudu, tena naomba kwa ukimya. Ninapojaa na mapendo nabusu miguu yako. Ee Rabi, umusamehee deni huyu mwenyi kukulalamikia: Ee Mwokozi uniondoe ku matope ya makosa yangu.

**IKOS**

Mwanamuke aliyepotea zamani mara moja akaonekana kuwa mwenyi akili, anachukia matendo ya haya ya zambi na furaha za dunia akiwaza haya ya hukumu na mateso yenyi kuwaongojea makahaba na washarati ambaye mimi ni wa kwanza, natetemeka, lakini zoezo inamizamisha katika upumbafu wangu. Mwanamuke mwenyi zambi yeye alitetemeka tena akaenda haraka kwako sababu ya kukulalamikia wewe Mkombozi wake: Ee mwenyi rehema kamili, ee mpenda wanadamu, uniondoe ku matope ya zambi zangu.

*Sinaksario Ya Watakatifu ya leo. Kisha tunasoma:*

Mu Kazi Tatu Takatifu na Mkubwa tunakumbuka ule mwanamuke wa zambi aliyepakaa manukato kichwa na miguu ya Bwana Yesu Kristu, mbele ya Mateso Yake. Ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu wewe, uliyepakaliwa manukato ya siri utuhuirumie sisi wenye zambi. kwani peke yako ni Mpenda- wanadamu. Amina.

WIMBO 8 HIRMOS

Kwa kutii amri ya mzulumu, wakawasha moto ya tanuru mara saba. Lakini vijana hawakuteketezwa, wao waliyozarau amri ya mfalme, wakalalamika: Enyi viumbe vyote vya Bwana, mwimbieni Bwana, msifuni milele.

Utukufu kwako, ee Mungu. . .

Ee Kristu, Mungu wa kuogopesha, mwanamuke aliyemwangia manukato ya bei mingi ku kichwa yako, akashika Miguu yako safi na mikono yake yenyi kuchafuka na akalalamika: Enyi viumbe vyote vya Bwana, mwimbieni Bwana, msifuni milele.

Tunamsifu Baba, Mwana na Roho Mutakatifu Bwana.

Mwanamuke mwenyi zambi ananawisha miguu ya Muumba na machozi yake tena anaipanguza na nywele zake. Alipotenda hivi akasamehewa makosa yote ya uzima wake. Analalamika: Enyi viumbe vyote vya Bwana, mwimbieni Bwana, msifuni milele.

Sasa na siku zote. . .

Fumbo ya kusamehe zambi inatimizika katika mwanamke mwenye kutubu, akitoa machozi yake na kupata rehema ya Mwokozi. Kwa kukiri kwake lakini analalamika: Enyi viumbe vyote vya Bwana, mwimbieni Bwana msifuni milele.

**KATAVASIA**: Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana: Kwa kutii amri ya mzulumu. . .

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tunamuheshimu kwa nyimbo na kumtukuza.

WIMBO 9 HIRMOS
Kujeni na roho safi na midomo yasipo kuchafuka, tumtukuzeni Mtakatifu kamili, Mama Mtakatifu kamili wa Emmanueli. Ni Yeye mwenyi kupeleka ombi letu kwa Mwana wake. Samehe roho zetu, ee Kristu Mungu, tena utuokoe.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu. . .
Asiye na shukrani, maskini mwenyi tamaa anahesabia bei ya manukato, hii zawadi stahili ya Mungu yenyi kulipa deni ya zambi zake; kwa hila yake Yuda anauzisha neema na mapendo ya Mungu. Samehe roho zetu, ee Kristu Mungu, tena utuokoe.

Utukufu Kwako, ee Mungu wetu. . .
Alipowaendea wakubwa wa makafiri, Yuda akawaambia: Mutanipa ninyi, nikiwatolea huyu Kristu munayetafuta? Akabadirisha ku zahabu ufariki wake na Kristu. Ee Bwana, samehe roho zetu na utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ni tamaa gani ilikupofusha. ewe YUda mbaya? Nani alikusahaulisha ile ulisikia: Watu wote si bure rohoni mwangu. Lakini ukakata kitumaini, ukajitundika, ewe mtoaji. Samehe roho zetu, ee Kristu Mungu, tena utuokoe.

**KATAVASIA**: Kujeni na roho safi. . .

**EKSAPOSTILARION**
Minaona chumba chako cha Arusi chenye kupambwa vizuri, ee Mwokozi wangu, na sina na mavazi ya kuingia nayo. Uangazie nguo ya nafsi yangu, ee Muletaji nuru na uniokoe. *(mara tatu)*

## MASIFU

**ZABURI** 148, **ZABURI** 149, **ZABURI** 150

Sauti ya kwanza
Ee Mwana wa Bikira, mwanamke mwenyi zambi akatambua ya kama wewe ni Mungu. Alitenda matendo yenyi kustahili machozi, akakuomba akilia: Fungua vifungo vya makosa yangu kama ninavyofungua nywele yangu; leta mapendo yako kwa huyu mwenyi kukupenda na mwenyi kustahili chuki, na nitakutangaza kwa watoza kodi, ee wewe Mwema tena mpenda wanadamu.

Kituo: Msifuni Bwana katika patakatifu pake, msifuni katika anga la uwezo wake.

Mwanamuke mwenyi zambi alichanganya machozi yake na manukato ya bei mingi na akayamwangia ku miguu yako Takatifu akayabusu, na ukamuhakikisha. Utusamehe, tena utuokoe, wewe uliyeteswa kwa ajili yetu.

Kituo: Msifuni kwa matendo yake makubwa, msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukubwa wake.

Wakati mwanamke mwenyi zambi alikuletea manukato, mfuasi wako yeye alisikilizana na makafiri; mwanamuke alifurahiwa kwa kukumwangia manukato ya bei mingi, mfuasi alienda haraka kuuzisha huyu asiye na bei, mwanamuke alimujua Bwana, mfuasi alitengana naye, mwanamuke alikombolewa, mfuasi yeye akawa mtumwa wa adui. Utoaji mbaya wa Yuda, toba

kubwa ya mwanamuke! Unipe hii toba, ee Mwokozi wangu, utuokoe, wewe uliyeteswa kwa ajili yetu.

Kituo: Msifuni kwa matoazi yanayolia, msifuni kwa matoazi yenye kuvuma sana. Kila mwenye pumzi amsifu Bwana.

Ole wake Yuda! Alimutazama mwanamuke mwenyi zambi akibusu miguu ya Bwana, lakini yeye aliwaza busu yake ya utoaji. Mwanamuke alifungua nywele zake, yeye alifungwa kwa hasira yake, akileta harufu mbaya ya ubaya wake pahali pa manukato. Ole wake Yuda! Ee Mungu, okoa roho zetu ku hii mateso.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya mbili
Mwanamuke mwenyi zambi alienda mbio kuuza manukato ya bei mingi sababu ya kumupakaa mfazili wake. Akamwambia mchuruzi: Unipe manukato ili nimupakae huyu alizima zote.

Sasa na siku zote. . . Sauti ya Sita
Ee Bandari ya wokovu, mwanamuke aliyezama katika zambi yake alipokupata, akakumwangia manukato yenyi kuchanganya na machozi yake, unitazame, wewe mwenyi kuongojea toba ya wakosefu! Ee Bwana, kwa rehema yako kubwa, uniokoe ku zambi zangu nyingi.

**DOKSOLOGIA KIDOGO**
**PADRI:** Tumazile ombi letu ku asubui kwa Bwana. . .

## APOSTIKHA

Sauti ya Sita
Leo Kristu anakuja nyumbani mwa mfarisayo na mwanamuke mwenyi zambi anangukia ku Miguu yake; anamusujudu akilalamika: Tazama huyu mwenyi kuzama katika zambi, tazama huyu mwenyi kukata matumaini sababu ya makosa yake, tazama huyu ambaye haukuchukizwa katika wema wako. Unisamehe zambi zangu na uniokoe, ee Bwana.

Kituo: Ee Bwana, asubui tulijazwa na rehema Yako tena tulifurahi. Tumefurahiwa siku zote za maisha yetu.

Ee Bwana, mwanamuke mwenyi zambi alikutolea nywele zake; Yuda akawanyoshea wasiyo na sheria mkono wake. Mwanamuke sababu ya kupata maondoleo ya zambi, Yuda sababu ya kupokea feza. Tunakulalamikia tena wewe uliyeuzishwa kwa kutukomboa: Ee Bwana, utukufu kwako.

Kituo: Tunaweza kufurahiwa kwa ajili ya siku tulizozarauliwa kwa ajili ya miaka tuliyoteswa. Tazama watumishi na viumbe vyako, ongoza wana wao.

Mwanamuke muovu tena mwenyi kuchafuka na zambi anajongea ku miguu yako akilia machozi anakuletea mapendo yake, ee Mwokozi, na anaungama mateso yako. Namna gani nitakunyanyulia macho yangu, ee Rabi? Umekuja wewe mwenyewe kumuokoa kahaba. Unifufue mimi kuzimuni ya mauti kama ulivyomufufua Lazaro kaburini kisha siku ine. Unipokee mimi maskini tena uniokoe, ee Bwana.

Kituo: Ninakusifu, ee Bwana, kwa moyo wangu wote, na ninaimba maajabu yako.

Mwanamuke aliyekata matumaini katika maisha yake akatambulikana kwa Bwana sababu ya mapendo yake, akaleta manukato, akakujongea na akalalamika: Usinitupe katika upotevu wangu, ee wewe aliyezaliwa kwa Bikira! Usizarau machozi yangu, ee wewe furaha ya Malaika! Unipokee mimi mwenyi kutubu, ewe Mwokozi wangu, kwa wema wako haukunikatae mimi mwenyi zambi.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . . Sauti ya Mnane

Ee Bwana, mwanamuke mwenyi zambi nyingi alipoona umungu wako, akachukua daraka ya Myrofori na anakuletea manukato mbele ya kuzikwa kwako. Analia akisema: Ole wangu, niko katika giza ya usharati, katika mapendo ya zambi ya giza, bila nuru. Pokea mawimbi ya machozi yangu, wewe uliyetokeza ku mawingu maji ya bahari. Inama ku malalamiko ya moyo wangu, wewe uliyeinamisha mbingu kwa umaskini wako wa kweli; ili niweze kubusu miguu yako takatifu kamili na kuipanguza na misokoto ya nywele zangu; hii miguu ambayo kwa muvuno ya upepo wa mangaribi ikamutetemesha Eva katika Paradizo na akajificha kwa woga. Nani atatazama hizi zambi zangu nyingi? Nani atapima urefu wa haki zako? Ee Mwokozi, Mkombozi wa roho! Usimzarau mtumishi wako, wewe ambaye rehema ni ya milele.

*Kisha, Padri:* Ni vema kumuungama Bwana. . . TRISAGION *na ingine desturi, sawa jana.*

## SAA YA TATU NA SAA YA SITA

*Ku Saa ya tatu kisha Zaburi za Saa kunafwata* ***KATHISMA*** *Kumi na Tisa; ku Saa ya Sita* ***KATHISMA*** *Makumi mbili. Ku Saa ya Tisa hakuna* ***KATHISMA****.*

*Ku Saa ya Sita Kisha Theotokion, kunafwata Tropari ya Unabii.*

Sauti ya Mbili

Leo baraza ya wadanganyifu inakusanyika na inakusudia mbaya juu yako. Leo Yuda anatangulia kujitundika kama faida ya uchuuzi wake. Kaifa anaungama ya kwamba wewe peke yako unaitikia mateso ya kutaka kwa ajili ya wote. Ee Mkombozi wetu, Kristu Mungu, utukufu kwako.

**PROKIMENON** Sauti ya mnane.

Zaburi 133 (134) Bwana akubariki toka Sayuni, yeye aliyeumba mbingu na dunia.

Kituo: Msifuni Bwana, enyi watumishi wote wa Bwana.

Somo la Unabii wa Ezekieli 2, 3-10 3, 1-27

Akaniambia: Mwana wa watu, ninakutuma kwa wana wa Israeli, kwa mataifa waasi walioniasi; wao na baba zao walinikosea, hata kufika leo. Nao wana hawana haya, nao ni wenye mioyo migumu; ninakutuma kwao; nawe utawaambia: Bwana Mungu anasema hivi. Nao, kama watasikia ao kama watakataa (maana wao ni nyumba ya kuasi), watajua hata hivi ya kama nabii amekuwa katikati yao. Nawe, mwana wa watu, usiwaogope, wala usiogope maneno yao, hata michongoma na miiba ikiwa pamoja nawe na unakaa katikati ya nge; usiogope maneno yao, wala usifazaike kwa nyuso zao hata wao ni nyumba ya kuasi. Na utawaambia maneno yangu, kama watasikia ao kama watakataa; maana wao ni waasi sana. Lakini wewe, mwana wa watu, sikia ninayokuambia; wewe usiwe mwenmye kuasi kama nyumba ile ya kuasi; fungua kinywa chako na kula ninachokupa. Na wakati nilipoangalia, tazama, mukono umenyoshwa kwangu, na tazama, gombo la kitabu lilikuwa ndani yake; akalitandika mbele yangu; limeandikwa ndani

na inje; maombolezo na huzuni na taabu ziliandikwa ndani yake. (3, 1-27) Akaniambia: Mwana wa watu, kula unachokuta; kula gombo hili, na kwenda, sema na nyumba ya Israeli. Hivi nikafungua kinywa changu, akanikulisha gombo. Akaniambia: Mwana wa watu, kulisha tumbo lako, na jaza matumbo yako na gombo hili ninalokupa. Halafu nikalikula; na lilikuwa kinywani mwangu kama asali kwa utamu. Akaniambia: Mwana wa watu, ondoka, kwenda kwa nyumba ya Israeli, na kuwaambia maneno yangu. Maana hukutumwa kwa taifa lenye kinywa kigeni, ama la lugha ya nguvu, lakini kwa nyumba ya Israeli; hapana kwa watu wengi wenye kinywa kigeni na lugha ya nguvu, maneno yao usiyoyaweza kufahamu. Hakika kama ningekutuma kwao, wangekusikiliza. Lakini nyumba ya Israeli hawatasikiliza; Kwa kuwa hawatanisikiliza; kwa maana nyumba nzima ya Israeli ni wagumu kwa kipaji cha uso na wenye moyo wa nguvu. Tazama, nimekufanya uso wako kuwa mugumu juu ya nyuso zao na kipaji chako kigumu juu ya vipaji vya nyuso zao. Kama almasi ngumu kuliko gumegume nimefanya kipaji cha uso wako; usiwaogope, wala usifazaike kwa nyuso zao, hata wao ni nyumba ya kuasi. Tena akaniambia: Mwana wa watu, maneno yangu yote nitakayokuambia, uyapokee moyoni mwako, na kuyasikia kwa masikio yako. Na ondoka, kwenda kwa wafungwa, kwa wana wa watu wako, useme nao na

kuwaambia: Bwana Mungu anasema hivi; kama watasikia ao kama watakataa. Halafu roho ikaninyanyua, nikasikia nyuma yangu sauti ya mushindo mukubwa ikisema: Utukufu wa Bwana ubarikiwe toka pahali pake. Nikasikia sauti ya mabawa ya viumbe hai wakati walipogusana, na sauti ya magurudumu kando yao, hata sauti ya mushindo mukubwa. Hivi roho ikaninyanyua na

kuniondosha; nikakwenda kwa uchungu, kwa moto wa roho yangu, na mukono wa Bwana ulikuwa juu yangu kwa nguvu. Halafu nikafika kwa wafungwa kwa Teli-Abibu waliokaa kando ya muto Kebari, na kwa pahali walipokaa, nikakaa pale katikati yao nikishangaa kwa siku saba. Na ilikuwa kwa mwisho wa siku saba, neno la Mungu likakuja kwangu likisema: Mwana wa watu, nimekuweka kuwa mulinzi juu ya nyumba ya Israeli; kwa hivi sikia neno kwa kinywa

changu uwape maonyo yanayotoka kwangu. Kama nikimwambia mwovu: Hakika utakufa; nawe humupi maonyo, wala huseni kwa kuonya mwovu kuacha njia yake ya uovu, kwa kuponyesha uzima wake; yule mwovu atakufa katika uovu wake; lakini damu yake nitataka mukononi mwako. Lakini kama ukionya mwovu, naye hageuki toka uovu wake, wala toka njia yake ya uovu, atakufa katika uovu wake; lakini umeponyesha nafsi yako. Tena, wakati mwenye haki anapogeuka toka haki yake, na anafanya uovu, na ninatia jiwe la kukwaza mbele yake, atakufa; kwa sababu wewe hukumupa maonyo, atakufa katika zambi yake, wala matendo yake ya haki aliyofanya hayatakumbukwa; lakini damu yake nitataka mukononi mwako. Hata hivi, kama ukionya mwenye haki, hata mwenye haki asikose, wala hatakosa, hakika ataishi, kwa sababu amepokea maonyo, nawe umeponyesha nafsi yako. Na mukono wa Bwana ulikuwa juu yangu pale; akaniambia: Simama, uende kwa inchi sawa; na nitasemezana nawe p[ale. Halafu nikaondoka, nikakwenda kwa inchi sawa, na tazama, utukufu wa Bwana ulisimama pale, kama utukufu nilioona kwa muto Kebari; nikaanguka kifudifudi. Halafu roho ikaingia ndani yangu, ikanisimamisha kwa miguu yangu; akasemezana nami na kuniambia: Kwenda ujifunge nyumbani mwako. Lakini wewe, mwana wa watu, watatia kamba juu yako na kukufunga nazo, wala hutatoka katikati yao; na nitafanyiza ulimi wako kuambatana na upande wa juu wa kinywa chako, uwe bubu, wala hutakuwa mwenye kuonya kwao; kwa kuwa wao ni nyumba ya kuasi. Lakini wakati ninaposemezana nawe, nitafungua kinywa chako na utawaambiaq: Bwana Mungu anasema hivi. Mwenye kusikia, asikie; na mwenmye kukataa, akatae; kwani wao ni nyumba ya kuasi.

**PROKIMENON** Sauti ya mbili.
Zaburi 134 (135) Enyi wote wenyi kumwogopa Bwana msifuni Bwana.
Kituo: Tukuzeni jina la Bwana, enyi wote watumishi wa Bwana.

# ESPERINOS NA LITURGIA YA VYENYI KUTAKASWA

Njooni, tumwinamia. . .
Zaburi 103 (104)

Ektenia Ukubwa
**KATHISMA** Kumi na Mnane.

TROPARIA YA MASIFU KWA SALA YA ASUBUI

Ee Mwana wa Bikira. . .
Mwanamuke mwenyi zambi. . .
Wakati mwanamuke mwenyi zambi. . .
Ole wake Yuda. . .
Mwanamuke mwenyi zambi alienda. . .
Ee bandari ya wokovu, mwanamuke aliyezama katika zambi yake. . .
Leo Kristu anakuja nyumbani mwa mfarisayo. . .
Ee Bwana, mwanamuke mwenyi zambi alikutolea mywele zake. . .
Mwanamuke muovu tena mwenyi kuchafuka na zambi. . .
Ee Bwana, mwanamuke mwenyi zambi nyingi. . .

**MWANGAZA UPOLE (ILARON)**

Somo la Unabii

**PROKIMENON** Sauti ya Ine.
Zaburi 135 (136). Msifuni Mungu wa mbingu, kwani Yeye ni mwema, kwa maana rehema yake ni ya milele.
Kituo: Msifuni Mungu wa miungu, kwa maana rehema yake ni ya milele.

Somo la Kitabu cha Kutoka 2, 11-22.
Na ilikuwa kwa siku zile wakati Musa alipokwisha kupata nguvu, akatoka kwa ndugu zake, akaangalia mizigo yao; akaona Mumisri akipiga Muebrania, mumoja wa ndugu zake. Akatazama huko na huko, na wakati alipoona hapana mutu, akapiga Mumisri, akamuficha ndani ya muchanga. Akatoka siku ya pili, na tazama, watu wawili wa Waebrania wakapigana; akamwambia yeye aliyekosa: Kwa nini unapiga jirani yako? Akasema: Nani aliyekuweka wewe mukubwa na mwamuzi huu yetu? Unafikili kuniua kama ulivyoua yule Mumisri? Musa akaogopa, akasema: Hakika neno hili limejulikana. Basi wakati Farao aliposikia neno hili, alitaka kuua Musa. Lakini Musa akakimbia toka uso wa Farao; akakaa katika inchi ya Midiani; akaketi kando ya kisima. Basi kuhani la Midiani alikuwa na binti saba; wakakuja kuteka maji, wakajaza mabirika kunywesha kondoo za baba yao. Wachungaji kondoo wakakuja, wakawafukuza; lakini Musa akasimama, akawasaidia na kunywesha kondoo zao. Na wakati walipokuja kwa Rueli baba yao, akasema: Namna gani mumekuja mbio leo? Wakasema: Mumisri alituponyesha toka mukono wa wachungaji, akatutekea maji vilevile na kunywesha kondoo. Akawaambia binti zake: Yeye ni wapi? Kwa nini muliacha mutu huyu? Mumwite ale chakula. Musa akafurahi kukaa na mutu yule; akamupa Musa Sipora binti yake. Akazaa mwana; akaita jina lake Gersomi, maana alisema: Nimekuwa mugeni katika inchi isiyo yangu.

**PROKIMENON** Sauti ya Ine.
Ee Bwana, rehema yako ni ya milele; usizarau kazi ya mikono yako.
Kituo: Nitamuungama Bwana kwa moyo wangu wote; nitakuimbia kwa Malaika wako.

*(Baraka ya Padri):* Nuru ya Kristu inangaza mwanadamu wote.

Somo la Kitabu cha Yobu 2, 1-10
Ilikuwa tena siku wakati wana wa Mungu walipokuja kujiweka mbele ya Bwana na Shetani alikuja katikati yao vilevile kujiweka mbele ya Bwana. Bwana akamwaambia Shetani: Unatoka wapi? Shetani akajibu Bwana, akasema: Ninatoka katika kuzungukazunguka duniani, na kutembea huku na huku ndani yake. Bwana akamwambia Shetani: Umeangalia mutumishi wangu Yobu? Maana hakuna mutu kama yeye duniani, mutu mukamilifu na haki, mwenye kuogopa Mungu, na kuepukana na uovu; naye angali anashikamana na utimilifu wake, hata ulipokuwa umenigeuza juu yake ili kumuharibu pasipo sababu. Shetani akajibu Bwana, akasema: Ngozi kwa ngozi, ndiyo, yote mutu aliyo nayo atatoa kwa ajili ya uzima wake. Lakini nyosha sasa mukono wako, na gusa mifupa yake na nyama yake, naye atakukufuru mbele ya uso wako. Bwana akamwambia Shetani: Tazama, yeye ni mukononi mwako; acha uzima wake tu. Basi Shetani akatoka mbele ya uso wa Bwana akapiga Yobu kwa majipu mabaya, toka wayo wa muguu wake hata utosi wa kichwa chake. Akatwaa kipande cha chungu kilichovunjika ili kujiparuza nacho; akaketi katikati ya majivu. Halafu muke wake akamwambia: Ungali unashikamana na utimilifu wako? Kufuru Mungu na kufa. Lakini akamwambia: Unasema kama mumoja wa wanawake wapumbafu anavyosema. NIni? Tupate mema mukononi mwa MUngu, nasi tusipate mabaya? Katika maneno haya yote Yobu hakukosa kwa midomo yake.

***PADRI** na **WAIMBAJI** wataimba sawa siku zingine hii wimbo:* " Maombi yangu ya elekezwe. .

Somo la Evangelio Matayo 26, 6-16
Basi wakati Yesu alipokuwa Betania, katika nyumba ya Simoni mukoma, mwanamuke mumoja akamukwendea, mwenye chupa cha marasi ya bei ya damani sana, akaimwanga juu ya kichwa chake wakati alipokuwa akiketi kwa chakula. Lakini wakati wanafunzi walipoona wakakasirika, wakisema: Kwa nini upotevu huu? Maana marasi hii ingaliweza kuunzwa kwa feza nyingi wakapewa masikini. Lakini Yesu akitambua, akawaambia: Kwa nini munataabisha mwanamuke? Maana ni kazi njema aliyonitendea. Kwa maana muna masikini pamoja nanyi siku zote; lakini hamuna mimi pamoja nanyi siku zote. Maana kwa kumwanga marasi hii juu ya mwili wangu, ameitenda kwa kunitayarisha kwa maziko yangu. Kweli ninawaambia ninyi, pahali po pote Habari Njema hii itakapohubiriwa katika dunia nzima, tendo hili alililitenda mwanamuke huyu litatajwa kwa ukumbusho wake. Halafu mumoja wa wale kumi na wawili aliyeitwa Yuda Iskariota, akakwendea wakubwa wa makuhani, akasemaq: Mutanipa mimi nini, nami nitamutoa mikononi mwenu? Wakamupimia vipande makumi tatu vya feza. Toka wakati ule alitafuta njia kumutoa mikononi mwao.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako

*Mfululizo wa Liturgia ya vyenyi kutakaswa.*

# SIKU YA INE MKUBWA

## SALA YA ASUBUI (ORTHROS)

*Msomaji: Trisagion. Eksapsalmos. Bwana ndiwe....na hii Apolitikion:*

Sauti ya Mnane

Wakati Wafuasi watukufu waliyooshwa miguu ku chakula cha karamu, walipokea nuru, kafiri, mgonjwa wakupenda feza, akajifunika giza. Akakutoa kwa waamzi waovu, wewe mwamzi wa haki. Ee ninyi wenyi kuwaza mali tazameni mwenyi tamaa anajitundika sababu ya mali. Ogopeni msifanane na roho isiyoweza kushibishwa iliyojaribu uovu wa hii namna juu ya Rabi wake. Wewe uliye Mwema kwa ajili ya mwanadamu wote, ee Bwana, utukufu kwako. *(mara tatu).*

*Hakuna* ***KATHISMA****.*

Somo la Evangelio kama ilivyoandikwa na Mtakatifu Luka 22, 1-39.

Na siku ya karamu ya mikate isiyotiwa chachu ilikuwa karibu, inayoitwa Paska. Wakubwa wa makuhani na waandishi walitafuta njia ya kumwua; kwa sababu waliogopa watu. Shetani akaingia Yuda, aliyeitwa Iskariota, naye alikuwa katika hesabu ya wale kumi na wawili. Akakwenda zake, akasema na wakubwa wa makuhani, na wakubwa wa askari, kwa njia gani atamutoa Yesu katika mikono yao. Wakafurahi, wakapatana kumupa feza. Akakubali, akatafuta nafasi kumutoa kwao kwa siri wakati makutano wasipokuwa karibu. Na siku ya mikate pasipo chachu ilifika ilipopasa kuchinja mwana-kondoo ya Pasaka. Akatuma Petro na Yoane, akisema: Kwendeni, mututengenezee Pasaka, tule. Wakamwambia: Unataka tuitengeneze wapi? Akawaambia: Tazama, wakati munapoingia muji, mutakutana na mwanamume anayebeba mutungi wa maji; mumufuate hata nyumba anapoingia. Na mutamwambia mwenye nyumba: Mwalimu anakuambia, chumba cha wageni ni wapi, pahali nitakapokula Pasaka pamoja na wanafunzi wangu? Na mutu yule atawaonyesha ninyi chumba kikubwa cha juu, na kimepambwa; kule wekeni vyote tayari. Walikwenda, wakaona kama alivyosema; wakatengeneza Pasaka. Saa ilipofika, akaketi pamoja na mitume yake kumi na wawili. Akawaambia: Kwa hamu kibwa nimetaka kula Pasaka hii pamoja nanyi mbele ya kuteswa kwangu. Kwani ninawaambia ninyi: Sitaikula tena kabisa hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. Akapokea kikombe, akashukuru, akasema: Twaeni hiki, mukagawanye katikati yenu; kwani ninawaambia ninyi, tangu sasa sitakunywa matunda ya muzabibu hata ufalme wa Mungu utakapokuja. Akatwaa mukate, akashukuru, akauvunja, akawapa, akisema: Huu ni mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi. Na tena kikombe nyuma ya kula, akisema: Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu inayomwangika kwa ajili yenu. Lakini tazama, mukono wake anayenitoa ni pamoja nami juu ya meza. Na kweli, Mwana wa watu anakwenda zake kama ilivyoamriwa; lakini ole wake yeye mutu yule, anayetolewa naye. Wakaanza kuulizana, ni nani katikati yao atakayefanya neno hili. Kulikuwa na mabishano katikati yao ni nani wao atakayekuwa mukubwa. Akawaambia: Wafalme wa Mataifa wanatawala juu yao; na wenye mamlaka juu yao wanaitwa wafanya uzuri. Lakini ninyi musiwe vile; lakini yeye aliye mukubwa katikati yenu, awe kama mudogo; naye aliye wa kwanza, kama yeye anayetumikia. Maana nani aliye mukubwa? Yeye anayeketi kwa chakula, ao yeye anayetumikia? Si yule anayeketi kwa chakula? Lakini mimi ni kati yenu kama mumoja anayetumikia. Ninyi wale walioshinda kukaa pamoja nami katika majaribu yangu. Nami ninawaweka ninyi ufalme, kama Baba yangu alivyoniwekea mimi, mupate kula na kunywa kwa meza yangu katika ufalme wangu, na kuketi juu ya viti vya ufalme, mukihukumu makabila kumi na mawili ya Israeli. Bwana akasema:

Simoni, Simoni, tazama Shetani amewataka awapepete ninyi kama ngano. Lakini nimekuombea, imani yako isipunguke; na wakati unapogeuka, usubutishe ndugu zako. Akamwambia: Bwana, mimi tayari kwenda pamoja nawe katika kifungo hata kufa. Akasema: Ninakuambia Patro jogoo hatawika leo hata unapokwisha kukana mara tatu ya kwamba hunijui. Akawaambia: Wakati nilipowatuma ninyi pasipo mufuko na ndaha na viatu, mulikosa kitu? Wakasema: Hapana. Halafu akawaambia: Lakini sasa mwenye mufuko autwae, na ndaha vilevile; naye asiye na upanga, auze vazi lake, anunue mumoja. Maana ninawaambia ninyi: Neno hili lililondikwa sharti litimizwe ndani yangu: Yeye alihesabiwa pamoja na wakosaji; sababu kuna mwisho wa maneno yale yaliyoandikwa juu yangu. Wakasema: Bwana, tazama, hapa ni panga mbili. Akawaambia: Inafaa. Akatoka kwenda zake hata kilima cha Zeituni kama alivyozobelea; wanafunzi wake wakamufuata.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwna, utukufu kwako.

**ZABURI** 50 (51)

## KANUNI

WIMBO 1 HIRMOS

Sauti ya Sita
Tawi lenyi kukauka linapaswa Bahari Nyekundu. Shimo la mawimbi limekauka. Pamoja ni njia ya watu tena kaburi ya waaskari. Wimbo ukaimbwa kwa Mungu. Amevaa utukufu, Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Hekima ya ndani ya Mungu, mwanzo wa vitu vyote tena mpaji wa uzima akajenga hekalu yake katika tumbo la Mama mtakatifu kamili asiyeolewa. Akatwaa mwili na amevaa utukufu, Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Hekima ya Mungu alipowafundisha marafiki zake mafumbo, anawatayarishia chakula cha kulisha roho yao. Akachanganya kikombe cha uzima wa milele kwa ajili ya waaminifu; tujongee na ibada tukilalamika: Amevaa utukufu, Kristu Mungu wetu, Mtukufu kamili.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Sisi wote waaminifu, tusikilize sauti ya hekima ya Mungu isiyoumbwa yenyi kutuita kwa hii mahubiri kubwa: Onjeni, anavyosema msikie ya kama mimi ni mpole. Lalamikeni: Kristu Mungu amevaa utukufu.

**KATAVASIA**: Tawi lenyi kukauka linapaswa Bahari. . .

WIMBO 3 HIRMOS
Ee Bwana wa vitu vyote, Mungu Muumba, mvumilivu, umejifanya maskini. Umeungana na kiumbe chako, wewe Paska ya wale uliyotaka kuwafia. Unajitoa kwao ukisema: Kuleni mwili wangu, mutasabitishwa katika imani.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mwema kamili, unajaza unawapa, wafuasi wako kikombe cha furaha chenyi kukomboa wanadamu, unajifanya wewe mwenyewe kuhani. Unasema: Kunyweni, mutasabitishwa katika imani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ee wewe usiye na zambi, uliwaambia Wafuasi wako: Mpumbafu ni huyu mtoaji aliye kati yenu. Hatatambua hivi vitu. Mpumbafu hataisikia. Ninyi, kaeni ndani yangu, mutasabitishwa katika imani.

**KATAVASIA**: Ee Bwana wa vitu vyote. . .

**SHEMASI**: Ektenia Kidogo.

**KATHISMA** Sauti ya kwanza
Huyu aliyeumba viziwa, mito na bahari anatuonyesha unyenyekevu kubwa. Anajifunga kitambaa kiuoni na anaosha miguu ya Wafuasi wake. Anajinyenyekeza kwa rehema yake ya milele tena, anatuamusha kuzimuni ya uovu, peke yake yeye mpenda wanadamu.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.
Kwa rehema yako ulijinyenyekeza na ukaosha miguu ya Wafuasi wako. Ukawatayarisha ku mashindano kimungu; Petro akatii ku amri yako takatifu. Wakati ulimuosha miguu, akakusihi utupe rehema yako kubwa.

Sasa na siku zote. . .
Ulikula pamoja na Wafuasi wako, ee Rabi, na kwa hii chakula uliwafunulia mafumbo ya sadaka yako takatifu kamili yenyi kutuokoa ku uharibifu, sisi wenyi kutukuza mateso yako takatifu.

WIMBO 4 HIRMOS
Ee Kristu, alipotambua fumbo yako isiyokadirika, nabii akisema: Ee Baba mwenyi rehema, ulifanya nguvu yako ya mapendo; ulituma, ee Mwema kamili, Mwana wako wa pekee katika dunia hii kama sadaka ya zambi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Ulipoenda katika mateso yako, ee chemchem isiyoteseka ya ukoo wa Adamu, ukawaambia marafiki zako, ee Kristu: Nilitaka kula hii Paska pamoja nanyi, kwani Baba alinituma mimi Mwana wake wa pekee duniani kama sadaka ya zambi.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Pakunywa kikombe, ee Msiyekufa, uliwaambia Wafuasi wako. Sitakunywa tena matunda ya mzabibu pamoja nanyi hapa chini, kwani Baba alinituma duniani hii kama sadaka ya zambi.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . .
Ee Bwana, uliwaambia marafiki zako: Nawaambia ninyi, ni divai mpya na
isiyokadirika mutakayokunywa pamoja nami katika ufalme wangu, mimi niliye Mungu wa miungu, kwani Baba alinituma duniani kama sadaka ya zambi.

**KATAVASIA**: Ee Kristu alipotabua. . .

WIMBO 5  HIRMOS

Walipoungama kwa mapendo na kujitolea kwa Kristu mfalme wa vitu vyote, Mitume wakaoshwa miguu yao takatifu itakayowaletea watu wote amani.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Hekima ya Mungu mwenyi kuzuia mawimbi ya kutisha ya maji ya angani, mwenyi kufunga uovu, mwenyi kukaza bahari, anatia maji katika kibakuli, Rabi anaoshwa miguu ya watumishi wake.

Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . .

Rabi anawaonyesha Wafuasi wake mfano wa unyenyekevu. Yeye mwenyi kuvika mbingu na mawingu, anajifunga kitamba kiunoni na anakunja magoti sababu ya kuosha miguu ya watumishi, yeye mwenyi kushika mkononi mwake pumzi ya wenyi hai wote.

**KATAVASIA**:  Walipoungama kwa mapendo. . .

WIMBO 6  HIRMOS

Ee Rabi, shimo ya mwisho ya zambi imeniangamiza, na nisipoweza kuvumilia zoruba yake, nakulalamikia kama Yona:  Uniondoe ku uharibifu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mwokozi, uliwaambia Wafuasi wako:  Munaniita Bwana na Rabi, ni mimi. Fanyeni hii munaona mimi nafanya.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Huyu msiyechafuka hahitaji kuoshwa miguu. Ninyi ni safi Wafuasi wangu, lakini si wote, kwani mmoja wenu anawazimu, ni mpumbafu.

**KATAVASIA**:  Ee Rabi, shimi ya mwisho. . .

**SHEMASI**:  Ektenia Kidogo

**KONTAKION**     Sauti ya mbili.

Mikono yake iliyopokea mkate mtoaji anainyosha kwa siri sababu ya kupokea bei ya huyu aliyeumba mwanadamu na mikono yake. Akakaa msiyeweza kusahihishwa, huyu Yuda mtumishi muongo.

**IKOS**

Tujongeeni na woga ku meza ya fumbo. Tupokeeni mkate na moyo safi, tukae karibu ya Rabi sababu ya kumuona akiosha miguu ya Wafuasi wake. Tufanye sisi pia hii tuliona ikifanyika, tukitii na kuosha miguu wamoja kwa wengine. Kwani Kristu aliwapa Wafuasi wake amri ya kufanya vivyo hivyo. Lakini haikusikilika kwa Yuda mtumishi muongo.

*Sasa tunasoma Sinaksario ya Watakatifu ya leo. Kisha tunasoma hii:*

Mukazi Ine Takatifu na Mkubwa Watakatifu wetu walitupatia kushangilia  siku Kuu ya Ine leo, nikusema: Ya kwanza:  Mashangilio ya Bwana Yesu kuosha miguu ya Wanafunzi wake, ya mbili, Karamu ya Siri, nikusema Bwana Yesu Kristu alitupatia Mwili na Damu Yake, ya tatu

Sala ya Bwana Yesu na ya ine utoaji wa mtoaji Yuda. Kwa Wewe wako kubwa, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

WIMBO 7 HIRMOS

Wana wa Babyloni hawakuogopa moto ya tanuru. Walipotupwa katikati ya moto wenye kufunikwa kwa umande, wakaimba: Umetukuzwa, ee Bwana, Mungu wa Baba zetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Alipotikisa kichwa Yuda akangukia katika uovu aliyokusudia. Alitafuta wakati wa kumtoa ahukumiwe huyu Mwamzi aliye Bwana wa wote tena Mungu wa baba zetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kristu aliwaambia marafiki zake: Mumoja wenu atanitoa. Wakashikwa na woga na uchungu; wakasahau furaha yao, wakasemezana: Ni nani basi, utuambieyo, ee Mungu wa baba zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ni huyu atachovya mkono wake pamoja nami katika sahani. Haikufazali yeye azaliwe. Mtoaji alitajwa kwa Mungu wa baba zetu.

**KATAVASIA**: Wana wa Babyloni. . .

WIMBO 8 HIRMOS

Wenyi heri vijana wa Babyloni waliposhindana na mauti sababu ya Sheria ya baba zao, wakazarau amri ya upumbafu ya mfalme. Walipoungana na moto usiyowateketeza, wakamwimbia mwenyezi wimbo wenyi kumstahili: Mtukuzeni Bwana, enyi viumbe vyake vyote. Msifuni milele.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Wenyi heri walikuwa wa Sayuni, Mitume wenye kuungana na neno la Mchungaji wao, walimufwata kama kondoo, na walipoungana naye, hawakutengana. Walipolishwa na neno kimungu, wakalalamika na shukrani: Mtukuzeni Bwana, enyi viumbe vyake vyote. Msifuni milele.

Tutukuzeni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Iskarioti mwenyi jina la machukizo anasahau amri za urafiki. Miguu uliyoosha inakutoa. Huyu alikula mkate wako, mwili wako Takatifu, ee Kristu, amekutekea mtego, yeye hakujua kulalamika: Mtukuzeni Bwana enyi viumbe vyake vyote. Msifuni milele.

Sasa na siku zote. . .

Yuda asiye na haya akapokea Mwili wenyi kukomboa zambi kwa Damu Takatifu iliyomwangika kwa ajili ya dunia. Hakusita kunywa hii Damu aliyouzisha kwa feza. Akasubutu kutukana na hakujua kulalamika: Mtukuzeni Bwana, enyi viumbe vyake vyote. Msifuni milele.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunasumjudu Bwana.

**KATAVASIA**: Wenyi heri vijana wa Babyloni. . .

**SHEMASI** ao **PADRI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tunamuheshimu kwa nyimbo na kumtukuza.

WIMBO 9  HIRMOS

Kujeni, enyi waaminifu, tufurahiwe na mapokeleo ya Rabi na ya chakula cha milele kilichotayarishwa katika chumba cha juu. Tunapofundishwa kwa Neno maana yake kubwa, tumtukuzeni na akili ya juu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Neno aliwaambia Wafuasi wake:  Nendeni mukatayarishe chakula katika chumba cha juu. Hii Paska yenyi kusabitisha roho itayarisheni katika fumbo, itayarisheni na mkate yasipo chachu ya ukweli, na tukuzeni nguvu ya neema.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Mimi ni mtu kweli apana mwenyi kuonekana; vivyo hivyo, ee badilisho ya ajabu, hali ninayo ni ya umungu. Tambueni basi ndani yengu Kristu mmoja tu mwenyi hali mbili safi ninaishi nazo na zilizo zangu.

**KATAVASIA**:   Kujeni, enyi waaminifu. . .

**SHEMASI**:   Ektenia kidogo.

EKSAPOSTIRARION.

Minaona chumba chako cha Arusi chenye kupambwa vizuri, ee Mwokozi wangu, na sina na mavazi ya kuingia nayo. Uangazie nguo ya nafsi yangu, ee Muletaji-nuru na uniokoe. *(mara tatu)*

## MASIFU

**ZABURI** 148,  **ZABURI** 149,  **ZABURI** 150.

Sauti ya mbili

Baraza ya Wayuda inakusanyika kwa kumtoa Muumba wa vitu vyote kwa Pilato. Enyi wakosefu, enyi watu wasiyo na sheria! Munamuhukumu mwamzi wa wenyi hai na waliokufa! Munamuzalumu huyu mwenyi kuponyesha mateso. Ee Bwana mvumilivu, rehema yako ni kubwa, utukufu kwako.

Kituo:   Msifuni kwa sauti ya baragumu. Msifuni kwa kinanda na kinubi.

Ee Bwana, wakati wa karamu Yuda kafiri alichovya mkono wake pamoja nawe katika sahani; akanyosha hii mkono kwa watu wasiyo na sheria sababu ya kupokea feza. Alijua kuhesabia bei ya manukato lakini hakuogopa kukuuzisha wewe hazina yasipo bei. Alinyosha miguu yake kwa kuiosha; akampa Rabi busu ya uongo sababu ya kumtoa kwa makafiri; alipokataliwa ku kundi la

Mitume, akatupa mbali yake ile feza makumi matatu na hakuona Ufufuo wako wa siku ya tatu. Ee Bwana mfufuliwa, utuhurumie.

Kituo:  Msifuni kwa ngoma na michezo, msifuni kwa nzenze na filimbi.

Yuda mtoaji na mdanganyifu alimtoa Mwokozi kwa busu ya uwongo. Rabi wa vitu vyote akauzishwa kwa makafiri kama mutumwa. Na yeye Mwana kondoo wa Mungu, akamfuata kama Mwana-Kondoo mwenye kwenda kutolewa sadaka, yeye Mwana wa Baba, peke yake mwenye huruma.

Kituo: Msifuni kwa matoazi yanayolia, msifuni kwa matoazi yenye kuvuma sana. Kila mwenye pumzi amsifu Bwana.

Yuda mtumishi muongo, mfuasi mwenye fitina, rafiki ya shetani aliyemfwata Rabi akatayarisha utoaji kwa siri, akasemezana ndani yake mwenyewe: Nitamtoa na nitapata feza. Alitafuta pia kuuzisha manukato na kumkamata Yesu kwa werevu; akampa busu yake na akamtoa Kristu. Na Bwana akamufwata kama mwana-kondoo mwenye kwenda kutolewa sadaka, peke yake mwema, peke yake mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Mwana-Kondoo aliyetanganiziwa na Nabii Isaya anaenda kutolewa sadaka kwa kutaka kwake na anatoa mgongo wake ku mapigo, machafu yake ku makofi. Hafiche Uso wake ku haya ya kutemewa mate, anahukumiwa ku lufu ya haya. Huyu asiye na zambi anaitikia yote kwa kutaka kwake sababu ya kuwafufua wote katika wafu.

**DOKSOLOGIA KIDOGO**

**PADRI**: Tumalize ombi letu. . .

## APOSTIKHA

Sauti ya Mnane

Leo baraza ya waovu inakusanyika juu ya Kristu, na kwa majivuno yao wanakusudia kumtoa msiye na zambi kwa Pilato sababu amuuwe. Leo feza inamuua Yuda anayepoteza uzima mara mbili, uzima wa mwili na uzima wa roho. Leo kaifa anatabiri bila kutaka. Afazali mutu mmoja afe kwa ajili ya watu wote. Alikuja kuteswa kwa ajili ya zambi zetu, sababu ya kutukomboa ku utumwa wa adui, kwani yeye ni Mwema tena mpenda-wanadamu.

Kituo: Huyu anayekula chakula changu amegeuka kuwa adui yangu.

Leo Yuda anatupia mbali mapendo ya uongo juu ya maskini, anafunua uso wa tamaa. Hashurulikie maskini, hatafute kuuzisha manukato ya mwanamuke mwenye zambi, lakini anauzisha manukato ya mbinguni na anajitwalia feza. Anaenda mbio kwa Wayuda, anawaaminia hawa watu wasiyo na sheria: Mutanipa ninyi kama nikiwatoleaye? Ee tamaa ya mtoaji! Nauzisha hazina ku bei raisi, anamaliza mambo kwa mapenzi ya wamunuzi; hatake bei mingi: Nauzisha

Bwana kama mtumwa mwenyi kukimbia. Wezi wanatupa daima ile iliyo ya bei mingi. Leo mfuasi anawatupia imbwa huyu aliye Mtakatifu. Furaha ya tamaa inamusirikisha juu ya Rabi wake. Tukimbieni hii kishawishi na tulalamikeni: Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

Kituo: Akatoa na akasemezana juu yake.

Kipimo cha utoaji wako kimejaa, ewe Yuda kafiri, ugonjwa wa tamaa unakuongoza ku chuki. Kama ulipenda mali, sababu gani ulimufwata huyu aliyehubiri umaskini? Kama alimpenda Bwana, sababu gani ulimuuzisha yeye asiye na bei? Ulinitoa ku lufu. Tetemeka, ee jua lalamika, ee dunia na kwa mahangaiko yako lalamika. Ee Bwana wa wema, utukufu kwako.

Kituo: Wamenishindanisha na neno la uovu.

Enyi waaminifu, hata mumoja asijongee kama hatayarishwe ku fumbo ya karamu; hata mumoja asijongee kama Yuda ku Meza Takatifu sababu ya kudanganya. Yeye alipopokea sehemu yake akajitenga ku Mkate wa uzima. Akaonekana kuwa mfuasi lakini kwa matendo yake ni muuaji. Alikula pamoja na Mitume na alifurahiwa pamoja na Wayuda. Kwa chuki yake akakubusu na kwa hii busu akakuuzisha wewe uliyetukomboa ku laana, ewe Mungu na Mwokozi wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . . . Sauti ya Tano

Ee Bwana, uliwafundisha Wafuasi wako kwa hii maneno: Ee rafiki zangu, kesheni! Woga wowote usiwatenge ninyi kwa mimi. Mateso ninayoteswa ni kwa ajili ya dunia. Musihangaike kwa ajili yangu, kwa sababu sikuja kusaidiwa lakini kusaidia na kutoa uzima wangu kwa kukomboa ulimwengu. Kama ninyi ni rafiki zangu fanyeni kama mimi. Anayetaka kuwa wa kwanza awe wa mwisho. Bwana awe mtumishi;kaeni ndani yangu mutazaa matunda kwani mimi ni mzabibu wa uzima. Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako, ewe aliye-juu, kutangaza alfajiri rehema yako na ukweli wako usiku kucha.

**PADRI**: Ni vema kumuungama Bwana, . . .

**MSOMAJI**: TRISAGION

Wimbo:

Wakati Wafuasi watukufu walipokea nunu kisha kuoshwa miggu ku chakula cha karamu Yuda kafiri mgonjwa wa kupenda feza akajifunika giza. Akakutoa kwa waamzi waovu, wewe Mwamzi wa haki. Ee ninyi wenyi kuwaza utajiri, tazameni mwenyi tamaa anajitundika sababu ya mali. Ogopeni, msifanane na roho isiyoweza kushibishwa iliyojaribu uovu wa hii namna juu ya Rabi yake. Wewe uliye mwema kwa ajili ya mwanadamu wote, ee Bwana, utukufu kwako.

# SAA YA KWANZA

Tropari ya Unabii, Sauti ya tatu

Ee Bwana, bila hasira ulipigwa makofi kwa ajili ya wanadamu, okoa uzima wetu ku uharibifu na utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . .

Okoa, ee Bwana, uzima wetu ku uharibifu na utuokoe.

Sasa na siku zote. . . .

Ee Bwana, bila hasira ulipigwa makofi kwa ajili ya wanadamu, okoa uzima wetu ku uharibifu na utuokoe.

**PROKIMENON** Sauti ya kwanza

Mataifa yote yajue ya kama jina lako ni Bwana

Kituo: Ee Mungu wangu, nani anaweza kuwa kama wewe.

Somo la Unabii wa Yeremia 11, 17-23 na 12, 1-15.

Kwa maana Bwana wa majeshi, aliyekupanda, amesema mabaya juu yako, kwa sababu ya maovu ya nyumba ya Israeli, na ya nyumba ya Yuda, waliyoyatenda juu ya nafsi zao wenyewe kwa kunikasirisha, wakifukizia Bali uvumba. Tena Bwana akanijulisha maneno haya, nami nikajua; halafu ulinionyesha matendo yao. Lakini mimi nilikuwa kama mwana-kondoo mupole anayechukuliwa kwenda kuchinjwa; wala sikujua ya kuwa wamefanya mashauri juu yangu, wakisema: Tuharibu muti pamoja na matunda yake, na tumukatilie mbali atoke katika inchi ya walio hai, ili jina lake lisikumbukwe tena. Lakini, ee Bwana wa majeshi, unayehukumu haki, unayejaribu viuno na moyo, nione malipizo yako juu yao; kwa maana nimekufunulia wewe neno langu. Basi ndivyo anavyosema Bwana juu ya watu wa Anatoti, wanaotafuta uhai wako, wakisema: Usifanye unabii kwa jina la Bwana, usife kwa mukono wetu. Kwa sababu hii Bwana wa majeshi anasema hivi: Tazama, nitawaazibu watu hawa; vijana watakufa kwa upanga; wana wao na binti zao watakufa kwa njaa; wala hapatakuwa na mutu atakayebaki kwao; maana nitaleta mabaya juu ya watu wa Anatoti, mwaka wa kuangaliwa kwao. (12, 1-15) Wewe ni mwenye

hakim ee Bwana, wakati ninapoulizana nawe, lakini nitasema nawe katika habari za haki. Kwa nini ya wabaya inasitawi? Kwa nini wote wanaotenda hila wanakaa salama? Umewapanda, hata wametia mizizi; wanasitawi, mupaka wanazaa matunda; katika vinywa vyao wewe ni karibu,

lakini katika mioyo yao wewe ni mbali. Lakini wewe, Bwana, unanijua mimi; umeniona, umejaribu moyo wangu, namna unavyokutegemea; uwakokote kama kondoo wanaokwenda kuchinjwa, uwaweke tayari kwa siku ya kuchinjwa. Hata wakati gani inchi itaomboleza, na majani ya inchi yote kukauka? kwa ajili ya mabaya yao wanaokaa ndani yake, nyama wameangamia na ndege pia; kwa sababu walisema: Hataona mwisho wetu. Kama ikiwa umepiga mbio pamoja nao wanaokwenda kwa miguu, nao wamekuchokeza, basi unaweza namna gani kushindana na farasi? na hata katika inchi ya utulivu wewe una salama, utafanya nini hapa katika mafuriko ya Yorodani? Kwa maana hata ndugu zako, na nyumba ya baba yako, wamekutenda mambo ya hila; ndiyo, wamepiga kelele nyuma yako; usiwasadiki, hata wakikuambia mema. Nimeacha nyumba yangu, nimetupa uriti wangu; nimetia mupenzi wangu katika mikono ya adui zake. Uriti wangu umekuwa kwangu kama simba polini; ametoa sauti juu yangu; kwa sababu hii nimemuchukia. Uriti wangu umekuwa kwangu kama ndege mwenye madoadoa, ndege wakali wanamuzunguka pande zote; kwendeni, kusanyeni pamoja nyama zote za poli, muwalete ili wale. Wachungaji wengi wameharibu shamba langu la mizabibu, wakakanyaga fungu langu chini ya miguu yao, wamefanya fungu langu zuri kuwa jangwa la ukiwa. Wamelifanya kuwa ukiwa, na kwa kuwa ni ukiwa linanililia; inchi yote imefanywa kuwa ukiwa, kwa sababu hapana mutu aliyeweka maneno haya moyoni mwake. Wenye kuharibu inchi wamepanda juu ya milima katika hangwa; kwa maana upanga wa Bwana utakula toka upande mumoja wa inchi hata upande wa pili wa inchi; hapana mwenye mwili atakayekuwa na salama. Wamepanda mgano, lakini watavuna miiba; wameumiza nafsi zao, lakini hawatakuwa na faida; na mutapata haya kwa ajili ya matunda yenu, kwa sababu ya kasirani kali ya Bwana. Bwana anasema hivi juu ya jirani zangu zote walio wabaya, wanaogusa uriti wangu nilioritisha watu wangu Israeli: Tazama, nitawangoa katika inchi yao, nami nitangoa nyumba ya Yuda isiwe kati yao. Tena itakuwa nyuma ya kuwangoa, nitarudi na kuwahurumia; nami nitawaleta tena, kila mutu aingie katika uriti wakem na kila mutu aingie katika inchi yake.

**PROKIMENON**. Sauti ya Sita.

**PADRI**: Kuaga.

## SAA YA TATU, SAA YA SITA, SAA YA TISA

WIMBO.

Wakati Wafuasi watukufu walipokea nuru kisha kuoshwa miguu ku chakula cha karamu, Yuda kafiri, mgonjwa wa kupenda feza akajifunika giza. Akakutoa kwa waamzi, wewe Mwamzi wa haki. Ee ninyi wenyi kuwaza utajiri, tazameni mwenyi tamaa anajitundika sababu ya mali. Ogopeni, msifanane na roho isiyoweza kushibishwa iliyojaribu uovu wa hii namna juu ya Rabi wake. Wewe uliye Mwema kwa ajili ya mwanadamu wote, ee Bwana, utukufu kwako.

**KONTAKION**

Mikono yake iliyopokea mkate mtoaji anainyosha kwa siri sababu ya kupokea bei ya huyu aliyeumba mwanadamu na mikono yake. Akakaa msiyeweza kusahihishwa, huyu Yuda mtumishi muongo.

# SALA YA MANGARIBI ( ESPERINOS)

Uhimidiwe Ufalme wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI**: Amina.

**MSOMAJI**: Njooni, tumwinamia na tumsujudu Mungu Mfalme wetu.
Njooni, tumwinamia na tumsujudu Kristu Yeye Mungu Mfalme wetu.
Njooni, tumwinamia na tumsujudu yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI** 103 (104)
ZABURI YA MANGARIBI: Bwana nimekuita. . .

Sauti ya mbili.
Wimbo ya Orthros

Baraza ya Wayuda. . . *(mara ya pili)*
Ee Bwana wakati wa karamu Yuda kafiri. . .
Yuda mtoaji na ndaganyifu. . .
Yuda mtumishi muongo. . .
Mwana kondoo aliyetangaziwe na Nabii Isaya. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Sauti ya Sita
Kweli, kweli, Yuda ni wa kizazi cha nyoka, wa kizazi cha wale waliyokula maana jangwani na wakamunungunikia mfazili, watu wasiyo na shukrani walikuwa tena na chakula kinywani mwao wakati walimunungunikia Mungu. Yeye kafiri, mkate wa mbinguni kinywani mwake, akatayarisha kumtoa Mwokozi. Ee mwenyi tamaa, ee muovu! Anauzisha huyu mwenyi kumulisha; anamtoa Rabi wake ku lufu akimubusu. Kweli mtoaji ni wa hii kizazi, anariti upotevu pamoja nao. Lakini wewe, ee Bwana, linda roho zetu ku hii uovu, wewe ambaye uvumilivu ni usiyiweza kusemwa.

**MWANGAZA UPOLE (ILARON)**

**SHEMASI**: Mangaribi ( Esperas) **PROKIMENON**

Sauti ya kwanza. **ZABURI** 139 (140)
Ee Bwana, uniokoe kwa muovu na uniopoe ku uzulumu.
Kituo: Huyu ambaye moyoni mwake anafikiri uongo wa siku nzima.

Somo la kitabu cha Kutoka 19, 10-19
Bwana akamwambia Musa: Kwenda kwa watu, uwatakase leo na kesho, na wavue mavazi yao, hata wawe tayari siku ya tatu; maana siku ya tatu Bwana atashuka kwa macho ya watu wote juu ya mulima Sinai. Na utaweka mipaka kwa watu pande zote ukisema: Mujiangalie wenyewe musipande mulima wala kugusa mupaka wake; mutu anayegusa mulima, hakika atauawa; mukono hautaugusa, lakini hakika atatupiwa mawe, ao kutobolewa; akiwa nyama ao mutu, hakika hataishi; wakati baragumu inapolia wakati murefu, halafu watapanda kwa mulima. Musa akaskuka toka mulima kwa watu, akatakasa watu; wakavua mavazi yao. Akawaambia watu:

Muwe tayari kwa siku ya tatu; musikaribie mwanamuke. Na ilikuwa siku ya tatu, wakati ilipokuwa asubui, zilikuwa radi na lalo, na wingu zito juu ya mulima, sauti ya baragumu nguvu sana; watu wote waliokuwa kambini wakatetemeka. Musa akatoa watu toka kambi kukutana na

Mungu; wakasimama kwa upande wa chini wa mulima. Mulima Sinai muzima ukatoa moshi, kwa sababu Bwana alishuka juu yake katika moto; moshi wake ukapanda kama moshi wa tanuru, mulima muzima ukatetemeka sana. Na wakati sauti ya baragumu ilipozidi kulia nguvu sana, Musa akasema, Mungu akamujibu kwa sauti.

**PROKIMENON** Sauti ya Saba.

Uniokoe kwa maadui zangu, ee Mungu, na uniopoe kwa wale wenye kusimama juu yangu.

Kituo: Uniopoe kwa wale wenye kutenda uovu.

Somo la Kitabu cha Yobu 38, 1-23 na 42, 1-6

Halafu Bwana akajibu Yobu toka upepo wa kuzunguka, akasema: Ni nani huyu anayetia mashauri giza kwa maneno yasiso na maarifa? Basi funga viuno vyako kama mwanamume, maana nitakuuliza neno, nawe uniambie. ULikuwa wapi wakati nilipoweka misingi ya dunia? Uniambie kama ukiwa na ufahamu. Ni nani aliyeamuru vipimo vyake, kama ukijua? Ao nani aliyenyosha kamba juu yake? Misingi yake ilifungwa juu ya nini? Ao ni nani aliyeweka jiwe lake

la pembeni; Wakati nyota za asubui walipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha? Ao ni nani aliyefunga bahari kwa milango, wakati inapofurika kama kwamba imetoka tumboni; wakati nilipofanya wingu kuwa vazi lake, na giza zito kuwa nguo ya kuifungia, na kuiagiza amri yangu, na kuweka makomeo na milango, nikasema: Utafika mupaka hapa; lakini hutapita; na hapa mawimbi yako ya majivuno yatazuizwa? Wewe uliamuru asubui tangu mwanzo wa siku zako, na kujulisha mapambazuko pahali pake; ili yapate kushika miisho ya inchi, na waovu wakungutwe mbali nayo? Yanabadiliswa kama udongo chini ya muhuri. Na vitu vyote vinatokea kama vazi; na waovu wanazuizwa nuru yao, na mukono ulionyanyuliwa unavunjika. Wewe uliingia chemchemi za bahari? Ao umetembea juu ya pahali pa siri ya vilindi? Malango ya mauti yamefunuliwa kwako? Ao umeona malango ya kivuli cha mauti? Umefahamu upana wa dunia? Uniambie kama ukijua maneno haya yote. Na wapi njia kwa kufika kwa makao ya nuru, na giza, pahali pake ni wapi: Upate kulipeleka hata mupaka wake, upate kufahamu njia inayokwenda kwa nyumba yake? Hakika unajua, maana umezalia wakati huu, na hesabu ya siku zako ni kubwa! Umeingia nyumba za hazina ya theluji, ao umeona nyumba za hazina ya mvua ya mawe, nilizoziweka akiba kwa wakati wa matata, kwa siku ya mapigano na vita? (42, 1 6)Halafu Yobu akajibu Bwana, akasema: Ninajua, unaweza kufanya mambo yote, na ya kama makusudi yako hayawezi kuzuizwa. Ni nani anayeficha mashauri pasipo maarifa? Kwa hivi nimesema maneno nisiyofahamu, mambo ya ajabu kunishinda mimi nisiyoyajua. Sikia, ninakusihi, nami nitasema; nitakuuliza, nawe uniambie. Nilisikia habari zako kwa kusikia kwa masikio; lakini sasa jicho langu limekuona, kwa hivi ninachukia nafsi yangu, na

ninatubu katika mavumbi na majivu.

Hakuna **PROKIMENON**

Somo la Unabii wa Isaya 50, 4-11

Bwana Mungu amenipa ulimi wa wale wanaofundishwa, nipate kujua namna ninavyoweza kumusaidia kwa maneno yangu yule aliyechoka. Ananiamsha asubui nyuma ya asubui, anaamsha sikio langu kusikia kama watu wanaofundishwa. Bwana Mungu amefungua sikio langu, na sikukataa wala sikurudi nyuma. Niliwatolea mugongo wangu wale wenye kupiga, na mashavu yangu wale wanaongoa ndevu; sikuficha uso wangu usipate haya na kutemewa mate. LakiniBwana Mungu atanisaidia: Kwa sababu hii sitapata haya; kwa sababu hii nimekaza uso wangu kama jiwe gumu, nami ninajua ya kuwa sitaona haya. Yeye anayenihesabu kuwa na haki ni karibu; ni nani atakayeshindana nami? Tusimame pamoja; ni nani aliye adui yangu?

anikaribie. Tazama, Bwana Mungu atanisaidia; ni nani atakayenihukumu kuwa mukosaji? Tazama, wale wote watachakaa kama vazi; nondo atawakula. Ni nani katikati yenu anayeogopa Bwana, anayetii sauti ya mutumishi wake? anayetembea katika giza, wala hana nuru, aamini jina la Bwana, na ategemee Mungu wake. Tazama, ninyi wote munaogonga moto, munaojifunga pande zote na mienge: mutembee katika nuru ya moto wenu, na katikati ya mienge muliyowasha. Mutapata maneno haya kwa mukono wangu: mutalala kwa huzuni.

**SHEMASI**: Ektenia kidogo

TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . . *(mara tatu),* (*tunaiimba sawa mu Juma),* Utukufu. . . Sasa. . . Nguvu ( Dinamis) Mungu Mutakatifu. . .

**PROKIMENON** Sauti ya Saba
Watawa wa watu wamekusanyika juu ya Bwana na juu ya Kristu wake.
Kituo: Sababu gani mataifa yanatetemeka, na watu wanafanya mashauri ya bure?

Somo la Barua 1 Korinto 11, 23-32
Kwa sababu nilipokea kwa Bwana nilivyowatolea ninyi vilevile, ya kwamba, Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mukate; akashukuru, akauvunja, na alisema: Twaeni, kuleni, huu ni mwili wangu, uliovunjika kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi. Vivyo hivyo alitwaa kikombe, nyuma ya kula, akisema: KIkombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni
hivi, kila mara munapokunywa kwa kunikumbuka mimi. Kwa sababu kila mara munapokula mukate huu, na kunywa kikombe hiki, munatangaza kufa kwa Bwana hata atakapokuja. Basi kila mwenye kula mukate huu na kunywa kikombe cha Bwana, isivyostahili atakuwa amejipatia kosa juu ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mutu ajihukumu mwenyewe, na kisha apate kula mukate na kunywa kikombe. Kwa sababu yeye anayekula na kunywa, asipostahili, anakula na kunywa hukumu kwake mwenyewe, asipotambua mwili wa Bwana. Kwa sababu hii wengi kwenu ni zaifu na wagonjwa, na wengi wamelala. Lakini kama tungejihukumu sisi wenyewe, tusingehukumiwa. Lakini wakati tunapohukumiwa, tunaazibiwa na Bwana, kusudi tusihukumiwe pamoja na dunia.

**WAIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

Sauti ya Sita
Kituo: Heri huyu mwenyi kutunza maskini; kwa maana siku ya mwisho Bwana atamuokoa.
Kituo: Adui zangu wamesema juu yangu: Wakati gani atakufa? Wakati gani jina lake litapotea?
Kituo: Huyu anayekula chakula changu amegeuka kuwa adui yangu.

**PADRI**: Hekima. Simameni.

Somo la Evangelio Matayo 26, 2-39 Yoane13, 3-17; Luka 22, 43-45; Matayo 26, 40-75; Matayo 27, 1-5
Munajua ya kama nyuma ya siku mbili Pasaka inakuja, na Mwana wa watu atatolewa asulubiwe. Halafu wakakusanyika wakubwa wa makuhani, na wazee wa watu kwa kiwanja cha kuhani mukubwa aliyeitwa Kayafa; wakafanya shauri ili wakamate Yesu kwa hila na kumwua. Lakini wakasema: Si kwa wakati wa siku kubwa ili kelele lisitokee katika watu. Basi wakati Yesu alipokuwa Betania, katika nyumba ya Simoni mukoma, mwanamuke mumoja akamukwenda, mwenye chupa cha marasi ya bei ya damani sana, akaimwanga juu ya kichwa chake wakati alipokuwa akiketi kwa chakula. Lakini wakati wanafunzi walipoona wakakasirika,

wakasema: Kwa nini upotevu huu? Maana marasi hii ingaliweza kuuzwa kwa feza nyingi, wakapewa masikini. Lakini Yesu akitambua, akawaambia: Kwa nini munataabisha mwanamuke? Maana ni kazi njema aliyonitendea. Kwa maana muna masikini pamoja nanyi siku zote; lakini hamuna mimi pamoja nanyi siku zote. Maana kwa kumwanga marasi hii juu ya mwili wangu, ameitenda kwa kunitayarisha kwa maziko yangu. Kweli ninawaambia ninyi, Pahali po pote Habari Njema hii itakapohubiriwa katika dunia nzima, tendo hili alilolitenda mwanamuke huyu litatajwa kwa

ukumbusho wake. Halafu mumoja wa wale kumi na wawili aliyeitwa Yuda Iskariota, akakwendea wakubwa wa makuhani, akasema: Mutanipa mimi nini, nami nitamutoa mikononi mwenu? Wakamupimia vipande makumi tatu vya feza. Toka wakati ule alitafuta njia kumutoa mikononi mwao. Basi kwa siku ya kwanza ya mikate pasipo chachu, wanafunzi wakakwendea Yesu wakisema: Ni wapi unapotaka tukutengenezee upate kula Pasaka? Akasema: Kwendeni mujini kwa mutu fulani mukamwambie: Mwalimu anasema, Wakati wangu ni karibu; kwako nitafanya Pasaka pamoja na wanafunzi wangu. Wanafunzi wakafanya kama Yesu alivyowaagiza; wakatengeneza Pasaka. Basi wakati mangaribi ilipokuja, akaketi kwa chakula pamoja na wanafunzi wale kumi na wawili; na wakati walipokuwa wakikula akasema: Kweli ninawaambia ninyi, Mumoja wenu atanitoa. Wakahuzunika sana, wakaanza kumwambia mumoja mumoja: Ni mimi Bwana? Akajibu, akasema: Yeye anayechovya pamoja nami katika sahani, ni huyu atakayenitoa. Mwana wa watu anakwenda zake, kama ilivyoandikiwa juu yake, lakini ole wake mutu yule anayetoa Mwana wa watu! ingalikuwa heri kwake yule mutu kama asingalizaliwa. Yuda aliyemutoa, akajibu, akasema: Ni mimi, Rabi? Akamwambia: Wewe umesema. Na wakati walipokuwa wakikula, Yesu akatwaa mukate, akaubariki na kuuvunja; akawapa wanafunzi, akasema: Twaeni mule; huu ni mwili wangu. Akatwaa kikombe akashukuru, akawapa akisema:

Kunyweni, ninyi wote, kwa maana hii ni damu ya Agano iliyomwangika kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la zambi. Lakini ninawaambia ninyi, Sitakunywa matunda ya mizabibu tangu sasa hata siku ile nitakapokunywa mapya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu. Na wakati walipokwisha kuimba, wakatoka inje kwenda mulima wa Mizeituni. Halafu Yesu akawaambia: Ninyi wote mutaanguka kwa ajili yangu usiku huu; kwa sababu imeandikwa: Nitapiga muchungaji, na kondoo za kundi watasambazwa. Lakini nyuma ya ufufuko wangu nitawatangulia ninyi kwenda Galilaya. Lakini Petro akajibu, akamwambia: Hata wote wakianguka kwa ajili yako, mimi sitaanguka kamwe. Yesu akamwambia: Kweli ninakuambia ya kama usiku huu mbele ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu. Petro akamwambia: Hata ikinipasa kufa pamoja nawe, sitakukana kabisa. Na wanafunzi wote walisema vilevile. Kisha Yesu akakwenda pamoja nao hata pahali pamoja jina lake Getesemane, akawaambia wanafunzi wake: Ketini hapa angali ninapokwenda kule kuomba. Akatwaa Petro na wana wawili wa Zebedayo pamoja naye, akaanza kuhuzunika na kufazaika sana. Halafu akawaambia: Roho yangu ina huzuni sana hata kufa; kaeni hapa na kuangalia pamoja nami. Akakwenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba akisema: Ee Baba yangu, kama ikiwezekana kikombe hiki kinipitie; lakini si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka. (Yoane 13, 3-17) Yesu akijua ya kwamba Baba amemupa vitu vyote mikononi mwake, na ametoka kwa Mungu, na anakwenda kwa Mungu, akaondoka kwa chakula, akaweka mavazi yake kando; akatwaa kitambaa, akafunga kiuno chake. Kisha akatia maji kwa kibakuli, akaanza kunawa miguu ya wanafunzi wake na kuipangusa kwa kitambaa alichojifunga, kiuno chake. Basi akafika kwa Simoni Petro: Na Petro aliwambia: Bwana, wewe unanawa miguu yangu? Yesu akamujibu, akamwambia: Hili ninalofanya sasa hulijui, lakini utalifahamu nyuma. Petro akamwambia: Hutanawa miguu yangu kamwe. Yesu akamwambia: Kama nisipokunawia wewe, huna shirika pamoja nami. Simoni Petro anamwambia: Bwana, si miguu yangu tu, lakini mikono yangu na kichwa changu vilevile. Yesu akamwambia: Yeye aliyeoga hahitaji ila kunawa miguu yake tu, lakini yeye ni safi kabisa: na ninyi ni safi, lakini si wote. Kwa sababu alijua mutu atakayemutoa; hivi alisema: Ninyi wote si safi. Basi alipokwisha kunawa miguu yao, na kutwaa mavazi yake, na kukaa tena, akawaambia: Munajua nililowafanyia ninyi? Munaniita Mwalimu na Bwana: na munasema

vema, sababu nilivyo hivi. Basi kama mimi Bwana yenu na Mwalimu wenu nimenawa miguu yenu, imewapasa ninyi kunawana miguu. Kwa sababu nimewapa ninyi mufano, mufanye sawasawa nilivyowafanyia ninyi. Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Mutummwa si mukubwa kuliko bwana yake; wala mutume si mukubwa kuliko yeye aliyemutuma. Kama munajua maneno haya, heri ninyi kama munayafanya. (Luka 22, 43-45) Malaika toka mbingu alitokea, akamupa nguvu. Naye alikuwa katika uchungu sana, akazidi kuomba kwa bidii; na jasho yake ilikuwa kama matone ya damu yanayoanguka kwa udongo. Alipoondoka katika kuomba, alikuja kwa wanafunzi wake, akawakuta wamelala kwa huzuni. (Matayo 26, 40-75) Akakuja kwa wanafunzi wake, akawakuta wakilala, akamwambia Petro: Hamukuweza kuangalia pamoja nami saa moja? Angalieni na kuomba, musiingie katika majaribu; roho ni tayari lakini mwili ni zaifu. Akakwenda tena mara ya pili, akaomba akisema: Ee Baba yangu, kama haiwezekani kwa kikombe hiki kunipitia ila nikikikunywa, mapenzi yako yatimizwe. Akakuja tena, akakwenda na kuomba mara ya tatu, akisema maneno yale tena. Halafu akakuja kwa wanafunzi, akawaambia: Laleni sasa na kupumzika; tazama, saa imekaribia na Mwana wa watu ametolewa mikononi mwa wenye zambi. Simameni twendeni; tazama, yule anayenitoa ni karibu. Na wakati alipokuwa akisema, tazama, Yuda, mumoja wa wale kumi na wawili akakuja, na pamoja naye makutano makubwa na panga, na magongo, waliotoka kwa wakubwa wa makuhani na wazee wa watu. Na yule aliyemutoa akawapa alama akisema: Yeye nitakayemubusu, huyu ndiye; mumukamate. Basi akakwendea Yesu mara moja, akasema: Salamu, Rabi; akamubusu. Yesu akamwambia: Rafiki, fanya neno ulilokuja kufanya. Halafu wakakuja na kunyosha mikono juu ya Yesu, wakamukamata. Na tazama, mumoja wao waliokuwa pamoja na Yesu, akanyosha mukono wake, akafuta upanga wake, akapiga mutumwa wa kuhani mukubwa, akamukata sikio. Halafu Yesu akamwambia: Rudisha upanga wako pahali pake; kwani wote wanaoshika upanga wataharibiwa kwa upanga. Ao unazania ya kuwa mimi siwezi kusihi Baba yangu, naye atanitumia sasa zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? Basi maandiko yatatimizwa namna gani ya kama sharti itokee hivi? Kwa saa ile Yesu akawaambia makutano: Mumetoka kunitwaa kama juu ya munyanganyi, wenye panga na magongo? Kila siku niliketi hekaluni nikifundisha, lakini hamukunikamata. Lakini maneno haya yote yamekuja ili maandiko ya manabii yatimizwe. Halafu wanafunzi wato wakamwacha, wakakimbia. Nao waliokamata Yesu wakamupeleka kwa nyumba ya Kayafa, kuhani mukubwa, pahali waandishi na wazee walipokusanyika. Lakini Petro alimufuata kwa mbali mupaka kiwanja cha kuhani mukubwa, akaingia, akaketi pamoja na watumishi aone mwisho. Basi wakubwa wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda wa uwongo juu ya Yesu, wapate kumwua; lakini hawakuuona, hata washuhuda wengi wa uwongo walikuja. Lakini nyuma wawili walikuja, wakasema: Mutu huyu anasema: Ninaweza kuharibu hekalu la Mungu na kulijenga tena kwa siku tatu. Kuhani mukubwa akasimama, akamwambia: Hujibu neno? Watu hawa wanakushuhudia wewe nini? Lakini Yesu akanyamaza. Kuhani mukubwa akamwambia: Ninakuapiza kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu. Yesu akamwambia: Wewe umesema; lakini ninawaambia ninyi. Tangu sasa mutaona Mwana wa watu akiketi kwa mukono wa kuume wa uwezo, na akikuja juu ya mawingu wa mbingu. Halafu kuhani mukubwa akapasua mavazi yake akisema: Amekufuru; tuna hitaji gani tena la washuhuda? Tazama sasa ninyi wote mumesikia kufuru yake. Munafikili nini? Wakajibu, wakasema: Anastahili kufa. Halafu wakamutemea mate kwa uso wake, na kumupiga makonde; weingine wakamupiga makofi wakisema: Tabiri kwa sisi, wewe Kristo; ni nani aliyekupiga? Basi Petro alikuwa akiketi inje katika kiwanja; kijakazi mumoja akakuja kwake akisema: Wewe ulikuwa pamoja ya Yesu wa Galilaya vilevile. Lakini akakana mbele yao wote, akisema: Sijui maneno unayosema. Na wakati alipotoka inje hata barazani, kijakazi mwingine akamwona, akawaambia wale waliokuwa pale: Mutu huyu alikuwa pamoja na Yesu Munazareti vilevile. Akakana tena na kiapo: Sijui mutu huyu. Nyuma ya wakati kidogo wale waliosimama pale wakakuja na kumwambia Petro: Hakika wewe ni mumoja wao; kwa sababu hata usemi wako unaonyesha hivi. Halafu akaanza kulaani na kuapa: Sijui mutu huyu. Na mara moja jogoo akawika. Petro akakumbuka neno Yesu alilosema: Mbele ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu.

Akatoka inje, akalia kwa uchungu. (Matayo 27, 1-5) Na wakati ilipokuwa asubui, wakubwa wote wa makuhani na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu kumwua; wakamufunga, wakamuchukua na kumupeleka kwa Pilato aliyekuwa liwali. KIsha Yuda aliyemutoa, wakati alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa, akatubu, akarudishia wakubwa wa makuhani na wazee vipande makumi tatu vya feza, akisema: Nimekosa wakati nilipotoa damu isiyo na kosa. Lakini wale wakasema: Hili ni nini kwetu? Uliangalie wewe mwenyewe. Akatupa vipande vya feza katika pahali patakatifu, akaondoka; akatoka inje akajitundika mwenyewe.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Mfululizo wa Liturgia ya Mtakatifu Basile Mkuu*

*Wakati wa kuingia kubwa pahali pa wimbo Wakeruvi, tunaimba Tropari ifwatayo:*

Sauti ya Sita

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku karamu yako ya fumbo, kwani sitafumbua siri yako kwa adui zako, sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa munyanganyi, nakuungamia. Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

*Hii inaimbwa mara tatu: Mara ya mbili mbele ya kuingia, mara moya kisha kuingia. Tena pahali pa:*

1) Kituo cha Komunyo 2)Tumeona nuru ya kweli na 3) Midomo yetu imejaa.

*Theotokion ya Liturgia iko Wimbo wa Tisa wa Kanuni ya Orthros.*

Sauti ya Sita

Kujeni, enyi waaminifu, tufurahiwe na mapokeleo ya Rabi na ya chakula cha milele kilichotayarishwa katika chumba cha juu. Tunapofundishwa kwa Neno maana yake kubwa, tumtukuzeni na akili ya juu.

Kuaga (Apolisis):

Yeye katika wema wake mkubwa, aliyeonyesha kwa kuwanawisha Wafwasi wake miguu ya kama unyenyekevu ulikuwa ni njia bora tena aliyejishusha kwa ajili yetu mpaka msalabani na kaburini, Kristo, Mungu wetu kweli. . .

# SIKU YA TANO MKUBWA

## SALA YA ASUBUI (ORTHROS)

*Elezo: Mwanzo wa Ibada angalia Mukazi moja Mkubwa asubui.*

Sauti ya Mnane.
Vituo: 1. Ee Bwana, tangu usiku roho yangu kwa sala inaongojea alfajiri yako, maana amri zako ni nuru duniani. Alliluia *(mara tatu*

2. Jifunzeni haki, ninyi wote wakaaji wa dunia. Alliluia *(mara tatu).*

3. Wivu utangukia watu wapotevu, sasa moto itawateketeza, maadui zako. Alliluia *(mara tatu).*

4. Uwaazibu, ee Bwana, uwaazibu vikali kwa mateso wenye sifa wote wa dunia. Alliluia *(mara tatu).*

WIMBO:

Sauti ya Mnane.
Wakati Wafuasi watukufu waliyooshwa miguu ku chakula cha karamu walipokea nuru, Yuda kafiri, aakakutoa kwa waamzi waovu, wewe mwamzi wa haki. Ee ninyi wenyi kuwaza mali, tazameni mwenyi tamaa anajitundika sababu ya mali. Ogopeni, msifanane na roho isiyoweza kushibishwa iliyojaribu uovu wa hii namna juu ya Rabi wake. Wewe uliye mwema kwa ajili ya mwanadamu wote, ee Bwana, utukufu kwako. *(mara tatu).*

### EVANGELIO YA KWANZA

(Yoane 13, 31-38), 14, 15, 16, 17 na 18, 1)
Basi wakati alipokwisha kutoka inje, Yesu akasema: Sasa Mwana wa watu ametukuzwa, na Mungu ametukuzwa ndani yake; Kama Mungu ametukuzwa ndani yake, Mungu atamutukuza ndani yake mwenyewe, na mara moja atamutukuza. Watoto wadogo, angali wakati kidogo nipo pamoja nanyi. Mutanitafuta, na sawasawa nilivyowaambia Wayuda ya kama: Pahali ninapokwenda ninyi hamuwezi kuja: Hivi sasa ninawaambia ninyi. Amri mpya ninawapa ninyi, mupendane; kama mimi nilivyowapenda ninyi, ninyi mupendane vilevile. Hivi watu wote watajua ya kama ninyi wanafunzi wangu, kama ninyi mukiwa na mapendo ninyi kwa ninyi. Simoni Petro akamwambia: Bwana, unakwenda wapi? Yesu akamujibu: Pahali ninapokwenda, huwezi kunifuata sasa; lakini utanifuata nyuma. Petro akamwambia: Bwana, kwa nini siwezi kukufuata sasa? Nitatoa uzima wangu kwa ajili yako. Yesu akamujibu: Utatoa uzima wako kwa ajili yangu? Kweli, kweli ninakuambia, jogoo hatawika hata utakapokwisha kunikana mara tatu. (14) Musifazaike mioyoni mwenu: munaamini Mungu, muniamini mimi vilevile. Katika nyumba ya Baba yangu ni makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia ninyi; ninakwenda kuwatengenzea ninyi pahali. Na kama ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali, nitakuja tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu; pahali ninapokaa mimi, mukae vilevile. Na pahali ninapokwenda munajua, na njia munajua. Tomasi akamwambia: Bwana, hatujui pahali unapokwenda, na tutajua njia namna gani? Yesu akamwambia: Mimi ndimi njia, na kweli, na

uzima: mutu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi. Kama mungalinijua mimi, mungalimujua Baba yangu vilevile; na tangu sasa munamujua na mumemwona. Filipo akamwambia: Bwana, utuonyeshe Baba, basi inatufaa. Yesu akamwambia: Nimekuwa pamoja nanyi wakati murefu na hukunijua, Filipo? Aliyeniona mimi, ameona Baba; namna gani unasema: Utuonyeshe Baba? Huamini ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu? Maneno ninayosema kwenu, sisemi kutoka kwangu mwenyewe; lakini Baba anayekaa ndani yangu anafanya kazi zake. Muniamini ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu; ao muniamini kwa sababu ya kazi zenyewe. Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye anayeniamini mimi, kazi ninazofanya

yeye atazifanya vilevile; na atafanya kazi kubwa kuliko hizi; kwa sababu ninakwenda kwa Baba yangu. Na mukiomba lo lote kwa jina langu, nitalifanya, Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Kama mukiomba neno gani kwa jina langu, nitalifanya. Kama mukinipenda, mutatii amri zangu. Na nitaomba Baba, naye atawapa ninyi Musaidizi mwingine, akae nanyi hata milele, Roho ya kweli, dunia isiyeweza kumupokea; kwani haimwoni wala haimujui: Lakini ninyi munamujua, kwa sababu anakaa pamoja nanyi, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima: nitakuja kwenu. Angali wakati mudogo, na dunia hainioni tena; lakini munaniona; kwa sababu mimi ni hai, nanyi mutakuwa hai vilevile. Katika siku ile mutajua ya kwamba mimi ni ndani ya Baba

yangu, na ninyi ndani yangu, na mimi ndani yenu. Aliye na amri zangu, na kuzitii, yeye ndiye mwenye kunipenda; naye anayenipanda atapendwa na Baba yangu, nami nitamupenda na kujionyesha mwenyewe kwaki. Yuda (siye Iskariota) akamwambia: Bwana, namna gani utajionyesha mwenyewe kwetu, wala si kwa dunia? Yesu akajibu, akamwambia: Kama mutu akinipenda atatii neno langu, na Baba yangu atamupenda, nasi tutakuja kwake, na tutafanya makao yetu kwake. Mutu asiyenipenda, hatii maneno yangu, na neno munalosikia si langu, lakini lake Baba aliyenituma. Maneno haya nimewaambia ninyi nikikaa pamoja na ninyi. Lakini Musaidizi, Roho Mutakatifu, Baba atakayemutuma kwa jina langu, yeye atawafundisha ninyi yote, na kuwakumbusha ninyi yote niliyowaambia ninyi. Salama ninawaachia ninyi: Salama yangu ninawapa ninyi; nami ninawapa ninyi si kama dunia inavyotoa. Musifazaike mioyoni

mwenu, wala musiwe na woga. Mulisikia ya kwamba niliwaambia ninyi, ninakwenda zangu, na nitakuja kwenu tena. Kama mungalinipenda, mungalifurahi, kwa sababu ninakwenda kwa Baba; kwa maana Baba yangu ni mukubwa kuliko mimi. Na sasa nimewaambia ninyi mbele inatokea, hata wakati inapotokea, mupate kuamini. Sitasema nanyi maneno mengi tena kwa sababu mukubwa wa dunia hii anakuja; na yeye hana kitu ndani yangu. Lakini dunia ijue ya kama ninapenda Baba; na kama Baba alivyoniagiza, ndivyo ninavyofanya. Simameni, tutoke hapa. Mimi ni muzabibu wa kweli, na Baba yangu ni mulimaji. Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda, analiondoa; na kila tawi linalozaa analisafisha, lizae matunda zaidi. Ninyi mumekwisha kuwa safi kwa sababu ya neno nililowaambia ninyi. Kaeni ndani yangu, na mimi ndani yenu. Sawasawa tawi lisivyoweza kuzaa matunda peke yake, kama halikai ndani ya muzabibu; hivi hamuwezi, musipokaa ndani yangu. Mimi ni muzabibu, nanyi matawi; mwenye kukaa ndani yangu, na mimi ndani yake, huyu anazaa sana kwa sababu pasipo mimi hamuwezi kufanya neno.

Mutu asipokaa ndani yangu, anatupwa inje kama tawi, na anakauka; na watu wanayakusanya, na kuyatupa kwa moto, yakateketea. Kama mukikaa ndani yangu, na maneno yangu yanakaa ndani yenu, mutaomba neno gani munalotaka, na mutafanyiziwa. Kwa hivi Baba yangu anatukuzwa, muzae matunda mengi; na mutakuwa wanafunzi wangu. Sawasawa Baba alivyonipenda mimi, hivi nilivyowapenda ninyi: mukae katika mapendo yangu. Kama mukitii amri zangu, mutakaa katika mapendo yangu; kama vile mimi nilivyotii amri za Baba yangu, nakukaa katika mapendo yake. Maneno haya nimewaambia ninyi, kusudi furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe. Hii ndiyo amri yangu, mupendane, kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna mwenye mapendo kuliko haya, mutu kutoa uzima wake kwa sababu ya rafiki zake. Ninyi ni rafiki zangu, kama mukifanya maneno ninayoagiza. Siwaiti ninyi tena watumwa, kwa kuwa mutumwa hjajui anayoyafanya bwana yake; lakini nimewaita ninyi rafiki, kwa sababu yote niliyosikia kwa Baba yangu nimewajulisha ninyi. Hamukunichagua mimi, lakini mimi niliwachagua ninyi, nami niliwaweka ninyi, mwende na muzae matunda, na matunda yenu yapate

kukaa: kusudi neno gani mutakaloomba Baba kwa jina langu awape ninyi. Maneno haya ninawaagiza ninyi, mupendane. Kama dunia ikiwachukia ninyi, munajua ya kama ilinichukia mimi mbele ya kuwachukua ninyi. Kama mungekuwa wa dunia, dunia ingependa watu wake; lakini kwa sababu ninyi si wa dunia, lakini nimewachagua ninyi toka dunia, kwa sababu hii dunia inawachukia ninyi. Kumbukeni neno nililowaambia ninyi: Mutumwa si mukubwa kuliko bwana yake. Kama wakinitesa mimi, watawatesa ninyi vilevile; kama walishika neno langu, watashika lenu vilevile. Lakini maneno haya yote watawafanya ninyi kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamujui yeye aliyenituma. Kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na zambi; lakini sasa hawana maneno ya kusema juu ya zambi zao. Mwenye kunichukia mimi anachukia Baba yangu vilevile. Kama nisingalifanya kazi katikati yao, asizofanya mwingine, wasingalikuwa na zambi; lakini sasa wametuona na kutuchukia mimi na Baba yangy vilevile. Lakini litimie neno lililoandikwa katika torati yao: Walinichukia bule. Lakini wakati Musaidizi anapokuja, nitakayemutuma toka Baba, Roho ya kweli, anayetoka kwa Baba, atanishuhudia; na ninyi ni washuhuda vilevile, kwa sababu mumekuwa pamoja nami tangu mwanzo. Maneno haya nimewaambia ninyi, musiwe mukaanguka. Watawatokeza ninyi kwa masunagogi; lakini saa inakuja wakati kila mutu anayewaua ninyi atazania ya kama anatumikia Mungu. Na maneno haya watawafanya ninyi, kwa

sababu hawakujua Baba, wala mimi. Lakini nimewaambia ninyi maneno haya, kusudi wakati saa yao inapokuja, mukumbuke ya kwamba niliwaambia ninyi. Na maneno haya sikuwaambia ninyi tangu mwanzo, kwa sababu nilikuwa pamoja na ninyi. Lakini sasa ninakwenda zangu kwake aliyenituma; na hakuna mumoja wenu anayeniuliza: Unakwenda wapi? Lakini kwa sababu nimewaambia ninyi maneno haya, huzuni imejaa mioyoni mwenu. Lakini mimi ninawaambia ninyi kweli, ni kwa faida yenu niondoke; kwa sababu kama siondoki, Musaidizi hatakuja kwenu; lakini kama nikikwenda, nitamutuma kwenu. Na wakati anapokuja, atahakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu; kwa maneno ya zambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa maneno ya haki, kwa sababu ninakwenda kwa Baba, na hamunioni tena; kwa maneno ya hukumu, kwa sababu mukubwa wa dunia hii amehukumiwa. Ningali na maneno mengi ya kuwaambia ninyi, lakini hamuwezi kuyabeba sasa. Lakini wakati anapokuja yule Roho ya kweli, atawaongoza ninyi katika yote yaliyo kweli: kwa sababu hatasemka kwa mamlaka uake mwenyewe; lakini maneno yote anayosikia atayasema; naye atawatangazia ninyi habari za maneno yatakayokuja. Atanitukuza mimi, kwa sababu atatwaa katika yaliyo yangu na kuwaambia ninyi. Yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa sababu ya maneno haya nilisema ya kwamba atatwa katika yaliyo yangu na kuwaambia ninyi. Wakati kidogo, nanyi hamunioni tena; na tena wakati kidogo na mutaniona, kwa sababu ninakwenda kwa Baba. Basi wengine wa wanafunzi wake walisemezana: Neno gani hili analosema kwetu, wakati kidogo, na hamunioni; na tena wakati kidogo, na mutaniona; kwa sababu ninakwenda kwa Baba? Basi walisema: Neno gani hili analosema, wakati kidogo? Hatukui analosema. Yesu alifahamu ya kwamba walitaka kumwuliza, akamwaambia: Munaulizana katikati yenu, maana ya neno lile nililosema: Wakati kidogo na hamunioni, na tena wakati kidogo na mutaniona? Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Mutalia na

kuomboleza, lakini dunia itafurahi; na ninyi mutakuwa na huzuni, lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha. Mwanamuke, wakati anapozaa, ana huzuni kwa sababu saa yake imekuja; lakini wakati anapokwisha kuzaa mutoto, hakumbuki tena uchungu, kwa sababu ya furaha ya kuzaliwa mutu katika dunia. Basi hivi ninyi sasa muna huzuni; lakini nitawaona ninyi tena, na mioyo yenu itafurahi, na hakuna mutu atakayewaondoshea ninyi furaha yenu. Na siku ile hamutaniuliza neno. Kweli, kweli ninawaambia ninyi, kila neno munaloomba Baba kwa jina langu, atawapa ninyi. Mupaka leo hamukuomba neno kwa jina langu: mwombe, na mutapata, furaha yenu itimizwe. Maneno haya nimewaambia ninyi kwa mufano: saa inakuja, wakati nisiposema nanyi tena kwa mufano, lakini nitawaambia ninyi waziwazi habari za Baba. Katika siku ile mutaomba kwa jina langu; nami sisemi nanyi ya kwamba nitawaombea ninyi kwa Baba; kwa maana Baba mwenyewe anawapenda ninyi, kwa sababu ninyi mumenipenda mimi, na kuamini ya kwamba nilitoka kwa

Mungu. Nilitoka kwa Baba, nami nimekuja katika dunia; tena ninaacha dunia, na ninakwenda kwa Baba. Wanafunzi wake wakasema naye:  Basi, sasa unasema waziwazi, na husemi mufano. Sasa tunajua ya kwamba unajua maneno yote, na huhitaji mutu akuulize; kwa hii tunaamini ya kwamba ulitoka kwa Mungu. Yesu akawajibu:  Munaamini sasa? Tazama, saa inakuja, ndiyo, imekwisha kufika, mutakaposambazwa, kila mutu kwake, na mutaniacha mimi peke yangu: lakini mimi si peke yangu, kwa sababu Baba yuko pamoja nami. Maneno haya nimewaambia ninyi, mupate kuwa na salama ndani yangu. Katika dunia mutapata mateso; lakini furahini mioyoni; mimi nimeshinda dunia. (17) Yesu alisema maneno haya, na kunyanyua macho yake kwa mbingu, akasema:  Baba, saa imefika; tukuza Mwana wako, kusudi Mwana wako akutukuze wewe. Sawasawa ulivyomupa uwezo juu ya wote wenye mwili, ili awape uzima wa milele wote uliomupa. Na huu ni uzima wa milele, wakujue wewe, Mungu pekee wa kweli, na Yesu Kristo, uliyemutuma. Mimi nimekutukuza katika dunia, kazi ile uliyonipa niifanye nimeimaliza. Na sasa unitukuze, Baba, pamoja nawe mwenyewe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe mbele ya kuwa dunia. Nilionyesha jina lako kwa watu wale ulionipa katika dunia; walikuwa wako, na ulinipa; nao wameshika neno lako. Sasa wamejua ya kwamba maneno yote uliyonipa yalitoka kwako; kwa sababu maneno uliyonipa nimewapa wao; nao waliyapokea, wakajua kweli ya kama nilitoka kwako, wakaamini ndiwe uliyenituma. Ninawaombea; siombei dunia, lakini hawa ulionipa, kwa sababu wao ni wako. Na wote walio wangu ni wako, na walio wako ni wangu, nami nimetukuzwa ndani yao. Nami si tena katika dunia, lakini hawa ni katika dunia, na ninakuja kwako. Baba Mutakatifu, uwalinde kwa jina lako wale ulionipa, wawe mumoja kama sisi. Wakati nilipokuwa pamoja nao katika dunia, niliwalinda kwa jina lako; wale ulionipa niliwachunga, wala hapana mumoja wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu; maandiko yatimizwe. Na sasa ninakuja kwako; na maneno haya ninayasema katika dunia, wawe na furaha yangu kutimizwa ndani yao. Nimewapa neno lako; na dunia iliwachukia, kwa sababu wao si watu wa dunia, kama mimi nisivyo wa dunia. Siombi ya kama uwaondoe katika dunia, lakini uwachunge kwa yule mwovu. Wao si wa dunia, kama mimi nisivyo wa dunia. Uwatakase kwa kweli; neno lako ni kweli. Hata sawasawa ulivyonituma katika dunia, hivi nilivyowatuma katika dunia. Na kwa ajili yao ninajitakasa mwenyewe, kusudi watakaswe vilevile katika kweli. Wala si hawa tu ninaowaombea, lakini wao vilevile watakaoniamini kwa sababu ya neno lao; ili wote wakae mumoja; kama wewe Baba ulivyo ndani yangu, na mimi ndani yako, wawe mumoja ndani yetu, dunia ipate kuamini ya kama ulinituma. Na utukufu ulionipa nimewapa, wakae mumoja kama sisi tulivyo mumoja; mimi ndani yao, na wewe ndani yangu, wakamilike na kuwa mumoja; dunia ijue ya kama ulinituma, na uliwapenda, kama ulivyonipenda mimi. Baba, ninataka sana hawa ulionipa wakae pamoja nami pahali nilipo, waone utukufu wangu ulionipa; kwa sababu ulinipenda mbele ya kuwekwa misingi ya dunia. Baba mwenye haki, dunia haikukujua, lakini mimi nilikujua; na hawa walijua ya kama ndiwe uliyenituma. Nami niliwajulisha jina lako, na nitalijulisha; hata mapendo uliyonipenda mimi

yawe ndani yao, nami ndani yao. (18) Wakati Yesu alipokwisha kusema maneno haya, akatoka pamoja na wanafunzi wake kwenda ngambo ya kijito Kiduroni, palipokuwa shamba; akaingia yeye na wanafunzi wake.

**WAIMBAJI**:  Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

WIMBO 1.

Sauti ya Mnane

Watawala wa watu wamekusanyika juu ya Bwana na juu ya Kristu wake. Wamenisumbua kwa maneno yao maovu; Bwana, bwana, usiniacheTumtolee Kristu nia zetu safi, tuwe marafiki zake, tutoeni sadaka ya uzima wetukwa ajili yake; tusisongwe na shuruli za uzima kama Yuda. Lakini kwa siriya mioyo yetu tulalamike:  Baba yetu uliye mbinguni, utuopoe na yule muovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ee Bikira usiyeolewa, ulizaa na ulikaa Bikira, ee Mama Mtakatifu kamili. EeMaria, Mzazi-Mungu, umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

WIMBO 2

Sauti ya Sita

Yuda alikwenda mbio kwa wakubwa wa makuhani na akawaambia:  Mutanipa ninyi kama nikiwatolea Yesu? Wewe ambaye walisema msiyeonekana, ulikuwapo kati yao. Samehe roho zetu, wewe mwenye kuona ndani ya mioyo yetu.

Tumtumikie Mungu na mapendo kama Maria ku chakula, tusijiachilie kutawaliwa na feza kama Yuda, tutakuwa daima naKristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ee Bikira, huyu uliyezaa kwa namna isiyokadirika, umuombe daima yeye mpenda-wanadamu, aokoe ku hatari wote wale wenye kukukimbilia wewe.

WIMBO 3

Sauti ya Pili

Ee Bwana mpenda-wanadamu, kwa sababu ya Ufufuo wa Lazaro, wana wa Waebrania walikulalamikia:  Hozanna! Lakini Yuda asiye na sheria hakutaka kusikia.

Ee Kristu Mungu, ku Karamu yako uliwaambia Wafuasi wako:  Mumoja wenu atanitoa. Lakini Yuda asiye na sheria hakutaka kusikia.

Wakati Yoanne alikuuliza, ee Bwana:  Ni nani huyu atakutoa? Ukamtaja na kipande cha mkate. Lakini Yuda asiye na sheria hakutaka kusikia.

Wayuda walitafuta kukuua sababu ya feza makumi ma tatu na sababu ya busu ya uongo; lakini Yuda asiye na sheria hakutaka kusikia.

Ee Kristu Mungu wetu, ulipoosha miguu ya Wafuasi wako, ukawaambia:  Mufanye hii munaona mimi nafanya. Lakini Yuda asiye na sheria hakutaka kusikia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ee Mtakatifu Mzazi-Mungu okoa watumishi wako, kwani kisha Mungu ni kwako tunakimbilia, ewe mlinzi wetu, ukuta usiyobomolewa.

SHEMASI AO PADRI: Ektenia Kidogo.

**KATHISMA** Sauti ya Saba

Ku Karamu uliwalisha Wafuasi wako na ulijua shauri la utoaji. Ku hii chakula ulimutaja Yuda ukijua ya kama ni msiyeongoka;kwani ulitaka kuwafunulia wote ya kwamba umejitoa ku lufu ya kutaka sababu ya kuokoa dunia kwa adui. Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako!

## EVANGELIO YA MBILI

Katika Mwevangelizaji Yoane (18, 1-28)

Wakati Yesu alipokwisha kusema maneno haya, akatoka pamoja na wanafunzi wake kwendangambo ya kijito Kiduroni, palipokuwa shamba; akaingia yeye na wanafunzi wake. Basi Yuda vilevile, yule aliyemutoa, alijua pahali pale; kwa sababu Yesu alikwenda kule mara nyingi pamoja na wanafunzi wake. Basi Yuda akikwisha kupokea k**IKOS**i cha askari, na watumishi wa wakubwa wa makuhani na Wafarisayo, anakuja kule na taa, na mienge, na silaha. Basi Yesu akijua maneno yote yatakayokuja juu yake, akatokea akawaambia: Munatafuta nani? Wakamujibu: Yesu Munazareti. Yesu anawaambia: Ni mimi. Na Yuda vilevile, aliyemutoa, alisimama pamoja nao. Basi wakati alipowaambia: Ni mimi, walirudi nyuma, wakaanguka chini. Basi akawauliza tena: Munatafuta nani? Wakasema: Yesu Munazareti. Yesu akajibu: Nimewaambia ninyi ya kwamba, ni mimi; basi kama munanitafuta mimi, mumwache hawa waende zao; litimizwe neno alilosema: Hawa ulionipa sikupoteza hata mumoja wao. Basi Simoni Petro alikuwa na upanga, akauvuta, akapiga mutumwa wa kuhani mukubwa, akakata sikio lake la kuume. Na jina lake mutumwa ni Malko. Basi Yesu akamwambia Petro: Rudisha upanga wako katika ala yake; kikombe alichonipa Baba, sitakikunywa? Basi kile k**IKOS**i na yule akida na wale watumishi wa Wayuda wakakamata Yesu, wakamufunga, wakamupeleka kwanza kwa Ana; kwa sababu alikuwa mukwe wake Kayafa, aliyekuwa kuhani mukubwa mwaka ule. Na Kayafa ndiye aliyewapa Wayuda shauri ya kwamba inafaa mutu mumoja afe kwa ajili ya watu. Na Simoni Petro alifuata Yesu, na mwanafunzi mwingine. Na yule mwanafunzi alikuwa amejulikana na kuhani mukubwa, akaingia pamoja na Yesu katika kiwanja cha kuhani mukubwa; lakini Petro alisimama inje kwa mulango. Basi yule mwanafunzi mwingine aliyejulikana na kuhani mukubwa, akatoka inje, akasema na kijakazi aliyengoja mulango, akaleta Petro ndani. Basi yule kijakazi aliyengoja mulango akamwambia Petro: Wewe vilevile ni mumoja wa wanafunzi wa mutu huyu? Akasema: Si mimi. Na wale watumwa na askari walikuwa wamefanya moto wa makaa; kwa sababu ilikuwa baridi; wakasimama na kuota moto, na Petro alisimama pamoja nao, akiota moto. Basi kuhani mukubwa akauliza Yesu juu ya wanafunzi wake, na juu ya mafundisho yake. Yesu akamujubu: Nilisema na dunia waziwazi; nilifundisha siku zote katika masunagogi, na katika hekale, pahali Wayuda wanapokusanyuka siku zote, wala kwa siri sikusema neno. Kwa nini unaniuliza? Uwaulize wao walionisikia ni nini niliyosema nao; tazama, wanajua niliyowaambia. Na wakati aliposema maneno haya, mumoja wa wale watumishi aliyesimama karibu, alipiga Yesu kofi, akisema: Unajibu kuhani mukubwa hivi? Yesu akamujibu: Kama nimesema vibaya, shuhudia yale mabaya; lakini kama nimesema vema, kwa nini unanipiga? Basi Ana alimutuma amefungwa kwa Kayafa kuhani mukubwa. Na Simoni Petro alisimama, akiota moto. Basi walimwambia: Wewe si mumoja wa Wanafunzi wake? Yeye alikana, na alisema: Si mimi. Mumoja wa wale watumwa wa kuhani mukubwa, akiwa jamaa ya mutu yule aliyekatwa sikio na Petro, akasema: Sikukuona katika shamba pamoja naye? Basi Petro alikana tena; mara moja jogoo akawika. Basi walipeleka Yesu kutoka kwa Kayafa hata nyumba ya hukumu; na ilikuwa mapema; lakini wao wenyewe hawakuingia ndani ya nyumba ya hukumu, wasiwe wakachafuka, lakini wapate kula Pasaka.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako

WIMBO 4

Sauti ya Tano

Leo Yuda anaacha Rabi na anapokea shetani. Tamaa ya feza inamupofusha; anapoteza nuru, inamupofusha. Namna gani basi ataona wazi yeye aliyeuzisha Nuru ku feza makumi tatu? Jua

limetoka kwa ajili yetu. Huyu aliyeteswa kwa ajili ya dunia;tena tumulalamikie: Wewe uliyeteswa na kuwahurumia wanadamu, ee Bwana, utukufu kwako.

Leo Yuda anadanganya ibada, amekua mgeni ku neema; yeye mfuasi amejifanya kuwa mtoaji. Kwa busu ya desturi ameficha utoaji; mpumbafu anataka feza makumi tatu kuliko mapendo ya Bwana. Anakuwa mwongozi wa baraza ya wasiyo na sheria. Sisi ambao Kristu ni wokovu, tumtukuzeni.

Sauti ya kwanza

Ndugu, tupendane wamoja kwa wengine kama ndugu katika Kristu, tusiwe na tafauti ku mateso ya jirani ili tusihukimiwe kama mtumishi ambaye feza ilifanya mgumu moyo wake ambao sikitiko haikufai kitu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Utukufu wako ulisikilika ulimwenguni, kwani ulizaa mwilini Muumba wa vitu vyote, ee Maria Mtakatifu Mzazi-Mungu, wewe usiyeolewa tena mtukufu kamili.

WIMBO 5

Sauti ya Sita

Mfuasi aliuzisha Rabi wake. Aliuzisha Bwana ku feza makumi tatu na kwa busu ya uwongo akamtoa kwa wasiyo na sheria ili auawe

Leo Muumba wa mbingu na dunia anawaambia Wafuasi wake: Tazameni wakati imekuja, Yuda anajongea kwa kuniuzisha. Hata mmoja wenu asinikane akiniona Msalabani kati ya wanyanganyi wawili; Mwana wa watu nateswa, mimi mpenda-wanadamu naokoa wale wenyi kunisadiki mimi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ku mwisho wa nyakati ulipata mimba na ulizaa Muumba wako kwa namna isiyokadirika. Umuombe aokoe roho zetu.

WIMBO 6

Sauti ya Saba

Leo Yuda anakesha ili amtoe Bwana Mwokozi wa milele wa ulimwengu, yeye mwenye kulisha makutano ya watu na mikate tano. Leo kafiri anamkataa Rabi, mfuasi anamtoa Bwana. Anauzisha ku feza huyu aliyelisha wanadamu manna.

Leo Wayuda wanamupigilia Bwana Msalabani, Yeye aliyegawanya bahari na mti na kuwavukisha jangwani. Leo kwa mkuki wamechoma ubavu wa huyu aliyetuma mapigo katika Misri kwa ajili yao. Wanamunywisha nyongo huyu aliyewanyesheshea manna.

Ee Bwana, ulipoenda kuteswa kwa kutaka kwako, ukawaambia Wafuasi wako: Hamuwezi kukesha hata saa moja pamoja nami, namna gani muliweza kuahidi kufa kwa ajili yangu? Tazameni Yuda yeye halale;anajiharikisha kunitoa kwa wasiyo na sheria. Amukeni, mukaombe! Hata mumoja wenu asinikane akiona nimepigiliwa Msalabani. Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Salamu, Mzazi-Mungu uliyechukua tumboni mwako huyu mbingu haiwezi kuchukua. Salamu, Bikira, uaguzi wa manabii, wewe ambaye Emmanueli aliangaa ndani yako. Salamu, Mama wa Kristu Mungu wetu.

SHEMASI AO PADRI: Ektenia Kidogo.

**KATHISMA** Sauti ya saba

Ee Yuda, ni mimi ilikusukuma kumtoa Mwokozi? Alikukataa ku kundi la Wafuasi wake? Alikukatalia kipaji cha kuponya magonjwa? wakati ulikula na wengine alikufukuza mezani? Wakati aliosha miguu ya Wafuasi alizarau ile yako? Umesahaliwa ku mema ngapi! Ubaya wako umefunuliwa, uvumilivu wa milele wa Kristu, umetangaziwa pamoja na rehema yake kubwa.

## EVANGELIO YA TATU

Katika Mwevangelizaji Matayo (26, 57-75)

Nao waliokamata Yesu wakamupeleka kwa nyumba ya Kayafa, kuhani mukubwa, pahali waandishi na wazee walipokusanyika. Lakini Petro alimufuata kwa mbali mupaka kiwanja cha kuhani mukubwa, akaingia, akaketi pamoja na watumishi aone mwisho. Basi wakubwa wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda wa uwongo juu ya Yesu, wapate kumwua; lakini hawakuuona, hata washuhuda wengi wa uwongo walikuja. Lakini nyuma wawili walikuja, wakasema: Mutu huyu anasema: Ninaweza kuharibu hekalu la Mungu na kulijenga tena kwa siku tatu. Kuhani mukubwa akasimama, akamwambia: Hujibu neno? Watu hawa wanakushuhudia wewe nini? Lakini Yesu akanyamaza. Kuhani mukubwa akamwambia: Ninakuapiza kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu. Yesu akamwambia: Wewe umesema; lakini ninawaambia ninyi. Tangu sasa mutaona Mwana wa watu akiketi kwa mukono wa kuume wa uwezo, na akikuja juu ya mawingu wambingu. Halafu kuhani mukubwa akapasua mavazi yake akisema: Amekufuru; tuna hitaji gani tena la washuhuda? Tazama sasa ninyi wote mumesikia kufuru yake. Munafikili nini? Wakajibu, wakasema: Anastahili kufa. Halafu wakamutemea mate kwa uso wake, na kumupiga makonde; weingine wakamupiga makofi wakisema: Tabiri kwa sisi, wewe Kristo; ni nani aliyekupiga? Basi Petro alikuwa akiketi inje katika kiwanja; kijakazi mumoja akakuja kwake akisema: Wewe ulikuwa pamoja ya Yesu wa Galilaya vilevile. Lakini akakana mbele yao wote, akisema: Sijui maneno unayosema. Na wakati alipotoka inje hata barazani, kijakazi mwingine akamwona, akawaambia wale waliokuwa pale: Mutu huyu alikuwa pamoja na Yesu Munazareti vilevile. Akakana tena na kiapo: Sijui mutu huyu. Nyuma ya wakati kidogo wale waliosimama pale wakakuja na kumwambia Petro: Hakika wewe ni mumoja wao; kwa sababu hata usemi wako unaonyesha hivi. Halafu akaanza kulaani na kuapa: Sijui mutu huyu. Na mara moja jogoo akawika. Petro akakumbuka neno Yesu alilosema: Mbele ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu. Akatoka inje, akalia kwa uchungu.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

WIMBO 7

Sauti ya Mnane

Watu wasiyo na sheria walikukamata, ee Bwana. Ukakubali na ukasema: Japo mumemuwa Mchugaji na kusambaza kondoo kumi na wawili, wao Wafuasi wangu, nina uwezo wa kuita majeshi kumi na mawili na zaidi ya Malaika. Lakini navumilia kusudi yatimizike mafumbo niliyowafunulia kwa maneno ya Manabii wangu. Ee Bwana, utukufu kwako.

Petro alikukana mara tatu;palepale akasikia maneno yako na akakutolea machozi ya toba. Ee Bwana, unifazilie na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Wote tumwimbieni Bikira Mtakatifu kamili, yeye mbebaji wokovu, paradizo nzuri, wingu la nuru ya milele, tukimwambia: Salamu.

WIMBO 8

Sauti ya mbili
Mutwambieni, enyi wasiyo na sheria, mumesikia ninyi juu ya Mwokozi wetu? Hakuweka sheria? Hakufundisha mafundisho ya manabii?Namna gani mulisubutu kutoa Neno la Mungu kwa Pilato, yeye Mwokozi wa roho zetu?

Asulubiwe! Ndivyo walivyolalamika watu wasiyo na shukrani waliyofurahia daima mema yako, na wakaomba wawafungulie muovu pahali pa mfazilii, wao wauaji wa wenye haki; lakini wewe, ee Kristu, ulinyamaza kimya ukavumilia makelele yao, ukaitikia kuteswa kwa ajili yetu sababu ya kutuokoa, wewe mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Kama vile hatusubutu kusema sababu ya zambi zetu nyingi, umuombe huyu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu! Kwani ombi la Mama linaweza kusaidia mingi, kwa Rabi, usizarau maombi, ewe safi kamili, kwani Yeye ni mwenyi huruma na anaweza kutuokoa, yeye aliyeteswa kwa kutaka kwake kwa ajili yetu.

WIMBO 9

Sauti ya Tatu
Wana wa Israeli walimuuzisha ku feza makumi tatu huyu mwenyi bei mingi. Kesheni na ombeni kusudi musianguke katika majaribu. Roho ni nguvu lakini mwili ni zaifu. Kwa hii mambo, kesheni.

Wamenilisha nyongo, na kwa kiu yangu wameninyuisha siki. Wewe, ee Bwana, unifufue na unitwae.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Mataifa yote yanakuimbia, ee Bikira Mtakatifu kamili, kwani ulizaa Kristu Mungu wetu ambaye katika wewe aliopoa mwanadamu ku laana.

Ektenia Kidogo

**KATHISMA** Sauti ya Mnane
Namna gani Yuda zamani mfuasi wako aliweza kufikiri kukutoa wakati alikula chakula chako, mdanganyifu na asiye na haki akawaendea wakubwa wa makuhani akawaambia: Mutanipa ninyi nikiwatolea huyu mwenyi kuvunja sheria na kukufuru sabato? Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako!

## EVANGELIO YA INE

Katika Mwevangelizaji Yoane (18, 28-40 na 19, 1-16)

Basi walipeleka Yesu kutoka kwa Kayafa hata nyumba ya hukumu; na ilikuwa mapema; lakini wao wenyewe hawakuingia ndani ya nyumba ya hukumu, wasiwe wakachafuka, lakini wapate kula Pasaka. Basi Pilato akawatokea inje, akasema: Ni mashitaki gani munayoleta juu ya mutu huyu? Wakajibu, wakamwambia: Kama huyu asingekuwa mwenye kufanya uovu, tusingemuleta

kwako. Basi Pilato akawaambia: Mumukamate ninyi wenyewe na mumuhukumu kwa torati yenu. Basi Wayuda wakamwambia: Sisi hatuna ruhusa ya kuua mutu; hata neno lake Yesu litimizwe alilolisema, akionyesha ni kufa gani atakakokufa. Basi Pilato akaingia nyumba ya hukumu tena, akaita Yesu, akamwambia: Wewe ni mufalme ya Wayuda? Yesu akajibu: Wewe unasema hivi wewe mwenyewe, ao watu wengine walikuambia habari zangu? Pilato alijibu:

Mimi Muyuda? Taifa lako na wakubwa wa makuhani walikuleta kwangu; umefanya nini? Yesu akajibu: Ufalme wangu si wa dunia hii; kama ufalme wangu ungekuwa wa dunia hii, watumishi wangu wangenipigania nisitolewe kwa Wayuda; lakini sasa ufalme wangu si wa dunia hii. Basi Pilato akamwambia: Wewe mufalme basi? Yesu akajibu: Wewe unasema ya kwamba mimi ni mufalme. Kwa ajili ya maneno haya nilizaliwa, na kwa ajili ya maneno haya nilikuja katika dunia, ili nishuhudie kweli. Kila mutu wa kweli anasikia sauti yangu. Pilato akamwambia: Kweli ni kitu gani? Na wakati alipokwisha kusema neno hili, alitokea Wayuda tena, akawaambia: Mimi sioni hata kosa moja kwake. Lakini kuna desturi kwenu, mimi kuwafungulia ninyi mutu mumoja wakati wa Pasaka; basi munataka niwafungulie ninyi Mufalme wa Wayuda? Basi wote wakalalamika tena, wakisema: Hapana mutu huyu, lakini Baraba. Na Baraba alikuwa munyanganyi. (19, 1-16)Hivi basi Pilato alitwaa Yesu, akamupiga na mijelele. Na askari walisokota taji ya miiba, wakaitia kwa kichwa chake, wakamuvika na vazi jekundu; wakakuja kwake, wakasema: Salamu, Mufalme wa Wayuda! Wakamupiga makofi. Pilato akatoka tena inje, akawaambia: Tazama ninamuleta inje kwenu, mujue ya kuwa sioni neno baya kwake. Basi Yesu akatoka inje, akivaa taji ya miiba, na vazi jekundu. Pilato akawaambia: Tazama mutu huyu! Basi wakati wakubwa wa makuhani wa askari walipomwona, wakapaza sauti, wakisema: Umusulibishe, umusulibishe! Pilato akawaambia: Mumutwae ninyi wenyewe, na kumusulibisha; kwa maana mimi sioni neno baya kwake. Wayuda wakamujibu: Sisi tuna sheria, na kwa sheria ile imemupasa kufa, kwa sabnabu alijifanya kywa Mwana wa Mungu. Basi wakati Pilato aliposikia neno hili, akazidi kuogopa; akaingia tena nyumba ya hukumu, akamwambia Yesu: Unatoka wapi? Lakini Yesu hakumujibu neno. Basi Pilato akamwambia: Husemi ni mimi? Hujui ya kama nina mamlaka ya kukusulibisha, na nina mamlaka ya kukufungua? Yesu akamujibu: Hungekuwa na mamlaka juu yangu hata kidogo, kama usingepewa toka juu; kwa sababu hii, yeye aliyenitia mikononi mwako ana zambi kubwa zaidi. Kutoka saa ile Pilato akatafuta kumufungua; lakini Wayuda wakapaza sauti, wakisema: Kama ukifungua mutu huyu, wewe si rafiki ya Kaisari; kila mutu anayejifanya kuwa mufalme anakataa Kaisari. Basi wakati Pilato aliposikia maneno haya, akaleta Yesu inje, akakaa juu ya kiti cha hukumu, pahali panapoitwa Pahali pa Mawe, lakini kwa Kiebrania Gabata. Na ilikuwa Maandalio ya Pasaka; na ilikuwa karibu na saa sita. Akasema na Wayuda: Tazama, Mufalme wenu! Lakini walipaza sauti: Umwondoshe, umwondoshe, umusulibishe! Pilato akawaambia: Nitasulibisha mufalme wenu? Wakubwa wa makuhani wakajibu: Hatuna mufalme ila Kaisari. Hivi basi akamutia katika mikono yao asulibiwe. Na walikamata Yesu, wakamupeleka; akatoka akibeba musalaba wake, hata pahali panapoitwa pahali pa Mufupa wa Kichwa, na kwa Kiebrania, Golgota: wakamusulibisha kule, na wengine wawili pamoja naye, hapa mumoja na kule mumoja, na Yesu katikati. Pilato akaandika anwani, na akaiweka juu ya musalaba. Na imeandikwa, Yesu Munazareti, Mufalme wa Wayuda.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

WIMBO 10

Sauti ya Sita

Huyu mwenyi kuvaa nuru nguo alikuwa uchi mbele ya waamzi wake. Alipigwa ku uso wake makofi ya mikono aliyeumba. Watu wasiyo na sheria wakapigilia Bwana wa utukufu msalabani. Hapo pazia ya hekalu ikapasuka, jua likapata giza halikuweza kuvumilia kuona Mungu kuzarauliwa, yeye ambaye viumbe vyote vinatetemekea. Kujeni, tumuabudu.

Mfuasi alikukana, mnyanganyi akalalamika: Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ee Bwana, leta amani duniani, wewe ambaye kwa ajili ya wokovu wa watumwa ulichukua mwili kwa Bikira ili tukutukuze kwa sauti moja, ewe mpenda-wanadamu.

WIMBO 11

Sauti ya Sita

Kwa yote uliwatendea Waebrania, wakakuhukumu Msalabani; wakakunywisha nyongo na siki. Uwape, ee Bwan, kadiri ya matendo yao, kwani hawakusikia kujishusha kwako.

Wana wa Waebrania hawakufurahia tu kwa kukutoa, ee Kristu, lakini tena walitikisa kichwa na kukutukana na kukuchekelea. Uwape, ee Bwana, kadiri ya matendo yao, kwani walitayarisha mashauri ya bure juu yako.

Wala udongo uliyotetemeka, wala mawe yaliyopasuka hazikuweza kuwahakikisha Waebrania, wala pazia ya hekalu, wala kufufuka kwa wafu. Uwape, ee Bwana, kadiri ya matendo yao, kwani walitayarisha mashauri ya bure juu yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . .

Ee Bikira Mzazi-Mungu, tulimutambua Mungu aliyepata mwili kwako, peke yako mtakatifu kamili, mbarikiwa kamili, Na tena, tunakuimbia daima na kukutukuza.

WIMBO 12

Sauti ya Mnane

Bwana anawaambia Wayuda hivi: Ee taifa langu, nilikutendea ninyi? Nilikusikitisha ku ninyi? Niliponyesha vipofu wako na nilitakasa wenye ukoma wako;niliamusha mtu aliyelala miaka mingi kitandani mwake. Ee Taifa langu, nilikutendea ninyi? Utanirudishia ninyi? Pahali pa manna umenipa nyongo, pahali pa maji umenipa siki, pahali pa mapendo yangu umenisulubisha Msalabani. Sitaivumilia. Nitawaita mataifa, wao watanitukuza pamoja na Baba na Roho, na nitawapa uzima wa milele.

Leo pazia ya hekalu imepasuka sababu ya kuwasitaki wasiyo na sheria. Leo jua limeficha nuru yake pakuona Bwana amesulubiwa.

Enyi Waalimu wa Israeli, wa Wayuda na wa Wafarisayo, kundi la Mitume limewalalamikia ninyi: Tazameni hekalu muliyobomoa. Tazameni Mwana-Kondoo muliyesulubisha na kumtoa kaburini. Lakini amefufuka kwa uwezo wake, musidanganyike enyi Wayuda. Ni yeye

aliyewaokoa ninyi baharini. Ni yeye aliyewalisha ninyi jangwani. Yeye ni Uzima, Nuru, yeye ni Amani ya dunia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Salamu Mlango wa mfalme wa utukufu, ambayo alipita peke yake aliye-juu na akaufunga kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**KATHISMA** Sauti ya Mnane

Wakati ulipofika kwa kaifa, ee Mungu, wakati ulipojitoa kwa Pilato, ee Mwamzi, majesi ya mbingu yakatetemeka kwa woga. Ulipanda Msalabani kati ya wanyanganyi wawili;peke yako usiye na zambi, ukawa pamoja na waovu sababu ya wokovu wa mwanadamu. Ee Bwana Mwema kamili, utukufu kwako.

## EVANGELIO YA TANO

Katika Mwevangelizaji Matayo (27, 3-32)

Kisha Yuda aliyemutoa, wakati alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa, akatubu, akarudishia wakubwa wa makuhani na wazee vipande makumi tatu vya veza, akisema: Nimekosa wakati nilipotoa damu isiyo na kosa. Lakini wale wakasema: Hili ni nini kwetu? Uliangalie wewe mwenyewe. Akatupa vipande vya feza katika pahali patakatifu, akaondoka; akatoka inje akajitundika mwenyewe. Wakubwa wa makuhani wakatwa vipande vile vya feza, wakasema: Si

halali kuviweka katika sanduku ya hazina, kwa sababu ni bei ya damu. Wakafanya shauri, wakanunua navyo shamba la mufinyazi liwe pahali pa kuzika wageni. Kwa hivi shamba lile lilitwa shamba la damu hata leo. Halafu likatimia neno lililosemwa na Yeremia nabii, akisema: Wakatwa vipande makumi tatu vya feza, bei yake aliyesabiwa kwa bei, wana wa Israeli waliyemuhesabu kwa bei; wakavitoa kwa shamba la mufinyanzi kama Bwana alivyoniagiza. Basi Yesu akasimama mbele ya liwali; liwali akamwuliza akisema: Wewe ni Mufalme wa Wayuda? Yesu akamwambia: Wewe unasema. Na wakati wakubwa wa makuhani na wazee walipomushitaki, hakujibu neno. Halafu Pilato akamwambia: Husikii maneno mengi wanayokushuhudia? Naye hakumujibu hata neno moja; hata liwali akashangaa sana. Basi kwa

wakati wa siku kubwa liwali kwa desturi alifungulia makutano mufungwa mumoja walivemutaka. Basi palikuwa na mufungwa wa kujulikana, aliyeitwa Baraba. Basi wakati walipokusanyika, Pilato akawaambia: Munataka niwafungulie ninyi nani? Baraba, ao Yesu anayeitwa Kristo? Kwa sababu alijua ya kuwa walimutoa kwa uwivu. Na wakati alipokuwa akiketi juu ya kiti cha hukumu, muke wake akatuma kwake akisema: Usiwe na neno na yule

mutu mwenye haki; kwa sababu nimeteswa maneno mengi leo katika ndoto kwa ajili yake. Basi wakubwa wa makuhani na wazee wakashawishi makutano ili waombe kwa Baraba na kuharibu Yesu. Lakini liwali akajibu, akawaambia: Ni nani katika hawa wawili munayetaka niwafungulie ninyi? Wakasema: Baraba. Pilato akawaambia: Basi, nitafanya nini na Yesu anayeitwa Kristo? Wakasema wote: Asulibiwe. Akasema: Kwa nini? Ametenda ubaya gani? Lakini wakazidi sana kupiga kelele, wakisema: Asulibiwe. Basi wakati Pilato alipoona ya kuwa hakuweza kufanya neno, lakini ya kama kelele lilizidi, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya makutano, akisema: Mimi sina kosa katika damu ya mutu huyu mwenye haki; ninyi mwangalie maneno haya ninyi wenyewe. Watu wote wakajibu, wakasema: Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu. Halafu akawafungulia Baraba, lakini akapiga Yesu mijeledi, na kututoa asulibiwe. Halafu askari za liwali wakachukua Yesu ndani ya Praitorio, wakakusanya kwake k**IKOS**i kizima. Wakamwondolea mavazi yake, wakamuvika nguo nyekundu. Wakasokota taji ya miiba, na kuiweka juu ya kichwa chake na tete mukononi mwake mwa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamuzihaki wakisema: Salamu, Mufalme wa Wayuda! Wakamutemea mate, wakatwa lile tete na kumupiga kichwani. Na wakati walipomuzihaki,

wakamwondolea nguo ile, wakamuvika mavazi yake mwenyewe, wakamuchukua inje kumusulidisha. Na wakati walipotoka, wakaona mutu wa Kurene, jina lake Simoni; huyu walimushurutisha ili abebe musalaba wake.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso Yako, ee Bwana, utukufu kwako.

WIMBO 13

Sauti ya Sita

Makutano ya Wayuda wakamwomba Pilato akusulubishe, ee Bwana. Hawakupata kosa kwako lakini wakamufungua Barabba muovu na wakakuhukumu wewe mwenyi haki kamili. Wakaamua kumwanga damu. Ee Bwana, uwape hii yenyi kuwaelekea, kwani walifikiri mawazo ya bure juu yako.

Huyu ambaye mbele yake vitu vyote vinatetemeka kwa woga na vinaimbia kwa luga yote, Kristu-Nguvu na Hekima ya Mungu, makuhani walimupiga ku uso na wakamunywisha nyongo. Na yeye alivumilia yote sababu ya kutuokoa ku zambi zetu kwa Damu yake, kwani Yeye ni Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Ee Mzazi-Mungu ambaye kwa neno la Malaika ukamzaa Muumba wako kwa namna isiyokadirika, umuombe aokoe roho zetu.

WIMBO 14

Sauti ya Mnane

Ee Bwana, wewe uliyesafiri pamoja na mnyanganyi ambaye mikono yake ni yenyi kuchafuka na damu, utuchukue pia pamoja naye, kwani Wewe ni mwema tena mpenda-wanadamu Mnyanganyi alisema neno fupi msalabani, lakini imani yake ilikua kubwa. Akapata wokovu palepale tena ni yeye wa kwanza kufungua milango ya Paradizo. Utukufu kwako, ee Bwana, wewe mwenyi kupokea toba yake.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Salamu, wewe ambaye kwa sauti ya Malaika ukapokea furaha ya ulimwengu; salamu, wewe uliyestahili kuwa Mama wa Kristu Mungu.

WIMBO 15

Sauti ya Sita

**(SIMERON KREMATE EPI KSILU)**

Leo ametundikwa Msalabani huyu aliyetundika inchi pa maji; *(mara tatu)*
Mfalme wa Malaika amevikwa taji ya miiba;
huyu aliyevika mbingu na mawingu amevikwa nguo nyekundu ya zihaka.
Huyu aliyeopoa Adamu katika Yordani anapokea makofi.
Bwana-Arusi wa Ekklezia ametobolewa misumari.
Mwana wa Bikira amechomwa mkuki.
Tunaabudu Mateso Yako, ee Kristu. Tunaabudu Mateso Yako, ee Kristu. *(mara tatu).*
Utufanye kuona Ufufuo wako Takatifu.

Tusishangilie hii sikukuu sawa Wayuda, kwani Kristu Paska yetu amejitoa sadaka kwa ajili yetu. Tujitakaseni ku uchafu wote na tumuombeni na moyo wa ukweli. Simama, ee Bwana, utuokoe, ewe mpenda-wanadamu.

Msalaba wako, ee Bwana, ni uzima na ulinzi wa watu wako. Wale wenyi kuutumainia wanakuimbia, ee Mungu wetu msulubiwa. Utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Alipokuona umesulubiwa, ee Kristu, huyu aliyekuzaa akalalamika: Ni fumbo gani hii ya ajabu ninaona, ee Mwanangu? Namna gani katika mwili unaweza kufa msalabani, wewe mpaji wa uzima?

**KATHISMA** Sauti ya Ine

Kwa Damu yako ya zamani umetukomboa ku laana ya sheria. Ulipopigiliwa Msalabani na kuchomwa mukuki ulimutirikizia mwanadamu uzima wa milele. Ee Mwokozi, utukufu kwako.

## EVANGELIO YA SITA

Katika Mwevangelizaji Marko. (15, 16-32)

Nao askari walimuchukua ndani ya kiwanja ndiyo Praitorio, wakakusanya pamoja kikosi kizima. Wakamuvika vazi jekundu, wakasokota taji ya miiba, wakamutia kichwani. Wakaanza kumusalimu: Salamu, Mufalme wa Wayuda! Wakamupiga kichwani kwa muti, wakamutemea mate, wakapiga magoti, wakamwabudu. Hata walipokwisha kumuchekea, wakamwondolea nguo nyekundu, wakamuvika mavazi yake mwenyewe, wakamuchukua inje ili wamusulibishe. Walishurutisha mutu aliyepita akitoka mashamba, Simoni Mukurene, baba ya Alesanduro na Rufu, ili achukue musalaba wake. Wakamuleta hata pahali palipoitwa Golgota, maana yake: Mufupa wa kichwa. Wakamupa mvinyo iliyotiwa manemane, lakini yeye hakuipokea. Wakamusulibisha, wakagawa mavazi yake, wakiyapigia kura, kila mutu atwae nini. ILikuwa saa tatu, nao walimusulibisha. Maandiko ya mashitaki yake yaliandikwa juu: Mufalme wa Wayuda. Pamoja naye wakasulibisha wanyanganyi wawili, mumoja mukono mwake wa kuume, na mumoja mukono wake wa kushoto. (Basi andiko likatimizwa linalosema: Alihesabiwa pamoja na wenye kuasi). Nao waliopita walimutukana wakitikisisha vichwa vya wakisema: Ha! wewe mwenye kuvunja hekalu na kulijenga katika siku tatu! Ujiokoe wewe mwenyewe, ushuke musalabani! Vile wakubwa wa makuhani wakamuzihaki wao kwa wao pamoja na waandishi,

wakasema: Aliokoa wengine, hawezi kujiokoa yeye mwenyewe. Kristo, mufalme wa Israeli, ashuke sasa musalabani, tupate kuona na kuamini. Hata wale waliosulibiwa pamoja naye wakamutukana.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso Yako, ee Bwana, utukufu kwako.

## H E R I

Sauti ya Ine.

Utukumbuke, ee Bwana, katika ufalme wako, wakati utakapokuja katika ufalme wako.

Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa mbingu ni wao.

Heri wenye huzuni, maana wao watatulizwa.

Heri wenye upole, maana wao watariti inchi.

Ni kwa sababu ya mti mmoja Adamu alifukuzwa katika Paradizo. Ni katika mti wa Msalaba mnyanganyi aliingiamo. Alipokula tunda; Adamu akakataa amri ya Muumba. Mnyanganyi

aliposulubiwa pamoja nawe akaungama ya kama Wewe ni Mungu mwenyi kujificha. Utukumbuke nasi pia, ee Mwokozi, katika ufalme wako.

Heri wenye njaa na kiu ya kupata haki, maana wao watashiba.

Watu wasiyo na sheria walinunua kwa Mfuasi Muumba wa Sheria. Wakamupeleka ku hukumu ya Pilato wakilalamika: Asulubiwe, wao aliyewalisha manna jangwani! Lakini sisi tufwate mfano wa mnyanganyi mwema na tulalamike na imani: Utukumbuke, ee Bwana, katika ufalme wako.

Heri wenye huruma, maana wao watahurumiwa.

Baraza kubwa inaamua, Wayuda waovu wanamulalamikia PIlato na ukali wakisema: Asulubiwe, huyu Kristu mwenye haki! Utufungulie Barabba! Lakini sisi, tumwambie neno la mnyanganyi mwenyi akili: Utukumbuke, ee Bwana, katika ufalme wako.

Heri wenyi moyo safi, maana wao watamwona Mungu.

Ee Kristu, ubavu wako wenyi kuleta uzima kama chemchem ya Edeni unamwangia Ekklezia yako sawa Paradizo ya kiroho. Hii Chemchem inagawanyika katika Evangeli ine yenyi kunywisha ulimwengu ikifurahisha viumbe na yakiwafundisha mataifa yote kuabudu na imani ufalme.

Heri wenye kuleta amani maana wao wataitwa wana wa Mungu.

Ulisulubiwa kwa kutaka kwako sababu ya kunitirikizia mimi rehema. Ubavu wako ulichomwa mkuki sababu ya kunipa chemchem ya uzima. Ulitobolewa misumari ili ukuu wa Mateso yako unifunulie ukubwa wa ufalme wako tena nikulalamikie: Ee Kristu, mpaji wa uzima, utukufu kwu Msalaba wako wenyi kuleta wokovu na kwu Mateso Yako.

Heri wenye kuzulumiwa sababu ya haki, maana ufalme wa mbingu ni wao.

Viumbe vyote vilitetemeka, ee Kristu, wakati vilikuona umesulubiwa msalabani;misingi ya inchi yalitikisika kwa woga;nyota zilifichama kwa woga wa uwezo wako;pazia ya hekalu ikapasuka, milima ilitikisika, mawe yakapasuka na mnyanganyi mwema akalalamika pamoja nasi: Unikumbuke katika ufalme wako.

Heri ninyi kama watu wanawatukana na kuwazulumu na kuwachongea kwa uwongo kila namna ya uovu kwa ajili yangu mimi.

Msalabani ulipasua hukumu juu yetu sisi, ee Bwana, wakati ulihesabiwa katika wafu; ulimufunga mzulumu mnyororo, uliwafungua wanadamu wote ku vifungo vya mauti katika Ufufuo wako ambao nuru inatujaza, ee Bwana mpenda-wanadamu, sisi wenyi kukulalamikia: Utukumbuke, ee Mwokozi, katika Ufalme wako.

Furahini, shangilieni, kwani tuzo yenu ni kubwa mbinguni.

Ee Bwana, ulipanda Msalabani, uliharibu nguvu ya mauti, uliondoa hukumu juu yetu sisi utupe toba ya mnyanganyi, wewe pepe yako mpenda-wanadamu, sisi wenye kukutumikia na imani, ee Kristu Mungu wetu, na wenyi kukulalamikia: Utukumbuke, ee Mwokozi, katika utukufu wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Enyi waaminifu, kwa moyo mmoja tumuombe na kumutukuza kama inavyostahili, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; Mungu mmoja katika Watu tatu, wasiyotengana, na bila mchanganyiko; Mungu msiyekaribika na mwenyi kutuokoa ku moto ya mateso.

Sasa na siku zote. . .

Ni mama, ee Kristu, anastahili kutuombea kwako. Bikira, alikuzaa; alikaa Bikira kisha kuzaa. Tunaweza, ee Bwana mwenyi huruma, kupata rehema tukikulalamikia: Utukumbuke, ee Mwokozi, katika ufalme wako.

**PROKIMENON** Sauti ya Ine

Waligawanya nguo zangu katikati yao, na wakaipigia kanzu yangu kura. Kituo: Mungu wangu, Mungu wangu, unisikilize. Kwa ninyi umeniacha?

## EVANGELIO YA SABA

Katika Mwevangelizaji Matayo (27, 33-54).

Na wakati walipofika pahali palipoitwa Golgota, maana yake Mufupa wa kichwa, wakamupa mvinyo iliyochanganyika na nyongo; na wakati alipoionja hakutaka kunwa. Na wakati walipokwisha kumusulibisha, waligawa mavazi yake katikati yao wakipiga kura; wakaketi na kumulinda pale. Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaki yake yaliyoandikwa: Huyu ni Yesu Mufalme wa Wayuda. Wakati huu wanyanganyi wawili walisulibiwa pamoja naye, mumoja kwa mukono wake wa kuume, na mumoja kwa kushoto. Nao waliopita njiani wakamutukana wakitikisisha vichwa vyao wakisema: Wewe mwenye kuvunja hekalu na kulijenga tena katika siku tatu, ujiokoe mwenyewe; kama ukiwa Mwana wa Mungu, shuka musalabani. Vile wakubwa wa makuhani wakimuzihaki pamoja na waandishi na wazee wakasema: Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa yeye mwenyewe. Yeye ni Mufalme wa Israeli; ashuke sasa musalabani na tutamwamini. Anaamini Mungu; amwokoe sasa kama anamutaka; kwa sababu alisema: Mimi ni Mwana wa Mungu. Wanyanganyi walisulubiwa pamoja naye walimutukana hivi vilevile. Basi toka saa sita giza lilikuwa juu ya inchi hata saa tisa. Na karibu na saa tisa Yesu alipaza sauti akisema: Eloi, Eloi, lama sabaktani; maana yake: Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? Na wengine wao waliosimama pale, wakati waliposikia, wakasema: Mutu huyu anaita Elia. Na mara moja mumoja wao akakimbia, akatwaa sifongo na kuijaza siki, akaitia juu ya muti, akamukunywesha. Wale wengine wakasema: Acha; tuone kama Elia anakuja kumwokoa. Yesu akatoa sauti kubwa tena, akatoa roho yake. Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; inchi ikatetemeka; miamba ikapasuka, makaburi

yakafunguliwa, na miili mingi ya watakatifu waliokwisha kulala ilifufuliwa; na wakitoka katika makaburi nyuma ya ufufuko wake, wakaingia katika muji mutakatifu na kutokea kwa watu wengu. Basi akida, nao waliokuwa pamoja naye wakilinda Yesu, wakati walipoona tetemeko la inchi, na maneno yaliyofanyika wakaogopa sana, wakisema: Kweli huyu alikuwa Mwana wa Mungu.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso Yako, ee Bwana, utukufu kwako.

**ZABURI** 50(51).

## EVANGELIO YA MNANE.

Katika Mwevangelizaji Luka (23, 32-49)

Na wawili wengine, watenda mabaya, walipelekwa pamoja naye kuuawa. Wakati walipofika pahali palipoitwa Mufupa wa Kichwa, kule walimusulibisha, na wale watenda mabaya, mumoja kwa mukono wa kuume, na mumoja kwa mukono wa kushoto. Yesu akasema: Baba, uwasamehe, kwa sababu hawajui neno wanalolifanya. Wakigawanya nguo zake, wakapiga kura. Watu wakasimama wakitazama. Lakini wakubwa wakamuzihaki, wakisema: Aliokoa wengine,

ajiokoe yeye mwenyewe kama yeye ni Kristo wa Mungu, Muchaguliwa. Askari vilevile wakamuzihaki, wakakuja kwake wakimupa siki, na kusema: Kama wewe ni mufalme wa Wayuda ujiokoe wewe mwenyewe. Na maandiko yaliandikwa juu yake kwa maandiko ya Kiyunani na Kiroma na ya Kiebrania, Huyu ni Mufalme wa Wayuda. Mumoja wa wale watenda mabaya waliotundikwa pamoja naye akamutukana, akisema: Si wewe uliye Kristo? Ujiokoe mwenyewe pamoja nasi. Lakini wa pili akamuhamakia, akisema: Huogopi hata Mungu, maana wewe ni katika hukumu ile ile? Na sisi kwa kweli, sababu tunapokea malipo yanayostahili kwa matendo yetu, lakini mutu huyu hakufanya neno lisilofaa. Akamwambia Yesu: Bwana, unikumbuke wakati unapokuja katika ufalme wako. Yesu akamwambia: Kweli ninakuambia, leo utakuwa pamoja nami katika Paradiso. Ilikuwa karibu na saa sita azuhuri, na giza lilikuwa juu ya inchi yote hata saa tisa; jua lilipunguka; pazia la hekalu likapasuka katikati. Yesu alipolia kwa sauti kubwa, akasema: Baba, katika mikono yako ninaweka roho yangu; na alipokwisha kusema maneno haya akatoa roho. Mukubwa wa askari, alipoona maneno haya, akatukuza Mungu akisema: Kweli mutu huyu alikuwa mwenye haki. Na makutano yote waliokusanyika kuangalia maneno haya, walipotazama maneno yaliyofanyika, wakarudi wakipigapiga vifua vyao. Rafiki zake zote na wanawake waliofuatana naye toka Galilaya, wakasimama mbali, wakiangalia

maneno haya.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

HIRMOS

Sauti ya Sita

Nitakuomba alfajiri, ewe mwenye rehema kamili, wewe uliyejishusha bila kubadilika, na ukavumilia hata Mateso. Ee Neno la Mungu, mpenda-wanadamu, unipe amani.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Watumishi wako, waovu wenyi miguu michafu, walipotakaswa katika ushirika ku Fumbo yako kimungu, wakapanda pamoja nawe toka Sayuni mpaka ku mlima wa mizeituni wakikuimbia, ee Kristu mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Enyi marafiki zangu, musishambuliwe kwa woga tazameni saa imekaribia. Nitafungwa na kuawa na makafiri. Ninyi mutasambazwa na mutaniacha, lakini nitawakusanya ili munitangaze mimi mpenda-wanadamu.

**KATAVASIA**: Nitakuomba alfajiri. . .

**SHEMASI AO PADRI:** Ektenia Kidogo.

**KONTAKION** Sauti ya Mnane

Kujeni tumtukuze huyu aliyeteswa Msalabani kwa ajili yetu. Maria alimuona juu ya mti na akasema: Japo umeteswa Msalabani, wewe ni Mwanangu na Mungu wangu.

**IKOS**

Maria Mwana-Kondoo jike alipoona Mwana-Kondoo wake amepeleka kutolewa sadaka akamufuata pamoja na wanawake wengine na akasema: Unaenda wapi, ee Mwanangu? Sababu gani unaenda haraka? Arusi ingine inafanyika ku kana? Ni kule unaenda kugeuza maji kuwa vinyo? Nitaenda pamoja nawe Mwanangu ao nitakuogojea, unijibu, usipite mbele yangu kimya, ee Wewe uliyenilinda mimi Safi. Kwani wewe ni Mwanangu na Mungu wangu.

*Sasa tunasoma Sinaksarion ya Watakatifu ya leo. Kisha hivi:*

Mu kazi Tano mkumbwa na takatifu tunakumbuka Mateso kwa ajili ya wokovu wetu ya Bwana Yesu Kristu Mungu na Mwokozi wetu, nikusema alivumilia kwa ajili yetu matusi, ma kofi, zihake, nguo nyekundu, tete, siki, misumari, mukuki na tena kabisa Msalaba wake na lufu, tena alipokea maneno ya ule munyanganyi aliyemuamini na alimukiri sawa Mungu wake kweli na Mwokozi. Ku wema yako kumbwa, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu utuhurumie. Amina.

Wimbo wa Mnane HIRMOS

Sanamu iliyosimikwa juu ya Mungu ikazikahiwa na Vijana Watakatifu? Baraza ya wasiyo na sheria inakusanyika juu ya Kristu na inafanya mashauri ya bure; inatafuta kuua huyu mwenyi kushika uzima mkononi mwake, ambaye viumbe vyote vinasifu na kumutukuza milele.

Utukufu Kwako, ee Mungu, utukufu kwako.

Ee Kristu, uliwaambia Wafuasi wako: Fukuzeni usingizi machoni mwenu; kesheni na muombe kusudi msianguke katika majaribu. Zaidi wewe Simoni, kwani mwenyi nguvu zaidi atapita katika majaribu kubwa. Ewe Petro, fahamu ya kama mimi ni huyu viumbe vyote vinasifu na kutukuza milele.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu. . .

Petro alilalamika: Ee Rabi, sitasema kamwe neno mbaya juu yako. Hata kama wengine wote watakukana mimi nitakufa pamoja nawe, kwa sababu nakuja: Sikufunuliwa neno hili na mwanadamu ila Baba yako aliyekufunua kwangu, wewe ambaye viumbe vyote vinasifu na kutukuza milele.

Tunamuhimidi Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Bwana tunamutukuza.

Bwana anasema: Ee Mwanadamu, haujui kabisa hekima na maarifa ya kimungu; haukufika chini ya haki zangu. Wewe ni mwanadamu, usijitukuze. Utanikana mara tatu. Mimi ambaye viumbe vyote vinasifu na kutukuza milele,

Sasa na siku zote

Bwana alisema: Ee Simoni Petro, unakataa hii nilikuambia, lakini mtumishi mumoja mwanamuke atakuonyeshayo sasa hivi: atakujongea wewe na atakuogopesha. Lakini kwa machozi yako ya uchungu utapata rehema yangu mimi ambaye viumbe vyote vinnasifu na kutukuza milele.

Tumsifu, tumtukuza, tumuabudu Bwana, tukimwimbia na kumshangilia milele

**KATAVASIA**: Sanamu iliyosimikwa juu ya Mungu ikazikahiwa. . .

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tunamuheshimu kwa nyimbo na kumtukuza.

WIMBO 9 HIRMOS

Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila Kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kundi la makafiri wapagani, baraza ya wadanganyifu inakusudia na inasimama mbele yako, ee Kristu. Inakuhukumu kufa kama muovu, wewe Muumba wa vitu vyote ambaye tunatukuza.

Utukufu kwako. . .

Makafiri walisahau Sheria. Walitafuna bure maneno ya manabii; Wanakukokotea kama mwana-Kondoo ku sadaka isiyo na haki wewe Rabi wa vitu vyote ambaye tunatukuza.

Utukufu kwa Baba. . .

Uzima umekuwa wa wapagani. Waandishi na makuhani, mateka ya chuki yao, wanamuteswa mpaji wa uzima ambaye tunatukuza.

Sasa na siku zote. . .

Ee Mfalme, walikuzunguka kwa kundi, walikupiga ku shavu, walikuuliza, walikushuhudia uwongo. Ulivumilia yote na ulituokoa.

**KATAVASIA**

Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu;uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

**SHEMASI AO PADRI**: Ektenia Kidogo.

**EKSAPOSTILARION**

Ee Bwana, kama kwa puda kidogo ulivyomstahilisha mnyanganyi katika Paradizo, uniangaze mimi pia na mti wa Msalaba wako na uniokoe *(mara tatu)*.

## EVANGELIO YA TISA

Katika Mwevangelizaji Yoane (19, 25-37)

Lakini karibu na musalaba wa Yesu alisimama mama yake, na ndugu muke ya mama yake, Maria mwanamuke wa Kleopa, na Maria Magdalene. Basi wakati Yesu alipoona mama yake, na yule mwanafunzi mupendwa akisimama karibu, akamwambia mama yake: Mwanamuke, tazama mwana wako! Halafu akamwambia yule mwanafunzi: Tazama, mama yako. Na kutoka saa ile mwanafunzi yule alimupeleka kwake. Nyuma ya maneno haya, Yesu akijua ua kama maneno yote yamekwisha kumalizwa, ili andiko litimizwe, akasema: Nini kiu. Palikuwa kule chombo kimejaa siki; wakajaza sifongo na siki, wakatia juu ya hisopo, wakatia kwa kinwa chake. Basi wakati Yesu alipopokea siki, akasema: Imekwisha; akainama kichwa chake, akatoa roho yake. Basi Wayuda, kwa sababu ilikuwa Maandalio, miili isikae juu ya musalaba siku ya sabato (kwa sababu siku ya sababto ile ilikuwa siku kubwa), wakaomba Pilato, miguu yao ivunjwe, na waondolewe. Basi askari walikuja, wakamuvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulibiwa pamoja naye; lakini wakati walipofika kwa Yesu, wakaona ya kama amekwisha kufa, hawakuvunja miguu yake; lakini mumoja wa askari alimuchoma mbavu yake kwa mukuki, na mara moja ilitoka damu na maji. Naye aliyeona alishuhudia, na ushuhuda wake ni kweli: na

yeye anajua ya kwamba anasema kweli, ninyi mupate kuamini. Kwa maana maneno haya yalifanyika, ili andiko litimie: Hapana mufupa wake utakaovunjwa. Na tena andiko lingine linasema: Watamutazama yeye waliyemuchoma.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

## MASIFU

Sauti ya tatu
Kila mwenye. . .

Wimbo:
Ee Israeli, mzaliwa wangu wa kwanza, umenitoa mara mbili: Umeniacha mimi Chemchem ya maji ya uzima na umejichimbulia kisima cha lufu; umenipigilia Msalabani na ukaomba wamufungue Barabba. Mbingu ilitetemeka kwa woga na jua lilificha miangaza yake. Lakini wewe Israeli haukutubu, lakini ukanitoa ku lufu. Uwasamehe, ee Baba Mtakatifu kamili, kwani hawajui ile wanayofanya.

Kila sehemu ya mwili wako takatifu ilitukanwa kwa ajili ya wokovu wetu: Kichwa chako kilivikwa taji ya miiba, Uso wako ulitemewa mate, mashavu yako yalipigwa makofi, midomo yako ilionja siki na nyongo, masikio yako yalisikia matusi ya makafiri, mabega yako yalipigwa; mkono wako ulishika tawi. Mwili wako wote ulipanuliwa Msalabani, viungo vyako vilitobolewa na misumari, ubavu wako ulichomwa kwa mkuki. Ee wewe uliyeteswa kwa ajili yetu na uliyetuopoa ku mateso, uliyejishusha mpaka ku hali yetu kwa ajili ya mapendo kwa mwanadamu na uliyetuinua, ee Mwokozi mwenyezi, utuhurumie.

Wakati uliposulubiwa, ee Kristu, viumbe vyote vilikuona na vikatetemeka kwa woga; udongo ikatetekema kwa woga wa uwezo wako. Leo kupazwa kwako ni kuanguka kwa Waebrania: Pazia ya Hekalu inapasuka katika vipande viwili, makaburi yanafunguka na wafu wanafufuka toka makaburi yao, akida anapoona hii muujiza anatetemeka. Mama yako mwenyi kusimama pembeni yako analia na kulalamika: Namna gani sitalia, namna gani sitapigapiga kifua pakukuona umetundikwa na kufufuka katika wafu, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya Sita
Waliondoa manguo yangu na wakanivika kanzu nyekundu. Walinivika taji ya miiba; wakaniweka tete mkononi Mwangu ili niwavunje kama chombo cha udongo.

Sasa na siku zote. . .
Nilitoa mabega yangu kwa kupigwa. Sikuficha uso wangu kwa kutemewa mate. Nilifika ku hukumu ya Pilato. Na niliteswa Msalabani kwa ajili ya wokovu wa dunia.

### EVANGELIO YA KUMI

Katika Mwevangelizaji Marko (15, 43-47)
Yosefu mutu wa Arimatea, mutu wa baraza mwenye heshima, naye mwenyewe alikuwa akitazamia ufalme wa Mungu vilevile, akafanya ujasiri, akaingia kwa Pilato, akamwomba mwili wake Yesu. Pilato akashangaa kwamba amekwisha kufa, akaita akida, akamwuliza kama amekufa wakati murefu. Alipojulishwa kwa yule akida, alimupa Yosefu maiti. Naye alinunua sanda, akamushusha, akamufunika kwa ile sanda, akamuweka katika kaburi lililochongwa mwambani; akafingirisha jiwe mbele ya mulango wa kaburi. Naye Maria Magdalene na Maria mama ya Yose walitazama pahali alipowekwa.
**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

**DOKSOLOGIA KIDOGO**

*Ektenia ukubwa:*

Tumaziza ombi letu. . . . . . . . . .

**EVANGELIO KUMI NA MOJA**

Katika Mwevangelizaji Yoane (19, 38-42)

Na nyuma ya maneno haya, Yosefu mutu wa Arimatea, akiwe mwanafunzi wa Yesu, lakini kwa siri (maana aliogopa Wayuda) akaomba Pilato ruhusa aondoe mwili wa Yesu, na Pilato alimupa ruhusa. Basi alikuja akaondoa mwili wake. Na Nikodemo alikuja vilevile, yule aliyekija kwanza kwa Yesu usiku, na alileta machanganyiko ya manemane na uude, karibu na ratli mia. Basi wakakamata mwili wa Yesu, wakaufunga na sanda ya kitani pamoja na yale manukato, kama desturi ya Wayuda katika maziko. Na pahali pale aliposulibiwa palikuwa shamba; na ndani ya shamba lilikuwa kaburi jipya, bado hajatiwa mutu ndani yake. Basi kule waliweka Yesu kwa sababu ya Maandalio ya Wayuda, kwa sababu kaburi lilikuwa karifu.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

## APOSTIKHA

Sauti ya Kwanza

Ee Kristu, viumbe vyote vilishikwa na woga wakati vilikuona juu Msalabani: Jua lilipata giza na udongo ikatikisika. Vyote viliteswa pamoja na Muumba wa vyote. Ee Bwana, wewe uliyevumilia Mateso kwa ajili yetu, utukufu kwako.

Kituo: Walijigawanyia nguo zangu na wamepigia kanzu yangu kura.

Sauti ya mbili

Enyi watu wakafiri na wasiyo na sheria, sababu gani munawaza mashauri ya bure? Sababu gani munahukumu ku lufu uzima wa ulimwengu? Hii ni muujiza! Tazama Muumba wa dunia ametolewa mikononi mwa watu wasiyo na sheria. Tazama mpenda-wanadamu ameinuliwa Msalabani sababu ya kuwakomboa Wafungwa ku Hadeze na wenye kumulalamikia: Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

Kituo: Wamenilisha nyongo, na kwa kiu yangu wameninywisha siki.

Ee Neno, Bikira Mtakatifu kamili anapokuona Msalabani analia na moyo wake wa umama unahuzunika kwa uchungu. Analia kwa uchungu rohoni mwake. Anaondoa nywele zake tena anararua uso yake anajipigapiga pa kifua akiomboleza: Ole wangu, ee Mwanangu Mtakatifu! Ole wangu ee Nuru ya hii dunia! Sababu gani umejificha machoni mwangu wewe Mwana-Kondoo wa Mungu? Yanaposikia hii maneno majeshi ya mbinguni yanatetemeka na kusema: Ee Bwana usiyejuliwa, utukufu kwako.

Kituo: Mungu ni Mfalme wetu tangu mbele ya nyakati, ameonyesha wokovu duniani.

Ee Kristu, alipokuona umetundikwa Msalabani, wewe Mungu na Muumba wa vitu vyote, huyu aliyekuzaa bila mbegu akalalamika na uchungu: Wapi uzuri wa uso wako, ee Mwanangu?

Sitaweza kuvumilia kukuona umesulubiwa bila haki. Ujiharikishe kuamka, nikuone umefufuka katika wafu siku ya tatu.

Utukufu kwa Baba. . .

Sauti ya Mnane

Ee Bwana, viumbe vyote vilishikwa na woga na vilitetemeka wakati vilikuona umeinuliwa Msalabani. Na ikaizuia dunia kuangamiza wale waliyokusulibisha. Ukaamuru hadeze ifungue wafungwa wake kusudi wafu wafufuke. Ee Mwamzi wa walio hai na wa wafu, haukuleta mauti lakini uzima. Ee mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . .

Sauti ya Mnane

Tazama waamzi waovu wanatoa hukumu yao. Yesu anahukumiwa;Yesu anahukumiwa afe Msalabani. Viumbe vyote vinalia pakuona Bwana amesulubiwa Msalabani. Uliteswa mwilini mwako kwa kunikomboa. Ee Bwana mwema kamili, utukufu kwako.

## EVANGELIO KUMI NA PILI

Katika Mwevangelizaji Matayo ( 27, 62-66)

Basi kesho yake, iliyo siku nyuma ya Matengenezo, wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walikusanyika kwa Pilato, wakisema: Bwana, tunakumbuka ya kama yule mudanganyifu alisema wakati alipokuwa angali hai: Nyuma ya siku tatu nitafufuka tena. Agiza basi kaburi lilindwe hata siku ya tatu, wanafunzi wake wasije na kumwiba na kuwaambia watu: Amefufuka toka wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita wa kwanza. Pilato akawaambia: Muna askari walinzi; kwendeni mulilinde kwa kadiri munavyoweza. Basi wakakwenda, wakalinda kaburi wakitia lile jiwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi.

**WAIMBAJI**: Utukufu ku Mateso yako, ee Bwana, utukufu kwako.

Ni vema kumuungama Bwana kuimbia Jina Lako, ewe uliye-juu kutangaza alfajiri rehema yako, ne ukweli wako usiku kucha.

**PADRI**: Ni vema kuungama Bwana, . . .

TRISAGION

Apolitikion. Sauti ya Ine.

Kwa Damu yako ya Samani umetukomboa ku laana ya sheria. Ulipopigiliwa Msalabani na kuchomwa mkuki ulimutirikizia mwanadamu uzima wa milele. Ee Mwokozi, utukufu kwako.

**PADRI**: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa. . . Hekima.

Kuaga (Apolisis): Utukufu, kwako, ee Kristu Mungu, matumaini wetu, utukufu kwako. Yeye aliyevumilia, kwa ajili ya wokovu wetu, kumtemea mate, kupigwa makofi na kutukanwa, msalaba na lufu, Kristo Mungu wetu kweli. . .

# SIKU YA TANO MKUBWA

## ESPERINOS YA EPITAFIOS

**PADRI**: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote hata milele na milele.

**MSOMAJI**: Amina.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu
Njooni tumwiname na tumsujudu Kristu Yeye Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu, aliye Mfalme wetu.

**ZABURI** 103(104) Zaburi ya Mangaribi: Bwana nimekuita... *(sauti ya kwanza).*

WIMBO YA MANGARIBI.

Sauti ya kwanza
Ondoa roho yangu katika kifungo chake. . .
Ee Kristu, viumbe vyote vilitetemeka kwa woga wakati vilikuona Msalabani. Jua lilififia. Inchi ikatetemeka. Yote iliteswa pamoja na Muumba wa vitu vyote.

Ee Bwana, wewe uliyevumilia Mateso kwa ajili yetu, utukufu kwako.

Sauti ya mbili
Enyi watu makafiri na wasiyo na sheria. . . *(Angalia yulu kwa Apostikha).*

Ee Neno, Bikira Mtakatifu kamili anapokuona. . . *(Angalia yulu kwa Apostikha)*

Ee Kristu, alipokuona umetundikwa Msalabani. . . (*Angalia yulu kwa Apostikha)*

Sauti ya Sita
Leo Mfalme wa vitu vyote anasimama mbele ya Pilato, Muumba wa ulimwengu ametolewa Msalabani kwa kutaka kwake kama Mwana-Kondoo mwenye kutolewa ku sadaka. Ametobolewa na misumari na kuchomwa mkuki, sifongo inanywisha huyu aliyenyeshesha manna. MKombozi wa dunia anapigwa usoni, Muumba wa wote anatukanwa kwa Watumwa wake.

Ee Mapendo ya Rabi aliyemuomba Baba yake kwa ajili ya Wayuda wake: Ee Baba, uwasamehe hii zambi, kwani watu hawa wasiyo na sheria hawajui kosa wanalotenda.

Utukufu kwa Baba. . Sauti ya sita.
Namna gani baraza ya wasiyo na sheria inaweza kuhukumu ku lufu Mfalme wa viumbe vyote bila kukumbuka mema yake? Aliikumbusha wakati aliposema: Ee taifa langu, nilikutendea ninyi? Sikujaza Yudea na miujiza? Sikufufua wafu na neno moja tu? Sikuponyesha vilema na wagonjwa wote? Unanirudishia ninyi? Unasahau mema yangu, unanipiga kwa vidonda pahali pa

kuniponyesha. Pahali pa uzima umenitoa ku lufu, unatundika mfazili Msalabani kama muovu. Mpana-sheria kama msiye na sheria, mfalme wa ulimwengu kama mwenyi kuhukumiwa. Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako!

Sasa na siku zote. . .

Tunaona fumbo ya ajabu ikitendeka leo. Msiyeguswa anakamatwa, huyu mwenyi kufungua Adamu ku laana anafungwa minyororo. Huyu mwenyi kutazama mafigo na mioyo anatazamiwa bila haki, gereza inafunga huyu aliyefunga kuzimuni. Wanamuonyesha Pilato huyu ambaye uso wake inatetemesha majeshi ya mbinguni. Muumba anapigwa ku uso na mkono wa kiumbe chake. Mwamzi wa wazima na wafu anahukumiwa Msalabani. Mwenyi kuharibu hadeze anafungwa kaburini. Kwa huruma yake anavumilia yote sababu ya kukomboa wanadamu ku

laana. Ee Bwana mvumilivu, utukufu kwako.

*Sasa Padri anafanya (Isodos) Kuingia pamoja na Evangelio na atasema:*

Hekima. Simameni.

MWANGAZA  UPOLE (ILARON)

**PROKIMENON** Sauti ya Ine

Zaburi 21 (22) Walijigawanyia nguo zangu na wamepigia kanzu yangu kura.

Kituo:  Mungu wangu, Mungu wangu, unisikilize, sababu gani umeniacha?

Somo la Unabii

Kitabu cha Kutoka 33, 11-23

Bwana akasema na Musa uso kwa uso, kama mutu anavyosema na rafiki yake. Kisha akarudi tena kwa kambi; lakini mutumishi wake Yosua, mwana wa Nuni, kijana, hakuondoka katika Hema. Musa akamwambia Bwana:  Tazama, unaniambia:  Toa watu hawa, nawe hukunijulisha ni nani utakayetuma pamoja nami. Lakini umesema:  Ninakujua kwa jina lako, na umepata neema mbele yangu. Basi sasa, ninakuomba, kama ikiwa nimepata neema mbele yako, unionyeshe sasa njia zako, ili nikujue hata nipate neema mbele yako; na fikili taifa hili lililo watu wako. Akasema:  Uso wangu utakwenda pamoja nawe, na nitakupa raha. Akamwambia:  Kama uso wako usipokwenda pamoja nami, usituchukue toka hapa. Kwa maana itajulikana kwa njia gani ya kama nimepata neema mbele yako, mimi na watu wako? Si kwa sababu unakwenda pamoja nasi, hata mimi na watu wako tutengwe na watu wote walio juu ya uso wa inchi? Bwana akamwambia Musa:  Nitafanya neno hili ulilosema vilevile:  Kwa maana umepata neema mbele yangu, na ninakujua kwa jina lako. Akasema:  Unionyeshe, ninakuomba. Utukufu kwako. Akasema:  Nitapitisha wema wangu wote mbele yako, na nitatangaza jina la Bwana mbele yako; na nitaonyesha neema kwake nitakayemwonyesha neema, na nitarehemu yeye nitakayemurehemu. Akasema:  Huwezi kuona uso wangu; kwa sababu mutu hawezi kuona uso wangu na kuishi. Bwana akasema:  Tazama, pahali ni hapa karibu nami, na utasimama juu ya mwamba; na itakuwa, wakati utukufu wangu unapopita, nitakutia pahali mwamba ulipopasuka, na nitakufunika na mukono wangu hata nitakapokuwa nimekwisha kupita; ba nitaondosha mukono wangu, na utaona mugongo wangu; lakini uso wangu hautaonekana.

**PROKIMENON**  Sauti ya Ine. Zaburi 34 (35)

Ee Bwana, hukumu wale wenyi kunikatalia haki yangu na wenyi kunigombanisha.

Kituo:  Chukua mkuki wako na ugao yako, simama unisaidie.

Somo la Kitabu cha Yobu 42, 12-17

Hivi Bwana akabariki mwisho wa Yobu kupita mwanzo wake:  naye alikuwa na kondoo elfu kumi na ine, na ngamia elfu sita, na jozi za ngombe elfu moja, na punda wake elfu moja. Alikuwa vilevile na wana saba na binti watatu. Akaita jina lake la kwanza Yemima; na jina lake la pili, Kezia; na jina lake la tatu, Kereni-hapuki. Na katika inchi ile yote hawakuwa wanawake

waliokuwa wazuri kama binti za Yobu: baba yao akawapa uriti kati ya ndugu zao wanaume. Nyuma ya maneno haya Yobu akaishi miaka mia moja makumi ine, akaona wana wake, na wana wa wana wake, hata vizazi vine. Hivi Yobu akakufa, muzee sana na mwenye siku nyingi.

Somo la Unabii wa Isaya 52, 13-15; 53, 1-12; 54, 1

Tazama, mutumishi wangu atafanya kwa akili; atatukuzwa na kunyanyuliwa juu, naye atakuwa juu sana. Kama vile wengi walishangaa juu yako, (uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mutu ye yote, na sura yake zaidi ya watoto wa watu), ndivyo atashitusha mataifa mengi; wafalme watamufungia vinywa vyao; maana maneno wasiyoambiwa watayaona, na maneno wasiyoyasikia

watafahamu. Ni nani aliyeamini habari zetu? Na mukono wa Bwana amefunuliwa nani? Maana atakua mbele yake kama chipuko, na kama shina katika inchi kavu; Yeye hana sura wala uzuri, na wakati tunapomwona hana uzuri hata tumutamani. Amezarauliwa na kukataliwa na watu; Mutu wa huzuni, na mwenye kujua taabu: Na kama mutu watu wanayemufichia nyuso zao, alizarauliwa, na hatukumuhesabu kuwa kitu. Kweli amechukua taabu zetu, na amebeba huzuni

zetu; lakini tulimwona akipigwa, akiteswa na Mungu, na kuhuzunishwa. Lakini aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu. Azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mumoja kwa njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maivu yetu sisi sote. Alionewa, na aliteswa,

lakini hakufungua kinywa chake; kama mwana-kondoo anayepelekwa kuchinjwa, na kama kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyoya yake; hakufungua kinywa chake. Aliondolewa kwa kuonewa na kuhukumiwa, na kwa kizazi chake, nani aliyewaza ya kuwa amekatiliwa mbali na inchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Wakamufanyia kaburi pamoja na waovu; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; hata yeye hakufanya jeuri, wala hila haikuonekana kinywani mwake. Hata hivi ilipendeza Bwana kumuchubua; amemuhuzunisha. Wakati utakapotolea nafsi yake kuwa zabihu kwa zambi, ataona uzao wake, atazidisha siku zake, na mapenzi ya Bwana yatasitawi katika mukono wake. Ataona ya taabu ya nafsi yake, naye atatulia: kwa maarifa yake mutumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki: Naye atachukua maovu yao. Kwa sababu hii nitamugawia sehemu pamoja na wakubwa, naye atagawa nyara pamoja na wahodari, kwa sababu alimwanga nafsi yake hata kufa, akahesabiwa pamoja na wale wenye kukosa. Na kuombea wenye kukosa. Na alichukua zambi za watu wengi, na kuombea wenye kukosa. Imba, wewe uliye tasa, wewe

usiyezaa; paza sauti yako kwa kuimba, piga kelele kwa furaha, wewe usiyekuwa na uchungu wa kuzaa; maana watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko watoto wake aliye na mume, Bwana anasema.

**PROKIMENON** Sauti ya Sita

Wamenitupa katika shimo refu, katika giza na kivuli cha mauti.

Kituo: Ee Bwana Mungu wa wokovu wangu, mchana na usiku nalalamika kwako.

Somo la barua ya Mtakatifu Paulo kwa waKorinto (1 Korinto 1, 18-32; 2, 1-2

Kwa sababu neno la musalaba kwao wanaipotea ni upumbafu; lakini kwetu sisi tunaookolewa ni uwezo wa Mungu. Kwa sababu imeandikwa: Nitaharibu akili ya wenye akili na nitakataa ufahamu wa wenye ufahamu. Mwenye akili ni wapi? Mwandishi ni wapi? Mwenye ubishi wa dunia hii ni wapi? Mungu hakufanya akili ya dunia hii kuwa upumbafu? Kwa sababu katika akili ya Mungu, dunia katika akili yake yenyewe haikujua Mungu, ilipendeza Mungu kwa upumbafu

wa neno linalohubiriwa kuwaokoa wanaoamini. Kwa sababu Wayuda wanataka alama, na Wayunani wanatafuta akili. Lakini tunahubiri Kristo aliyesulibiwa, kwa Wayuda ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upumbafu; lakini kwao wanaoitwa, Wayuda na Wayunani vilevile, ni Kristo nguvu ya Mungu na akili ya Mungu. Kwa sababu upumbafu wa Mungu una akili zaidi ya watu;

na uzaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya watu. Maana angalieni mwito wenu, ndugu, ya kwamba, si wengi wenye akili ya mwili, si wengi wenye nguvu, si watu wakubwa wengi, wanaoitwa; lakini Mungu alichagua vitu vipumbafu vya dunia kupatiza wenye akili haya; na Mungu alichagua vitu zaifu vya dunia kupatiza vitu vya nguvu haya; na vitu vinyonge vya dunia na vitu

vinavyozarauliwa Mungu alichagua, na vitu visivyo kufanya vitu vilivyo viwe bule: kusudi hata mwili mumoja usijisifu mbele ya Mungu. Lakini kwa yeye ninyi ni katika Yesu, aliyefanyizwa na Mungu kuwa kwetu akili, na haki, na utakaso na ukombozi; hata sawasawa ilivyoandikwa: Yeye mwenye kujisifu, ajisifu katika Bwana. Nami, ndugu, wakati nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri ninyi ushuhuda wa Mungu kwa maneno makubwa, wala kwa maneno ya akili. Maana nilikusudia nisijue neno moja katikati yenu, ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa.

WAIMBAJI: Alliluia *(mara tatu).*

Zaburi 68 (69) Sauti ya Tano.
Kituo: Ee Mungu, uniokoe, kwani maji yameingia mpaka rohoni mwangu.

Kituo: Wamenilisha nyongo, na kwa kiu yangu wameninywisha siki.

Kituo: Macho yao yafungwe ili wasione.
Somo la EVANGELIO Matayo 27, 1-38 Luka 23, 39-43 Matayo 27, 39-54 Yoane 19, 31-42 na Matayo 27, 55-61) Katika Mwevangelizaji Matayo (27, 1-38)

Na wakati ilipokuwa asubui, wakubwa wote wa makuhani na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu kumwua; wakamufunga, wakamuchukua na kumupeleka kwa Pilato aliyekuwa liwali. Kisha Yuda aliyemutoa, wakati alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa, akatubu, akarudishia wakubwa wa makuhani na wazee vipande makumi tatu vya veza, akisema: Nimekosa wakati nilipotoa damu isiyo na kosa. Lakini wale wakasema: Hili ni nini kwetu? Uliangalie wewe mwenyewe. Akatupa vipande vya feza katika pahali patakatifu, akaondoka; akatoka inje akajitundika mwenyewe. Wakubwa wa makuhani wakatwa vipande vile vya feza, wakasema: Si halali kuviweka katika sanduku ya hazina, kwa sababu ni bei ya damu. Wakafanya shauri, wakanunua navyo shamba la mufinyazi liwe pahali pa kuzika wageni. Kwa hivi shamba lile lilitwa shamba la damu hata leo. Halafu likatimia neno lililosemwa na Yeremia nabii, akisema: Wakatwa vipande makumi tatu vya feza, bei yake aliyesabiwa kwa bei, wana wa Israeli waliyemuhesabu kwa bei; wakavitoa kwa shamba la mufinyanzi kama Bwana alivyoniagiza. Basi Yesu akasimama mbele ya liwali; liwali akamwuliza akisema: Wewe ni Mufalme wa Wayuda? Yesu akamwambia: Wewe unasema. Na wakati wakubwa wa makuhani na wazee walipomushitaki, hakujibu neno. Halafu Pilato akamwambia: Husikii maneno mengi wanayokushuhudia? Naye hakumujibu hata neno moja; hata liwali akashangaa sana. Basi kwa

wakati wa siku kubwa liwali kwa desturi alifungulia makutano mufungwa mumoja walivemutaka. Basi palikuwa na mufungwa wa kujulikana, aliyeitwa Baraba. Basi wakati walipokusanyika, Pilato akawaambia: Munataka niwafungulie ninyi nani? Baraba, ao Yesu anayeitwa Kristo? Kwa sababu alijua ya kuwa walimutoa kwa uwivu. Na wakati alipokuwa akiketi juu ya kiti cha hukumu, muke wake akatuma kwake akisema: Usiwe na neno na yule

mutu mwenye haki; kwa sababu nimeteswa maneno mengi leo katika ndoto kwa ajili yake. Basi wakubwa wa makuhani na wazee wakashawishi makutano ili waombe kwa Baraba na kuharibu Yesu. Lakini liwali akajibu, akawaambia: Ni nani katika hawa wawili munayetaka niwafungulie ninyi? Wakasema: Baraba. Pilato akawaambia: Basi, nitafanya nini na Yesu anayeitwa Kristo? Wakasema wote: Asulibiwe. Akasema: Kwa nini? Ametenda ubaya gani? Lakini wakazidi sana kupiga kelele, wakisema: Asulibiwe. Basi wakati Pilato alipoona ya kuwa hakuweza kufanya neno, lakini ya kama kelele lilizidi, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya makutano, akisema: Mimi sina kosa katika damu ya mutu huyu mwenye haki; ninyi

mwangalie maneno haya ninyi wenyewe. Watu wote wakajibu, wakasema: Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu. Halafu akawafungulia Baraba, lakini akapiga Yesu mijeledi, na kumutoa asulibiwe. Halafu askari za liwali wakachukua Yesu ndani ya Praitorio, wakakusanya kwake kikosi kizima. Wakamwondolea mavazi yake, wakamuvika nguo nyekundu. Wakasokota taji ya miiba, na kuiweka juu ya kichwa chake na tete mukononi mwake mwa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamuzihaki wakisema: Salamu, Mufalme wa Wayuda! Wakamutemea mate, wakatwa lile tete na kumupiga kichwani. Na wakati walipomuzihaki, wakamwondolea nguo ile, \ wakamuvika mavazi yake mwenyewe, wakamuchukua inje kumusulidisha. Na wakati walipotoka, wakaona mutu wa Kurene, jina lake Simoni; huyu walimushurutisha ili abebe musalaba wake. Na wakati walipofika pahali palipoitwa Golgota, maana yake Mufupa wa Kichwa, wakamupa mvinyo iliyochanganyika na nyongo; na wakati alipoionja hakutaka kunywa. Na wakati walipokwisha kumusulibisha, waligawa mavazi yake katikati yao wakipiga kura; wakaketi na kumulinda pale. Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaki yake yaliyoandikwa: Huyu ni Yesu Mufalme wa Wayuda. Wakati huu wanyanganyi wawili walisulibiwa pamoja naye mumoja kwa mukono wake wa kuume, na mumoja kwa kushoto. Luka 23, 39-43 Mumoja wa wale watenda mabaya waliotundikwa pamoja naye akamutukana, akisema: Si wewe uliye Kristo? Ujiokoe mwenyewe pamoja nasi. Lakini wa pili akamuhamakia, akisema: Huogopi hata Mungu, maana wewe ni katika hukumu ile ile? Na sisi kwa kweli, sababu tunapokea malipo yanayostahili kwa matendo yetu, lakini mutu huyu hakufanya neno lisilofaa. Akamwambia Yesu: Bwana, unikumbuke wakati unapokuja katika ufalme wako. Yesu akamwambia: Kweli ninakuambia, leo utakuwa pamoja nami katika Paradiso. (Matayo 27, 39-54) Nao waliopita njiani wakamutukana wakitikisisha vichwa vyao wakisema: Wewe mwenye kuvunja hekalu na kulijenga tena katika siku tatu, ujiokoe mwenyewe; kama ukiwa Mwana wa Mungu, shuka musalabani. Vile wakubwa wa makuhani wakimuzihaki pamoja na waandishi na wazee wakasema: Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa yeye mwenyewe. Yeye ni Mufalme wa Israeli; ashuke sasa musalabani na tutamwamini. Anaamini Mungu; amwokoe sasa kama anamutaka; kwa sababu alisema: Mimi ni Mwana wa Mungu. Wanyanganyi waliosulibiwa pamoja naye walimutukana hivi vilevile. Basi toka saa sita giza lilikuwa juu ya inchi hata saa tisa. Na karibu na saa tisa Yesu alipaza sauti akisema: Eloi, Eloi, lama sabaktani; maana yake: Mungu wangu, MUngu wangu, kwa nini umeniacha? Na wengine wao waliosimama pale, wakati waliposikia, wakasema: Mutu huyu anaita Elia. Na mara moja mumoja wao akakimbia, akatwaa sifongo na kuijaza siki, akaitia juu ya muti, akamukunywesha. Wale wengine wakasema: Acha; tuone kama Elia anakuja kumwokoa. Yesu akatoa sauti kubwa tena, akatoa roho yake. Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; inchi ikatetemeka; miamba ikapasuka, makaburi yakafunguliwa, na miili mingi ya watakatifu waliokwisha kulala ilifufuliwa; na wakitoka katika makaburi nyuma ya ufufuko wake, wakaingia katika muji mutakatifu na kutokea kwa watu wengu. Basi akida, nao waliokuwa pamoja naye wakilinda Yesu, wakati walipoona tetemeko la inchi, na maneno yaliyofanyika wakaogopa sana, wakisema: Kweli huyu alikuwa Mwana wa Mungu. Yoane 19, 31-42 Basi Wayuda, kwa sababu ilikuwa Maandalio, miili isikae juu ya musalaba siku ya sabato ( kwa sababu siku ya sabato ile ilikuwa siku kubwa), wakaomba Pilato, miguu yao ivunjwe, na wandolewe. Basi askari walikuja, wakamuvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulibiwa pamoja naye; lakini wakati walipofika kwa Yesu, wakaona ya kama amekwisha kufa, hawakuvunja miguu yake; lakini mumoja wa askari alimuchoma mbavu yake kwa mukuki, na mara moja ilitoka damu na maji. Naye aliyeona alishuhudia, na ushuhuda wake ni kweli: na yeye anajua ya kwamba anasema kweli, ninyi mupate kuamni. Kwa maana maneno haya yalifanyika, ili andiko litimie: Hapana mufupa wake utakaovunjwa. Na tena andiko lingine linasema: Watamutazama yeye waliyemuchoma. Na nyuma ya maneno haya, Yosefu mutu wa Arimatea, akiwa mwanafunzi wa Yesu, lakini kwa siri (maana aliogopa Wayuda) akaomba Pilato ruhusa aondoe mwili wa Yesu, na Pilato alimupa ruhusa. Basi alikuja akaondoa mwili wake. Na Nikodemo alikuja vilevile, yule aliyekuja kwanza kwa Yesu usiku, na alileta machanganyiko ya manemane na uude, karibu na ratli mia. Basi wakakamata mwili wa Yesu,

wakaufunga na sanda ya kitani pamoja na yale manukato, kama desturi ya Wayuda katika maziko. Na pahali pale aliposulibiwa palikuwa shamba; na ndani ya shamba lilikuwa kaburi jipya, bado hajatiwa mutu ndani yake. Basi kule waliweka Yesu kwa sababu ya Maandalio ya Wayuda, kwa sababu kaburi lilikuwa karibu. (Matayo 27, 55-61) Na wanawake wengi walikuwa pale wakitazama kwa mbali, wao waliofuata Yesu toka Galilaya wakimutumikia; katikati yao alikuwa Maria Magdalene, na Maria mama ya Yakobo na Yose, na mama ya wana wa Zebedayo. Hata ilipokuwa mangaribi, tajiri mumoja wa Arimatea alikuja, aliyeitwa Yosefu, naye vilevile alikuwa mwanafunzi wa Yesu. Mutu huyu akakwendea Pilato, akamwaomba mwili wa Yesu. Halafu Pilato akaagiza apewe. Yosefu akatwaa mwili wake, akaufunga ndani ya nguo safi ya kitani, akauweka ndani ya kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani; akanfirisha jiwe kubwa mbele ya mulango wa kaburi, akakwenda zake. Na Maria Magdalene alikuwa pale, na Maria mwingine, wakiketi mbele ya kaburi.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

SHEMASI AO PADRI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.

**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Bwana mwenyezi, Mungu wa mababu, tunakuomba, utusikie na ukatuhurumie.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya wa madini na wakristu waorthodoksi wote.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu. . . . *(jina lake).*
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristo.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinzi, usamehe na maondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, wadini wote na wakristu waorthodoksi ambao wanakaamo na wanakutana katika muji huu (*ao nyumba ya watawa),* wa parokia, na walakini na wapotani wa hekalu hii takatifu.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya watulivu na wenye heri, wajengaji wa hekalu hii takatifu, kwa ajili ya Baba na ndugu zetu wanaofariki ambao wanaolala kwa madini na kwa ajili ya waorthodoksi wanaolala hapa na popote.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya wafazili wa hekalu hii takatifu na heshima kwa ajili ya wapaji, kwa ajili ya wote wanaotumikamo na wanaoimbamo na kwa ajili ya watu wote walipo hapa ambao wanakujongea kwa rehema kubwa na nyingi.
**MSOMAJI**: Bwana, hurumia.
**PADRI**: Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda wanadamu na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI**: Amina.
**MSOMAJI**: Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi, umehimidiwa u, ee Mwana na Mungu wa Baba zetu, jina lako limehimidiwa na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi tunavyokutumaini wewe. Ee Bwana umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa u, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana, huruma yako ni ya milele usitutoangalie sisi, viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki

kukuimbia ni kwako, utukuufu ni wako, wa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SHEMASI**: Tuumalize ombi letu la mangaribi kwa Bwana.

**WAIMBAJI**: Bwana, hurumia.

**SHEMASI**: Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.

**WAIMBAJI**: Amina.

**SHEMASI** Mangaribi hii kamili iwe timilifu, takatifu, tulivu, yasio zambi, tuombe kwa Bwana. **WAIMBAJI**: Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI**: Malaika wa amani, mlinzi wa roho na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

**WAIMBAJI**: Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI** Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe kwa Bwana.

**WAIMBAJI**: Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI** Vilivyovyema na vifaavyo kwa roho zetu, tena kuwe amani katika dunia, tuombe kwa Bwana.

**WAIMBAJI**: Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI**: Kuyamaliza maisha yetu inabaki, katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.

**WAIMBAJI**:

Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI**: Tuombe ili mwisho wa maisha yetu uwe kikristo, kwa amani, bila aibu, tena tuone mufano mzuri mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

**WAIMBAJI**: Utupe, ee Bwana.

**SHEMASI**: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda Malkia wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristo Mungu.

**WAIMBAJI**: Kwako, ee Bwana.

**PADRI**: Kwa kuwa u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI**: Amina.

**PADRI**: Amani kwa wote.

**WAIMBAJI**: Na kwa roho yako.

**SHEMASI**: Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.

**WAIMBAJI**: Kwako, ee Bwana.

*Sala ya kuinamisha nayo kichwa kwa sauti ya chini:*

Ee Bwana Mungu wetu uliyeinamisha mbingu na ukashuka kwa ajili ya wokovu wa binadamu, uwatazamie watumishi wako na uriti wako kwa sababu wewe u Kuhani Mshindaji na rafiki wa watu. Usiyeongoja masaidio ya watu, kwa kuwa wao wamewazia huruma yako na kutumaini ukombozi wako, uwachunge mangaribi na usiku huu hata na wakati wowote kwa maadui, na kwa vitendo vidogo vya Shetani asiye na mafaa ya akili na mwenye mawazo mabaya.

***PADRI** anapaza sauti:* Kwa kuwa uwezo wa ufalme wako uhimidiwe na utukuzwe Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI**: Amina.

## APOSTIKHA

Sauti ya mbili

Wakati mtu wa Arimathea alipokushusha umekufa Msalabani, wewe Uzima wa wote, akakumimia manukato, ee Kristu, akakufunga sanda. Tena mwenye kujaa na mapendo akakumbatia kwa moyo na kwa midomo Mwili wako Takatifu kamili. Lakini aliposhikwa na woga, akasema na furaha akitetemeka: Utukufu kwa ukubwa wako, ewe Mpenda-wanadamu.

Kituo: Bwana ameingia katika Ufalme wake, amevaa nuru.

Wakati ulipowekwa kaburini mpya kwa ajili ya wokovu wa wote kama ukombozi wa wote, hadeze ilizihakiwa na ikaogopa; makomeo yake ikavunjwa, milango yake iliondolewa. Makaburi yalifunguka, wafu wakafufuka. Kwa hii wakati Adamu mwenyi shukrani akakulalamikia: Utukufu kwa ukubwa wako, ewe mpenda-wanadamu.

Kituo: Alikazaulimwengu hautatikisika.

Wakati ulipoacha Mwili wako kuwekwa kaburini, wewe ambaye Umungu wako ni usiyoweza kuhadisiwa tena usiyosikilika, ee Kristu, ulifungua boma ya mauti na uliacha wazi manyumba ya hadeze; kwa hii saa ukaleta baraka yako ya kimungu, utukufu wako na nuru yako kwa hii sabato.

Kituo: Ee Bwana, makao yako inastahili utakatifu siku nyingi.

Ee Kristu, wakati majeshi ya mbinguni yalikuona wamekuchongea kwa uwongo, wamekutendea kama mwenyi kudanganya kwa wasiyo na sheria, yakatetemeka pakuona uvumilivu wako wa kweli. Lakini mbele ya jiwe lililowekwa kaburini kwa mikono iliyochoma ubavu wako Takatifu, yakafurahiwa kwa ajili ya wokovu wako na yakalalamika: Utukufu kwa ukubwa wako, ewe mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Sauti ya Tano

Wewe mwenye kuvaa nuru kama nguo, Yosefu na Nikodemu walikushusha pa mti wa Msalaba na mbele ya mwili wako, bila kaburi, wakaomboleza kwa uchungu na wakasema wakilia: Ole, ee Yesu mpole kamili! Jua lililokuona Msalabani limepata giza na inchi imetikisika kwa woga; pazia la Hekalu likapasuka na nimekuona ukivumilia kwa ajili yangu kifo cha kutaka. Namna gani nitakuzika, ee Mungu wangu? Sanda gani nitakufunika? Na mikono gani nitagusa Mwili wako Takatifu? Wimbo gani nitaimbia kifo chako? Ewe mwenye rehema kamili, natukuza mateso yako! Naimbia maziko yako na Ufufuo wako nikilalamika: Ee Bwana, utukufu kwako!

Sasa, ee Bwana. . (Luka 2, 29)

Wimbo: Sauti ya mbili:

Muheshimiwa Yosefu alishusha Msalabani Mwili wako Takatifu, akaufunga sanda safi na akauzika na manukato kaburini mupya.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Karibu ya kaburi Malaika aliwatokea wanawake Watakatifu akawaambia: Manukato inawafaa wafu, lakini Kristu ni huru ku uharibifu wote.

Kuaga (Apolisis):

Utukufu kwako, ee Mungu matumaini wetu, utukufu kwako. Yeye, kwa ajili ya sisi Wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu, alikubali kwa kutaka kwake kuteswa mwilini, Msalabani na hata kaburini, Kristo, Mungu wetu kweli, kwa maombezi ya Mzazi Mungu Bikira Maria. . .

*Wakati tunapoimba hii troparia tutaweka Epitafios-Mfano wa Maziko ya Kristu-katikati ya kanisa sababu ya kuitukuza. Tutaweka pa meza Takatifu mbele ya Orthros ya Paska.*

# SIKU YA SITA MKUBWA

## SALA YA ASUBUI (ORTHROS)

**PADRI**: Ahimidiwe Mungu wetu daima. . .
**MWIMBAJI**: Amina. Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Ee Bwana okoa watu wako. . .

**PADRI**: Utukufu ku Utatu Mtakatifu, wa asili moja, wenyi kuleta uzima, na usiyotengana, sasa na siku zote, hata milele na milele.
**WAIMBAJI**: Amina.

EKSAPSALMOS

Sauti ya mbili
Bwana ndiwe Mungu, amefunuliwa kwetu, . . .

Sauti ya mbili
Muheshimiwa Yosefu alishusha Msalabani Mwili wako Takatifu, akaufunga sanda safi na akauzika na manukato kaburini mupya.

Utukufu kwa Baba. . .
Wakati uliposhuka ku mauti, ewe Uzima usiyokufa, hadeze ikauawa kwa nuru ya Umungu wako. Wakati ulipowafufua wafu kuzimuni; majeshi yote ya mbinguni yalikulalamikia: Ee Kristu Mungu wetu, mpaji wa uzima, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . .
Karibu ya kaburi Malaika aliwatokea wanawake watakatifu akawaambia: Manukato inawafaa wafu, lakini Kristu ni huru ku uharibifu wote.

**SHEMASI**: Tena na tena ku amani tumwombe Bwana. . . .

**KATHISMA**. Sauti ya kwanza
Alipopokea Mwili wako kwa Pilato, Yosefu wa Arimathea akaufunika sanda safi na akaupakaa manukato takatifu; akauweka kaburini mpya, na Wanawake Watakatifu waliokuja asubui mapema kaburini wanakulalamikia: Ee Kristu, utuonyeshe Ufufuo wako kama ulivyosema.

Utukufu kwa Baba. . .
Ee Kristu, utuonyeshe Ufufuo wako kama ulivyosema.

Sasa na siku zote. . .
Makundi ya malaika wanaogopa pakuona kaburini, kama mufu, huyu msiyekufa, yeye mwenye kukaa katika kifua cha Baba. Wanamuzunguka, na pamoja na wafu wa hadeze, wanamutukuza kama Muumba na Bwana.

**ZABURI** 50 (51)

# KANUNI

WIMBO 1   HIRMOS  Sauti ya Sita

Zamani Bwana alizika mzulumu chini ya mawimbi ya bahari, wana wa taifa lililofukuziwa walizika Mwokozi wao udongoni. Lakini sisi, kama mabikira wa Israeli tumwimbie Bwana: Kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana, ni wimbo wa kwa heri ninaimba pa kaburi yako; lakini kaburi yako imenifungulia milango ya uzima na lufu yako ilikuwa mauti na hadeze.

Utukufu kwa Baba. . .

Majeshi ya mbinguni na majeshi ya dunia yalipokuona pa kiti cha juu mbinguni na kaburini hapa chini yakashituka kwa hii lufu. Hii jambo ilipita wazo leo. Hayakuweza kuvumilia pa kuona Muumba wa uzima wote amelala katika kauti.

Sasa na siku zote. . .

Kwa kujaza vyote na utukufu wako ulishuka chini ya udongo; hali yangu niliyoriti kwa Adamu haikuweza kukimbia machoni mwako, na kwa kupotea kwangu kaburi yako imenifanya kuwa mpya, ee mpenda-wanadamu.

**KATAVASIA**:  Zamani Bwana alizika. . .

WIMBO 3  HIRMOS

Ee wewe uliyetundika inchi pa maji, kiumbe ilipokuona umetundikwa kule Kalvario ikashikwa na woga kubwa na ikapaza sauti:  Hakuna aliye Mtakatifu kuliko wewe Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ulionyesha alama za maziko yako wakati ulipozidisha miujiza lakini leo ni kwa wakaaji wa hadeze ulionyesha mafumbo yako, ee Mungu-Mtu; na wanapaza sauti:  Hakuna aliye Mtakatifu kuliko wewe Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mwokozi, wakati ulipanua mikono Yako na ulifunikwa sanda kaburini, uliunganisha wale waliotengana zamani. Ulikomboa wafungwa waliokulalamikia:  Hakuna aliye Mtakatifu kuliko wewe Bwana.

Sasa na siku zote. . .

Wewe ambaye hauwezi kuenea katika kitu hata kimoja, kwa kutaka kwako wanakufungia kaburini. Matendo yako yalifunua uwezo wako kwa wale wenyi kukuimbia:  Hakuna aliye Mtakatifu kuliko wewe Bwana.

**KATAVASIA**:  Ee wewe uliyetundika inchi. . .

**KATHISMA**.  Sauti ya kwanza.

Ee Mwokozi, maaskari waliolinda kaburi yako walianguka kama wafu, wakaangaziwa na mwangaza iliowaangazia wanawake na ikawahubiri Ufufuo wako. Utukufu kwako, wewe

mwenyi kuharibu mauti! Tunaangukia ku miguu yako, wewe Mfufuliwa kaburini, ee wewe peke yako Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine hii).*

WIMBO 4 HIRMOS
Alipotambua kujishusha kwako kimungu Msalabani, Habakuki akapaza sauti mwenyi kujaa na woga: Ee Mwema kamili, uliangamiza nguvu ya watawala wakatiuliungana na wakaaji wa hadeze, wewe Mfalme wa vitu vyote.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu. . .
Ee Mwokozi, leo unatakasa siku ya saba, hii siku zamani ulitakasa wakati ulipumzika kisha kuumba viumbe vyako, kwa sababu unaumba ulimwengu na unautengeneza kwa Sabato yako na kwa mafundisho yako.

Utukufu kwa Baba. . .
Ee Neno, ni kwa uwezo wako kamili ulishinda roho yako ilitengana na mwili, ukavunja pamoja vifungo vya mauti na ile ya hadeze nguvu yako.

Sasa na siku zote. . .
Ee Neno kwa kuja kwako Hadeze ilijazwa na uchungu wakati iliona mwanadamuamekuwa Mungu, Mutu mwenyi vidonda nyingi amejazwa na uwezo, hii ono ya woga ikamwacha kusema.

**KATAVASIA**: Alipotambua. . .

WIMBO 5 HIRMOS

Ee Kristu, wakati rehema yako kimungu ilionekana kwa sisi, Isaya akaona nuru yako ikainuka usiku na asubui akalalamikia: Wafu wataamuka, wakaaji wa kaburi watasimama, na watu wote wa dunia watashangilia.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Ee Muumba, unawafanya wana wa dunia kuwa wapya, wewe uliyewaumba, na unachukua udongo wao. Kaburi na sanda yanafunua fumbo yako, ee Neno: Kwa sababu mshauri mwema anaonyesha nia ya Baba yako ambaye kwa ukarimu wake, ananifanya kuwa mpya katika nafsi yako.

Utukufu kwa Baba. . .
Unageuza mufu kwa lufu yako, na mwenyi kuharibika kwa kaburi yako unawapa wafu hali isiyoharibika kwa sababu wewe ni Mungu, unamufanya kuwa wa milele huyu ulichukua hali yake. Kwani mwili wako haikuona uharibifu, ee Bwana, na roho yako haikukaa katika hadeze huko ulikuwa mgeni.

Sasa na siku zote. .
Ulizaliwa kwa Msiyeolewa, ee Muumba wangu, na ku ubavu wako wenye kuchomwa mkuki unaumba kiumbe mpya kwa ajili ya Adamu wa pili Eva mpya. Ulilala usingizi wa ajabu, usingizi uliyo chemchem ya uzima, na uliamka mzima, ewe mwenyezi.

**KATAVASIA**: Ee Kristu wakati rehema. . .

WIMBO 6   HIRMOS

Yona alimezwa katika tumbo la samaki lakini hakukaa mule, alitangulia kuonyesha mateso yako na maziko yako. Alitoka mu tumbo la nyama kama katika chumba cha arusi akiwaambia maaskari:  Mushunga paka majivuno na uwongo, lakini muliacha rehema.

Utukufu kwako, ee Mungu. . .

Uliondolewa ku uzima, ee Neno, lakini haukutengana na mwili uliyochukuwa; hata kama Hekalu yako ilibomolewa wakati wa Mateso yako, hata kama umungu wako na Mwili wako ilikuwa kitu moja katika hii hali mbili wewe peke yako ni Mwana wa Mungu, Mungu tena Mutu.

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani ya Adamu ilikuwa ni lufu ya mwanadamu, lakini apana ya Mungu, kwa sababu kama hali ya uvumbi ya mwili wako iliteswa, hali yako ya umungu haikuteseka. Uliingiza uharibifu katika hali isiyoharibika na kwa Ufufuo wako ulifunua chemchem ya uzima isiyoharibika

Sasa na siku zote. . .

Hadeze inatawala wanadamu, lakini ufalme wake si wa milele. Ni wewe, ee Mwenyezi, ulipolala kaburini, kwa mkono wako wa ufalme ulivunja minyororo ya mauti. Uliwahubiri wale waliolala tangu zamani ukombozi wa kweli, ee Mwokozi, ukawa Mzaliwa wa kwanza katika wafu.

**KATAVASIA**:  Yona alimezwa katika tumbo. . .

**SHEMASI** ao **PADRI**:  Tena na tena. . .

**KONTAKION**     Sauti ya Sita

Tunaona anakufa Huyu aliyefunga Hadeze. Anafunikwa sanda na kupakaliwa manukato. Msiyekufa anawekwa kaburini kama mufu tena Wanawake wanakuja kumupakaa manukato wakilia kwa uchungu na wakipaza sauti:  Hii Sabato imebarikiwa katika yote, kwa sababu Kristu mwenyi kulala atafufuka siku ya tatu.

**IKOS**

Huyu aliye na vyote aliinuliwa Msalabani tena viumbe vyote vinaomboleza pakumuona ametundikwa uchi juu ya mti. Jua linaficha nuru yake, nyota inapoteza mwangaza wao, kwa woga kubwa inchi inatetemeka, bahari inakimbia, na mawe yanapasuka. Makaburi yanafunguka, miili ya Watakatifu yanafufuka. Hadeze inalalamika, Wayuda wanafanya shauri sababu ya kuficha Ufufuo wa Kristu:  Hii Sabato imetakaswa katika yote, kwa sababu aliyelala atafufuka siku ya tatu.

*Sasa tunasoma Sinaksario ya Watakatifu ya hii siku ya leo. Kisha tunasoma hivi:*

Muposho Mkubwa na Takatifu tunashangilia Maziko ya Mwili Takatifu ya Bwana Mungu Yesu Kristu kwa ajili yake kizazi  yetu muzima ilipanda kwa uzima ya milele.

WIMBO 7   HIRMOS

Muujiza wa kweli! Huyu aliyeopoa vijana watakatifu ku tanuru ya moto anawekwa kaburini. Ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia:  Ee Mungui mkombozi, umehimidiwa.  Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Hadeze ilipigwa moyoni pakumupokea Huyu ambaye ubavu ulichomwa mkuki. Imelala yenye kuteketezwa kwa moto kimungu. Ni kwa ajili ya kutuokoa na tunaimba: Ee Mungu mkombozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu. . .

Kaburi heshimiwa yenyi kupokea Muumba kama amelala. Ameonekana kama hazina kimungu ya uzima; ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu mkombozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu. . .

Hadeze ilipigwa moyoni pakumupokea huyu ambaye ubavu ulichomwa mkuki; imelala yenye kuteketezwa kwa moto kimungu. Nikwa ajili ya kutuokoa na tunaimba; ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kaburi heshimiwa yenyi kupokea Muumba kama amelala. Ameonekana kama hazina kimungu ya uzima; ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamuimbia; Ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

Utukufu kwa Baba. . .

Uzima wa ulemwengu anaitika kuwekwa kaburini kama ilivyo sheria ya wenye kufa. Lakini hii kaburi inajifunua kuwa chemchem ya Uzima. NI kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

Sasa na siku zote. . .

Katika hadeze, Kaburini na katika Edeni mulikuwa Umungu moja na usiyotengana na Kristu pamoja na Baba na Roho Mtakatifu. Ni kwa ajili yetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkombozi, umehimidiwa.

**KATAVASIA**: Muujiza wa kweli!. . .

WIMBO 8 HIRMOS

Inama kwa woga, ee mbingu, na tetemekeni ninyi misingi ya inchi kwani tazama Mungu wa mbinguni amehesabiwa katika wafu. Amepokelewa kama mgeni kaburini. Enyi watoto, mtukuzeni; Enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu. . .

Hekalu safi kamili limebolewa na linasimamisha nyumba ya Daudi yenye kubomolewa. Huyu mwenye kukaa juu kabisa ya mbingu Adamu wa pili, anashuka chini kabisa ya Hadeze sababu ya kumuamusha yule wa kwanza, Enyi watoto mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Tunahimidi Baba, Mwana na Roho Mutakatifu, Bwana.

Nguvu ya Mitume inaanguka, lakini kwa uhodari Yosefu wa Arimathea alipokuona uchi na umekufa, wewe Mungu aliye juu kabisa akaomba mwili wako na akaufunika sanda akipaza sauti: Enyi Watoto, Mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni, enyi mataifa, msifuni milele.

Sasa na siku zote, hata milele

Ee Muujiza, ee rehema, ee uvumilivu wa kweli huyu mwenye kukaa juu kabisa ya mbingu anavumilia kufungwa katika jiwe lenyi kufungiwa, na Mungu anatendewa kama muongo. Enyi Watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana.

**KATAVASIA**: Inama kwa woga, ee mbingu. . .

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tunamuheshimu kwa nyimbo na kumtukuza.

WIMBO 9 HIRMOS
Usilie, ee Mama, wakati unapoona kaburini Mwana wako uliyezaa bila mbegu. Nitafufuka, nitakutukuzwa kama Mungu nitashangilia katika utukufu wa milele wale wenyi kukusifu kwa imani na mapendo.

Utukufu kwa Baba. . .
Ee Mama yangu, ni kwa kutaka kwangu udongo umenifunika; walinzi wa Hadeze wanatetemeka pakuniona nimevaa mavazi ya kisasi yenyi damu, kwa sababu kwa Msalaba nimepiga maadui zangu, na kama Mungu nitafufuka na nitakutukuza.

Sasa na siku zote. . .
Viumbe vifurahi na wanadamu washangilie: Hadeze aliye adui imenyanganywa, wanawake wakuje na manukato kukutana nami, mimi niliyekomboa Adamu na Eva na wazao wao wote, mimi nitakayefufuka siku ya tatu.

**KATAVASIA**: Usilie, ee Mama, wakati. . .

***KISHA TUNAANZA STASIS***

## KUSIMAMA WA KWANZA

Uzima Kaburini, uliwekwa ee Kristu na jeshi la Malaika walistajabu, wakitukuza kujishusha Kwako.

Je Uzima unakufa je unakaa Kaburini. Unnangusha ufalme wa mauti, ukafufua wafu kwa Hadeze.

Tunakutukuza, ee Yesu Mufalme, na tunaheshimu maziko na mateso Yako, ulituokoa nayo toka uharibifu.

Uliyeweka kipimo nchini, unakaa Kaburini kidogo, leo Yesu Mufalme wa wote ukifufua wafu toka Kaburi.

Rabi wa wote, anaonekana mufu, akiwekwa Kaburini jipya, aliyeonyesha tuburi tupu.

Kama munyanganyi, Kristu ulihesabiwa ukitustalisha sisi wote, toka ubaya mwenye kuponda kisingino.

Yeye ni muzuri sana, kuliko wana wa watu, anaonekana kama mufu bila sura, aliyepamba hali ya wote.

Mambo gani ya ajabu! Mambo gani mapya! Muletaji-uzima anachukuliwa bila pumuzi mikononi mwa Yosefu.

Ulishuka Kaburini, na haukutoka kamwe, kifuani cha Baba ee Kristu; Hii ni ya mushangao na ya ajabu.

Jeshi la malaika, inajiharikisha pamoja, na Yosefu na Nikodimo kwa kuweka, Kaburini Huyu asiye-kuingia.

Yesu Muletaji-uzima, ukikufa ukiweka chini, ulileta uzima kwa mimi, niliyekufa juu ya kosa mbaya.

Ee Kristu uliwekwa, Kaburini mupya, ukafanya mupya hali ya watu, ukifufuka toka wafu sawa Mungu.

Rabi ulishuka chini, kwa kuokoa Adamu lakini haukumupata chini, na ulishuka kumutafuta kuzimuni.

Neno, nuru yako kubwa, ilipofichwa chini, inchi inatikisika kwa woga, na jua ilificha nuru Yake.

Mwokozi unakufa, kwa kutaka Kwako sawa mutu, na ulifufua watu wote sawa Mungu, toka Kaburi na vilindi ya zambi.

Bikira safi sawa Mama, akitosha machozi, juu Yako, ee Yesu aliita: Ee Mwana nitakuzika je?

Kwa lufu yako Mwokozi, unarudisha Adamu kwa uzima, aliyekufa kwa ajili ya uivu; Wewe ulionekana Adamu mupya.

Ee wokozi, kundi la malaika, kilipokuona mufu kwa ajili yetu, kilificha uso yao kwa mabawa.

Ulichomwa ubavuni, Wewe uliyepata ubavu, toka Adamu na kuumba Eva, ukatosha maji ya usafisho.

Mulinzi wa uzima, alionekana mufu kwa mashituko malaika waliita: Mungu alifungwa Kaburini je?

Kwa kutaka Kwako, Yesu ukishuka chini, toka chini ulirudisha mbinguni, wale walioanguka toka kule.

Ninaabudu mateso, ninaimbia maziko, ninatukuza uwezo wako ee Mwema, ninaponyeshwa nayo toka uharibifu.

Kwa kutaka Kwako, Mwokozi ukishuka chini, ulileta uzima, kwa wafu, uliwapandisha mu utukufu wa Baba.

Mukononi mwako, uliyeumba Adamu kwa udongo, ulifanyika mutu kwa ajili yake, ukasulibiwa kwa kutaka kwako.

Ole kwangu Nuru yangu! Ole kwangu Nuru ya dunia! Bikira aliita kwa maombolezo: Ee Yesu Mupendwa sana wangu.

Ee Mungu Neno, ee furaha yangu, je navumilia maziko ya siku tatu. Sawa Mama sasa matumbo inapasuliwa.

Nani atanipa maji, na chemchem ya machozi, ili nililie Yesu Mupendwa wangu. Bikira Muzazi-Mungu aliita.

Nitakuona waakti gani, Nuru mbele ya milele, shangwe na furaha ya moyo wangu. Bikira aliita kwa maombolezo.

Kwa kutaka kwako, uliwekwa Kaburini lakini unaisha na utafufua wafu, kama ulivyosema, Mwokozi wangu.

Utukufu kwa Baba...

Tunakuimbia, ee Neno Mungu wa wote tena Baba na Roho Mtakatifu tukitukuza maziko yako kimungu.

Sasa na siku zote...

Tunakuita Mwenye-heri, ee Muzazi-Mungu Safi, na tunaheshimu maziko ya siku tatu, ya Mwana wako na Mungu wetu.

*Sasa tunaimba tena wimbo ya kwanza:*

Uzima Kaburini, uliwekwa ee Kristu na jeshi la Malaika walistajabu, wakitukuza kujishusha Kwako.

Elezo: *Kisha tunasema kuambatisha kidogo na kupaza sauti:*

Kwa kuwa jina lako limehimidiwa na ufalme wako umetukuzwa wa baba na wa Mwana na wa Roho Mtakatrifu sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## KUSIMAMA WA PILI

Inastahili, kukutukuza ewe Muletaji-uzima, uliyetandika mikono Musalabani na kuvunja uwezo wa adui.

Inastahili, kukutukuza ewe Muumba wa wote, kwani kwa mateso Yako tulifanyika, waioteswa na wasioharibika.

Inchi ilitetemeka, na jua ilijificha, ee Kristu, wakati wewe Nuru isiyomwisho, uliposhuka Kaburini kwa mwili.

Maserafimi, kwa woga wanakuona, bila kutengana na Baba, na chini kama mu uliyelala.

Pazia la hekalu, linapasuka kwa usulubisho wako, na miangaza inaficha nuru yao, ulipojificha, ee Jua, chini.

Huyu aliyeumba, katika mwanzo inchi alishuka chini, sawa mufu bila pumuzi. Ee Mbingu ogopa kwa maono.

Kujeni tuimbe, maombolezo kimungu Kristu, kama mbele wanawake kwa marasi, ilitusikie «salamu» pamoja.

Neno uko kweli, manukato isiyomalizika; kwa hii wanawake walikupa manukato, kama mufu kwa wewe uliye-hai.

Mungu alipotembea, kwa paradizo Adamu aliogopa, lakini sasa aliposhuka hadezeni, huyu anafurahia Mufufuliwa.

Yosefu akikuficha, kwa heshima kaburini mupya, anaimba wimbo ya maombolezo kwa maziko yako, ee Mwokozi.

Je nitafunga, macho lako mazuri na midomo. Je nitakuzika kama mufu ee Neno. Yosefu alisema kwa woga.

Jua linangaa kisha usiku, na Wewe utangaa, ukifufuka kisha mauti, kama toka chumbani cha arusi.

Muumba Mwokozi, inchi ikikupokea ndani yake, inatetemeka kwa woga, na inaamusha wafu kwa tetemeko.

Nikodimo na Yosefu, kwa marasi waliokupakaa, ee Kristu na kukufunika, wakaita: Ogopa, inchi yote.

Ee Neno uko, Mletaji-uzima na haukuna, Wayuda waliokusulibisha; lakini ulifufua wafu wao.

Neno katika mateso, haukuwa na sura ao uzuri. lakini ukifufuka uliangaa na ulileta nuru kwa watu.

Ulishuka mwilini, ewe Nuru usiyomwisho, na jua lilififia muchanani halikuvumilia likuone.

Ee Mwokozi, jua na mwezi ikipata giza, ilifananisha watumishi, waliovaa nguo nyeusi.

Ukilala kidogo, ulileta uzima kwa wafu, na ukifufuka ulifufua waliolala wa zamani ee Mwema.

Kama mwari, ukichomwa ubavuni wako, ee Neno ulileta uzima kwa wana, ukiwanywisha damu ya uzima.

Yosua zamani, alisimamisha jua kwa kushinda adui; lakini Wewe ulilificha kwa kushinda ukubwa wa giza.

Ee Mwema, ulibaki mu kifua cha Baba na ulijifanya mutu kwa mapenzi Yako ukashuka kuzimuni, ee Kristu.

Aliyetundika inchi, baharini aliondolewa Msalabani, akalala ndani yake bila pumuzi, na inchi ilitetemeka sana.

Jua ililiogopa, likikuomba ewe Nuru isioonekana, Kristu wangu na lilififia lilipokuona Kaburini bila pumuzi.

Alililia, Mama Yako Safi kamili, aliokuona Kaburini Mungu Neno, bila mwanzo na usiosemwa.

Mama safi kamili, wakati alipokuona kama mufu, ee Kristu kwa uchungu alisema: Usikawisha uzima katika wafu.

Hadeze ya ogopesho, wakati alipokuona, ee Jua lisilokufa la utukufu, aliogopa na kuacha wafu kwa haraka.

Waaminifu wote, tunakutukuza usulibisho na ufufuo wako, ee Kristu tuliyokombolewa, toka mauti kwa maziko yako.

Utukufu kwa Baba...

Mungu Baba, Neno na Roho bila mwanzo simamisha bokora ya wafalme, juu ya wakafiri kama Mwema.

Sasa na sisku zote...

Bikira safi kamili, uliyezaa Uzima simamika makwazo ya kanisa na uipatiye amani kama mwema.

*Tena tunaimba wimbo ya kwanza:*

Inastahili, kukutukuza ewe Muletaji-uzima, uliyetandika mikono Musalabani na kuvunja uwezo wa adui.

*Kisha tunasema kuambatisha Kidogo na kupaza sauti hivi:*

Kwa kuwa Wewe ndiwe Mutakatifu, ee Mungu wetu, uliyekaa katika kiti cha utukufu cha Kheruvimi, na Kwako tunatoa utukufu, pamoja na Baba yako musiyemwanzo na Roho zako Mtakatifu kamili, Mwema na Muletaji-uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**KUSIMAMA WA TATU**

Vizazi vyote vyanatolea, wimbo kwa maziko yako, ee Kristu wangu.
Yosefu toka muti, akikushusha Wewe, anakuzika Kaburini.
Wanawake walikuja, wakileta Manukato Kwako, ee Kristu wangu.
Kuja kiumbe kiote, tutolee nyimbo, kwa maziko ya Muumba.
Wote pamoja na wanawake, tumupakale Yeye, aliye-hai kama mufu.
Yosefu mwenye-heri, zika mwili wa Kristu, Muletaji-uzima.
Wale waliokula mana (mukate), walitobola kisingino, juu ya Mwema.
Wale waliokula mana, walitolea siki na nyongo kwa Mwokozi.
Umazimu gani kubwa, na uwaji ya walioua, Kristu na Manabii.
Kama mutumishi mupumbafu, mwanafunzi alitoa, kilindi ya akili.
Yuda mutu wa hila, akiuzisha Mwokozi alikuwa mufungwa.
Kama Solomono alisema, kinywa cha Waebrania, ni shimo ya wote.
Bjia ya Waebrania, ni njia kubwa ya michongoma na mitego.
Yosefu na Nikodimo, wanazika Muumba kama inavyofaa.
Mwokozi Muletaji-uzima, utukufu kwa uwezo wako, uliyeshusha Hadeze.
Safi, kamili akikuona, ee Neno uliyolala, alilia kama Mama.
Ah! Kipua mupendwa, Mwana wangu mupendwa, uzuri wako ulishuka wapi?
Mama yako safi, alisukuma kwa macho ulipokufa ee Neno.
Wanawake kwa manukato, walikuja kupakaa, Kristu Manukato kimungu.
Ee Mungu wangu, unaua mauti kwa lufu kwa uwezo wa umungu wako.
Mudanganyifu amedanganyiwa, Adamu anakombolewa, kwa akili yako, ee Mungu.
Mama tako Safi, analia na kuombleza kwa kifo chako, ee Mwokozi.
Malaika walishangaa, kwa maziko ya ajabu, ee Muumba wa wote.
Wanawake walimimia, kaburi kwa marasi wakikuja asubui mapema *(mara tatu).*
Kwa ufufuo wako, leta amani kwa Kanisa,, na wokovu kwa taifa.
Utukufu kwa Baba...
Utatu Mutakatifu, Baba, Mwana na Roho hurumia watu.

Sasa na siku zote...
Bikira utustahilishe, tuone ufufuo wa Mwana wako.
*Tena tunaimba wimbo wa kwanza*
Vizazi vyote vyanatolea, wimbo kwa maziko yako, ee Kristu wangu.

*Sasa tunaimba Mahimidi ya Ufufuo ( Evlogitaria).*

Sauti ya Tano
Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.
Makusanyo ya Malaika yalistaajabu ukikuona umehesabiwa mfu, tena kuiharibu nguvu ya kifo, ee Mwokozi, na kumfufua Adamu pamoja nawe, hata kuwapa uhuru kwa mateka wote wa kuzimu.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.
Enyi Binti wanafunzi kwa nini munayachanganya machozi na manukato kwa huzuni? Malaika aliyemeta Kamurini, aliwanenea wanawake walioleta manukato: Tazameni kaburi na kufahamu, maana Mwokozi amefufuka shimoni.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.
Alfajiri mapema wanawake walioleta manukato, walijiharikisha kwenda kaburini pako, ee Bwana, wakiomboleza. Walakini walimuona malaika mbele yao, aliyewaambia: Wakati wa maombolezo umekwisha kuisha; musilinieni na kuwahubiri mitume neno la ufufuo.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki yako.
Wanawake walioleta manukato wakija nayo kaburini pako, ee Mwokozi, walimusikiliza Malaika, ambaye kwa sauti kubwa aliwanenea; munamuzania ndiye aliye hai kuwa katika wafu? Maana kwa kuwa Mungu amefufuka shimoni.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.
Tumsujudu Baba, tena Mwana, na Roho Mutakatifu, Utatu Mutakatifu, hali ya asili moja, tunapaliza sauti pamoja na Waserafi, tukisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, wewe, ee Bwana.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Ewe Bikira, ukimzaa Mpaji wa uhai, umemkomboa Adamu na zambi, tena umempa Eva furaha kisha huzuni, na hawa wanaoanguka na uzima, wamerudishwa na yeye, aliyepata mwili nawe, Yu Mungu binadamu.

Alliluia, Alliluia, Alliluia, tukufu kwako. ee Mungu *(mara tatu).*

SHEMASI AO PADRI: Tena na tena...

*Pahali pa* ***EKSAPOSTILARION****, tunaimba mara tatu hii:*
Sauti ya mbili
Bwana Mungu wetu ni we Mtakatifu. *(mara tatu).*

## MASIFU

Sauti ya mbili
Kila mwenye pumzi amsifu Bwana. . .

Kituo: Kuwafanya hukumu iliyoandikwa, huo wa watawa wake wote.

Leo kaburi inamupokea Huyu mwenyi kushika viumbe mkononi mwake. Jiwe linamufunika huyu aliyefunika mbingu kwa uzuri. Uzima inalala, Hadeze inatetemeka, Adamu anafunguliwa ku minyororo yake. Ulitimiza Sabato ya milele pakutupatia Ufufuo wako Takatifu kamili katika wafu.

Kituo: Msifuni Bwana katika patakatifu pake. . .

Hii ni ono tunaona machoni mwetu? Hii ni Sabati gani? Mfalme wa milele alipotimiza nia yake kwa Mateso, anapumzika kaburini akitupatia Sabato mpya. Tena tumulalamikie: Amka, ee Bwana, sababu ya kuhukumu dunia, kwani Ufalme wako ni wa milele, wewe ambaye rehema ni ya milele.

Kituo: Msifuni kwa ajili ya ahadi zake zote. . .

Kujeni, tuone Uzima wetu amelala kaburini kusudi afufue wale wenye kulala kaburini. Kujeni, tuone leo Mwenye kulala aliyetoka katika kabila la Yuda. Tumulalamikie kama Nabii: Umejinyosha kwa kulala kama simba, nani ataweza kukuamusha, ee Mfalme? Lakini wewe kwa nguvu ya uwezo wako, amka; Wewe uliyejitoa kwa kutaka kwako kwa ajili yetu, ee Bwana, utukufu kwako.

Kituo: Msifuni kwa matoazi yanayolia sana. . . Sauti ya Sita

Yosefu aliomba mwili wa Yesu na akauweka mu kaburi yake mpya, kwani alipashwa kutoka kaburini kama katika nyumba ya arusi. Ee wewe Bwana uliyeharibu ufalme wa mauti, uliyewafungulia wanadamu milango ya Paradizo, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . .
Musa mkubwa alisema: "Na Mungu akabariki siku ya Saba". Matangulizi ya hii siku ya leo. Tazama Sabato yenyi kubarikiwa; tazama siku ya kupumzika, kwa sababu leo Mwana wa pekee wa Mungu alipumzika kwa kazi zake zote katika lufu yake. Anashangilia Sabato mwilini mwake, tena kwa Ufufuo wake anarudi katika utukufu wake wa kwanza akitupatia uzima wa milele, kwa sababu Yeye ni Mwema tena mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote. . . Sauti ya mbili
Wewe ni mbarikiwa kamili, ee Bikira Mzazi-Mungu, kwa sababu huyu aliyepata mwili kwako alifunga Hadeze minyororo, alimwita Adamu. Aliharibu laana na alikomboa Eva. Alishinda mauti na alituita ku uzima. Ndio maana katika nyimbo zetu tunasema: Mbarikiwa ni Kristu Mungu wetu aliyetaka hivi. Utukufu kwako.

## DOKSOLOGIA KUBWA

*Wakati waimbaji wanaimba:* Mungu Mutakatifu ile ya mwisho pole-pole, *Padri ataweka Nguo Takatifu ya Epitafios pa kichwa yake na pamoja na waaminifu wote watajunguka pembeni ya Kanisa. Njiani wataimba pole-pole Mungu Mutakatifu na kisha Wimbo ya Epitafios. Wakati watarudi Padri atasimama katikati ndani ya Kanisa na atasema na sauti yake nguvu:*

Tusikilize. Amani kwa wote. Hekima.

*Kisha yeye anaimba Apolitikion hii, na anafukiza na chetezo pembeni ya Epitafios.*

Wakati ulishuka ku mauti, Uzima usiyo kufa, hapa uliregeza kuzimu, kwa unara wa umungu wako; na wakati ulifufua wafu waliyolala kuzimu, ezi zote za mbinguni zilipaza sauti; Mpaji wa uzima Kristu, ee Mungu wetu utukufu kwako.

Yosefu muheshimiwa alishusha mwili wako takatifu msalabani;akaifunika sanda safi na akaizika na manukato kaburini mpya.

Karibu ya Kaburi Malaika aliwatokea wanawake Watakatifu akawaambia: Manukato inawafaa wafu, lakini Kristu ni huru ku uharibifu wote.

Tropari ya unabii

Sauti ya Pili
Wewe mwenye kushika mipaka ya ulimwengu, ulipenda kuzikwa kaburini sababu a kukomboa wanadamu ku zambi yao katika Hadeze. Ulifufuka, ulitupatia zima, ee Wewe Mungu msiyekufa.

**PROKIMENON** Sauti ya Ine

Amka, ee Bwana, utusaidie na utukomboe kwa ajili ya jina Lako.
Kituo: Ee Mungu, masikio yetu yalisikia, na Baba zetu walitufundisha.

Unabii wa Ezekieli (37, 1-14)
Mukono wa Bwana ulikuwa juu yangu, akanichukua inje kwa Roho ya Bwana, akaniweka chini katika bonde; likajaa na mifupa. Akanifanya kuizunguka pande zote; na tazama, ilikuwa mingi sana juu ya uso wa bonde; na tazama, ilikuwa mikavu sana. Akaniambia: Mwana wa watu, mifupa hii inaweza kuishi? Nikajibu: Ee Bwana Mungu, wewe unajua. Akaniambia tena: Tabiri juu ya mifupa hii uiambie: Ee ninyi mifupa mikavu, sikieni neno la Bwana. Bwana Mungu anasema hivi kwa mifupa hii: Tazameni, nitafanya pumuzi kuingia ndani yenu na mutaishi. Na nitaweka mishipa juu yenu na kuleta nyama juu yenu, na kuwafunika ninyi na ngozi, na kutia pumuzi ndani yenu, na mutaishi, na mutajua ya kama mimi ni Bwana. Basi nilitabiri sawasawa

nilivyoagizwa; na wakati nilipotabiri, ilikuwa sauti, na tazama, tetemeko la inchi, mifupa ikakaribiana, mufupa kwa mufupa wake. Nikaangalia, na tazama, mishipa ilikuwa juu yao, nyama ikatokea, na ngozi iliifunika; lakini pumuzi haikuwa ndani yao. Halafu akaniambia: Tabiri kwa upepo, tabiri, mwana wa watu, ukauambie upepo: Bwana Mungu anasema hivi: Toka katika pepo ine, ee pumuzi, ukawapuzie hawa waliouawa, waishi. Basi nikatabiri sawasawa alivyoniagiza, pumuzi ikawaingia, wakaishi wakasimama juu ya miguu yao, jeshi kubwa sana. Halafu akaniambia: Mwana wa watu, mifupa hii ni nyumba nzima ya Israeli; tazama, wanasema: Mifupa yetu imekauka, na taraja yetu imepotea; tumekatiwa mbali kabisa. Kwa hivi tabiri,

ukawaambie, Bwana Mungu anasema hivi:  Tazameni, nitafungua makaburi yenu, na kuwapandisha ninyi toka makaburi yenu, ee ninyi watu wangu; na nitawaleta ninyi kwa inchi ya Israeli. Na mutajua ya kama mimi ni Bwanja, wakati nitakapokwisha kufungua makaburi yenu, na kuwapandisha ninyi toka makaburi yenu, Ee watu wangu. Na nitaweka roho yangu ndani

yenu, na mutaishi, na nitawaweka ninyi katika inchi yenu wenyewe na mutajua ya kama mimi Bwana niliyasema, na kuyafanya Bwana anasema.

**PROKIMENON** Sauti ya Saba

Amka, ee Bwana Mungu wangu, ili mkono wako itukuzwe, usisahau maskini wako milele.

Kituo: Nitakukiri kwa moyo wangu wote, ee Bwana, nitatangaza maajabu yako

Somo la Barua ya Mtakatifu Paulo kwa Wakorinto (1 Korinto 5, 6-8 na Galatia 3, 13-14. . .

Wa ndugu, kujisifu kwenu si kuzuri. Hamujui ya kwamba chachu kidogo inachacha fungu zima? Mujisafishe na kutoa chachu ta zamani, mupate kuwa fungu jipya, kama mulivyo pasipo chachu. Kwa sababu Kristo, Pasaka yetu, amekwisha kutolewa kwa ajili yetu; basi, tufanye karamu, si kwa chachu ya zamani, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, lakini kwa mukate usiochachwa,

ndio moyo safi na kweli. Kristo alitukomboa kwa laana ya torati, akiwa alifanywa laana kwa ajili yetu, kama ilivyoandikwa:  Amelaaniwa kila mutu aliyetundikwa juu ya muti; ili baraka ya Abrahamu ifikie Mataifa kwa Yesu Kristo; tupate kupokea ahadi ya Roho kwa imani.

**WAIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu),*

Sauti ya Tano

Kituo: Mungu asimame, adui zake wasambazwe, na wenye kumchukia wakimbie mbele ya uso wake. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe;

Kituo: Kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.

Kituo: Ndivyo waovu wanavyopotea mbele ya Mungu. Lakini wenye haki wanafurahi, wanashangilia.

Somo la Evangelio kama ilivyoandikwa na Mtakatifu Matayo (27, 62-66).

Basi kesho yake, iliyo siku nyuma ya Matengenezo, wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walikusanyika kwa Pilato, wakisema:  Bwana, tunakumbuka ya kama yule mudanganyifu alisema wakati alipokuwa angali hai:  Nyuma ya siku tatu nitafufuka tena. Agiza basi kaburi lilindwe hata siku ya tatu, wanafunzi wake wasije na kumwiba na kuwaambia watu:  Amefufuka toka wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita wa kwanza. Pilato akawaambia:  Muna askari walinzi; kwendeni mulilinde kwa kadiri munavyoweza. Basi wakakwenda, wakalinda kaburi wakitia lile juwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

SHEMASI ao PADRI: Ektenia: Tuseme sisi wote. . .

Ektenia: Tumalize ombi letu la Asubui kwa Bwana. . .

# SIKU YA SITA MKUBWA

*Saa ya Kwanza, ya Tatu, ya Sita na ya Tisa kama desturi.*

Tropari:
Yosefu muheshimiwa alishusha mwili wako Takatifu Msalabani; akaifunika sanda safi na akaizika na manukato kaburini mpya.

**KONTAKION**
Tunaona anakufa Huyu aliyefunga Hadeze. Anafunikwa sanda na kupakaliwa manukato. Msiyekufa anawekwa Kaburini kama mufu tena wanawake wanakuja kumupakaa manukato wakilia kwa uchungu na wakipaza sauti: Hii Sabato imebarikiwa katika yote, kwa sababu Kristu mwenye kulala atafufuka siku ya tatu.

ESPERINOS
*(kunafwata Liturgia ya Mtakatifu Basile Mkubwa)*

Njooni, tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu,
Njooni, tumwinamie na tumsujudu Kristu yeye Mungu Mfalme wetu,
Njooni, tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI** 103 (104): Umsifu Bwana, ee roho yangu. . .
SHEMASI AO PADRI: Ektenia Ukubwa.
Zaburi ya Mangaribi: Bwana nimekuita, unisikilize. . . Maombi yangu. . .

Kituo: Toka vilindini nimekulilia, ee Bwana. Bwana, sikia sauti yangu.
Sauti ya kwanza

Pokea, ee Bwana Mtakatifu, maombi zetu za mangaribi, na utupatie maondoleo ya zambi zetu; kwa maana ni wewe peke uliyeonyesha ku ulimwengu Ufufuo.

Kituo: Masikio yako yasikilize sauti ya kusihi kwangu.

Mataifa, tembeyeni pembeni ya Sayuni na mumuzunguke, na mumutukuze ndani yake Yeye aliyefufuka katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyetukomboa ku maovu yetu.

Kituo: Kama wewe Bwana, ukihesabu maovu, ee Bwana, nani atayesimama? Lakini usameni pamoja nawe, ili uogopwe.

Kujeni mataifa, tumusifu, na tumwabudu Kristu, tutukuze Ufufuo wake katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyekomboa dunia katika udanganyifu wa adui.

Kituo: Ninangojea Bwana, nafsi yangu inangoja, na ninatarajia neno lake.

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulituopoa ku tamaa mbaya, kwa Ufufuo Wako unatukomboa ku uharibifu, Utukufu Kwako, ee Bwana.

Sauti ya Mnane

Kituo: Nafsi yangu inangoja Bwana, kuliko walinzi wanaongoja asubui; ndiyo, walinzi wanaongoja asubui. Ee Israeli, utarajie Bwana.

Kituo: Maana pamoja na Bwana ni rehema, na pamoja naye ukoombozi mwingi. Naye atakomboa Israeli na maovu yake yote.

Leo Hadeze inalia tena inapaza sauti ikisema: Uwezo wangu umeondolewa, nimepokea mufu mwenye kufanana na wafu wote, lakini siwezi kumuchunga. Ameninyanganya wale walikuwa mu utawala wangu; nilichunga wafu wafungwa tangu milele; yeye amewafufua wote. Ee Bwana, utukufu kwa Msalaba na kwa Ufufuo wako. *(mara ya pili)*

Kituo: Musifu Bwana, ninyi mataifa yote; mumutolee, ninyi watu wote. KIituo: Maana rehema yake kwetu ni kubwa; na kweli ya Bwana inakaa milele.

Leo Hadeze inalia tena inapaza sauti: Ufalme wangu umevunjwa, Mchungaji mwenye kusulubiwa amefufua Adamu; naondolewa wafungwa wangu, na wale nilimeza kwa nguvu yangu nimewatapika. Msulubiwa ameacha makaburi wazi, utawala na mauti unabomoka. Ee Bwana, utukufu kwa Msalaba na kwa Ufufuo wako. *(mara ya pili)*

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya Sita

Musa mkubwa alisema: " Na Mungu akabariki siku ya Saba" Matangulizi ya ajabu ya hii siku ya leo: Tazama Sabato yenyi kubatiziwa; tazama siku ya kupumzika, kwa sababu leo Mwana wa pekee wa Mungu alipumzika kwa kazi zake zote katika lufu yake. Anashangilia Sabato mwilini mwake, tena kwa Ufufuo wake anarudi katika utukufu wake wa kwanza akitupatia uzima wa milele, kwa sababu Yeye ni Mwema tena mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote. . THEOTOKION Sauti ya kwanza.

Utukufu wa ulimwengu, uliyopandwa kwa watu, na ulizaa Bwana, mlango wa mbinguni, tumusifu Bikira Maria, wimbo wa wasiyo mwili, na pambo ya waaminifu; kwa sababu Yeye alikuwa mbingu, na Hekalu la ulungu; yeye alipomoa ukuta ya adui, alibadilisha kwa amani, na alifungua ufalme. Basi pakuwa na hii, nanga ya imani, tuiko na mlinzi, Bwana aliyezaliwa Kwake. Kwa hivi kuwa na moyo, kwa na moyo taifa la Mungu; kwa sababu Yeye anagobanisha adui sawa mwenyezi.

MWANGAZA UPOLE (ILARON)

Somo la 15 Unabii, lakini tunasoma paka Unabii ya Tatu

SOMO LA MWANZO (1, 1-13)

Katika Mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia. Na dunia ilikuwa ukiwa na utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa kilindi; Roho ya Mungu akatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema: Nuru iwe: na nuru ilikuwa. Mungu akaona nuru ya kama ilikuwa vizuri; Mungu akatenga nuru na giza. Mungu akaita nuru Muchana na giza aliita Usiku. Na ilikuwa mangaribi na ilikuwa asubui, siku moja. Mungu akasema: Iwe nafasi katikati ya maji, itenge maji na maji. Mungu akafanya nafasi, akatenga maji yaliyo chini ya nafasi na maji yaliyo juu ya nafasi; na ilikuwa hivi. Mungu akaita nafasi Mbingu. Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya pili. Mungu akasema: Maji chini ya mbingu yakusanyike kwa pahali pamoja na inchi kavu ionekane; na ilikuwa hivi. Mungu akaita inchi kabu Inchi, kusanyiko la maji akaita Bahari. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Mungu akasema: Inchi itoe majani, mboga ikitoa mbegu, na muti wa

matunda ukizaa matunda ya namna yake, mbegu yake iliyo ndani yake, juu ya inchi; na ilikuwa hivi. Inchi ikatoa majani, mboga ikitoa mbegu ya namna yake, na muti ukizaa matunda, mbegu yake iliyo ndani yake, ya namna yake. Mungu akaona ya kama ilikuwa vema. Na ilikuwa mangaribi, na ilikuwa asubui, siku ya tatu.

Unabii ya Yona tunasoma:

Basi neno la Bwana lilikuja kwa Yona, mwana wa Amitai, likisema: Simama uende kwa Ninawe, muji ule mukubwa, ulie juu yake; kwa maana maovu yao yamepanda mbele yangu. Lakini Yona akasimama kukimbia hata Tarsisi toka uso wa Bwana; akashuka hata Yofa, akakuta merikebu ikikwenda Tarsisi, akalipa bei yake, akashuka ndani yake kwenda pamoja nao kwa Tarsisi toka uso wa Bwana. Lakini Bwana akatuma pepo nyingi baharini, na ilikuwa tufani kubwa baharini hata merikebu ilikuwa karibu na kuvunjika. Nao baharia waliogopa, wakalia kila mutu kwa mungu wake; wakatupa baharini vyombo vilivyokuwa katika merikebu ipate kuwa nyepesi kwao. Lakini Yona alikuwa ameshuka mbavuni mwa merikebu; akalala na alikuwa na usingizi. Basi kapiteni akakuja kwake, akamwambia: Una nini, Ee mutu unayelala usingizi? Amka uombe Mungu wako, labda Mungu atatufikili, hata tusipotee. Wakasemezana kila mutu na mwenzake: Kujeni, tupige kura, tujue kwa sababu ya nani ubaya huu ni juu yetu. Hivi wakapiga kura ikaangukua Yona. Halafu wakamwambia: Utuambie, tunakuomba, kwa sababu ya nani ubaya huu ni juu yetu; kazi yako nini? na unatoka wapi? inchi yako wapi? nawe ni mutu wa kabila gani? Akawaambia: Muebrania mimi, na ninaogopa Bwana, Mungu wa mbingu, aliyeumba bahari na inchi kavu. Halafu watu wakaogopa sana, wakamwambia: Kwa sababu gani umefanya hili? Kwa maana watu wakajua ya kuwa amekimbia toka uso wa Bwana, kwa sababu aliwaambia. Kisha wakamwambia: Tutakufanyia nini, bahari iwe kimya kwetu? Kwa maana bahari ilizidi kuchafuka. Akawaambia: Munitwae na kunitupa katika bahari; hivi bahari itakuwa kimya kwenu; kwa maana ninajua ya kwamba kwa sababu yangu tufani kubwa hii ni juu yenu. Hata hivi watu wakavuta sana wapate kufika tena kwa pwani; lakini hawakuweza; kwa sababu hii wakalia kwa Bwana, wakisema: Tunakusihi, Ee Bwana, tunakusihi tusipotee kwa sababu ya uzima wa mutu huyu, wala usitie juu yetu damu safi; kwa maana wewe, ee Bwana, umefanya sawasawa ilivyokupendeza. Hivi wakatwa Yona, wakamutupa katika bahari; ikaacha kuchafuka kwake. Ndipo watu wakaogopa Bwana sana; Wakatoa zabihu kwa Bwana, wakaapa viapo. Bwana akatayarisha samaki mukubwa kumeza Yona; na Yona alikuwa tomboni mwa samaki siku tatu, muchana na usiku. . Halafu Yona akaomba Bwana, Mungu wake, tumboni mwa samaki. Akasema: Kwa sababu ya mateso yangu nimeomba Bwana, Akaniitikia; Toka tumboni mwa Hadeze nimelia, ukasikia sauti yangu. Kwa maana umenitupa vilindini, katika moyo wa bahari, Garika imenizunguka; mawimbi yako yote na garika zako zote zimepita juu yangu. Nikasema: Nimetupwa mbali na macho yako, hata hivi nitatazama tena kwa hekalu lako takatifu. Maji yamenizunguka hata nafsi; kilindi kimenizunguka; majani bule yamefunga kichwa changu. Nikashuka hata chini ya milima; inchi na mafungo yake yamenizunguka milele; hata hivi umepandisha uzima wangu toka kaburi, ee Bwana Mungu wangu. Wakati nafsi yangu ilipozimika ndani yangu, nikakumbuka Bwana, na maombi yangu yamefika kwako katika hekalu lako takatifu. Wenye kuchunga mambo ya bule ya uwongo wanaacha rehema zao. Lakini nitatoa

zabihu kwako kwa sauti ya kushukuru; nitalipa kiapo nilichoapa; wokovu unatoka kwa Bwana. Na Bwana alisema na samaki, akatapika Yona juu ya pwani. Na neno la Bwana lilikuja kwa Yona, mara ya pili, likisema: Simama uende kwa Ninawe, muji mukubwa ule, uuhubiri habari ninayokuambia. Hivi Yona akasimama, akakwenda kwa Ninawe, sawasawa na neno la Bwana. Basi Ninawe ulikuwa muji mukubwa sana, wa safari ya siku tatu. Yona akaanza kuingia mujini kwa safari ya siku moja, akalia, akasema: Bado siku makumi ine na Ninawe utaangamizwa. Watu wa Ninawe wakaamini Mungu; wakatangaza kafunga chakula, wakavaa gunia, toka mukubwa hata mudogo sana katikati yao. Habari zikafika kwa mufalme wa Ninawe, akasimama toka kiti chake cha ufalme, akaondosha mavazi yake juu yake, akavaa gunia, akakaa katika majivu. Akafanya tangazo, akawaambia katika Ninawe kwa amri ya mufalme na wakubwa

wake akisema: Wala mutu wala nyama, wala ngombe wala mbuzi wasionje kitu; wasile chakula wala wasinywe maji, lakini wavae gunia, watu na nyama, na walie na nguvu kwa Mungu; ndiyo wageuke kila mutu toka njia yake mbaya, na toka ukali ulio mikononi mwao. Nani anayejua ya kama Mungu hatageuka na kujuta, na kuacha kasirani yake kali, tusipotee? Mungu akaona

matendo yao, ya kama wakageuka toka njia yao mbaya; Mungu akajuta mabaya aliyoyasema atawafanyia, wala hakuyafanya. Lakini Yona aliona uchungu sana; akakasirika. Akaomba Bwana, akisema: Ninakuomba, ee Bwana, si hili nililosema wakati nilipokuwa katika inchi yangu? Kwa sababu hii nilifanya mbio kukimbia hata Tarsisi; jwa sababu nilijua ya kuwa wewe ni Mungu wa neema, ukijaa na huruma, si mwepesi wa kukasirika, na wa rehema nyingi, ukijuta mabaya. Kwa sababu hii sasa, ee Bwana, ondosha kwangu, ninakusihi, maisha yangu, kwa maana ni vema kwangu kufa kuliko kuishi. Bwana akasema: Unafanya vizuri kukasirika? Kisha Yona akatoka mujini, akakaa kwa upande wa mashariki wa muji, akajifanyia kibanda kule, akakaa chini yake kwa kivuli hata aone nini itakayotokea juu ya muji. Bwana Mungu akatengeneza boga, akaiotesha juu ya Yona iwe kivuli kwa kichwa chake kwa kumuponyesha toka huzuni yake. Basi Yona akafurahi sana kwa sababu ya boga. Lakini Mungu akatengeneza mududu wakati wa asubui kesho yake; akapiga boga, ikakauka. Na ilikuwa wakati jua lilipotoka, Mungu akatengeneza pepo za mashariki nyingi; jua likapiga kichwa cha Yona hata akazima roho, akajiombea afe, akasema: Ni vema kwangu kufa kuliko kuishi. Mungu akamwambia Yona: Unafanya vizuri kukasirika kwa sababu ya boga? Akasema: Ninafanya vizuri kukasirika hata kufa. Bwana akasema: Umehurumia boga usiyotumikia wala usiyootesha; iliyoota usiku na iliyopotea usiku; nami nisihurumie Ninawe, muji ule mukubwa; ndani yake ni watu wengi zaidi ya elfu mia na makumi mbili wasiotambua mukono wao wa kuume wala mukono wao wa kushoto; na ngombe wengi vilevile?

Somo la Unabii wa Danieli (3, 1-28)

Nebukadneza mufalme akafanya sanamu ya zahabu, urefu wake juu ulikuwa mikono makumi sita, na upana wake mikono sita: Akaisimamisha katika inchi sawa ya Dura, katika wilaya ya Babeli. Halafu Nebukadneza mufalme akatuma kukusanya maamiri na wasimamizi na maliwali, waamuzi, na wenye kutunza hazina, washauri, na mawakili, na watawala wa wilaya zote, waje kwa kuanzisha ibada ya ile sanamu Nebukadneza mufalme aliyoisimamisha. Halafu maamiri na wasimamizi, na maliwali, waamuzi, watunza hazina, washauri na mawakili na watawala wote wa wilaya walikusanyika kwa kuanzisha ibada ya sanamu Nebukadneza mufalme aliyoisimamisha; wakasimama mbele ya sanamu Nebukadneza aliyoisimamisha. Halafu muleta habari akapiga kelele akisema: Mumeamriwa hivi, ee watu, mataifa na lugha, wakati mutakaposikia sauti ya panda, nafilimbi, na kinubi, na nzenze, na santuri, na zomari, na namna zote za ngoma, sharti mwanguke chini na kuabudu sanamu ya zahabu Nebukadneza mufalme aliyoisimamisha; na mutu ye yote asiyeanguka na kuabudu atatupwa saa ile ile katika tanuru ya moto unaowaka. Kwa sababu hii wakati ule, wakati watu wote waliposikia sauti ya panda na filimbi na kinubi, na nzenze, na santuri, na zomari, na namna zote za ngoma, watu wote, mataifa yote na lugha zote wakiaanguka na kuabudu sanamu ya zahabu Nedukadneza mufalme aliyoisimamisha. Basi kwa wakati ule Wakaldea wengine walikaribia, wakashitaki Wayuda. Wakajibu na kumwambia Nebukadneza mufalme: Ee mufalme, ishi milele. Wewe, ee mufalme, ulitoa amri, ya kuwa kila mutu atakayesikia sauti ya panda na filimbi na kinumbi, na nzenze na santuri, na zomari, na namna zote za ngoma ataanguka na kuabudu sanamu ya zahabu, na mutu ya yote asiyeanguka na kuabudu atatupwa katika tanuru ya moto unaowaka. Kuna Wayuda wengine uliowaweka juu ya mambo ya wilaya ya Babeli, Sadiraki, Mesaki na Abedenego; watu hawa, ee mufalme, hawakukuheshimu: hawatumikii miungu yako, wala kuabudu sanamu ya zahabu uliyoisimamisha. Halafu Nebukadneza akatoa amri kwa hasira na gazabu yake kuleta Sadiraki, Mesaki na Abedenego. Basi wakaleta watu hawa mbele ya mufalme. Nebukadneza akajibu na kuwaambia: Ni kwa kusudi, ee Sadiraki, Mesaki na Abedenego, hamutumikii mungu wangu

wala kuabudu sanamu ya zahabu niliyoisimamisha? Sasa kama mukiwa tayari wakati mutakaposikia sauti ya panda, na filimbi, na kinubi, na nzenze na santuri, na zomari na namna zote za ngoma, kuanguka na kuabudu sanamu niliyoifanya, ni vema; lakini kama musipoabudu,

mutatupwa saa ile ile katika tanuru ya moto unaowaka; na ni nani mungu ule utakaowaokoa ninyi na mikono yangu? Sadiraki, Mesaki na Abedenego wakajibu na kumwambia mufalme: Ee Nebukadneza, hatuhitaji kukujibu katika neno hili. Kama ni hivi, Mungu wetu tunayemutumikia anaweza kutuokoa na tanuru ya moto unaowaka, naye atatuokoa na mukono wako, ee mufalme. Lakini kama sivyo, ujue, ee mufalme, ya kuwa hatutatumikia miungu yako wala kuabudu

sanamu ya zahabu uliyoisimamisha. Halafu Nebukadneza akajaa gazabu, na sura ya uso wake ikabadilika juu ya Sadiraki, Mesaki na Abedenego; basi akasema na kuamuru watie moto ile tanuru mara saba kuliko desturi yake ya kutiwa moto. Akaamuru watu wengine wenye nguvu waliokuwa katika jeshi lake kufunga Sadiraki, Mesaki na Abedenego, na kuwatupa katika tanuru ya moto uliowaka. Halafu watu wale wakafungwa ndani ya suruali zao na kanzu zao, na joho zao, na mavazi yao, mengine, wakatupwa katika tanuru ya moto uliowaka. Basi kwa sababu amri ya mufalme ilikuwa ya haraka, na tanuru ilikuwa moto sana, ulimi wa moto ukawa watu wale walioshika Sadiraki, Mesaki na Abedenego. Watu hawa watatu, Sadiraki, Mesaki na Abedenego

wakaanguka wamekwisha kufungwa katika tanuru ya moto uliowaka. Halafu Nebukadneza mufalme akashangaa, akasimama kwa haraka; akawaambia washauri wake: Hatukutupa watu watatu wakiwa wamekwisha kufungwa katikati ya moto? Wakajibu na kumwambia mufalme: Ni kweli, ee mufalme. Akajibu na kusema: Tazama, ninaona watu wane, nao wamefunguliwa wanatembea katikati ya moto, wala hawaumizwi: na sura yake yule wa ine ni kama mwana wa Mungu. Kisha Nebukadneza akafika karibu na mulango wa tanuru iliyowaka moto; akatoa maneno na kusema; Sadiraki, Mesaki na Abedenego, ninyi watumishi wa Mungu aliye juu, tokeni, muje hapa. Halafu Sadiraki, Mesaki na Abedenego wakatoka katikati ya moto. Na maamiri, na wasimamizi na maliwali na washauri waliokuwa wamekusanyika, waliona watu hawa ya kuwa moto haukuwa na uwezo juu ya miili yao, wala nyole za vichwa vyao hazikuungua, wala suruali zao hazikubadilika, wala harufu ya moto haikuwapata. Nebukadneza

akatoa maneno na kusema: Abarikiwe Mungu wa Sadiraki, Mesaki na Abedenego aliyetuma malaika yake na kuponyesha watumishi wake waliomwamini, na kugeuza neno la mufalme, na wametoa miili yao ili wasitumikie wala kuababu mungu mwingine ila Mungu wao wenyewe.

*Ku mwisho ya Unabii ya Tatu Waaminifu wote mu Kanisa wanalamuka na Musomaji atasoma moja-moja shairi ya Zaburi na waimbaji wote wataimba hivi:*

Mumuhimidi Bwana na mutukuzeni milele na milele.

**MSOMAJI**:
Enyi nyote, viumbe vya Bwana, mkuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Enyi nyote, Malaika wa Bwana, mbingu za bwana, mkuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Enyi maji ya juu ya anga, mawazo yote ya Bwana, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi jua na mwezi, nyota za mbinguni, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi nyote, mvua na mawingu, enyi nyote pepo, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi moto na hari, kipwa na masika, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi umande na sakitu, gandamizi na baridi, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi barafu na seluji, usiku na muchana, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi mwanga na giza, umeme na mawingu, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi milima na vilima, mimea yote mchipukayo katika inchi, mkuzeni Bwana, kwake. . .

Enyi chemchemi, bahari na mito, nyangumi na vyote vitembeavyo majini, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi nyote ndege za angani, nyota wanyama wa porini na mifugo, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi wanadamu, ewe nyumba ya Israeli, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi Makuhani, watumishi wake, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Enyi mioyo na roho za watu wema, enyi Watakatifu na wanyenyekevu wa moyo, mkuzeni Bwana, kwake utukufu. . .

Hanania, Azaria, Mishaeli, mkuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Mitume, Nabii ma Mashahidi wa Bwana mkuzeni Bwana. . .

Tunamsifu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.
Bwana tunamuhimidi na tunamutukuza milele na milele.

Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamsujudu Bwana.
Bwana tunamuhimidi na tunamutukuza kwa milele wote.

*Pahali pa TRISAGION tunaimba:*

Ninyi wote muliobatizwa katika Kristu, mumevaa Kristu. Alliluia. *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Umevaa Kristu. Alliluia. Nguvu ( Dinamis): Ninyi wote. . .

**PROKIMENON** Sauti ya Tano
Inchi yote ikuabudu na ikuimbie, iimbie jina Lako, ewe Mungu aliye-juu.
Kituo: Paza sauti kwa furaha, ee inchi yote, imbia utukufu wa Jina Lake.

Somo la Barua ya Mtakatifu Paulo kwa Waroma (Rom. 6, 3-11)
Wa ndugu, ao hamufahamu, sisi sote tuliobatizwa katika Yesu Kristo, tulibatizwa katika kufa kwake? Hivi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika kufa: hata kama Kristo alivyofufuka toka wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo tutembee katika upya wa uzima vilevile. Kwa maana kama tulivyoungwa pamoja naye katika mufano wa kufa kwake, tutakuwa katika mufano wa ufufuko wake vilevile; tukijua neno hili, ya kama mutu wetu wa zamani alisulibiswa pamoja naye, mwili wa zambi uharibiwe, tusitumikie zambi tena: kwa sababu yeye aliyekufa amekwisha kuhesabiwa haki toka zambi. Lakini kama tulikufa pamoja na Kristo, tunaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye vilevile; tukijua ya kuwa Kristo akikwisha kufufuka toka wafu, hakufi tena; wala kufa hakumutawali tena. Kwa kule kufa kwake, alikufa zambi mara moja: lakini kwa kule kuishi kwake, anaishi kwa Mungu. Hivyo ninyi mujihesabu wenyewe kuwa wafu kwa zambi, lakini walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.

*Pahali pa Alliluia, tunaimba mstari ya Zaburi 81 (82).*

Sauti ya Saba
Simama, ee Mungu, hukumu dunia, kwani utariti mataifa yote.

*(Hii kituo inakuwa pahali pa Alliluia kisha kila Kituo).*

Kituo: 1. Mungu anasimama katika kusanyiko la Miungu, kati ya Miugu anatoa hukumu.
Simama, ee Mungu. . .

Mpaka wakati gani mtahukumu pasipo haki, na kuwapendeleza waovu?
Simama, ee Mungu. . .

Mupeni haki maskini na yatima. Wao wanaoteswa na wenye hitaji kubwa muwatendee kwa haki.
Simama, ee Mungu, . . .

Ponyesheni maskini na wenye hitaji; muwaokoe toka mukono wa waovu.
Simama, ee Mungu, . . .

Hawajui wala hawatambui; wanakwenda katika giza.
Simama, ee Mungu. . .

Misingi yote ya inchi imetikisika.
Simama, ee Mungu. . .

Mimi nimesema: Ninyi ni miungu, ninyi wote ni wana wa Yule aliye-juu, lakini mutakufa kama wanadamu, na kuanguka kama, wakubwa.
Simama, ee Mungu, . . .

Somo la EVANGELIO kama ilivyoandikwa na Mtakatifu Matayo (28, 1-20)
Basi wakati sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalene na Maria mwingine wakakuja kuona kaburi. Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la inchi; kwani malaika ya Bwana akashuka toka mbinguni, akakuja na kufingirisha jiwe mbali, akaketi juu yake. Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka, wakakuwa kama wafu. Malaika akajibu, akawaambia

wanawake: Musiogope; kwa sababu ninajua ya kama munatafuta Yesu aliyesulibiwa. Yeye si hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Kujeni mwone pahali Bwana alipolala. Na kwendeni mbio muwaambie wanafunzi wake: Amefufuka toka wafu. Tazama, anawatangulia ninyi kwenda Galilaya; pale mutakapomwona; tazama, nimekwisha kuwaambia ninyi. Wakaondoka upesi kutoka kaburi na woga na furaha kubwa, wakakimbia kupasha wanafunzi wake habari. Na tazama, Yesu alikutana nao akisema: Salamu. Wakamukaribia, wakamushika kwa miguu, wakamwabudu. Kisha Yesu akawaambia: Musiogope; kwendeni muwaambie ndugu zangu waende Galilaya, na pale wataniona. Basi wakati walipokuwa wakikwenda, tazama, wengine wa askari walinzi walikuja mujini, wakawaambia wakubwa wa makuhani maneno yote yaliyotokea.

Na wakati walipokusanyika pamoja na wazee, na kufanya shauri, wakawapa askari feza nyingi wakisema: Semeni, Wanafunzi wake wakakuja usiku, wakamwiba wakati tulipolala. Na neno hili likisikiwa na liwali, tutasemezana naye musipate matata. Basi wakatwaa zile feza, wakafanya kama walivyofundishwa. Neno hili likaenea kati ya Wayuda hata leo. Lakini wale wanafunzi kumi na mumoja wakakwenda Galilaya, mupaka mulima ule aliowaagiza Yesu. Na wakati

walipomwona, wakamwabudu; lakini wengine waliona shaka. Yesu akakuja kwao, akawaambia akisema: Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mutakatifu; mukiwafundisha kushika maneno yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi ni pamoja nanyi siku hata mwisho wa dunia. Amina.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

***Kwendelesha Liturgia ya Mtakatifu Basile Mkubwa***

*Wakati wa kuingia kubwa tunaimba hii Wimbo ya Keruvikon:*

Kila mwenye pumzi anyamaze, asimame na woga na atetemeke; aweke mbali wazo lote la dunia. Kwani Mfalme wa Wafalme na Bwana wa mabwana anajongea ili ajitoe mu sadaka na awe chakula cha Waaminifu. Makundi ya Malaika wanamutangulia na Watawala, wenye uwezo, Wakeruvi wenye macho mengi na Waserafi wenye mabawa sita wenyi kujifunika uso, wakiimba: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu.

Wimbo wa Komunyo.
Sauti ya Ine.
Bwana ameamuka kama mtu mwenyi kulala; alifufuka sababu ya kutuokoa.

*Pahali pa: Tumeona. . . tutaimba hii wimbo:*
Ee Bwana utukumbuke, sawa vile ulikumbuke ya Munyanganyi katika ufalme wa mbingu.

*Kisha Kuaga (Apolisis), hatutatoka Kanisani, matunda ya mtini na ya mtende yanagawanywa pamoja na mkate na vinyi. Kisha ni mwanzo wa somo la Matendo ya Mitume.*

# SIKU KUU YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU

## SALA YA ASUBUI (ORTHROS).

**PADRI**: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa. . . Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako. Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji, roho. . .

**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .

**PADRI**: Kwa kuwa ufalme, uwezo. . .

**MSOMAJI**: Bwana hurumia (Mara kumi na mbili). Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Njooni tumwinamie. . . **ZABURI** 50 (51).

*Kisha tunafuata **KANUNI** MBELE YA UFUFUO WA BWANA YESU KRISTU*

WIMBO 1 HIRMOS

Sauti ya Sita.
Zamani Bwana alizika mzulumu chini ya mawimbi ya bahari, wana wa taifa lililofukuziwa walizika Mwokozi wao udongoni. Lakini sisi, kama mabikira wa Israeli tumwinambie Bwana: Kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Ee Bwana, ni wimbo wa kwa heri ninaimba pa Kaburi Yako; lakini Kaburi Yako imenifungulia milango ya uzima na lufu Yako ilikuwa mauti na hadeze.

Utukufu kwa Baba. . .
Majeshi ya mbinguni na majeshi ya dunia yalipokuona pa kiti cha juu mbinguni na Kaburini hapa chini yakashituka kwa hii lufu. Hii jambo ilipita wazo lao: Hayakuweze kuvumilia pa kuona Muumba wa uzima wote amelala katika mauti.

Sasa na siku zote. . .
Kwa kujaza vyote na utukufu wako ulishuka chini ya udongo; hali yangu niliyoriti kwa Adamu haikuweza kukimbia machoni mwako, na kwa kupotea kwangu Kaburi yako imenifanya kuwa mpya, ee Mpenda-wanadamu,

**KATAVASIA**: Zamani Bwana alizika mzulumu. . .

WIMBO 3 HIRMOS
Ee Wewe uliyetundika inchi pa maji, kiumbe ilipokuona umetundikwa kule Kalvario ikashikwa na woga kubwa na ikapaza sauti: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Ulionyesha alama za maziko yako wakati ulipozidisha miujiza, lakini leo ni kwa wakaaji wa hadeze ulionyeshe mafumbo Yako, ee Mungu- Mutu; na wanapaza sauti: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mwokozi, wakati ulipanua mikono Yako na ulifunikwa sanda Kaburini, uliunganisha wale waliotengana zamani. Ulikomboa wafungwa waliokulalamikia: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana.

Sasa na siku zote. . .

Wewe ambaye hauwezi kuenea katika kitu hata kimoja, kwa kutaka kwako wanakufungia Kaburini. Matendo Yako yalifunua uwezo wako kwa wale wenyi kukuimbia: Hakuna aliye Mtakatifu kuliko Wewe Bwana Mpenda- Wanadamu.

**KATAVASIA**: Ee Wewe uliyetundika inchi pa maji, . . .

**PADRI**: Tena na tena ku amani tumwombe Bwana. . . .

**KATHISMA** Sauti ya kwanza

Ee Mwokozi, maaskari waliolinda Kaburi Yako walianguka kama wafu, wakaangaziwa na mwangaza iliowaangazia wanawake na ikawahubiri Ufufuo wako. Utukufu Kwako, Wewe mwenyi kuharibu mauti! Tunaangukia ku miguu yako, Wewe mfufuliwa Kaburini, ee Wewe peke Yako Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . *(mara ingine hii wimbo).*

WIMBO 4 HIRMOS

Alipotambua kujishusha kwako kimungu Msalabani, Habakuki akapaza sauti mwenyi kujaa na woga: Ee Mwema kamili, uliangamiza nguvu ya watawala wakati uliungana na wakaaji wa Hadeze, wewe Mfalme wa vitu vyote.

Utukufu kwako, ee Bungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mwokozi, leo unatakasa siku ya saba, hii zamani ulitakasa wakati ulipumzika kisha kuumba vyumbe vyako, kwa sababu unaumba ulimwengu na unautengeneza Sabato yako na kwa mafundisho yako.

Utukufu kwa Baba. .

Ee Neno, ni kwa uwezo wako kamili ulishinda roho yako ilitengana na mwili, ukavunja pamoja vifungo vya mauti na ile ya Hadeze kwa nguvu Yako.

Sasa na siku zote. . .

Ee Neno kwa kuja Kwako Hadeze ilijazwa na uchungu wakati iliona mwanadamu amekuwa Mungu, Mutu mwenyi vidonda nyingi amejazwa na uwezo, hii ono ya woga ikamwacha bila kusema.

**KATAVASIA**: Alipotambua kujishusha Kwako kimungu. . .

WIMBO 5 HIRMOS

Ee Kristu, wakati rehema yako kimungu ilionekana kwa sisi, Isaya akaona nuru yako ikainuke usiku na asubui akalalamikia: Wafu wataamuka, wakaaji wa Kaburi watasimama, na watu wote wa dunia watashangilia.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Muumba, unawafanya wana wa dunia kuwa wapya, Wewe uliyewaumba na unachukua udongo wao. Kaburi na sanda yanafunua fumbo Yako, ee Neno: Kwa sababu mshauri mwema anaonyesha nia ya baba yako ambaye kwa ukarimu wake, ananifanya kuwa mpya katika Nafsi Yako.

Utukufu kwa Baba. . .

Unageuza mufu kwa lufu yako, na mwenyi kuharibika kwa Kaburi yako unawapa wafu hali isiyoharibika kwa sababu Wewe ni MUngu, unamufanya kuwa wa milele huyu ulichukua hali yake. Kwani mwili wako haikuona uharibifu, ee Bwana, na roho yako haikukue katika Hadeze huko ulikuwa mgeni.

Sasa na siku zote. . .

Ulizaliwa kwa Msiyeolewa, ee Muumba wangu, na ku ubavu wako wenye kuchomwa mkuki unaumba kiumbe mpya kwa ajili ya Adamu wa pili Eva mpya. Ulilala usingizi wa ajabu, usingizi uliyo Chemchem ya uzima na iliamka mzima, ewe Mwenyezi.

**KATAVASIA**: Ee Kristu, wakati rehema. . .

WIMBO 6 HIRMOS

Yona alimezwa katika tumbo la Samaki lakini hakukua mule, alitangulia kuonyesha Mateso yako na maziko yako. Alitoka mu tumbo la nyama kama katika Chumba cha Arusi akiwaambia maaskari: Muchunga paka majivuni na uwongo, lakini muliacha rehema.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Uliondolewa ku uzima, ee Neno, lakini haukutengana na mwili uliyochukuwa: Hata kama Hekalu yako ilibomolewa wakati wa Mateso yako, hata kama umungu wako na mwili wako ilikuwa kitu moja katika hii hali mbili wewe peke yako ni Mwana wa Mungu, Mungu tena Mutu.

Utukufu kwa Baba. . .

Zamani ya Adamu ilikuwa ni lufu ya mwanadamu, lakini apana ya Mungu, kwa sababu kama hali ya uvumbi ya mwili wako iliteswa, hali yako ya umungu haikuteseka. Uliingiza uharibifu katika hali isiyoharibika na kwa Ufufuo wako ulifunua Chemchem ya uzima isiyoharibika.

Sasa na siku zote. . .

Hadeze inatawala wanadamu, lakini ufalme wake si wa milele. Ni Wewe, ee Mwenyezi, ulipolala Kaburini, kwa mkono wako wa ufalme ulivunja minyororo ya mauti. Uliwahubiri wale waliolala tangu zamani ukombozi wa kweli, ee Mwokozi, ukawa Mzaliwa wa kwanza katika wafu

**KATAVASIA**: Yona alimezwa katika tumbo. . .

**PADRI**: Ektenia kidogo.

**KONTAKION** Sauti ya mbili

Tunaona anakufa Huyu aliyefunga hadeze. Anafunikwa sanda na kupakaliwa manukato. Msiyekufa anawekwa kaburini kama mufu tena wanawake wanakuja kumupakaa manukato wakilia kwa uchungu na wakipaza sauti: Hii Sabato imebarikiwa katika yote, kwa sababu Kristu mwenyi kulala atafufuka siku ya tatu.

**IKOS**

Huyu aliye na vyote aliinuliwa Msalabani tena viumbe vyote vinaomboleza pakumuona ametundikwa uchi juu ya muti. Jua linaficha nuru yake, nyota inapoteza mwanagaza wao, kwa woga kubwa inchi inatetemeka, bahari inakimbia, na mawe yanapasuka. Makaburi yanafunguka, miili ya Watakatifu yanafufuka. Hadeze inalalamika, Wayuda wanafanya shauri sababu ya kuficha Ufufuo wa Kristu: Hii Sabato imetakaswa katika yote, kwa sababu Kristu aliyelala atafufuka siku ya tatu.

*Sinaksario ya Watakatifu ya leo. Na kisha tunasoma hii:*

Muposho Takatifu na Mkubwa tunashangilia Maziko ya Mwili ya Mungu wetu Bwana Yesu Kristu na Kushuka kwake kwa Hadeze, kwa ajili wao kizazi ya watu ilirudi kwa uzima ya milele. Amina.

WIMBO 7 HIRMOS

Muujiza wa kweli! Huyu aliyeopoa vijana watakatifu ku tanuru ya moto anawekwa Kaburini. Ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu mkobozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Hadeze ilipigwa moyoni pakumupokea Huyu ambaye ubavu ulichomwa mkuki. Imelala yenye kuteketezwa kwa moto kimungu. NI kwa ajili ya kutuokoa na tunaimba: Ee Mungu mkobozi, umehimidiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Kaburi heshimiwa yenyi kupokea Muumba kama amelala. Ameonekana kama hazina kimungu ya uzima; ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkobozi, umehimidiwa.

Utukufu kwa Baba. . .

Uzima wa ulimwengu anaitika kuwekwa Kaburini kama ilivyo sheria ya wenye kufa. Lakini hii Kaburi inajifunua kuwa chemchem ya Uzima. Ni kwa ajili ya wokovu wetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkobozi, umehimidiwa.

Sasa na siku zote. . .

Katika Hadeze, Kaburini na katika Edeni mulikuwa Umungu moja na usiyotengana na Kristu pamoja na Baba na Roho Mtakatifu. Ni kwa ajili yetu na tunamwimbia: Ee Mungu Mkobozi, umehimidiwa.

**KATAVASIA**: Muujiza wa kweli! Huyu aliyeopoa. . .

WIMBO 8 HIRMOS

Inama kwa woga, ee mbingu, na tetemekeni ninyi msingi ya inchi kwani tazama Mungu wa mbinguni amehesabiwa katika wafu. Amepokelewa kama mgeni Kaburini, Enyi watoto, mtukuzeni; Enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Hekalu safi kamili limebomolewa na linasimamisha nyumba ya Daudi yenye kubomolewa. Huyu mwenye kukaa juu kabisa ya mbingu, Adamu wa pili, anashuka chini kabisa ya Hadeze sababu ya kumuamusha yule wa kwanza. Enyi watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa, msifuni milele.

Tunahimidi Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Bwana.

Nguvu ya Mitume inanguka, lakini kwa uhodari Yosefu wa Arimathea alipokuona uchi na umekufa, Wewe Mungu aliye juu kabisa, akaomba mwili wako na akaufunika sanda akipaza sauti: Enyi watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni, enyi mataifa, msifuni milele.

Sasa na siku zote. . .

Ee Muujiza, ee rehema, ee uvumilivu wa kweli. Huyu mwenye kukaa juu kabisa ya mbingu anavumilia kufungwa katika jiwe lenyi kufungiwa, na Mungu anatendewa kama muogo. Enyi Watoto, mtukuzeni; enyi makuhani, mwimbieni; enyi mataifa msifuni milele.

**KATAVASIA**: Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Inama kwa woga, ee mbingu, na tetemekeni. . .

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimuheshimu kwa nyimbo, na kumutukuza.

WIMBO 9 HIRMOS

Usilie, ee Mama, wakati unapoona Kaburini Mwana wako uliyezaa bila mbegu. Nitafufuka, nitakutukuzwa kama Mungu nitashangilia katika utukufu wa milele wale wenyi kukusifu kwa imani na mapendo.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Mama yangu, ni kwa kutaka kwangu odongo umeniifunika; walinzi wa Hadeze wanatetemeka pakuniona nimevaa mavazi ya kisasi yenyi damu, kwa sababu kwa Msalaba nimepiga maadui zangu, na kama Mungu nitafufuka na nitakukutukuza.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Viumbe vifurahi na wanadamu washangilie: Ee Hadeze aliye adui imenyanganywa, wanawake wakuje na manukato kukutana nami, Mimi niliyekomboa Adamu na Eva na wazao wao wote, Mimi nitakayefufuka siku ya tatu.

**KATAVASIA**: Usilie, ee Mama, wakati unapoona. . .

**MSOMAJI**: TRISAGION: Mungu Mutakatifu. . .

Apolitikion

Wakati ulishuka ku mauti, uzima usiyo kufa, hapo uliregeza kuzimu, kwa unara wa umungu wako; na wakati ulifufua wafu waliyolala kuzimu, ezi zote za mbinguni zilipaza sauti; Mpaji wa uzima Kristu, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

**PADRI**: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Tena tunakuuomba kwa ajili ya waorthodoksi wote.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya mwarkiepiskopu *(jina lake)* na kwa ajili ya ndugu zetu wote katika Kristu.

**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristo.
**MWIMBAJI**: Bwana hurumia *(mara tatu).*

**PADRI**: Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mupenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na Kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milel na milele.
**MWIMBAJI**: Amina.
**PADRI**: Aliyefufuka katika wafu Kristu Mungu wetu kweli, kwa maombezi ya Mzazi Mungu Bikira Takatifu Mama Wake Maria. . .

*Kisha ndani ya Kanisa watazimisha mishumaa yote na Waimbaji wataingia ndani ya Fasi Takatifu (Ieron) na wataimba wote pamoja Eothinon ya Saba hii:*

Tazama giza na asubui, kwa nini Maria unasimama mbele ya Kaburi. Una giza mingi ndani ya akili yako, kwa ajili ya hii giza unatafuta Yesu amewe kwa wapi. Lakini ona Wanafunzi wanaokimbia mbio pamoja, namna gani walitimiza alama ya ufufuo kwa sanda na kitambaa na walikumbuka Maandiko juu ya hii mambo. Pamoja nao na kwa njia yao na sisi tukikusadiki tunakuimbia wewe Kristu muletaji-uzima.

*Kisha Padri atavaa manguo yake ya utukufu na atasimama mbele ya mlango mkubwa Takatifu na ataanza kuimba hivi:*

Kujeni mupokee nuru, toka Nuru isiyo mwisho na mumutukuze Kristu, aliyefufuka katika wafu.

*Hii wimbo Padri ataimba mara nyingi mupaka Waaminifu wote watawakisha mishumaa yao. Kisha waimbaji wataanza kutoka inje, Padri na Waaminifu wote na wataimba hii wimbo:*

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi wimbiwe kwa Malaika mbinguni na utustahilishe sisi wa dunia kukutukuze kwa mioyo safi.

*Wakati watafika inje ya kanisa pa fasi yenye kutayanishwa vizuri, Padri atasema:*

Na tumsihi Bwana Mungu wetu atustahilishe, kusikia Evangelio Takatifu.
**MWIMBAJI**: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

**PADRI**: Hekima; inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.
**MWIMBAJI**: Na kwa roho yako

**PADRI**: Somo la Evangelio Takatifu ilioandikwa na Mwevangelisti Marko. Tusikilize. (16, 1-8)
Hata sabato ilipokwisha kupita Maria Magdalene na Maria mama ya Yakobo na Salome walinunua manukato, wapate kwenda kumupakaa. Hata asubui mapema sana, siku ya kwanza ya juma, wakakwenda kaburini, wakati jua lilipotoka. Wakasemezana: Nani atakayetufingirishia lile jiwe mbele ya mulango wa kaburi? Hata walipotazama, waliona ya kuwa jiwe limekwisha kufingirishwa, nalo lilikuwa kubwa sana. Wakaingia kaburini, wakaona kijana ameketi upande wa kuume, amevaa nguo nyeupe. Wakashangaa. Naye aliwaambia: Musishangae, munatafuta Yesu wa Nazareti aliyesulibiwa; amefufuka, hayuko hapa. Tazama pahali walipomuweka. Lakini kwendeni mukawaambie wanafunzi wake, na Petro, ya kwamba anawatangulia ninyi kwenda

Galilaya. Mutamwona kule kama alivyowaambia ninyi. Wakatoka, wakakimbia toka kaburini; kwa maana walitetemeka na kustaajabu; wala hawakumwambia mutu neno, sababu waliogopa.

**MWIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

*Kisha Padri anafukiza na chetezo mara tatu Evangelio na anasema:*

Kwa Utatu Mtakatifu, Wenye asili moja, Muumba wa uhai, usiotengana, utukufu uwe daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

**MWIMBAJI**: Amina.

**PADRI**: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima. *(mara tatu).*

*Kisha Padri atasema shairi moja-moja ya Zaburi 67( 68) na waimbaji wataimba:* Kristu alifufuka. . .

Mistari:

1. Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele yake.
2. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe; kama nta inavyoyeyuka mbele ya moto.
3. Hivi waovu wapotee mbele ya Mungu, lakini wenye haki wafurahi.
4. Hii ndiyo siku aliyofanya Bwana, tushangilie na kufurahiwa nayo.

Utukufu kwa Baba. . . Kristu alifufuka. . .

Sasa na siku zote. . . Kristu alifufuka. . .

*Kisha Padri atapaza sauti:* Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda nauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi.

**WAIMBAJI**: . . . aliwapatia uzima.

**PADRI**: Ku amani tumwombe Bwana. . . (Ektenia mkubwa)

*Kisha tunafuata **KANUNI** YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU*

*Wimbo wa Mtakatifu Yoane Damaskinos*

WIMBO 1 HIRMOS

Ufufuo ni leo mataifa tuangazwe Paska ya Bwana Paska. Kwani toka mauti kwa uzima na toka inchi kwa mbingu, Kristu Mungu ulitupitisha sisi tuliyoimba wimbo wa ushindi.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Tusafishe mahasa na tutaona kwa nuru ya Ufufuo isiyoweza kukaribia, Kristu mwenye kungaa kama umeme na tumusikilize wazi aseme furahini na tuimbe wimbo wa ushindi. (*mara ya mbili).*

Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . .

Mbingu zifurahi kama inavyostahili na inchi ishangilie na dunia yote yenyi kuonekana na isiyonekana ifanye Karamu, kwani Kristu alisimama mwenye furaha ya milele.

**KATAVASIA**: Ufufuo ni leo. . .

Kristu alifufuka. . . *(mara tatu)* na kisha:

Yesu akifufuka Kaburini kama alivyosema, alitupatia sisi uzima wa milele na rehema kubwa.

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...

**PADRI**: Kwa kuwa ni Kwako uwezo na utawala na nguvu na utukufu ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

WIMBO 3 HIRMOS

Kujeni kunywe kinywaji kipya chenye kufanyika kwa ajabu si toka mwamba isiyopandwa, lakini toka Kaburi pahali Kristu alitosha chemchem ya uzima usiyoharibika na juu yake tunasimamishwa.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Sasa vyote vilijazwa kwa nuru mbingu na inchi na vilindi, basi kiumbe chote kifanye Karamu ya Ufufuo wa Kristu juu yake kilisimamishwa.

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . .

Jana nilizikwa pamoja na wewe Kristu, leo ninasimama pamoja na wewe mufufuliwa. Nilisulibiwa pamoja na wewe jana, wewe mwenyewe unitukuze, ee Mwokozi katika Ufufuo wako.

**KATAVASIA**: Kujeni kunywe kinywaji kipya. . .

Kristu alifufuka *(mara tatu).* Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena..

**PADRI:** Kwa kuwa Wewe ni Mungu wetu, na Kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata...

*Kisha Msomaji anasoma Hipakoi:*

Waliposadiki alfajiri, wakakuta jiwe limekwisha fingirishwa Kaburini, Maria na wenzake wakasikia Malaika akawauliza: Sababu gani munatafuta miongoni mwa wafu Yeye aliye hai katika nuru ya milele. Tazameni utepe: Nendeni mbiyo kuelezea wote ya kwamba Bwana amefufuka akishinda mauti Mitume wako ukawapa amani, ee wewe unayetuokoa na kutujaza Ufufuo.

WIMBO 4 HIRMOS

Katika zamu kimungu Habakuki aliyesema neno ya kimungu, asimame pamoja nasi na aonyeshe Malaika muletaji-nuru na mwenye kupaza sauti kubwa! Leo wokovu umekuja duniani na ya kama Kristu alifufuka sawa mwenyezi.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Kristu anaonekana mume sawa alifungua tumbo la Bikira, na anaitwa Mwana Kondoo sawa analiwa, huyu ni Paska yetu wasipo kilema ma sawa hakuonja zambi na anaitwa mukamilifu sawa Mungu wa kweli.

Utukufu kwa Baba. . .

Sawa Mwana Kondoo wa mwaka moja taji ya wema mwenye kubariki wa kwetu ametolewa sadaka, kwa kutaka kwake, juu ya wokovu wa wote, Paska ya ficho na tena toka Kaburi jua muzuri, la haki aliangaa kwa sisi.

Sasa na siku zote. . .

Daudi baba wa Mungu alicheza na kuruka, mbele ya Sanduku ya kivuli cha sheria, lakini taifa takatifu la Mungu wanaona timizo ya mifano; tufurahi katika Mungu kwani, Kristu alifufuka sawa mwenyezi.

**KATAVASIA**: Katika zamu kimungu Habakuki. . .
Kristu alifufuka *(mara tatu)*. Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...
**PADRI:** Kwa kuwa u Mungu Mwema na mpenda wanadamu na Kwako tunakutolea utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata...

WIMBO 5 HIRMOS
Asubui mapema tuamuke pahali pa manukato tutolee sifa kwa Rabi, na tutaona Kristu jua la haki lenyi kuleta uzima kwa wote *(mata ya mbili).*

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.
Wafu waliokuwa wafungwa wa minyororo ya Hadeze wakikukazia macho, kwa rehema yako isiyohesabiwa, ee Kristu; walijiharikisha kwa nuru wakatembea kwa shangwe na kupiga mwendo kwa kushangilia Paska ya milele. *(mara ya pili)*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Tujongeeni na mishumaa mikononi kwa Kristu mwenye kutokea Kaburini kama Bwana Arusi, na tufanye Karamu pamoja na kundi lenye kupenda Karamu ya Paska ya Mungu inayoleta wokovu.

**KATAVASIA**: Asubui mapema tuamuke. . .
Kristu alifufuka *(mara tatu)*. Yesu akifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...
**PADRI:** Kwa kuwa Jina lako liheshimiwa na utukufu kamili limetakaswa na kutukuzwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote...

WIMBO 6 HIRMOS
Ulishuka katika vilindi vya udongo, na ulivunja mapigo ya milele iliyochunga wafungwa, ee Kristu, na kisha siku tatu kama Yona alitoka kwa samaki ulifufuka ku Kaburi. *(mara ya pili).*

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.
Ukichunga alama muzima, ee Kristu ulisimama kwa Kaburi, wewe usiyeharibu Bikira wa Mama yako kwa kuzaliwa kwako na ulitufungulia milango ya Paradizo. *(mara ya pili).*

Utukufu kwa Baba. . . sasa na siku zote. . .
Mwokozi wangu mwenye kuishi na kutolewa sadaka pasipo kuchinjwa, sawa Mungu ulijitoa kwa Baba kwa kutaka kwako, ulifufua Adamu na uzao wake wote pamoja nawe wakati wa ufufuo wako kaburini

**KATAVASIA**: Ulishuka katika vilindi. . .
Kristu alifufuka *(mara tatu)*. Yesu akifufuka Kaburini. . .
**SHEMASI:** Tena na tena...
**PADRI:** Kwa kuwa Wewe u Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu na Kwako tutautoa utukufu, kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hate...

**KONTAKION** Sauti ya Mnane

Ulipolala Kaburini, ee Bwana msiyekufa ulivunja nguvu ya Gehena na ulifufuka kwa ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukiwamuru wabebaji-manukato kwa wafurahiwe; ukiwaangalia Mitume wako ukawapa amani, ee wewe unayetuokoa na kutupa ufufuo.

**IKOS**

Wakati jua ya mbele ya jua zamani uliposhuka Kaburini, wanawake wabebaji manukato walikutafuta kama siku, walijiharikisha asubui mapema mumoja kwa mwingine wakiambiana: Rafiki zangu wapenzi, tuendeni tupakae marasi, mwili wenye-kuleta uzima wa yule aliyezikwa unayefufua adamu wenye kuanguka kulala Kaburini; tuendeni, tujiharikishe, sawa Waakili, na tumuabudu na tumutolee marasi sawa zawadi, yeye mwenye kufungwa si kwa sanda ya kitoto,

lakini kwa sanda ya maziko; na tulie, na tulalamike: Simama, ee Rabi, wewe mwenye kuleta Ufufuo kwa wenye kuanguka.

*Sinaksarion ya Watakatifu ya leo. Kisha tunasoma:*

Mu Juma Mukubwa na Tatakatifu ya Paska tunashangilia Ufufuo ubebaji-Uzima wa Bwana Yesu Kristu Mungu na Mwokozi wetu.

*Kisha tunasoma hii:*

Tukikwisha kufikiri ufufuo wa Kristu, tumsujudu Mtakatifu wetu Bwana Yesu aliye peke yake bila zambi, Ee Kristu, tunamsujudu Msalaba wako, tunauimbia na kuutukuza Ufufuo wako takatifu, kwa sababu wewe ni Mungu wetu, hatumjue tena mwengine ila wewe, jina lako tunalitaja, njooni Waaminifu wote tusujudie Ufufuo Takatifu wa Kristu; na tazama, kwa Msalaba wake furaha inaonekana ulimwengu kote, bila ukomo tumutukuze Bwana na tuimbie Ufufuo wake, kwani alipoteswa Msalabani kwa ajili yetu amebadilisha kifo chake. *(mara tatu).*

Yesu alifufuka Kaburini kama alivyosema, alitupatia sisi uzima wa milele na rehema kubwa. *(mara tatu).*

WIMBO 7 HIRMOS

Huyu aliyeponyesha watoto ku tanuru ya moto akijifanya mutu, anateswa kama mwenye kuweza kufa na kwa mateso anavika mwili wa kufa uzuri na uzima usiyoharibika, huyu peke yake ni Mungu wa Mababu mubariki wanamutukuzwa kamili.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana.

Wanawake kwa mawazo kimungu walipoleta manukato wakakimbia mbio nyuma yako, lakini walipokutafuta na machozi sawa mutu mwenye kuweza kufa, walikuabudu na furaha sawa Mungu aliye hai, walipasha habari njema ya Paska ya siri kwa Wanafunzi wako, ee Kristu.

Utukufu kwa Baba. . .

Tunafanya Karamu ya kufa kwa mauti na kushusha kwa Hadeze na malimbuko ya kuja kwa uzima ingine, uzima wa milele, na kwa kuruka tunamusifu yeye mtengenezaji aliye peke yake Mungu wa mababu, mubarikiwa na mutukuzwa kamili.

Sasa na siku zote. . .

Kweli usiku unayoleta wokovu na nuru, nitakatifu na siku Kuu, na ulitangaza habari mbele ya siku yenye kuleta nuru ya Ufufuo, na katika usiku huu Nuru ya milele inaangaza mwili yote kwa Kaburi. *(mara ya pili).*

**KATAVASIA**: Huyu aliyeponyesha Watoto ku tanuru. . .
Kristu alifufuka *(mara tatu)*. Yesu alifufuka kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...
**PADRI:** Kwa kuwa uwezo ya ufalme wako ubarikiwa na utukuzwa ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu...

WIMBO 8 HIRMOS
Hii siku kusanyiko Takatifu siku ya kwanza ya juma siku ya ufalme na utawala, Karamu ya makaramu na siku Kuu ya siku Kuu na katika hii siku tunabarikia Kristu kwa milele.

Utukufu kwa Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana. .
Kujeni tushariki ku uzao mupya wa muzabibu, kwa furaha kimungu, na ufalme wa Kristu katika siku kubwa ya Ufufuo, na tumusifu sawa Mungu kwa milele.

Tunamuhimidi Baba, Mwana, na Roho Mutakatifu Bwana.
Ee Sayuni, nyanjua macho yako pande zote na uone, kwani tazama Watoto wako wenye kwangaa kama nyota wamefika Kwako, toka mangaribi na Kaskazini na Bahari na Mashariki na katika wewe wanatukuza Kristu kwa milele.

Sasa na siku zote. . .
Baba mwenyezi na Neno na Roho hali moja katika sura tatu, kupita hali na kuliko Mungu tumebatizwa kwako na tunakutukuza milele yote.

Tunahimidi, tunatukuza na tunasujudu Bwana.
**KATAVASIA**: Hii siku kusanyiko Takatifu siku ya kwanza. . .
Kristu alifufuka *(mara tatu)*. Yesu alifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: Tena na tena...
**PADRI:** Kwa kuwa imabarikiwa Jina lako na imetukuzwa Ufalme wako ya Baba, na ya Mwana, na ya Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata...

WIMBO 9 HIRMOS

**SHEMASI**: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru. . .

Shairi: Malaika aliita Mujaliwa neema Bikira Safi, Salamu na tena nitasema Salamu, Mwana wako alifufuka siku ya tatu Kaburini.

Ungae, ungae Yesuralema mupya kwa sababu utukufu wa Bwana umepambazuka juu yako. Cheza sasa na shangilia, ee Sayuni, na wewe Muzazi Mungu Safi furahi, katika Ufufuo wa Mwana wako.

Shairi: Tukuza, ee nafsi yangu, yeye aliyefufuka, Kaburini siku ya tatu Kristu muletaji uzima.

Ah kimungu! ah mupendwa, ah nzuri sana ni sauti yako! Kwani ulihaidia bila uwongo ya kama utakuwa pamoja nasi, hata mwisho wa milele, ee Kristu na sisi Waaminifu wenye kuchunga hii nangaa ya matumaini tunashangilia.

Utukufu kwa Baba. . .

Tukuza, ee nafsi yangu utawala wa umungu usiyotengwa ku aina tatu. Ah Paska Kubwa na zabihu, ee Kristu! ah Akili na Neno na Nguvu ya Mungu, utupatie tushirikiane nawe, waziwazi kwa siku ya milele ya ufalme wako.

Sasa na siku zote. . .

Salamu Bikira, salamu, salamu Mubarikiwa, salamu Mutukuzwa kwani Mwana wako alifufuka siku ya tatu Kaburini. Ah kimungu! ah mupendwa, ah nzuri sana ni sauti yako!. . .

**KATAVASIA**: Malaika aliita Mujaliwa neema. . . Ungae, ungae. . .

Kristu alifufuka. . . *(mara tatu)*. Yesu alifufuka Kaburini. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo: tena na tena...

**PADRI:** Kwa kuwa ya nakusifu majeshi yote ya mbinguni na kuleta utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata...

**EKSAPOSTILARION** Sauti ya mbili

Kwa mwili, ee Mufalme na Bwana ulipolala kama mutu mwenye kuweza kufa, ulifufuka siku ya tatu; ukisimamisha Adamu toka uharibifu na uliharibu mauti, ewe Paska uzima usiyoharibika Mwokozi wa dunia. *(mara tatu)*

## MASIFU

Kila mwenye pumuzi. . . Mumusifu. . . Sauti ya kwanza.

*Tunaimba sifa Ine ya Ufufuo na sifa Ine ya Paska. Toka Kitabu ya Paraklitiki kwa sauti ya Kwanza pa fasi ya Masifu tunaimba wimbo ya Ine, hivi:*

Kituo: 1. Musifuni kwa matendo yake makuu, musifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.

Tunasifu, ee Kristu, mateso yako kwa wokovu wetu, na tunatukuza Ufufuo wako.

Kituo: 2. Musifuni kwa mvumo wa baragumu, musifuni kwa kinanda na kiumbi.

Bwana, wewe uliyevumilia Msalaba, na uliharibu mauti, na ulifufuka katika wafu, tuliza uzima wetu, kwa kuwa Wewe ni mwenyezi peke yako.

Kituo: 3. Musifuni kwa ngoma na michezo, musifuni kwa nzenze na filimbi.

Ee Kristu, wewe uliyeteka Hadeze, na ulifufua mutu, kwa ufufuo wako, utustahilishe kwa moyo safi, tukusifu na kukutukuza.

Kituo: 4. Musifuni kwa matoazi yavumayo tamu; musifuni kwa matoazi yavumayo sana. Kwa mwenye pumuzi na amsifu Bwana.

Tukitukuza ukubali Kwako, unaofaa kwa Mungu, tunakusifu, ee Kristu; ulizaliwa kwa Bikira, na ulikuwa msiyetengana na baba; uliteswa sawasawa na mutu, na ulivumilia Msalaba, kama ulivyotaka; ulifufuka toka Kaburi, sawa ulitoka kwa chumba cha arusi, juu ya wokovu wa dunia, Ee Bwana, utukufu kwako.

STIKHIRA YA PASKA     Sauti ya tano

Kituo:   1. Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele ya uso wake.

Paska zabihu leo imeonekana kwetu. Paska mupya takatifu, Paska ya siri. Paska iheshimiwa kamili Paska Kristu Mwokozi, Paska bila doa, Paska Kubwa, Paska ya waaminifu, Paska iliyotufungulia milango ya Paradizo, Paska iliyotakasa Waaminifu wote.

Kituo:  2. Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe; kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.

Kujeni Wanawake mulioona na kutangaza habari, ambieni Sayuni! pokea kwa sisi habari njema ya furaha ya Ufufuo wa Kristu. Furahi, cheza na shangilia, ee Yerusalema, kwa kuona Mufalme Kristu mwenye kutokea Kaburini kama Bwana arusi.

Kituo:  3. Hivi waovu wapotee mbele ya uso wa Mungu na wenye haki wafurahi.

Wanawake wabebaji manukato asubui mapema walisimama mbele ya Kaburi ya Muletaji-uzima, walipata Malaika mwenye kukaa juu ya jiwe na huyu akawaambia akasema; kwa nini munatafuta Yeye aliye hai katika wafu, kwa nini munalilia Yeye asiyeharibika katika uharibifu; mwendeni mukawapashe Wanafunji wake habari.

Kituo:  4. Hii ni siku aliyofanya, tufurahi na kushangilia ndani yake.

Paska ya furaha, Paska Bwana Paska, Paska iheshimiwa kamili ilizika kwetu. Paska kwa furaha tukumbatiane, ah Paska ukombozi wa sikitiko, kwani leo ku Kaburi Kristu akiangaa kama Bwana arusi, akitoka chumbani mwake alijaza wana wake kwa furaha, na kusema muwapashe Mitume habari.

DOKSASTIKON    Sauti ya Tano.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana, na kwa roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ufufuo ni leo tuangazwe ku Karamu, tukumbatiane mumoja kwa mwingine. Tuseme wa ndugu, na wale waliotuchukia tusamehe wale wenyi, kwa sababu ya Ufufuo na hivi tupaze sauti: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima.

*Na mara ingine*:  Kristu alifufuka. . . *(mara tatu).*

# LITURGIA TAKATIFU YA MTAKATIFU YOANE KRISOSTOMO

**PADRI**: Uhimidiwa Ufalme wa Baba. . .
**MWIMBAJI**: Amina.
**PADRI**: Kristu alifufuka. . . *(mara tatu)*

***PADRI** atasema Mistari ya Zaburi 67( 68):*
Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe, wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele ya uso yake.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Hivi waovu wapotee mbele ya Mungu na wenye haki wafurahi.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Hii ni siku aliyofanya tufurahi na kushangilia ndani yake.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Utukufu kwa Baba. . .
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Sasa na siku zote. . .
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .
**PADRI**: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa awale waliokuwa ndani ya kaburi
**WAIMBAJI**: aliwapatia uzima.
**PADRI** ao **SHEMASI**:
Ku amani tumwombe Bwana. . . *Ektenia ukubwa.*

### ANTIFONON YA KWANZA

Musomaji: Mushangilie Mungu, ee inchi yote.
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Muzazi Mungu. . .

**MSOMAJI**: Mwimbe utukufu wa jina lake;tukuzeni sifa yake.
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Mzazi Mungu. . .

**MSOMAJI**: Mmwambieni Mungu: Kazi zako ni za hofu kabisa!
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Mzazi- Mungu. . .

**MSOMAJI**: Inchi yote watakuabudu, na wataimba kwako.
**WAIMBAJI**: Kwa maombi ya Mzazi- Mungu. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Kwa maombi ya Mzazi- Mungu. . .

**SHEMASI**: Ektenia kidogo.

## ANTIFONON YA MBILI

**MSOMAJI**: Mungu aturehemu na atubariki.
**WAIMBAJI**: Utuokoe, ee wewe Mwana wa Mungu, aliyefufuka katika wafu. . .

**MSOMAJI**: Atuangazie uso wake na atuhurumie.
**WAIMBAJI**: Utuokoe, ee wewe Mwana wa Mungu, aliyefufuka katika wafu. . .

**MSOMAJI**: Njia yako ijulikane duniani, wokovu wako katika mataifa yote.
**WAIMBAJI**: Utuokoe. . .

**MSOMAJI**: Watu wakusifu, ee Mungu; watu wote wakusifu.
**WAIMBAJI**: Utuokoe. . .

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye Mwana wa peke. . .

## ANTIFONON YA TATU

**MSOMAJI**: Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele yake.

**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka katika wafu. . .

**MSOMAJI**: Kama moshi inavyopeperushwa, hivi uwapeperushe kama taa inavyoyeyuka mbele ya moto.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .

**MSOMAJI**: Hivi waovu wapotee mbele ya uso wa Mungu na wenye haki wafurahi.
**WAIMBAJI**: Kristu alifufuka. . .

## KUINGIA (ISODIKON)

Katika Makusanyo yenu, mtukuzeni Mungu, mtukuzeni Bwana, enyi wazao wa Israeli. Utuokoe, ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, tunaokuimbia. Alliluia.

*Kisha:* Kristu alifufuka *(mara tatu).*

**HIPAKOI:**
Waliposadiki alfajiri, wakakuta jiwe limekwisha fingirishwa Kaburini, Maria na wenzake wakasikia Malaika akawaambia: sababu gani manatafuta miongoni mwa wafu Yeye aliye hai katika nuru ya milele? Tazameni utepe: Nendeni mbiyo kuelezea wote ya kwamba Bwana amefufuka akishinda kifo, Mwana wa Mungu aokoaye wanadamu.

**KONTAKION**:
Ulipolala Kaburini, ee Bwana Msiyekufa ulivunja nguvu ya Gehena na ulifufuka kwa ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukiwamuru wabebaji-manukato kwa kufurahiwa; ukiwaangalia Mitume wako ukawapa amani, ee wewe unayetuokoa na kutupa ufufuo.

**SHEMASI**: Tumwombe Bwana.
**PADRI**: Kwa kuwa Wewe ni Mtakatifu, ee Mungu wetu na kwako tunautoa. . .

**WAIMBAJI**: Ninyi wote muliobatizwa katika Kristu, mumevaa Kristu.

**MATENDO YA MITUME (APOSTOLOS) (1, 1-9)**

Katika kitabu cha kwanza, Teofilo, nilikuandikia mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha, hata siku ile alipochukuliwa juu nyuma ya kuagiza kwa Roho Mutakatifu mitume aliowachagua, na nyuma ya kuteswa kwake aliwatokea, akawaonyesha kwa alama nyingi ya kuwa yuko hai, akaonekana nao kwa muda wa siku makumi ine, na kusema nao maneno ya ufalme wa Mungu. Hata, akikutana nao, akawaagiza wasitoke Yerusalema, ila wangoje ahadi ya

Baba muliyosikia kwangu; kwani Yoane alibatiza kwa maji, lakini ninyi mutabatizwa katika Roho Mutakatifu nyuma ya siku si nyingi. Wakati walipokutanika wakamwuliza, wakisema: Bwana, utarudishia Waisraeli ufalme wao tena wakati huu? Akawaambia: Si maneno yenu kujua nyakati wala majira Baba aliyoweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mutapokea nguvu wakati Roho Mutakatifu anapokuja juu yenu, nanyi mutakuwa washuhuda wangu katika

Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria, hata mupaka wa dunia. Akikwisha kusema maneno haya, akanyanyuliwa nao wakitazama, wingi likamupokea toka macho yao.

**WAIMBAJI**: Alliluia *(mara tatu).*

**EVANGELION YA YOANE 1, 1-17)**

Katika mwanzo alikuwa Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa Mungu. HUyu kwa mwanzo alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote vilifanyika kwa huyu; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyika. Ndani yake ulikuwa uzima, an uzima ulikuwa nuru ya watu. Na nuru ilingaa katika giza na giza halikuishinda. Palitokea mutu ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yoane. Huyu alikuja kwa ushuhuda, ili ashuhudie nuru, watu wote wapate kuamini kwa huyu. Huyu hakuwa nuru ile, lakini alikuja ashuhudie nuru ile. Ilikuwa nuru ya kweli inayotia nuru kila mutu anayekuja katika ulimwengu. Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu ulifanywa naye na ulimwengu haukumutambua. Alikuja kwake, nao walio wake hawakumupokea. Lakini wote waliomupokea aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu, ndio wale walioamini jina lake. Waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili; wala si kwa mapenzi ya mutu, lakini kwa Mungu. Na Neno alifanyika ya mwili, akakaa kwetu, tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli. Yoane akamushuhudia, akapaza sauti yake, akisema: Huyu ndiye niliyemusema habari

zake. Anayekuja nyuma yangu amekuwa mbele yangu, kwa maana alikuwa mbele yangu. Na katika utimilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema. Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mukono wa Musa, neema na kweli zilikuja kwa mukono wa Yesu Kristo.

**WAIMBAJI**: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Pahali pa wimbo*: Niwajibu kweli leo, *tutaimba hii:*

Sauti ya tano

Malaika aliita Mujaliwa neema, Bikira Safi, salamu na tena nitasema salamu, Mwana wako alifufuka siku ya tatu Kaburini.

Ungae, ungae Yesusalema mupya, kwa sababu utukufu wa Bwana umepambazuka juu yako. Cheza sana na shangilia, ee Sayuni, na ewe Muzazi Mungu Safi furahi katika Ufufuo wa Mwana wako.

*Mbele ya hii sala ya mwisho Padri atasoma Mafundisho ya Mtakatifu Baba yetu Yoanno Kristostomo. Kisha yake tunaimba Apolitikion yake:*

Mtu wowote mwabudu tena rafiki wa Mungu afurahiwe juu ya mwangaza huiwa siku kuu nzuri. Mtumishi wowote mwema awe na furaha kubwa kwa ajili ya Bwana wake! Yule alijitolea katika mafungo apate kupokea sasa mushahara wake! Yule alitumika tangu saa ya kwanza apokee sasa mushahara wake wa kweli kweli. Kama mumoja alikuja kisha saa ya tatu afurahiwe siku hiyi na

kuyishukuru! Kama mumoja alichelewa mpaka saa sita, asikuwe na shaka, kwa sababu hapoteze kitu! Kama kuna mmoja aliongojea mpaka saa tisa, ajongee bila shaka! Kama kuna mmoja alichelewa mpaka saa kumi na moja, asiwe na haya ya ukosefu wa huhudi yake, kwa sababu Rabi ni mweme, anapokea wa mwisho kama vile wa kwanza. Anapokea ku mapumziko yule wa saa ya kumi na moja sawa mtumishi wa saa ya kwanza. Anahurumia wa mwisho tena anatunza wa kwanza. Analeta kwa huyu, na anahurumia mwengine. Anapokea ku mapumziko yule wa saa ya kumi na moja sawa mtumishi wa saa ya kwanza. Anahurumia wa mwisho tena anatunza wa kwanza. Analeta kwa huyu, na anahurumia mwengine. Anapokea matendo tena anakubali mwoyo mwema kwa mapendo. Anaheshimia tendo tena anasifu nia nzuri. Kwa hivi, muwe wote na furaha ya Bwana wenu; wa kwanza kama wa mbili, mutapokea tunzo lake. Watajiri sawa wamaskini, wenyi kukataa na wavivu muungane wote juu ya kusifu siku hiyi. Kama mulifunga ao hamukufunge, leo mufurahiwe. Meza iko tayari, kuleni wote; mwana ngombe eko tayari, hata mmoja asirudi na njaa. Mukubali wote ku karamu ya imani, ku hazina ya wema. Hata mumoja asisikitike juu ya umaskini wake, kwa sababu Ufalme unaonekana kwa ajili ya wote. Hata mumoja asilielie juu ya makosa yake, kwa sababu huruma unatokea kaburini. Hata mumoja asiogope lufu, kwa sababu kifo ya Bwana ilitukomboa wote; alimaliza lufu kisha kufa kwake. Yeye alishuka katika wafu, kwa kifo chake ameshinda mauti. Alijaza lufu na uchungu wakati mwili wake ulishuka kuzimu ya wafu. Na kwa hiyo Nabii Isaya alieleza ya kama: Lufu lulisirika wakati mulipatana ku udongo. Lufu ilizania ya kama ni mwili wa wanadamu, lakini alikuwa Mungu mbele yake; ilizania ya kama ni mwanadamu, lakini ni mtawala wa mbingu; ilikamata kile iliona, ilianguka kwa sababu haikujue umungu wake.

Ee lufu, wapi ushindi wako?
Kaburi, wapi ushindi wako?
Kristu amefufuka, lakini wewe unanguka chini. *(Taifa anajibu: Amefufuka)*
Kristu amefufuka, mashetani wanaanguka.
Kristu amefufuka, malaika wanafurahiwa.
Kristu amefufuka, tazama uzima unatawala.
Kristu amefufuka, hakuna wafu kaburini.
Kwa sababu Kristu amefufuka katika wafu waliotangulia kulala.
Kwa kuwa Utukufu na Uwezo ni kwake milele na milele. Amina.

**APOLITIKION YA MTAKATIFU YOANE** Sauti ya Mnane

Kwa kinywa chako kama taa, neema imechuruzika na ulimwengu uliangaziwa, umevumbua hazina ya uadili, umetuonyesha ukuu wa unyenyekevu. Utafundishe kwa kinwa chako, ewe Baba wetu Yoane Krisostome, utuombee kwa Mwana, Kristu Mungu, ili mioyo zetu ziokoke.

*Waimbaji awataimba:* Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa. . . *lakini wataimba mara tatu:* Kristu alifufuka katika wafu. . .

*Padri ku mwisho ya Liturgia atapaza sauti na msalaba pa mukono yake atasema mbele ya waaminifu wote:* Kristu alifufuka. *Waaminifu watajibu:* Kweli alifufuka. *(Vile watafanya mara tatu). Kisha padri atasema:* Utukufu kwa Ufufuo wake Takatifu wa siku tatu.

*Waaminifu watamujibu:* Tunasujudu Ufufuo wake wa siku tatu.

*Na kisha watu wote wataimba*: Kristu alifufuka katika wafu kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya Kaburi, aliwapatia uzima.

# SALA YA MANGARIBI YA MAPENDO KWA SIKU YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU

**PADRI**: Utukufu kwa Utatu Mtakatifu, wenye asili Moja, Muumba wa uhai, usiotengana daima sasa na siku zote, hata milele na milele.

**WAIMBAJI**: Amina.

**PADRI**: Kristu alifufuka *(mara tatu).*

**WAIMBAJI**: *(mara sita)* .

Na mistari ya Zaburi 67 (68) sawa ku mwanzo ya Liturgia ya Ufufuo.

*Kisha **PADRI** Ektenia mkubwa .*

**WAIMBAJI**: Bwana nimekuita. . . Sauti ya mbili.

Kituo: Kama wewe Bwana, ukihesabu maovu, ee Bwana, nani atasimama? Lakini usamehe pamoja nawe, ili wakaogope.

Kujeni tumwabudu huyu aliyezaliwa na Baba mbele ya milele, Mungu neno aliyechukuwa mwili, kwa Bikira Maria; kwa sababu alivumiliya Msalaba, alijitoa ku maziko, kama alivyotaka, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mtu mpotevu.

Kituo: Ninangojea Bwana, nafsi yangu inangoja, na ninatarajia neno lake.

Kristu Mwokozi wetu, alizimisha maandiko mabaya ya ndani zetu, kwa kuipigilia Msalabani, na aliharibu nguvu ya mauti. Tuabudu Ufufuo wake wa siku tatu.

Kituo: Nafsi yangu inangoja Bwana, kuliko walinzi wanaongoja asubuhi; ndiyo, walinzi wanaongoja asubuhi. Ee Israeli, utarajie Bwana.

Tuimbeni Ufufuo wa Kristu pamoja na malaika wakuu; kwa maana huyu ni Mkombozi, na Mwokozi wa roho zetu; na maogopesho ya utukufu, na nguvu ya uwezo, eko nakuja tena, kuhukumu dunia aliyeumba.

Kituo: Maana pamoja na Bwana ni rehema, na pamoja naye ukombozi mingi. Naye atakomboa Israeli na maovu yake yote.

Malaika alihubiri ya kuwa wewe ni Rabi, mwenye aliyesulubiwa na aliyezikwa, na aliwaambia wanawake; kujeni tazameni, pahali alipolala Bwana, kwani amefufuka, kama alivyosema, kwa kuwa yeye ni mwenyezi; ndiyo maana tunabudu, wewe peke msiye kufa. Kristu Mpaji wa uzima, utuhurumie.

Kituo: Musifu Bwana, ninyi mataifa yote; mumutolee, ninyi watu wote.

Kwa Msalaba wako ulivunja, apizo la muti; kwa maziko yako uliharibu, nguvu ya mauti; na kwa Ufufuo wako, uliangaza ukoo wa wanadamu; kwa hii, tunalalamika, ee Kristu mwema, na Mungu wetu Utukufu kwako.

Kituo: Maana rehema yake ni kubwa; na kweli ya Bwana inakaa milele. Musifu Bwana.

Mbele yako Bwana, milango ya mauti ilifunguka na woga; wachungaji wa kuzimu pakukuona walipata woga; kwa maana ulivunja milango ya shaba, na kuzuia makomeo ya chuma, na ulituondoa ku giza, na kivuli cha mauti, na kupasua mafungo yaliyotufunga.

Utukufu kwa Baba. . .
Pakuimba wimbo wa wokovu, tunaimba ku kinywa kujeni wote mu nyumba ya Bwana, tusujudu na tuseme; ee Wewe uliyesulubiwa pa muti, na uliyefufuka katika wafu, na uliye mu kifua cha baba, hurumia zambi zetu.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION Sauti ya mbili
Kivuli cha sheria kinafifia, kwani ilikuja neema; sawa kichaka kiliwaka moto bila kuteketezwa, hivyo ulizaa Bikira, na ulibaki Bikira; pahali pa nguzo ya moto, jua la uhaki lilipanda pa fasi ya Musa, Kristu, wokovu wa mioyo zetu.

MWANGAZA UPOLE (ILARON). . .

**PROKIMENON**
Ni nani aliye Mungu Mukubwa, kama Mungu wetu, Wewe ni Mungu wa pekee, aliyetenda matendo wa ajabu.

**MSOMAJI**: Ee Mungu, ulionyesha mataifa yako nguvu yako.

Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
Kituo: Na nikasema: sasa mitaanza; Hii ni mageuzo ya Mukono wa Kuume wa Mwenyezi
**WAIMBAJI**: Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .
**MSOMAJI**: Nilikumbuka matendo ya Bwana na nilifurahi.
**WAIMBAJI**: Ni nani aliye Mungu Mkubwa. . .

**PADRI**: EVANGELIO katika Mwevangelisti Yoanne (20, 19-25).

*Hii Evangelio iko baraka ya Kanisa yetu ya kuisoma katika lugha mbalimbali.*

Basi mangaribi ya siku ile ile, ikiwa siku ya kwanza ya juma, wakati milango ilipofungwa pahali walipokuwa wanafunzi kwa sababu ya kuogopa Wayuda, Yesu akakuja, akasimama katikati, akasema nao: Salama kwenu. Naye akikwisha kusema maneno haya, akawaonyesha mikono yake na mbavu zake. Basi wanafunzi wakafurahi wakati walipoona Bwana.

Basi Yesu akasema nao mara ya pili: Salama kwenu; kama Baba alivyonituma mimi, ninawatuma ninyi vilevile. Naye wakati alipokwisha kusema maneno haya, akawapulizia, akawaambia: Mupokee Roho Mutakatifu. Wo wote mukiwasamehe zambi, zinasemehewa kwao, na wo wote mukiwafungia zambi, zinafungwa kwao.

Lakini Tomasi, mumoja wa wale kumi na wawili, anayeitwa Mupacha, hakuna pamoja nao wakato alipokuja Yesu. Basi wanafunzi wengine wakamwambia: Tumeona Bwana.

Lakini akawaambia: Nisipoona katika mikono yake alama za misumari, na kutia kidole changu katika alama za misumari, na kutia mukono wangu katika mbavu zake, sitaamini hata kidogo.

**PADRI**: Tuseme sisi wote. . .
**MSOMAJI**: Ee Bwana utujalie Mangaribi hii kutulinda na zambi, . . .

**PADRI**: Tumalize ombi letu la Mangaribi kwa Bwana. . .

APOSTIKHA

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, uliangaza ulimwengu nzima, na uliita tena kiumbe chako; Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

*Kisha tunaimba WIMBO ya PASKA (Angalia Masifu ya Orthros ya Paska:*

Sauti ya tano
1. Paska zabihu leo imeonekana kwetu, Paska mupya Takatifu. . .
2. Kujeni Wanawake. . .
3. Wanawake Wabebaji manukato. . .
4. Paska ya furaha, Paska ya Bwana Paska. . .
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Ufufuo ni leo na tuangazwe kwa Karamu. . .

**KUAGA (APOLISIS)**

**UTUKUFU KWA UTATU MUTAKATIFU**
**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIOS**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA**
**1999**